Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

13 APRILI, 2012

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Nne – Tarehe 13 Aprili, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

Mwenyekiti (*Mhe. Jenista J. Mhagama*) *Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba ya Mkutano wetu wa Saba wa Bunge ambao leo ni kikao cha Nne, Katibu.

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge leo hatuna Hati za Kuwasilishwa Mezani kwa hiyo tunaenda moja kwa moja kwenye maswali yaliyopo kwenye Ratiba ya Shughuli za leo na swali la kwanza linaenda ofisi ya Waziri Mkuu na litaulizwa na Mhehsimiwa Rukia Kassim Ahmed Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 39

**Shule ya Kolo kuwa na Wanafunzi watatu Kidato cha Nne**

**MHE. RUKIA K. AHMED** aliuliza:-

Kukosekana kwa walimu wa kutosha, vifaa vya maabara na mazingira magumu katika shule ya Sekondari ya Kolo-Wilaya ya Kondoa kumesababisha wanafunzi wengi kuacha

shule na kubakiwa na wanafunzi watatu (3) tu katika Kidato cha Nne:-

(a) Je, Serikali inawasaidiaje wanafunzi hao waliokumbwa na kadhia hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba wanafunzi hao wana haki ya kupata elimu kama wanafunzi wengine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo kuhusu walimu na wanafunzi katika shule ya Sekondari Kolo kwa kipindi cha miaka minne ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2008 shule ilikuwa na walimu 5 na wanafunzi 36, mwaka 2009 shule ilikuwa na walimu 3 na wanafunzi 28, mwaka 2010 shule ilikuwa na walimu 5 na wanafunzi 26, mwaka 2011 shule ilikuwa na walimu 7 na wanafunzi 25. Kwa sasa shule hii ina jumla ya walimu 10 kwa takwimu hizi hakuna mwaka ambao shule hiyo ilikuwa na wanafunzi watatu.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua haki ya watoto kupata elimu na hivyo imekuwa inahakikisha kuwa wanafunzi wa shule zote nchini ikiwemo Kolo wanapata elimu kwa kuzingatia sheria na miongozo inayotawala utoaji wa elimu nchini. Serikali pia imekuwa ikihakikisha wanafunzi wote nchini wakiwemo wa Kolo wanapata huduma ua elimu ipasavyo kwa kupanga walimu pamoja na uboreshaji miundombinu ya shule. Aidha, Serikali inatambua kuwepo

shule ya Sekondari ya Changaa iliyokuwa na wanafunzi watatu wa kidato cha nne mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, shule ya Changaa iliyoanza mwaka 2006 ilikuwa na wanafunzi 22 waliosajiliwa kidato cha kwanza mwaka 2008, kati ya hao, wanafunzi 3 waliacha shule kwa utoro mwaka 2010 na wanafunzi 16 walihamia katika shule ya sekondari ya Ula mwaka 2009 na mwaka 2010 na hivyo kubakia na wanafunzi 3. Serikali kwa kutambua umuhimu wa wanafunzi hawa watatu kupata elimu ipasavyo iliwasaidia kwa kuwahamishia katika shule ya sekondari ya Ula ambako walifanyia mtihani wa kidato cha Nne mwaka 2011. Mwaka huu shule hii imepangiwa walimu wanne, wawili wamesharipoti na hivi sasa ina jumla ya walimu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge kuendelea kuwahamasisha wananchi wa Halmashauri kuchangia ujenzi wa nyumba za walimu za kutosha pamoja na majengo mengine ili kuwavutia walimu kwa kuwa na mazingira bora ya kuishi na kufundishia.

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a)Je, Serikali haioni kama kukosekana kwa elimu katika baadhi ya Wilaya ni kudumaza Wilaya hiyo kimaendeleo?

(b) Je, Serikali haioni kama iko haja ya kuongezewa mishahara walimu pamoja na mafao mengine ili nao waweze kuhamasika na wasomeshe watoto vizuri?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU-ELIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukosekana kwa elimu baadhi ya Wilaya hili kwa sasa limeshafanyiwa kazi kwa sababu kila Wilaya ina shule za Msingi zilizo katika kila Kijiji na hata kitongoji kilicho kikubwa katika Wilaya zetu.

Lakini pia tuna shule za Sekondari sasa katika kila Kata na sasa tuna jumla ya sekondari 3242 kwa Kata zote nchini ambazo zina uwezo wa kupokea vijana kutoka shule za msingi zilizopo ndani ya Kata yenyewe. Hii ina maana kwamba Serikali imepania kutoa elimu katika kila Wilaya katika shule zake za msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la uongezaji wa mishahara ni kweli kwamba hata mimi nilipokuwa nafanya ziara kwenye Wilaya mbalimbali nchini na kukutana na Walimu, nilipokuwa natoa nafasi ya wao kuchangia katika uboreshaji wa elimu hiyo ilikuwa ni moja ya hoja zao ambazo wanazieleza na Serikali tumelichukua, na kwa bahati nzuri sana Walimu wameshafikisha ombi hili kwa Rais kupitia Chama cha Walimu Tanzania na Rais aliwaahidi kwamba analichukua analifanyia kazi na anaweza kufanyia kazi hilo kadri fedha za Serikali zinavyoweza kupatikana ili pia kuboresha sekta hii na kuwafanya walimu waweze kufanya kazi yao vizuri. Ahsante sana

**MHE. AMOS G. MAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kuniona. Naomba kumwuliza Waziri kwamba matatizo yaliyopo katika Sekondari ya Kolo yapo katika sehemu kubwa sana ya Tanzania na hasa Jimbo la Mvomero ukizingatia kwamba hatuna walimu wa kutosha kuna walimu watatu tu katika sekondari moja hasa Unguru Mascat walimu wanne na maeneo mengi katika Tarafa ya Mgeta;

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuongeza walimu wa kutosha kupitia Bunge hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) :** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya jitihada za kutosha za kuongeza idadi ya walimu nchini ili kusaidia kupunguza ugumu wa kazi ya

walimu waliopo sasa kwa kuwaongezea idadi ya walimu ili wafundishe kwa urahisi na kufanyakazi zao kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 Serikali iliajiri walimu 9226 wakiwepo wa Shule za Msingi na Sekondari na wote tuliwasambaza nchi nzima, mwaka huu tumeongeza idadi hiyo mara tatu zaidi kwamba tumeajiri walimu 24,621 walimu wa shule za msingi kati ya hao ni 11,379 na pia walimu 13242 ni wa sekondari. Na walimu wote wameshasambazwa nchi nzima na kufikia mwezi Machi tarehe 30 mwaka huu, walimu 21,681 wamesharipoti kwenye vituo mbalimbali.

Walimu wa shule za msingi kati ya hao 10,491 wamesharipoti na walimu 11,190 wamesharipoti kwenye shule mbalimbali za sekondari nchini. Mpango huu wa ajira utaendelea kuongezeka kadiri ambavyo wamedahiliwa kupata mafunzo ya ualimu kwenye Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ualimu nchini ili kuongeza idadi ya Walimu na kuweza kupunguza mzingo kama nilivyosema wa Walimu waliopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni jitihada ya Serikali ya kuweza kuboresha sekta ya elimu na walimu hawa ni pamoja na wale ambao tumewapeleka Wilaya ya Mvomero Mkoani Morogoro.

**MWENYEKITI:** Itakuwa ni vizuri kama orodha hiyo Naibu Waziri ikasambazwa kwa Wabunge wote ili waweze kuona mgawanyo wao na kwa kila Wilaya na namna matatizo yalivyobaki katika Wilaya angalau kila Mbuneg aweze kujua mwenendo wa tatizo hilo kwenye Wilaya yake. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU-ELIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha hiyo itapatikana kufikia saa saba mchana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Said Mohammed Mtanda, Mbunge wa Mchinga.

Na. 40

**Ahadi ya Ujenzi wa Daraja Kati ya Mchinga I na Mchinga II**

**MHE. SAID M. MTANDA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa nchi aliahidi ujenzi wa daraja la kuunganisha Mchinga I na Mchinga II:-

(a) Je, ujenzi huo utaanza lini?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zitatumika kwa kazi yote hadi kukamilika kwa daraja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhehsimiwa Rais aliahidi kujenga daraja kuunganisha Mchinga I na Mchinga II kutokana na adha wanayoipata wananchi wa maeneo hayo. Eneo hilo ni Mkondo wa bahari ambao hujaa maji katika miezi ya Agosti hadi Novemba kuanzia saa 10 jioni hadi saa 2 usiku (*highest tide mark*) ambazo kule wanaziita Bamvua.

Kwa kuzingatia ahadi hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi imekamilisha usanifu wa daraja hilo ili kazi ya ujenzi iweze kuanza. Kazi ya ujenzi imepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2012/2013.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu uliofanyika umebainisha kwamba zinahitaji shilingi 380,294,000/- ili kukamilisha ujenzi wa daraja hilo hadi kutumika. Fedha hizi zimeombwa na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi katika bajeti ya 2012/2013 kupitia maombi maalum.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa kuanza kutekeleza baadhi ya ahadi ambazo zilitolewa katika kipindi cha uchaguzi uliopita katika Jimbo langu. Lakini nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa tayari Serikali imepokea maombi lakini Serikali haijasema wazi kwamba maombi hayo yamekubaliwa ili kuwaondoa hofu wananchi wa Jimbo la Mchinga hususani watumiaji wa barabara ile inayotoka Mchinga I, II hadi kule Kijiweni kwamba maombi haya yamekubaliwa na sasa wananchi wakae tayari kusubiri utekelezaji wake katika kipindi hiki cha mwaka 2012/2013.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Serikali mimi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mtanda kwa kutoa shukrani kwa sababu ameonesha na neno la Mungu linasema shukuruni kwa kila jambo. Amekuwa mkweli hapa maana yake nilifikiri kwamba hatasema ukweli, Rais alipokwenda pale katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi alitoa ahadi mbili, ahadi ya kwanza ilikuwa ni kwa ajili ya kituo cha afya cha Kitomanga, zimejengwa wodi mbili pale na Makamu wa Rais Dkt. Mohamed Gharib Bilal, amekwenda pale akaenda kuzindua na kufungua kituo kile kwa maana ya hizo wodi mbili. Kwa hiyo, anavyoshukuru hapa namwelewa.

Pia nimshukuru pia Mheshimiwa Mtanda kwamba ni Mbuneg makini ambaye anafuatilia sana masuala haya yanayohusu Jimbo lake la Uchaguzi, kila siku asubuhi ukiamka unamkuta pale kwangu mpaka inafika mahali namwambia Mtanda sasa inatosha. Kwa hiyo nashukuru kwamba hili amelitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusingeweza kujenga hizo wodi na Bamvua hapo hapo kwa mwaka huu, mimi nataka nimwahidi hapa, hela zinazohitajika kwa ajili ya Bamvua pale Mheshimiwa Saidi na Wabunge ni milioni mia tatu na themanini, sasa anataka kusema kwamba zimepitishwa, nikisema zimepitishwa hapa nitapata mgogoro hapa Wabunge wataniuliza mlizipitishia wapi, hela zote zinapitishiwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumthibitishia ni kwamba tarehe 16 Mwezi wa Nne mwaka huu, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi pamoja na Mkoa watakutana na Hazina kwa ajili ya kuzungumzia maombi haya maalum hasa ikizingatiwa kwamba hii ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona ningependa kumwuliza Waziri kwamba ahadi ya Rais ya kujenga barabara kutoka Singino hadi Hospitali ya Wilaya pale Kinyonga imefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote Mheshimiwa Harrison Mwakyembe alipokuwa anazungumza hapa Naibu Waziri wa Ujenzi alieleza jinsi ambavyo tumekuwa tunatatua haya matatizo, huwezi kufanya vyote kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Nataka nimthibitishie Mbunge kama hii ni ahadi ya Rais, ahadi ya Rais haina mdahalo hapa wala huwa hatuzungumzi

yale ni maelekezo yametolewa kazi yetu sisi ni kwenda kufanya kama ilivyoelekezwa.

Kwa hiyo, nitakwenda kumwona ili aniambie barabara hiyo ni ipi niiangalie halafu nijue kwamba mkakati wa kufanya kazi hiyo ukoje.

Na. 41

**Migogoro ya Ardhi Mwanza.**

**MHE. EZEKIA D. WENJE** aliuliza:-
Migogoro ya ardhi imekithiri sana katika maeneo mengi hapa nchini ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Mwanza maeneo ya Luchelele, Capripoint na Bugarika na Serikali ilishaahidi kushughulikia tatizo hilo lakini mpaka sasa haijafanya hivyo.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu ahadi hiyo ya kuja kutatua migogoro hii ya muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Dibogo Wenje, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilipata mkopo kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaza kwa ajili ya kupima viwanja katika maeneo ya Nyegezi, Buswelu, Nyamhongolo, Kiseke, Luchelele na Bugarika. Katika kutekeleza upimaji viwanja katika maeneo ya Luchelele Ziwani na Bugarika Wilaya ya Nyamagana, Serikali ilitwaa maeneo ya wananchi kwa makubaliano ya kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiini cha migogoro ni madai ya fidia pamoja na wananchi kupewa viwanja kufuatia maeneo hayo kutwaliwa na Serikali kwa ajili ya mradi wa upimaji viwanja 3,500 unaoendelea katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Ili kutatua migogoro hii, Halmashauri imelipa fidia kwa wananchi 1,268 kiasi cha shilingi bilioni 2.63. Wananchi 234 waliobaki hawajalipwa fidia ya shilingi milioni 381.5 ambazo zinatarajiwa kulipwa ifikapo Mei, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Luchelele jumla ya wananchi 229 wanadai fidia baada ya uthamini kufanyika. Kati ya hao wananchi 119 tayari wamelipwa fidia ya shilingi milioni 186.2 yakiwemo makaburi. Aidha, wananchi waliobaki waliokuwa na viwanja katika maeneo ambayo yanapitiwa na miundombinu ya barabara, shule na masoko wamepatiwa viwanja mbadala na hawakulipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi 92 katika eneo la Luchelele ambao walikuwa na maimarisho ya nyumba, maboma na misingi ndani ya viwanja walimilikishwa viwanja hivyo kama wenyeji kwenye maeneo hayo hivyo hawakulipwa fidia. Aidha, wananchi waliokuwa wamekodishwa mashamba kutoka kwa wenye ardhi/mashamba walilipwa fidia ya mazao yao kwa mujibu wa sheria.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwenye eneo la Luchelelena Bugarika katika Jimbo langu kuna matatizo kweli kwenye sekta ya ardhi na Waziri amekiri pale kwamba kuna wengine hawajalipwa fidia na wanategemea kulipwa mwaka 2015.

Hawa watu wanaishi hapa sasa kama mtu hajapewa fidia mpaka leo hawezi wakafanya *development* yeyote kwenye ardhi yake hata kama nyumba inataka kudondoka, lakini ukweli ni kwamba alivyosema kwenye majibu ya Waziri kwamba kuna wengine walipewa ardhi mbadala ya kwenda na badala yake hawakupewa fidia,

Mimi ndiyo natoka Jiji la Mwanza kuna migogoro mikubwa, hizo takwimu zinazosomwa hapo kwmaba kuna watu walilipwa kabisa walio wengi, kuna wengine hawakupewa hata hizo fidia zinazosemwa hapo, kuna wengine hawakupewa ardhi

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa Wenje

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba na niliuliza hapa kwenye Bunge lililopita kwamba Waziri aje arekebishe haya. Je kwa ile ardhi aliyotwaa Waziri wa Ardhi sasa Serikali inasema watakuja lini ili tukae kule Mwanza ili haya matatizo yatatuliwe? Naomba waje mimi nimetoka Mwanza nayajua haya matatizo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ezekia Wenje Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Kwanza kwa ajili ya rekodi kwa sababu nimemsikia Mheshimiwa Wenje anazungumza habari ya mwaka 2015 sikusema mwaka 2015 tumesema mwaka 2012/2013 hiyo kwanza tuwekane vizuri. Kwa ajili ya rekodi pia kwa sababu Mheshimiwa Wenje ni rafiki yangu namfahamu mimi ninayo orodha ya watu wote waliolipwa fidia kwa majina ninayo hapa. Kwa hiyo, hii Mheshimiwa Wenje ni kunionea tu kusema kwamba mimi nimekuja hapa hawajalipwa na nini mimi ninayo orodha yote tuje tukaketi pale ofisini tuchukue jina moja moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tumia *microphone* usikike vizuri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Naitumia, huu ni msisitizo tu. *(Makofi/Kicheko)*

Asubuhi ya leo nimezungumza na Wilson Kabwe ambaye ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mwanza na nikamwambia sikiliza bwana mimi nakwenda majina ninayokwenda kusoma na nakwenda kuwaambia Wabunge na majibu ninayokwenda kutoa ni haya. Sasa tukubaliane akaniambia Mheshimiwa majibu hayo yamekaa sawa sawa kabisa. Lakini ninachotaka kusema hapa ni kwamba hakuna mahali popote ambapo tunaongopa.

Hawa wananchi ambao tumesema kwamba hawakulipwa na wananchi ambao walikuwa na eneo ambalo halina kitu chochote ni ardhi tu iko pale. Sasa ardhi hii kama umeichukua wewe kama Halmashauri unapokwenda kumpa ardhi nyingine pale unampa ardhi tu inaonekana na ile na bahati nzuri wala siyo mbali kwa sababu najua anaweza akaleta suala la *proximity* kwamba kama ardhi iko Ihungu hapa halafu ukampeleka Hombolo thamani yake zitatofautiana na hayo yote nilimwuliza hayo. Kwa hiyo, ninachotaka kukuthibitishia Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ambao nimesema hawalikulipwa, hawakulipwa kwa sababu hakukuwa kuna kitu chochote hakukuwa kuna mimea hakukuwa kuna mihogo, hakukuwa kuna maharage kwa hiyo ndio maana ya kutokulipwa. *(Makofi)*

Sasa kama kuna *argument* nyingine mimi nataka niseme kwa niaba ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tuko tayari tukae na Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Ezekia Wenje njoo ofisi ile ni ya kwako njoo tuzungumze tuseme kwamba ni nini tunazungumza hapa tuweze kukuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho amesema kwamba angehitaji Serikali iende kule. Mimi sina tatizo wala Wizara ya Ardhi haina tatizo. Lakini nataka niseme hapa kwamba tunayo Serikali pale Mwanza, tunayo pale Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, tunayo *Regional Secretariat* iko pale, tunayo Halmashauri iko pale. Zile zote zinatakiwa zifanye kazi hiyo. Lakini kama Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba kuna haja ya sisi wote kwenda kule sisi hatutakuwa na matatizo. Mheshimiwa George Mkuchika yuko hapa ataniagiza mimi nitakwenda kule na Mheshimiwa Waziri Mkuu tutakwenda kufanya kazi hiyo. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ardhi lililoko Mwanza ni sawa na matatizo yaliyoko Shinyanga na matatizo haya yanahitaji Wizara kufika *field* kuweza kutatua matatizo haya na siyo kuyatatua mezani kama Mheshimiwa Naibu Waziri anavyoeleza.Muda mrefu sisi Wabunge tumekuwa tunaomba Wizara ya Ardhi ifike kwenye maeneo yetu kuweza kutatua matatizo haya ambayo watuhumiwa wakubwa ndio hao watumishi wa Halmashauri. Sasa tukisema Serikali iko kule wakati hao ndio wanaotuhumiwa kusababisha migogoro hiyo ndio hapo tunapotofautiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itueleze ni lini watafika Shinyanga, watafika Mwanza ili kuweza kutatuta matatizo hayo kwenye *field* siyo kwenye meza? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nadhani suala la msingi sasa ni kwenda kuangalia matatizo hayo kwa uhalisia wake ili kuyapatia utatuzi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nimhakikishie Mheshimiwa Maselle kwamba kwa kuwa mahitaji yamekuwa kwamba tufike sisi wenyewe ili kushirikiana nao kutatua kero

hizo baada ya mkutano huu wa Bunge tutaketi pamoja na wenzetu wa TAMISEMI na kupanga ratiba ya kwenda Kanda ya Ziwa kushughulikia kero hizi za ardhi. Tutawajulisha Wabunge haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, nadhani hilo ni jambo la msingi.

Na. 42

**Kurekebisha Bei ya Mazao ya Mahindi na Maharage**

**MHE. JITU V. SONI (K.n.y. MHE. MARTHA J. UMBULLA)** aliliuza:-

Mazao ya mahindi na maharage yanalimwa kwa wingi Mkoa wa Manyara lakini kinachowakatisha tamaa wakulima hao ni bei ndogo ya mazao hayo.

Je, Serikali iko tayari kuweka bei nzuri ya Mahindi na Maharage ili kuhamasisha wakulima kuzalisha kwa wingi na kuwalisha majirani zetu wa Kenya na wengine?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za mazao makuu ya chakula hususan mahindi na mtama hutegemea nguvu ya soko. Serikali haina utaratibu wa kuweka au kupanga bei za mazao hayo. Huduma inayotolewa na Serikali ni kuwapatia wakulima taarifa kuhusu bei za mazao hayo katika masoko ya mazao hayo yaliyopo katika miji Mikuu ya Mikoa.

Bei hizo hutangazwa katika vyombo vya habari hususan Redio, magazeti na sasa kupitia ujumbe wa maandishi katika simu ya viganjani. Huduma hiyo huratibiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu huu wa ununuzi wa mazao Serikali katika Mkutano wa 11 Kikao cha 4 cha Bunge lako Tukufu ilitangaza bei ya mahindi ambayo yatanunuliwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) kuwa ni shilingi 350/= kwa kilo moja ya mahindi. Serikali inafahamu kwamba be inayotumiwa na *NFRA* hutoa mwongozo tu kwa wakulima wengine wanapowauzia wanunuzi binafsi mahindi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuwahimiza wakulima kujiunga katika Vyama vya Ushirika na kuuza mazao yao kupitia utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalanani. Kwa kufanya hivyo wakulima wataepuka uwezekano wa udanganyifu wa bei unaofanywa na wanunuzi binafsi. Aidha, Serikali ikishirikiana na wadau wa maendeleo imeanza mchakato wa kuanzisha soko la mitaji ya mazao *(Agricultural Commodity Exchange Market)* kupitia soko hilo wakulima watakuwa na fursa zaidi ya kupata bei ya mazao yao kulingana na nguvu ya soko na kwa njia ya uwazi zaidi kuliko ilivyo sasa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa azma ya kilimo kwanza ni kuboresha kilimo ili wakulima waweze kuzalisha mazao ya biashara na chakula kwa tija. Lakini pia wapate masoko ya uhakika. Naibu Waziri alivyoeleza ni kwamba bei ya mazao yaliyotajwa haipangwi na Serikali. Lakini mara nyingi sasa hivi Serikali imekuwa na tabia kwa mfano mazao ya maharage ambayo ilikuwa kwenye swali la msingi inazuia hayo mazao kuuzwa nje ya nchi au katika masoko ya uhakika. Kwa mfano mbaazi, maharage na mazao mengine ambayo mkulima amejitahidi kulima bila msaada wowote anaopata kutoka kwa Serikali na anazuiwa kuuza nje.

(a)Je, hilo soko la uhakika Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba haitaweka kizuizi tena? (*Makofi*)

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa mkulima anapata mbegu bora kwa mazao yake. Kwa mfano zao la maharage, mpunga, mbaazi, kunde na mazao mengine. Leo hii Serikali inatoa mbegu ya mahindi tu. Lakini haya mazao mengine ambayo wakulima wanazalisha kwa wingi, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia hiyo mbegu bora ili waweze kuzalisha kwa tija zaidi na waweze kupata mazao mengi zaidi ambayo hayatakuwa na magonjwa na mambo mengine. Hiyo mbegu bora ni lini Serikali itawahakikishia watapata? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jitu Soni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuzuia mazao kuuzwa nje ya nchi kwa kawaida Serikali si nia yetu kuzuia kabisa kwamba mazao yasiende nje lakini kama tulivyoeleza tunaangalia hali ya chakula nchini kwa wakati huo. Hata tulipozuia wakati ule wote mnaelewa kwamba hali ilikuwa mbaya katika nchi jirani kwenda mpaka Somalia, mpaka Sudan wote walikuwa wanategemea kwetu. Kwa hiyo, kama tungeruhusu tu wakati ule nafaka na kila kitu kiende bila shaka mambo yangetugeuka pamoja na ziada ya tani milioni 4.1 tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kifupi tu ni kwamba sheria ya *Export Ccontrol* Namba 381 inamruhusu Mheshimiwa Waziri kuzuia mazao kwa muda tu na hasa yale mazao aina ya nafaka na jamii za kunde kuzuia kwa muda mpaka hali inapokuwa nzuri. Lakini mara hali inapokuwa nzuri tunaruhusu mazao haya yanakwenda. Kwa mfano tangu tumeruhusu baada ya hali kuwa nzuri tani 140,379 zimekwisha

kwenda nje hata maharage yamo na mahindi, mchele na ngano. Kwa hiyo, sheria ile siyo kwamba inazuia tu muda wote hapana. Tunafanya hivyo wakati tunapoona hali ni mbaya, hali inapokuwa nzuri tunaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu bora sisi utaratibu wetu ni huo kwamba vituo vyetu vya utafiti kila mara vinapotoa mbegu bora za mazao yoyote na kila zinapotoka tunawataarifa wakulima kwamba mbegu aina fulani imetoka. Kazi yetu ni hiyo na tunaendelea kutoa mbegu hiyo na kuwafahamisha wakulima ili waweze kuipata mbegu hiyo pale inapopatikana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Jitu Soni kwamba tuwasiliane ili ajue mbegu bora zinavyopatikana. Mimi nina hakika anajua maana vituo vyote mwenyewe ni mdau mkubwa anajua. Kila inapotoka mbegu basi tuwape taarifa waweze kuipata kwa wakati.

**MHE. MARIAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba nimwuliza Naibu Waziri swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mkoa wa Arusha unaongoza kwa kilimo cha mboga mboga na matunda na wengi wa wakulima hao ni wanawake. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha wanawake hawa wanapata soko la uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali kwa ufupi la Mheshimiwa Mariam Msabaha kama ifuatavyo:-

Ningemshauri Mheshimiwa Msabaha tupate muda tuwasiliane niweze kumtambulisha kwa *Horticultural Association of Tanzania* pale Arusha. Watu hawa wana msaada mkubwa sana kuhusu kilimo cha mboga mboga na wataweza pia kukusaidia namna ya kuzalisha mazao haya na kuyapatia soko. Watu wengi wamejitahidi na wamewafikia ikiwa ni pamoja na wahitimu wa vyuo vikuu ambao hawakupata kazi

wakaamua kuingia kwenye mazao kama haya kupitia *Horticultural Association of Tanzania.*

Kwa hiyo, naomba kwa kweli ameuliza swali la msingi naomba tukitumie chombo hiki na mimi niko tayari kabisa kumuelekeza jinsi ya kukitumia ili waweze kupata soko la mazao haya.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Msimu uliopita wakulima wa mahindi Mkoa wa Ruvuma kule Mbinga na Peramiho walipata shida sana na taarifa nilizonazo bado mahindi wanayo. Jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anajibu swali kuhusu korosho alionyesha juhudi za Serikali za kutafuta fedha kwa ajili ya kununua zile korosho kupitia Benki Kuu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza yale mahindi ambayo wakulima wa Mbinga na Paramiho ambayo wanayo mpaka sasa kwa sababu nao ni Watanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kayombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipokuwa nafuatilia suala hili nimegundua pia kwamba tunalo tatizo la takwimu maana wakati mwingine tunasema mahindi yako mengi tunatoa na takwimu lakini tunapofuatilia tunakuta takwimu zile tena siyo sahihi. Kwa mfano tulipata taarifa kwamba ziko tani 2000 za mahindi Ludewa, habari imekwenda mpaka kwa Mheshimiwa Rais, tukatuma aende NFRA wamejiandaa walipofika kule wamenunua tani 370.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna tatizo kidog la takwimu. Lakini nataka bado nikubaliane na Mheshimiwa Kayombo kwamba inaelekea mahindi bado yapo kwa sababu kiashiria ni bei katika Mikoa ambayo bei iko juu ya bei ya

wastani ambayo ni shilingi 430 mikoa ya Nyanda za Juu Kusini bado bei iko chini kwa maana ya kwamba mahindi hayo bado yako kule.

Kwa hiyo, tutajitahidi sasa tuna utaratibu tunawauzuia *World Food Program* fedha tunazozipata tunazitumia tena kununua mahindi ambayo bado yako mikononi mwa wakulima. Wala hatutasubiri tena kwamba mpaka tungojee tusubiri tutakapopata mikopo hapana. Tunapouza mahindi *NFRA* tunawaagiza waende kununua mahindi kule ambako taarifa zimepatikana.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Kayombo pia waendelee kutupa hizo taarifa na mimi nitawaagiza *NFRA* wakishauza mahindi yao fedha zile zinazopatikana wanakwenda kuyanunua.

Na. 43

**Migogoro ya Ardhi Wilaya ya Geita**

**MHE. DONALD K. MAX** aliuliza:-

Migogoro ya Ardhi katika Wilaya ya Geita imekithiri hasa viwanja vya shule ambapo walimu wanasumbuka kuhudhuria kesi kwenye Mahakama za Ardhi:-

(a) Je, kwa nini Maafisa Ardhi wanaohusika na usumbufu huu hawawajibishwi?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuleta Tume ya Uchunguzi haraka kufuatia viwanja vilivyoporwa katika shule tatu za Wilaya ya Geita?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI. NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kama ilivyo kwa watumishi wengine Serikali huwawajibisha watalaam wa sekta ya ardhi mara inapothibitika kuwa wamekiuka maadili ya kazi na taaluma zao ambapo huchukuliwa hatua ama za kisheria au za kinidhamu kutegemeana na uzito wa kosa walilotenda.

Ili kuweka vigezo vya kupima utendaji na kubainisha udhaifu wa maafisa ardhi na fani nyinginezo Serikali ilitunga sheria zinazosimamia taaluma zao ikiwemo sheria ya kusimamia miradi ya wapima na wathamini ya mwaka 1985 na Sheria ya Kusimamia Taaluma ya Maafisa mipangomiji *(Town Planners Registration Act)* ya mwaka 2007.

Vile vile Serikali inaangalia uwezekano wa kutunga sheria ya kusimamia maadili ya Maafisa Ardhi kama ilivyo kwa taaluma nyingine za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2011/2012 Serikali ilichukua hatua za nidhamu kwa watumishi watano wa sekta ya ardhi waliothibitika kuwa waamekiuka maadili ya kazi na taaluma zao.

Kati ya watumishi hao watatu walitoka Makao Makuu ya Wizara na wawili ni wa Halmashauri ya Miji na Wilaya hivyo waliwajibishwa na mamlaka zao za ajira. Uchunguzi unaendelea juu ya utovu wa nidhamu wa maafisa kadhaa wenye tuhuma za ukiukaji wa maadili ya kazi na taaluma zao na hatua inayostahiki itachukuliwa mara uchunguzi utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzikumbusha Halmashauri za Miji na Wilaya kuwa ndizo zenye mamlaka ya kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji wa sekta zote ikiwemo sekta ya ardhi kwenye maeneo yao kupitia Mabaraza ya Madiwani. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe wa Mabaraza hayo wana nafasi kubwa ya kuchangia usimamizi wa watendaji hao kupitia Kamati za Halmashauri zao. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Geita kuwa Wizara yangu iko tayari kushirikiana nao katika kuondoa na kupunguza migogoro ya ardhi Wilaya ya Geita.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa migogoro ya ardhi kati ya wananchi na baadhi ya shule za sekondari na msingi katika Wilaya ya Geita. Migogoro hiyo ni pamoja na mgogoro wa mpaka wa ardhi kati ya Shule ya Msingi Nyarubanga na mwananchi mmoja, mgogoro wa mpaka kati ya Shule ya Msingi ya Nyankumbu na mwananchi mwingine, mgogoro wa mpaka kati ya Shule ya Sekondari ya Bugando na mwananchi mmoja.

Kati ya migogoro hiyo, mgogoro kati ya Shule ya Msingi Nyankumbu na mgogoro wa ardhi kati ya Shule ya Sekondari Bugando na mwananchi mmoja ilishughulikiwa na Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Geita na kumalizika. Mgogoro uliopo kwenye shule ya msingi ya Nyarubanga unaendelea kushughulikia mamlaka hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu kwa kutambua kero na hasara zinazosababishwa na migogoro ya ardhi nchini imeunda Kamati Teule kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya ardhi nchini kote. Moja ya hadidu za rejea za Kamati hiyo ni kufuatilia na kupata ufumbuzi wa kudumu kwa migogoro iliyopo maeneo yote ya nchi ikiwemo kanda ya Ziwa ambayo inajumuisha Wilaya ya Geita.

Hivyo ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuunda Tume ya Uchunguzi wa migogoro ya viwanja vilivyoporwa katika shule Wilayani Geita utafanyika tu endapo kamati hii itashindwa kutoa ufumbuzi wa migogoro hiyo.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya migogoro ya ardhi yakika Wilaya ya Geita yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo Kahama na hasa Kahama Mjini ambako maeneo ya wazi, maeneo ya Serikali na viwanja ambavyo wamegawiwa wananchi wa kawaida yamekuwa yakivamiwa na watu wenye pesa kwa msaada wa Maafisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya, jambo ambalo katika vipindi tofauti limesababisha uvunjifu wa amani.

Je, Serikali inasema nini kuhusu watu wenye hulka hii na lini Waziri atakuja Kahama kujionea mwenyewe kwa macho yake udhalimu unaofanywa na Maafisa wa Ardhi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri inaonekana tatizo hili sasa liko karibu nchi nzima.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimepokea taarifa yake juu ya migogoro ya ardhi itokanayo na uvamizi wa viwanja vya wazi na viwanja vya Umma kwa ujumla unaofanywa na watu wa kisaidiwa na Maafisa Ardhi katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kudhibitisha kwamba sina shaka juu ya tuhuma hizi dhidi ya Maafisa Ardhi kwa kuwa Mheshimiwa James Lembeli, yeye mwenyewe ni Mwenyekiti

wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na kwa hivyo napenda kumshukuru sana kwa taarifa hiyo.

Naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kama nilivyosema wakati nikijibu swali la nyongeza lililoulizwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba tutashauriana na wenzetu wa TAMISEMI na kupanga ratiba ya kwenda Kanda ya Ziwa kushughulikia kero zote zilizopo katika Mikoa hiyo napenda kurudia uthibitisho huo kwamba tutafanya hivyo na tutafanya hivyo mara baada ya Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kama ambavyo nilisema katika jibu la swali la msingi kwamba Wizara yangu imepokea mrejesho kutoka kwa wananchi maeneo mbalimbali ya nchi na ni kutokana na taarifa hizo ndiyo sababu tukaunda Kamati Teule, tumeunda Kamati ambayo imeanza kazi hii mwezi uliopita na kwamba itaenda maeneo yote ya nchi kuchambua kero zilizopo, kusikiliza na kupata ufumbuzi.

Lakini kwa kuwa kipo kilio kikubwa cha Waheshimiwa Wabunge kwamba katika maeneo yao kuna kero hizi na kwamba wanayo imani kwamba Mawaziri wakifika kule suluhisho litapatikana kwa haraka, tutapanga ratiba ya kutembelea Mikoa mbalimbali nchini ili kwa kushirikiana na Viongozi wa Mikoa hiyo, pamoja na Viongozi wa Wilaya zinazohusika tupate ufumbuzi wa kudumu wa kero hizo. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ratiba hiyo ikishapangwa tutaomba Waheshimiwa Wabunge ratiba hiyo wapatiwe. Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 44

**Nyumba Zilizokuwa za Mashirika ya Umma Nchini**

**MHE. ZARINA S. MADABIDA** aliliuza:-

Serikali ilichukua nyumba zake zote na nyingi zilizokuwa za Mashirika ya Umma yaliyovunjwa na kuziweka chini ya Mamlaka ya Wakala wa Majengo *(TBA):-*

(a) Je, Wakala wa Majengo ilichukua jumla ya nyumba ngapi kutoka Serikalini na Mashirika ya Umma?

(b) Je, ni nyumba ngapi kati ya hizo zimeuzwa na fedha kiasi gani zimepatikana?

(c) Je, wakala wa majengo imejenga nyumba ngapi na kwa thamani gani na je ni nyumba ngapi zimeingizwa kwenye ubia na kujenga majengo makubwa na wawekezaji binafsi na kwa masharti gani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Desemba 2011 nyumba zilizochukuliwa na wakala wa majengo kutoka Serikali ni 2,923 na kutoka kwenye Mashirika ya Umma ni 4,571.

(b) Hadi Septemba 2011 jumla ya nyumba zilizouzwa ni 6204 na sio 7494 kama ilivyoingizwa hapa kwa makosa ambapo hadi tarehe 29/3/2012 wakala wa majengo ulikuwa umekusanya kiasi cha Tshs. 54,300,857,283.55 sawa na asilimia 85.51% ya makusanyo ya kiasi cha Tshs. 63,499,134,753.50

yanayotarajiwa kupatikana kutokana na mauzo ya nyumba hizo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala wa majengo hadi Machi, 2012 umejenga nyumba na majengo mengine 1043 kutoka na Tshs. 47,855,194,925.80 zinazotokana na mauzo ya nyumba.

Aidha, nyumba zilizoingizwa kwenye ubia na kujengwa majengo makubwa ni tatu nyumba katika viwanja Na. 45 na 46 Chimara Road karibu na Hospitali ya *Ocean Road* na nyumba katika kiwanja Na. 266 katika kona ya Chole na *Haile Selassie Road* Oysterbay, vyote vikiwa jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala wa majengo uliingia ubia na mwekezaji kwa masharti kwamba thamani ya kila jengo isipungue shilingi bilioni 12 na kwamba asilimia 25 ya kila jengo itakuwa mali ya wakala wa majengo na asilimia 75 ya mwekezaji. Serikali imeagiza wakala wa majengo kupitia upya sera yake ya ubia kwa lengo ya kuboresha mikataba yake na wawekezaji ili kuupa wakala maslahi mapana zaidi kuliko sasa.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili tu madogo:-

(a) Je, ni kweli kwamba hati zilizotumika kuchukua mikopo na mwekezaji ni hati za viwanja hivyo ambavyo zimebadilishwa jina na kusomeka jina la mwekezaji?

(b) Kama hiyo ni kweli kwa nini basi wakala wa majengo asingechukua mwenyewe mkopo na akapata asilimia 100 badala ya kupata asilimia ndogo 25? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Zarina Madabida kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba Serikali imetoa maagizo kwa wakala kupitia upya sera yake ya ubia kwa sababu hatukuridhika vile vile kutokana nah ii *arrangement* iliyopo sasa hivi.

Ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Madabida kwamba tumeliona hilo hata sisi na tungeomba  kwa sababu tuko katika mchakato wa kupitia hiyo mikataba, ningeomba aiachie Serikali halafu baadaye tunaweza tukaongea kuhusu hilo suala.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati Serikali inatekeleza sera yake ya kuchukua na kuuza baadhi ya nyumba za Serikali, kwa bahati mbaya au kwa makusudi, ilichukua nyumba za baadhi ya Vijiji katika Jimbo la Rombo hususan Kata ya Makiidi zilizojengwa kwa nguvu za wananchi kwa ajili ya Maafisa Ugani na Maafisa Kilimo na Maafisa Mifugo.

Jitihada kubwa sana zimefanywa ili kurejeshwa nyumba hizo, lakini imeshindikana. Sasa wananchi wametishia kwenda Mahakamani.

Je, Serikali iko tayari kuiagiza Mamlaka inayohusika kufuatilia jambo hili ili nyumba hizo zirejeshwe kwa wananchi na wazitumie kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge Selasini swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kweli hii taarifa ya wananchi katika Jimbo lake la uchaguzi la Rombo kuamua kwenda Mahakamani ndiyo

naipata sasa hivi, mimi ningemwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hatuhitaji kuingia kwenye malumbano na wananchi na kwenye mgogoro wa kisheria usio na lazima, naomba tuonane basi baada tu ya kipindi hiki cha maswali nielewe suala lenyewe likoje, limekaaje na tuweze kuangalia kama kuna uwezekano wa kuepusha mambo hayo kwenda Mahakamani.

Na. 45

**Taarifa Zilizotolewa na Kitengo cha Hali ya Hewa**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Je, kwa nini kitengo cha masuala ya hali ya hewa nchini kinashindwa kutoa taarifa sahihi za Hali ya Hewa ambazo zingeweza kunusuru maafa yaliyotokea Jijini Mbeya na Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA) inatoa taarifa za utabiri wa Hali ya Hewa na tahadhari kwa Umma kwa vipindi na nyakati mbalimbali mapema kama ilivyokuwa mwishoni mwa mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 7 Septemba, 2011, Mamlaka ya Hali ya Hewa ilitoa taarifa kwenye vyombo vya habari juu ya uwezekano wa kutokea kwa mafuriko kwenye Mikoa yenye mwelekeo wa mvua za msimu wa vuli katika Mikoa ya Kaskazini mwa nchi na Mikoa inayopata msimu mmoja wa mvua hususan Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, ukiwemo Mkoa wa Mbeya.

Aidha, tarehe 20 Desemba, 2011 Mamlaka hiyo ilitoa taarifa nyingine kupitia vyombo vya habari kuhusu uwezekano wa kutokea mafuriko katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo Mkoa wa Mbeya na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la taarifa hizo lilikuwa kuwezesha mamlaka na taasisi mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Miji, Manispaa, Wilaya,Vijiji na taasisi nyingine pamoja na wananchi wenye kuchukua hatua zinazofaa ili kupunguza madhara ambayo yangeweza kutokea katika sehemu za nchi ikiwemo Jiji la Dar es Salaam na Mbeya. Pale wananchi walipozingatia tahadhari na ushauri kwa kuchukuliwa hatua ziliwezesha kuepukana na athari za maafa kama vile mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa hizo za Mamlaka ya Hali ya Hewa, Ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa taarifa kwa Umma kupitia vyombo vya habari mwanzoni mwa mwezi Novemba, 2011 juu ya kuchukua tahadhari kutokana na athari zinazoweza kutokea kutokana na mvua za vuli za mwezi Oktoba hadi Disemba, 2011. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilizitaka Kamati za Maafa kwenye ngazi za Mikoa, Wilaya hadi Vijiji kujiandaa kukabiliana na maafa endapo yangetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingependa kuchukua nafasi hii kutoa pole nyingi kwa wale wote waliopatwa na maafa katika matukio ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa katika maeneo ya Mikoa wa Dar es Salaam, Mbeya na sehemu nyingine nchini. Aidha, Serikali inatoa rai kwa wananchi wote kuzingatia taarifa zitolewazo na Mamlaka ya Hali ya Hewa ikiwemo hali ya mvua za msimu pamoja na tahadhari zitolewazo na Mamlaka na kuchukua hatua zinazotakiwa na kwa wakati. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amejaribu

kutoa taarifa zilizotokea hapa nchini, nilichokuwa nahitaji mimi ni kutoa taarifa sahihi, taarifa ni kweli zinatolewa nakiri hivyo. Katika siku ya juzi walitoa taarifa ya *Tsunami* bahati mbaya haikutokea na katika mwezi wa mwisho wa mwezi wa kumi na mbili wa mwaka jana, kulitokewa na taarifa za mvua kubwa na mafuriko lakini bahati mbaya mvuo haikutokea.

Sasa pamekuwa na *contradiction,* wakitoa taarifa mvua kutokea haitokei, wakitoa taarifa *Tsunami* kutokea haitokei na wasipotoa taarifa mafuriko yanatokea.

(a) Je, Serikali haioni kufanya hivi ni kuwafanya wananchi kukosa imani na Mamalaka ya Hali ya Hewa, hali ambayo ni hatari kwa Taifa letu kwa sababu siku nyingine watu watapuuzia hii taarifa. Hilo ndiyo swali la kwanza.

(b) Katika misimo ya kilimo taarifa za hali ya hewa ni muhimu na ni sahihi kabisa zinahitajika sana ili kuweza kuwezesha watu wetu kulima vizuri na kuwafanikisha kuzalisha vizuri.

Lakini taarifa nyingi za watu wa Mamlaka ya Hali ya hewa katika Mikoa kama ya Nyanda za Juu Kusini imekuwa haitoki, kwa mfano katika Jimbo la Mbozi Magharibi, kipindi cha mwezi wa kumi na mbili, mvua ilinyesha, wananchi wakalima lakini baadaye jua likawaka kali na imeleta ukame na sasa wananchi wanalia njaa.

Je, ni kwa nini sasa taarifa zao nyingi hawatoi hata zinazohusisha na masuala ya ukame? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *Tsunami,* haya masuala ya matukio ya Hali ya Hewa sisi tunashirikiana na taasisi mbalimbali duniani na hizi zinaratibiwa na *UNESCO* ambayo ni *Inter-Organisational Committee,* hizi Kamati zinatuletea taarifa, sisi *TMA* tulipata ile taarifa na kweli tetemeko lilitokea lenye ukubwa wa *rikta 8.7,* ile taarifa ya yale mawimbi yanayotoka Indonesia lazima yalikuja kupiga hapa na ama hakika siku ile kulikuwa na mvua kali Dar es Salaam.

Serikali ilibidi itoe tahadhari, lakini ule mtikisiko ulianza kupungua na yumkini ile jioni tulileta taarifa ya kuboresha ile hali tuliyokuwa nayo kwamba kiwango cha ile tahadahari kimetoka katika daraja la tatu kimekuja mpaka daraja la kwanza. Kwa hiyo, hatari hiyo haikuwepo.

Hii ni taratibu za kisayansi, mimi sioni Mamlaka ya Hali ya Hewa imekosea wapi na imesema kitu ambacho si kweli wapi? Huu ni ukweli mtupu na ni Sayansi imetumika, isabati imetumika na maeneo ya *statistic* na *probability* yote yametumika. Kwa hiyo, ilikuwa ni utaalamu sahihi kabisa, nafikiri *TMA* inastahili pongezi badala ya lawama.(*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la hali ya hewa ya mvua ni kweli mimi nimpe pole Mheshimiwa Silinde kwa kutokea ukame, lakini huu kutokea ukame pale Mbozi Magharibi ni maeneo mengi ukame ulitokea, lakini haya masuala tayari tulikwishakuambiwa na *TMA,* baadhi ya maeneo kutakuwa na upungufu wa mvua na kwamba wananchi wabadilishe ulimaji kama ni mahindi kulima mtama pamoja na mihogo na haya yalikuwa yametabiriwa na taasisi yetu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Kwa hiyo, tutaendela kutoa taarifa hizi kadiri takwimu zinavyopatikana ili wananchi wapunguze hasara kwenye kilimo na taasisi yetu ndiyo sehemu moja ya taarifa hizi kwenye kilimo, kwenye uvuvi katika usafiri na kwingineko.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mimi nina swali dogo tu la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri ambaza hali ya hewa wanazifanya, walikuwa na mpango wa kununua rada za kuangalia masuala ya hali ya hewa angaa za juu ili zisaidie kutoa takwimu sahihi za hali ya hewa nchini na walipanga kuziweka katika Kanda mbalimbali. Je, mpango huu upo bado au ndiyo umefifia? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari Mbunge wa Viti Maalum kama ifuataavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli rada moja tayari Serikali imekwisha kununua na iko hapa Dar es Salaam, rada nyingine inanunuliwa itapelekwa Mwanza na hii nikutaarifu tu kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu ni kwamba sisi Tanzania katika masuala ya utabiri, tumepata hata zawadi kwa sababu tunatoa taarifa ambazo ni sahihi na dunia nzima inazitumia.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini haiko Dar es Salaam. Hapa ni Dodoma. Nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Munde?

Na. 46

**Ukarabati wa Reli na Mabehewa**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH** aliuliza:-

Suala la ukarabati wa Reli na Mabehewa ni kero ya muda mrefu kwa wananchi wa Mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga,Mwanza na Katavi.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mfupi na mrefu wa ukarabati? Na ukarabati huu utaanza lini?

(b) Je, Serikali inaweza kuainisha ukarabati wa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa huduma za reli zinarejeshwa katika hali yake ya kawaida, Serikali ina mipango na mikakati ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na mikakati iliyopo ni kukarabati reli kwa kutandika reli ya uzito wa ratili 80 kwa yadi kutoka Kitaraka ambayo ni Manyoni Magharibi hadi Malongwe (km 89). Mradi huu unatarajiwa kuanza Mei, 2012 na kukamilika baada ya miezi 12. Reli ziko bandarini pale ni kiasi cha kuzipeleka kwenye eneo tu. Aidha, Serikali itaendelea na mradi wa kuinua kiwango cha reli kati ya Kaliua na Mpanda umbali wa kilometa 9 kwa kutumia mataruma yenye uzito wa ratili 56.5 kwa yadi badala ya uzito wa ratili 45 kwa yadi. Kazi ya kuimarisha na kupanua tuta la reli kati ya Kaliua na Mpanda umbali wa kilometa 5 litamilika Mei, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatua ya muda mfupi na za haraka ya kuongeza uwezo wa kusafirisha abiria na mizigo, Serikali kupitia Kampuni ya Reli *Tanzania (TRL)* itaiwezesha kampuni hiyo kukodi injini 13 za treni kati ya mwaka 2012/2013. Aidha, katika kuongeza uwezo na ufanisi wa reli kati ya mwaka 2012/2013 Serikali kupitia *TRL* itakarabati mabehewa ya abiria 31 na mabehewa ya mizigo 165.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na mikakati ya Serikali ni kujenga reli mpya kutoka Dar es Salaam hadi Isaka (km 971) kwa kiwango cha Kimataifa *(standard gauge)* ambayo itaunganishwa na reli mpya ya kutoka Isaka hadi Kigali nchini Rwanda (km 497) na Keza hadi Musongati nchini Burundi (km 197) kwa kushirikiana na nchi za Rwanda na Burundi. Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa reli hii unafanywa na kampuni ya *CANARAIL* kutoka CANADA. Kazi hii ilianza tarehe 17 Februari, 2012 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2013. Aidha, usanifu huo unagharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB) African Development Bank.*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH**: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa reli hii ina umri wa zaidi ya miaka 100 na haijawahi kubadilishwa. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiahidi kila siku kuikarabati reli hii kwa kiwango cha kuridhisha na bila kufanya hivyo na pamoja na majibu mazuri ya kisiasa ya Mheshimiwa Waziri ambayo nimeanza kuyasikia toka 1975 akina Mama Mosi Tambwe wakiwa Wabunge bila mafanikio yoyote. *(Makofi)*

Naomba *commitment* ya Serikali inayoonyesha *action programme* yenye kuambatana na ratiba ya ukarabati wa reli hii?

Swali la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kati ya kilometa 3,000 na zaidi zilizopo za reli amekarabati kilometa 89 tu na kwa kuwa nchi yoyote duniani inategemea sana kupandisha uchumi wake kwa kutumia reli.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuongeza safari za treni ili kurahisisha na kuondoa adha inayowakabili wananchi Tabora, Katavi, Mwanza na Shinyanga? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inatumia pesa kila mwaka kukarabati sehemu ambazo ni korofi. Zile sehemu korofi kilomita 89 ndiyo tumekarabati. Tumetumia pesa nyingi kuweka tuta na vizuizi vya mafuriko pale Gulwe, tumetandika reli upya baada ya mafuriko ya Gode Gode kwa kiasi cha pesa nyingi zaidi ya bilioni tatu. Kwa hiyo Serikali ina *commitment* kurekebisha maeneo haya. Pia katika mpango wetu wa kuboresha reli ndiyo maana tutajenga kiwango cha *standard gauge* ambayo maandalizi yake yanafanyika sasa hivi. Huo mpango uko tayari na Mheshimiwa Munde mimi naomba nimkarabishe, anaweza kuja Ofisini tukamwonyesha ule m pango unaotekelezeka.

Hivi juzi tu Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa shilingi bilioni 45 katika ukarabati wa reli hii hii ya kati. Kiasi ambacho tunaweka utaratibu wa kukarabati injini, tunaweka utaratibu wa kukodi injini. Sasa hivi kuna watalaam wetu wa TRL wako Afrika Kusini wanaziangalia zile injini ambazo zinaweza kuwa na uwezo wa *axolot* ambayo ni zaidi ya 13.7 ambazo madaraja yetu yanaweza kutumia. Kwa hiyo jitihada za Serikali inazifanya ili kuhakikisha hii reli inaendelea kuhudumia wananchi pamoja na mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari za treni utaratibu wetu. Sasa hivi treni ni kweli inaanzia Dodoma kwenda Kigoma na Mpanda. Lakini muda si mrefu tutakuwa tumekamilisha ukarabati pale Gode Gode ambapo mafuriko yalikuwa yanatusumbua. Ule ukarabati ukikamilika hivi punde treni itaanza kutoka Dar es Salaam inakwenda mpaka Tabora inakwenda Kigoma na inakwenda Mpanda. Treni ya kutoka Tabora kwenda Mwanza injini zinakarabatiwa hapa kwenye Karakana yetu Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimekwenda nimeangalia ule ukarabati na kwa bahati nzuri vipuri vimeshafika. Tuna changamoto kubwa moja, hizi injini huwezi

kwenda kuchukua kwenye *shelf* zile *spare parts,* vile vipuri, lazima ufanye *order.* Na ukifanya *order* inachukua kama miezi mitatu vile vipuri ndiyo vinapatikana. Namwomba Mheshimiwa Munde na Waheshimiwa wenzangu wanaotoka katika Kanda zinazopita hii reli waiamini Serikali yao. Sisi tutakarabati ile reli, tutakarabati mabehewa na treni itaendelea kutoka Dar es Salaam-Mwanza. Dar es Salaam-Kigoma. Dar es Salaam-Mpanda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majibu yamekuwa marefu sana na muda umetutupa. Naomba tuendelee na swali linalofuata. Linaulizwa na Mheshimiwa Hamad Ally Hamad, Mbunge wa Magogoni na linaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Hamad?

Na. 47

**Malipo kwa Fidia kwa Askari Polisi Waliorudishwa Kazini**

**MHE. HAMAD ALI HAMAD** aliuliza:-

Kuna Askari Polisi ambao walifukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali lakini baada ya kutoridhika walikwenda Mahakamani na ikaamuliwa kuwa hawana hatia na hivyo warudishwe kazini na kulipwa haki zao; hata hivyo wapo ambao hawajalipwa haki zao hadi leo:-

Je, Serikali inawaeleza nini Askari hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za nidhamu kwa Jeshi la Polisi zipo tofauti kulingana na cheo alicho nacho askari. Hizi

zinaanzia katika ngazi za Makamanda wa Mikoa na Vikosi, Inspekta Jenerali wa Polisi, Tume ya Utumishi ya Jeshi la Polisi na Magereza na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wapo askari ambao baada ya kukamilisha utaratibu wa mashitaka ya kinidhamu wamekuwa hawaridhiki na maamuzi. Hivyo hutumia haki yao ya kwenda katika Mahakama Kuu na kuomba maamuzi hayo yatazamwe upya, yaani *"Judicial Review of Administrative Action".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ninachoweza kuwaambia askari hao ni kwamba nawakaribisha ofisini kwangu ili tuangalie maamuzi hayo ya Mahakama husika na kuchukua hatua zinazostahili.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mahakama ndiyo yenye Mamlaka ya kutafsiri Sheria na kutoa haki na kwa sababu wahusika hawa walishafika Wizarani mara kadhaa bila mafanikio.

Je, Serikali haioni kwamba kutokutekeleza agizo hili la Mahakama kwamba inavunja Sheria?

(b) Kwa kuwa imekuwa ni kawaida kwa Serikali kusuasua katika kutoa haki kwa matokeo kama haya. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unaliambia nini Bunge hili, ni lini watu hawa watapatiwa haki zao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kesi hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge

anazitaja, Serikali ilikata rufaa na tunasubiri Mahakama ya Rufani ifanye maamuzi. Serikali kama tunavyofahamu ikishiriki katika kesi hizo na ikishindwa katika *stage* ya Mahakama Kuu na yenyewe ina haki ya kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufani. Baada ya Mahakama ya Rufani kutoa maamuzi maamuzi hayo yanatekelezwa kama ilivyotakiwa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema muda umetutupa mkono. Sasa nitamwita Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo. Swali hilo linaenda Wizara ya Maji.

Na. 48

**Kampuni ya Maji ya DAWASCO Kufanyiwa Ukaguzi**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Kampuni ya *DAWASCO* imekuwa ikipata Hati zenye Kasoro kwenye hesabu zake kwa miaka minne mfufulizo sasa.

Aidha, wananchi wamekuwa wakilalamika kuhusu matatizo ya kiutendaji ya Kampuni hiyo, hali inayopelekea kuathiri upatikanaji wa maji, Kampuni upata hasara ya mabilioni kutokana na upotevu wa maji wakati wananchi wengi hususan wa Jimbo la Ubungo wanashida kubwa ya maji:-

(a) Je, Serikai ina mpango gani wa kufanya ukaguzi maalum wa kifedha na wa ufanisi kwa DAWASCO ili kuweka mifumo bora kwa ajili ya uwekezaji unaotarajiwa kufanywa?

(b) Je, Serikali iko tayari kufanya ukaguzxi wa mtandao wa mabomba kwani kuna malalamiko mengi kuhusu mtandao huo na uharibifu unaendelea katika mabomba hayo yaliyotandazwa muda mrefu bila maji kutoka?

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani kufuatia hasara iliyotokana na kutotekelezwa kikamilifu kwa mapendekezo ya CAG toka mwaka wa fedha 2007/2008 kuhusu upotevu uliokithiri wa maji unaofanywa na *DAWASCO?*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, *DAWASCO* hufanyia ukaguzi wa hesabu zake na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(Control and Auditor General – CAG)* ambaye amekabidhiwa dhamana hiyo. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 *CAG* alifanya ukaguzi maalum wa utendaji wa kiufundi *(Technical Performance Audit).*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, malakamiko mengi yanayotolewa na wateja wa Kampuni yanahusiana na tatizo la upatikanaji wa maji. Uzalishaji wa maji kwa sasa kutoka kwenye vyanzo vya Ruvu Chini, Ruvu Juu na Mtoni ni wastani wa mita za ujazo lita 270,000 na mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ni mita za ujazo 450,000. Upungufu uliopo wa mita za ujazo 180,000 ndiyo chimbuko la malalamiko yaliyopo.

*DAWASCO* imeanzisha Idara maalum inayoshughulikia upotevu wa maji ambapo katika Idara hiyo vimeundwa Vikosi Kazi vinavyofanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mtandao wa mabomba na kufanyia matengeneo yanayostahili ili kupunguza kiwango cha maji yanayopotea.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza mpango wa CAG kuhusu upotevu wa

maji ni pamoja na kutekeleza mwaka hadi mwaka kwa mkakati wa kufunga dira na kuongeza ufanisi wa usomaji wa dira hizo.

Pia upo mkakati wa kupunguza maji yasiyolipwa *(Non-Revenue Water-NRW)* kufikia asilimia 35 ifikapo mwaka 2013. Mpaka sasa upotevu wa maji *(NRW)* umepungua kutoka asilimia 68 hadi asilimia 42.

Mkakati huu unatekelezwa kwa kuweka mitandao rasmi ya kuunga wateja kama ilivyofanyika kwenye maeneo ya Kimara, Tabata, Kibangu na Mlandizi.

Pia zoezi hili linaendelea kwenye maeneo ya Tegeta, Boko na baadaye litaendelea katika maeneo ya Mbezi hadi Kibaha pamoja na Bunju hadi Bagamoyo. Kufunga dira kwa wateja wote ni zoezi ambalo linaendelea kufanyika katika maeneo yote ya Jiji la Dar es Salaam.

Kwa hivi sasa jumla ya wateja 105,000 sawa na asilimia 85 wamefungiwa dira za maji. Hadi ifikapo tarehe 30 Juni, 2012 wateja wote watakuwa na dira za maji.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza i katika sehemu (a) ya majibu Mheshimwia Naibu Waziri amesema kwamba kwenye mwaka wa fedha 2010/2011 ukaguzi maalum wa utendaji wa kifundi wa *DAWASCO* ulifanyika.

Lakini hakueleza matokeo. Sasa mimi ninazo *correspondence* za ndani kidogo za siri za Serikali zinazoonyesha kwamba katika kipindi hicho cha ukaguzi kulikuw na malalamiko vile vile kuhusiana na tatizo la kiufundi la ubora wa maji. Sasa kwa kuwa baadhi ya taarifa hizo kidogo nyingine zimeanza kuandikwa na vyombo vya habari. Hapa ni gazeti la wiki hii tu inasema ripoti maalum maji ya *DAWASCO* hatari.

Ningependa kupata jibu kutoka kwa Serikali kutokana na ukaguzi huu wa kiufundi uliofanyika. Je, wananchi wa Dar es Salaam wawe na uhakika gani juu ya ubora wa madawa yaliyokuwa yakiwekwa kwenye maji katika kipindi cha mwezi Juni 2010 mpaka mwishoni mwa mwaka 2011 ili wawe na uhakika kwamba maji waliyotumia wakati huo yalikuwa ni safi na salama?

Swali la pili, katika sehemu (b) na (c) ya majibu Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza mipango mbalimbali. Lakini nina ripoti hapa ya ukaguzi ya ufanisi ya mwaka huu wa 2012 ambayo inaeleza kwamba tatizo lililopo ni udhaifu wa usimamizi kwa upande wa *EWURA, DAWASA* na Wizara ya Maji juu ya kusimamia mikataba na makubaliiano na *DAWASCO.*

Sasa ningependa kuuliza swali kwa kuwa mwaka mmoja uliopita Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi kwamba angekuja Jimboni pale Ubungo ili kwa pamoja tushughulikie masuala ya biashara haramu ya maji na uzinduzi wa miradi iliyokwama ya King'ong'o, Mavurunza, Mbezi na kwingineko.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa baada ya Mkutano huu wa Bunge atekeleze ile ahadi ambayo mwaka mmoja umepita bila utekelezaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niwatangazie Watanzania kwamba maji yanayotolewa kwa Jiji la Dar es Salaam ni ya ubora unaokubalika. Kwa sababu vipimo vinapimwa kunzia maabara, kule kwenye chanzo na kule ambako tunaanza kusambaza kwenye yale matenki. Kwa hiyo, tumekuwa tunafanya hii *check up* kila *section* maji yale kwamba yana ubora.

Sasa taarifa ambazo zinaandikwa kwenye magazeti naomba niseme siyo rasmi. Kwa sababu hazijatolewa na Serikali na kama kuna mtu yoyote ambaye amekuwa anazungumza hajapata kibali cha kuzungumza kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo hilo hatukubaliani nalo. *(Makofi)*

Pili, kuhusu suala la kwenda naye kutembelea na kuangalia malalamiko ya watu wanaofanya biashara haramu ya maji. Suala hilo mimi nakubali tunaweza tukafanya. Kwa sababu ndiyo kazi zetu. Suala ambalo hatukubaliani ni la baadhi ya watu wawe wanafanya biashara hizi. Kwa hiyo, kama kuna maeneo mtu yoyote anayafahamu kwamba kuna mtu anayefanya biashara haramu, basi atujulishe ili tuweze kuchukua hatua zinazostahili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nimesema muda umenitupa sana na bado tuna maswali mengi. Naomba mkubali tuendelee na swali Namba 49 linaenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na linaulizwa na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda. Bado tuna maswali kama manne na muda umebakia dakika kumi tu. Mheshimiwa Mary Pius Chatanda?

Na. 49

**Kupandisha Hadhi ya Kituo cha Afya Mombo kuwa Hospitali**

**MHE. MARY P. CHATANDA** aliuliza:-

Kituo cha Afya katika Mji Mdogo wa Mombo kinahudumia zaidi ya watu 38,282 lakini kina upungufu wa Madaktari, Wataalam wa Dawa za Usingizi, Maafisa Uuguzi, Wahudumu Wasaidizi na uchakavu wa majengo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipandisha hadhi Kituo hicho na kuwa hospitali kamili ili kukidhi mahitaji yanayoendana na ukuaji wa Mji huo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuongeza fedha zinazoingizwa na *MSD* kwa ajili ya dawa na vifaa kutokana na majukumu makubwa ya Kituo hicho ikiwemo upasuaji mkubwa unaotokana na majeruhi wengi wa ajali kwenye barabara ya Dar es Salaam – Arusha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakipandisha Kituo cha Afya cha Mombo kuwa Hospitali iwapo kitakidhi vigezo muhimu vilivyowekwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii vya kuwa Kituo cha Afya kama ifuatavyo:-

Kuwepo kwa wodi za kulaza wagonjwa, wodi ya magonjwa ya kawaida kwa wanawake na wanaume, wodi ya watoto, wodi ya wanawake wajawazito wanaongoja kujifungua, wanaojifungua na waliokwishajifungua, wodi ya upasuaji ya wanawake na ya wanaume. Jengo la huduma za upasuaji, huduma za maabara ngazi ya hospitali, huduma za radiolojia, huduma za wagonjwa wa nje, watumishi wa kutosha kulingana na mahitaji ya kituo ngazi ya hospitali, huduma za wagonjwa wa nje, watumishi wa kutosha kulingana na mahitaji ya kituo ngazi ya hospitali, huduma za kuhifadhi maiti na huduma za dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha vigezo hivyo Baraza la Halmashauri litatakiwa kuidhinisha ombi la kupandisha Kituo hiki, kisha Halmashauri kuomba rasmi Kituo hicho kupandishwa hadhi kuwa Hospitali. Wizara baada ya kupokea ombi hilo, itawatuma Wataalamu kufanya ukaguzi kabla ya kibali kutolewa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hutoa mgawo wa fedha kwa Vituo Vya Umma vya Huduma za Afya kulingana na idadi ya wananchi wanaohudumiwa na Kituo. Fedha hizo huingizwa kwenye akaunti ya Kituo iliyopo Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* Dar es Salaam ili kukiwezesha Kituo kuagiza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji. Kutokana na ongezeko la mahitaji ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi linalotokana na ongezeko la watu na sehemu vituo vilipo; kwa mfano vilivyo barabarani, Wizara itaongeza mgawo wa fedha kwa kuzingatia mahitaji halisi. Aidha, Wizara imekuwa ikitoa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo kwa ajili ya kuhudumia majeruhi wanaotokana na ajali za barabarani.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vigezo vyote hivyo vilivyotamkwa vipo; na kwa kuwa Baraza la Halmashauri la Wilaya linaweza likapitisha kwa mujibu wa utaratibu ambao umeelezwa. Je, Wizara itakuwa tayari kuharakisha kutoa Mtaalamu ili kibali hicho kiweze kupatikana bila kuwa na urasimu?

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kituo hiki cha Mombo kinapokea majeruhi wengi wa ajali kama nilivyoeleza kwenye swali langu la msingi. Je, Serikali itakuwa tayari kuwapa angalau majokofu ili kuweza kuhifadhi miili ya maiti hizo ambazo zinakuwa zimetokea kwenye ajali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mary Chatanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba Kituo hicho sasa hivi kimekidhi haya yote ambayo nimeyazungumza. Naomba nimweleze vigezo ambavyo vimekamilika mpaka sasa hivi na ambavyo havipo. Kwa sasa hivi katika Kituo hicho cha Afya cha Mombo, kuna huduma za wogonjwa wa nje na ndani tu ambazo ni wodi mbili, huduma ya upasuaji mdogo majipu na kushona vidonda vidogovidogo, huduma za mama na mtoto, huduma za ushauri nasaha na kupima VVU, huduma za maabara kwa kiwango cha kawaida tu za kituo cha afya, huduma za kutoa damu kwa wagonjwa, huduma za matibabu ya wagonjwa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na huduma za kuzalisha akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ambazo hazipo ni za radiolojia ambazo ni muhimu, huduma za kuhifadhi maiti majengo machache na chakavu ukilinganisha na mahitaji, huduma za dawa ni sawasawa na mgawo wa vituo vingine vyote vya afya. Idadi ya watumishi haikidhi mahitaji, wodi za kulaza wagonjwa zipo mbili tu pamoja na kwamba hakuna wodi ya upasuaji wa wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge, akashauriane na Halmashauri watekeleze haya yote ambayo nimesema hayapo. Nitampa hii orodha ikikamilika. Sisi tutakwenda kukagua, tutawapa kibali pamoja na kutoa mahitaji yote yanayohitajika. Kwa kuwa zinatokea ajali nyingi na maiti zinakuwepo, wanaomba wapate jokofu kwa ajili ya kuhifadhia maiti. Mimi naomba nimshauri kwamba, watengeneze chumba cha kuhifadhia maiti halafu ndiyo jokofu litakwenda. Kwa sababu, tukiwapelekea jokofu sasa hivi, hawatakuwa na mahali pakuweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwa kutukumbusha, pale ni kituo muhimu kwa ajili ya kuhudumia majeruhi na tutashirikiana na yeye pamoja na Halmashauri kuhakikisha kwamba tunapatengeneza paweze kutoa huduma stahiki kwa majeruhi wa ajali.

Na. 50

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilayani Kilolo**

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA** aliuliza:-

Serikali imeweka dhamira ya kujenga Vyuo vya Ufundi *(VETA)* katika kila Wilaya ili kuongeza ajira kwa vijana:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Wilayani Kilolo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzi ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Wilaya, Serikali imedhamiria kujenga vyuo vipya ama kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(Focal Development Colleges – FDC),* kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika ngazi ya Wilaya. Aidha, katika kutekeleza mpango huo, kipaumbele kinatolewa kwa kuanza na Wilaya ambazo hazina vyuo vya aina hiyo hata vya binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilolo ina vyuo sita vya mafunzo ya ufundi stadi; vitano vikiwa chini ya umiliki wa Mashirika ya Kidini na kimoja kikiwa chini ya Jumuiya ya Wazazi. Pia katika Wilaya hiyo, kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Ilula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba nichukue fursa hii, kumfahamisha Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla kuwa, mpango wa Serikali ni kutumia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ilula, badala ya kujenga kipya. Aidha, naomba kuwashauri Wazazi na Vijana wa Wilaya

ya Kilolo, kutumia Vyuo vya Ufundi Stadi vilivyopo Wilayani humo, wakati Serikali ikiendelea na juhudi zake za kutafuta fedha za kukiwezesha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ilula kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake na kwamba mpango uliopo ni kutumia Chuo cha Maendeleo kilichopo Ilula kufanya kiwe Chuo cha *VETA:-*

(a) Napenda kumjulisha kwamba, Chuo hicho kipo katikati ya Mji Mdogo wa Ilula na hakuna nafasi hata ya kupanua. Je, katika maagizo hayo kuna mpango gani wa Serikali na lini Chuo hicho cha Maendeleo kitaweza kuanza kutoa mafunzo hayo?

(b) Vyuo vya *VETA* vimekuwa vikitoa mafunzo kwa ajili ya utengenezaji wa magari, mambo ya umeme, ufundi uashi, upakaji rangi na mengineyo. Je, Serikali haioni sasa huu ni wakati mwafaka kupanua Mtaala wa *VETA* ili vijana wetu wengi wanaohitimu Kidato cha Nne na Darasa la Saba waweze kuchukua mafunzo ya ujasiriamali pamoja na usindikaji wa mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na nyanya, mbogamboga na matunda ambayo yanapatikana sehemu nyingi katika nchi hii ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Kilolo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Msolla, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nafasi ndogo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi pale Ilula; katika utekelezaji wa azma hii ya kuwezesha Chuo hicho kuweza kutoa mafunzo ya ufundi stadi, tutafanya tathmini ambayo itawezesha Chuo hiki kuwa na uwezo wa kutoa mafunzo hayo na ikiwa hakitaweza kutoa mafunzo kwa kukidhi mahitaji ya Wilaya, azma ya kuijengea Wilaya Chuo cha Ufundi Stadi ipo

palepale. Azma hii tumesema tutaifanya kwa nchi nzima kwa kila Wilaya, lakini tutakwenda awamu kwa awamu ili tuweze kufanikiwa kulitekeleza hili kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu hizi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tutaanza na wale ambao hawana kabisa Chuo cha Ufundi Stadi; kwa maana ya kwamba kiwe cha Serikali ama kisiwe cha Serikali. Kwa hiyo, hili tutaliangalia vizuri.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupanua Mtaala wa *VETA* ili uweze kuingiza masomo ya ujasiriamali na kadhalika, hivi sasa tupo katika mpango huo; tunafanya tathmini ya kila Wilaya kifundishwe kitu gani ili stadi zinazofundishwa katika ile Wilaya, ziendane na kazi ambazo zinaendana na Wilaya hiyo. Kwa hiyo, kabla ya kujenga Chuo tunafanya stadi maalum ambayo inatoa stadi ambazo zinahitajika katika Wilaya hiyo na aina ya ufundishaji sasa hivi tumeibadilisha ili ujasiriamali uwe katika mafunzo hayo namba moja, lakini namna ya kufundisha pia tunaiita *Competence Based Training,* ndiyo ambayo tutaitumia ili iwezeshe kutoa mafundi stadi bora kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Na. 51

**Mji wa Ng'hungumalwa Kupatiwa Umeme wa Gridi ya Taifa**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. MANSOOR S. HIRAN)** aliuliza:-

Ni muda mrefu sana Serikali imekuwa ikiahidi kuupatia Mji wa Ng'hungumalwa umeme wa Gridi ya Taifa:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mpango wa kupeleka umeme katika Mji wa Ng'hungumalwa na Vitongoji vya Sangu, Mwaluja na Tarafa za Mwamashimba, Nyamilama na Kata

zingine ambapo pana shughuli za kiuchumi kama vile *Cotton Ginneries* na mashine za kusaga/kukoboa nafaka?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mansoor Shanif Hirani, Mbunge wa Kwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali iliahidi hapa Bungeni kupeleka umeme kwenye maeneo aliyoyataja, ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB),* wangefadhili ujenzi wa njia ya umeme, wakati ujenzi wa kituo cha usambazaji umeme cha Mabuki, kingegharimiwa na *TANESCO.* Utaratibu huo uko palepale ambapo maeneo hayo yapo kwenye mpango wa kupatiwa umeme kupitia Mradi wa *Electricity V,* unaofdhiliwa na Benki hiyo ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB).* Umeme katika mji huu utatokea Kituo cha Kupozea Umeme cha Mabuki hadi Kijiji cha Mwalujo. Mshauri Mwelekezi wa Mradi ameshapatikana na ameshasaini Mkataba na *TANESCO* kwa kuanza kazi. Inatarajiwa mikataba kwa wakandarasi wawili watakaopatikana, yaani mkandarasi wa ujenzi wa njia ya umeme *(Distribution Network)* na Mkandarasi wa ujenzi wa vituo vya kupozea umeme *(Substations)* itasainiwa mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vitakavyonufaika na Mradi huo ni Runele, Ng'hungumalwa, Mwahaya, Mirwungu, Mwalujo Ginnery (Rintex), Kawekamo, Mwamashimba Mission, Shirima, Sangu Ginnery (African Ginning Ltd), Gurumwa, Malemve, Jojiro na Nyamilama. Gharama za Mradi ni Dola za Marekani milioni 29.6, ambazo zitatumika katika ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 33, yenye urefu wa Kilometa 95 katika Wilaya ya Kwimba. *Transformer* 17 zitafungwa kwenye Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, Mradi huu umechelewa kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)* na hivyo kuchelewesha Mradi huu na mingine inayofadhiliwa na Benki hiyo. Hata hivyo, hatua ya kuridhisha imefikiwa katika mazungumzo ya kukamilisha ufadhili wa Mradi huu baina ya Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Benki hiyo. Kutokana na hatua hiyo, inatarajiwa kwamba, kazi za ujenzi wa Mradi zinatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2012. Kwa kuwa Mradi huu umechelewa na unahusisha maeneo mengi yakiwemo ya Wilaya za Bukombe, Magu, Misungwi na Sengerema, utatolewa ufafanuzi katika taarifa ya utekelezaji wa Mradi huu itakayotolewa baada ya kukamilika kwa majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Wilaya ya Kwimba kuwa na subira wakati Serikali ikifuatilia utekelezaji wa Mradi huu kwa karibu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba niishukuru Serikali kwa maelezo mazuri, lakini naomba nimwulize maswali mawili Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kukubaliana na mimi kwamba Mradi huu umekuwa wa muda mrefu na ahadi nyingi ambazo hazitekelezeki?

(b) Wananchi wa Vijiji vya Talo, Ibindo, Maligisu, Kadashi na Centre Kabila, kupitia Mpango wa *REA;* ni lini umeme wao utaanza kupelekwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Richard Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mradi huu unaofadhiliwa na *African Development Bank,* hiki kipande cha kwanza cha Ng'hungumalwa, kwa maana ya Wilaya ya Kwimba na maeneo ya Bukombe, hii Miradi imeanza kujadiliwa tangu 2007/2008 lakini matatizo yaliyokuwepo hapo ni makubaliano baina ya *African Development Bank,* Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na *TANESCO.* Kusema kweli, kila wanapokwenda hatua moja wanarudi tena nyuma kujadili na kukubaliana; kwa hiyo, imechelewa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nadhani tumefikia hatua nzuri sana; maana sasa kwa miezi hii mitatu iliyobaki mpaka Agosti 2012, kinachojadiliwa sasa ni wale Wakandarasi wa *Distribution Network* na *Sub-Stations* zile. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hapa walipofikia wamefikia pazuri. Kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi kwamba, kadiri watakavyokuwa wanaenda na sisi tutakuwa tunatoa taarifa ya utekelezaji ya makubaliano yanayofikiwa ili wananchi wa Wilaya zote hizi za Bukombe, Kahama na Sengerema, wote wajue utekelezaji wa Mradi umefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la Talo kwenda Kabila Centre, huu ni Mradi unaotekelezwa na *REA* haupo kwenye *African Development Bank.* Una kama kilometa 35 na kusema kweli namshukuru Mheshimiwa Mbunge, ameufuatilia sana. Utekelezaji wake mwanzoni ulikuwa unafikiriwa uanze kutokea Lamadi, Magu kwenda mpaka Kabila Centre, lakini kwa hizi kilometa 60, hakuna wateja. Kutokea Talo, ambako ndiyo Jimboni kwa Mheshimiwa Mbunge, umeme unatokea Ngudu – Talo – Kabila Centre, pana hivi vijiji kama Ibindu, Kadashi, Nyashana, Maligusu na Kabila Centre yenyewe ambavyo ni vijiji vikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli kabisa Mradi utatekelezwa; *REA* wamekubali na tumekubaliana kwamba, 2012/2013 Mradi huu uanze kupewa kazi ya *Tender Documents*

na mambo mengine yaanze ili Mradi upate utekelezaji. Una wateja wengi na una watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwaombe radhi sana. Labda nirejee maagizo ya Mheshimiwa Spika; wakati mwingine maswali ya nyongeza na majibu ya maswali hayo yamekuwa marefu na hivyo mnaona tumetumia tena dakika za ziada kama sita hivi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni, inanipasa maswali haya mawili yaliyobakia tuyaache kwa siku ya leo, yatarejeshwa Ofisi ya Bunge na yatapangiwa muda mwingine. Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi sana, mtapewa taarifa ya maswali haya yataulizwa tena siku gani hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa taarifa hiyo, naomba nitoe matangazo machache niliyonayo hapa Mezani, kabla sijamwita Katibu atuendeleze katika hatua inayofuata. Ipo orodha ya wageni, ambayo nimeipokea hapa Mezani.

Wageni wa kwanza waliopo katika Ukumbi wa Spika ni Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge Mstaafu na Mwenyekiti wa Bodi ya *SSRA.* Tunakukaribisha sana Mheshimiwa Kaboyonga na tunafurahi uko hapa leo na ninaamini Muswada wa leo unahusu sana shughuli ambayo umekabidhiwa na Taifa. *(Makofi)*

Wapo wageni wanane wa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani, wakiongozwa na Ndugu Mwemba Burton Mwemba. Ningeomba hawa wageni wasimame; karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Ester Bulaya, wakiongozwa na Catherine Bulaya. Ningeomba wasimame; karibuni sana. Ninafikiri yule mdogo ni mwanawe kama sikosei.

Naye tunamkaribisha aone shughuli za mama yake hapa. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Ezekia Wenje, ambaye ni Bwana Fred Lukanga, Katibu wa CHADEMA wa Wilaya ya Nyamagana. Ningeomba asimame. *(Makofi)*

Wapo wageni 12 wa Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Mgosi Kabaka, ambao ni Wakurugenzi Wakuu wa Mifuko ya Jamii nchini, wakiongozwa na Ndungu Sauli Kinemela, Kamishna wa Kazi. Ningeomba Wakurugenzi wetu wa Mifuko wasimame mahali popote walipo ama wawakilishi wao. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 29 wa Mheshimiwa Mary Chatanda, ambao ni Walimu wa Shule ya Msingi Boma kutoka Halmashauri ya Mji wa Korogwe. Tungeomba hao walimu wasimame. Karibuni sana walimu na tena tunaona idadi kubwa hapo ni ya akina mama, kwa hiyo, tunawapongeza wanawake kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Wapo wageni wanane wa Mheshimiwa Ismail Aden Rage na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum. Ninaambiwa hao ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi wakiongozwa na Mstahiki Meya. Ningeomba wasimame kwa umoja wao. Karibuni sana wageni wetu kutoka Tabora. *(Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni hawa wafuatao; wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Dar es Salaam. Ninaomba wasimame; karibuni sana.

Wapo wanachama 16 kutoka *Fast Light Trust* ya Kilimanjaro wanaoshiriki tuzo za *Mount Kilimanjaro Environmental Award.* Ningeomba na wao wasimame; karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi kumi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Ningeomba wanafunzi kutoka Dodoma nao wasimame. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niwatangazie matangazo ya kazi. Kwanza, nimeagizwa na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, niwataarifu Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 13 kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika kwenye Ukumbi wa Basement kuanzia saa saba mchana. Kwa hiyo, Wajumbe wote wa Kamati hiyo mnaombwa kuhudhuria kikao hicho.

Mheshimiwa Mama Anna Margareth Abdallah, Mwenyekiti wa *TWPG*, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote Wanachama *TWPG* kuwa Jumapili tarehe 15 kutakuwa na semina kuanzia saa tano asubuhi. Semina hiyo itafanyika Ukumbi wa Pius Msekwa, tafadhali mnaombwa kuhudhuria semina hiyo. Semina hiyo ni kwa ajili ya Wabunge Wanawake tu, naomba niliwekee msisitizo zaidi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa James Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwa na wao leo tarehe 13 kutakuwa na kikao cha Kamati, kitakachofanyika Ukumbi Namba 219, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala, kuanzia saa tano asubuhi. Nimetoa kibali kwa Kamati tatu kwa sababu ya umuhimu wa mambo ambayo wameniletea Wenyeviti hapa Mezani. Kwa hiyo, ninaomba Wajumbe wa Kamati hiyo saa tano waende.

Nimeombwa pia na Mheshimiwa Dkt. Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa, leo tarehe 13 Aprili, 2012, saa saba mchana, kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 13, saa tano asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niseme kuwa nimetoa pia kibali kwa Kamati hiyo kukutana saa hizi kwa maelekezo niliyopewa na Mheshimiwa Mwenyekiti ya umuhimu wa jambo hilo.

Nimeombwa pia na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo na yeye anaomba Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo, wakutane leo Ijumaa, tarehe 13 kuanzia saa tano asubuhi, katika Ukumbi wa *Basement,* Jengo la Ukumbi Mpya. Wajumbe wanaomba kukutana muda huo bila kukosa kwa kuzingatia shughuli ambayo na mimi nimeiona, nimeidhinisha hapa wakutane muda huu.

Waheshimiwa Wabunge, nimeagizwa na kuombwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Shughuli za Bunge, niwatangazie Wabunge wote kuwa kesho kutakuwa na semina inayohusu anuani za makazi na *symbol* za posta na mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji kutoka anolojia kwenda digitali, saa nne, katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hiyo itakayotolewa na Wizara ya Maliwasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo, ameniomba hapa niwaelekeze Waheshimiwa Wabunge kuwa pamoja na semina hiyo, vilevile Viongozi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *UCAF*, watatoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa mpango wake wa kuweka mawasiliano katika maeneo yasiyovutia wawekezaji. Kwa hiyo, shughuli hiyo nayo

itakwenda sambamba na hiyo semina siku hiyo hiyo ya kesho. Waheshimiwa Wabunge, nadhani tangazo hili ni muhimu sana kwetu na hasa kwa wale Wabunge ambao wamekuwa wakifuatilia sana masuala ya mawasiliano na minara ya simu katika maeneo yao. Kwa hiyo, huyu Mkurugenzi atakuwa hapa kesho. Ninaomba sana tujitahidi kumwona ili tutatue kero za wananchi kwenye upande huo wa mawasiliano.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo Mezani, naomba sasa nimwite Katibu tuendelee na hatua inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 *(The Social Security Laws (Amendments) Act, 2012)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Katibu, sasa naomba nimwite mtoa hoja wa Muswada huu, aweze kutupa maelezo; Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi za Jamii *(The Social Security Laws (Amendments) Act, 2012*), pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Kamati yako ya Bunge kwa Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wako Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini na Wajumbe wa Kamati, kwa ushirikiano wao mkubwa sana katika maandalizi ya Muswada huu. Aidha,

shukrani za pekee ziende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Mwandishi Mkuu wa Sheria na Wasaidizi wake, kwa kazi kubwa ya kuandika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa madhumuni ya kuiwezesha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, kufanya kazi yake kikamilifu na kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Muswada umeandaliwa kwa kuwashirikisha Wadau wote wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, wakiwemo Wafanyakazi, Waajiri na Serikali, ikiwemo Mifuko yenyewe kupitia Vikao vya Wadau na pia Baraza la Ushauri wa Masuala ya Kazi Jamii na Uchumi, yaani *RESCO.* Kimsingi, wadau wote waliunga mkono mapendekezo yaliyomo katika Muswada huu.

Muswada ulishasomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza, yaani *First Reading,* mnapo tarehe 1 Februari, 2012 na sasa unawasilishwa Bungeni kwa mara ya pili na ya tatu ili uweze kujadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yaliyomo ndani ya Muswada huu, yatawezesha kupanuliwa kwa wigo wa wanachama kwenye Mfuko kwa kuruhusu wafanyakazi wanaoingia kwenye ajira kwa mara ya kwanza ama kujiajiri wenyewe ili waweze kujiunga na Mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii ambao umeanzishwa kwa sheria ya Bunge. Mapendekezo ya Muswada pia yanakusudia kuoanisha Sheria za Mifuko na Sheria za Mamlaka. Maeneo yanayoainishwa katika Muswada huu ni pamoja na kufanya tathmini ya mali na madeni ya Mifuko, yaani *actuarial valuation* na uwasilishaji wa taarifa ya tathmini hiyo kwenye mamlaka, uwasilishaji wa taarifa za fedha za kila mwaka za Mfuko kwa mamlaka na Mifuko kuwekeza kwa kufuata miongozo ya uwekezaji, yaani *investment guidelines* iliyowekwa na Benki Kuu kwa kushirikiana na mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu nane; sehemu ya kwanza inaweka masharti ya utangulizi ambayo inajumuisha Jina la Muswada na maudhui ya kutungwa kwa Sheria hii. Sehemu ya pili inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa *(LAPF)*, Sura ya 407. Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu namba tatu cha sheria hii kwa kufuta, kuongeza na kurekebisha baada ya tafsiri ya maneno na misamiati iliyotumika katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada pia unapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Mfuko huo wa *LAPF* kwa kufuta jina la sasa la Mfuko na kupendekeza jina jipya ambalo linaondoa dhana ya awali iliyoanzisha Mfuko huo uliolenga wanachama kutoka sekta moja ili kuongeza wigo wa wanachama kutoka Hifadhi ya Jamii hasa baada ya kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 hususan kifungu namba 30. Aidha, kifungu cha 22 kinapendekeza kufanya marekebisho ili kutoa haki kwa mfanyakazi ambaye anaachishwa kazi aweze kulipwa mafao ya pensheni au mafao ya mkupuo, yaani *gratuity*. Pamoja na pendekezo la kurekebisha kifungu cha 22, inapendekezwa kuongezwa kifungu kipya cha 24(a) ili kutambua mamlaka ya udhibiti wa Hifadhi ya Jamii hususan wajibu wa Mfuko kuwasilisha taarifa ya tathmini ya mali na madeni kwa mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada pia unapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 27(a) ili kumwezesha mwajiliwa ambaye baada ya kufikia umri wa kustaafu kwa lazima na bado anaendelea kutoa michango yake katika Mfuko kuwa na stahili ya kulipwa *bonus.* Muswada pia unapendekeza kupitia kifungu cha 49, uwekezaji wa Mfuko uzingatie mwongozo wa uwekezaji utakaotolewa na Benki Kuu kwa kushirikiana na mamlaka. Aidha, Muswada huu unapendekeza kufuta kifungu cha 65 na kuanzisha kifungu kipya ili kutoa uwezo kwa Mkurugenzi Mkuu, Mkaguzi Mkuu au Mfanyakazi

yeyote wa Mfuko ambaye amethibitishwa na Bodi kufungua mashtaka ya jinai dhidi ya mtu ambaye atavunja masharti ya kifungu cha 71 baada ya kupata kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka, yaani *DPP.* Sehemu hii pia inapendekeza kufanyiwa marekebisho Jedwali la Kwanza kuhusu Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ili kuzingatia utatu kutimiza vigezo vya Shirika la Kazi Duniani ambalo Tanzania ni Mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Taifa ya Mfuko wa Bima ya Afya, Sura ya 395 *(The National Health Insurance Fund Act, Cap. 395).* Inapendekeza marekebisho katika Sheria hii kwa lengo la kuainisha Sheria hii na Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135. Marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu hii ni pamoja na kuweka tafsiri mbalimbali ya maneno ambayo yatatumika katika Sheria. Pia marekebisho haya yanakusudia kuweka masharti ambayo yataiwezesha Bodi kuangalia upya viwango vya michango kwa kuzingatia kanuni, miongozo na maelekezo yanayotolewa na mamlaka. Aidha, marekebisho yanayokusudia kuweka masharti ili kuipa Bodi uwezo wa kutoa maelekezo kwa Mfuko kufanya tathmini ya mali na madeni ya Mfuko kila baada ya miaka mitatu au wakati wowote itakapopendekezwa na mamlaka. Sehemu hii pia inapendekeza kuweka masharti ambayo yataipa mamlaka uwezo wa kuelekeza Bodi kuwasilisha taarifa yake ya tathmini ya mali na madeni kwa mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50 *(The National Social Security Fund Act, Cap. 50).*

Ili kuboresha utendaji wa kazi, sehemu inapendekeza marekebisho katika Sheria kwa lengo ya kuoanisha Sheria yenyewe na Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135. Marekebisho

yanayopendekezwa katika sehemu hii ni pamoja na kufuta baadhi ya tafsiri ya maneno na kuweka tafsiri mpya. Vilevile tafsiri ya maneno mapya imeongezwa. Marekebisho mengine yanayopendekezwa yana lengo ya kuipa mamlaka uwezo wa kuamua kiwango cha pensheni atakayopewa mwanachama kwa mwezi kwa kuzingatia tathmini ya mali na madeni ya Mfuko, yaani *actuarial valuation*. Aidha, Muswada unapendekeza kukifanyia marekebisho kifungu cha 62 cha Sheria kwa kuweka masharti ambayo yataitaka Bodi ya Wadhamini kutekeleza Sera ya Utekelezaji kwa kufuata miongozo ya uwekezaji itakayotolewa na Benki Kuu kwa kushirikiana na mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya Muswada inahusu marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma, Sura ya 372, yaani *The Parastatal Organization Pension Scheme Act, Cap. 372.* Marekebisho haya yanahusu Jina la Sheria pamoja na dhamira ya kuepusha dhana ya kuwa Mfuko huu ni kwa ajili ya kuhudumia Sekta ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali tu, wakati Sheria yenyewe sasa inahusu pia waajiriwa wa makampuni binafsi na watu kutoka katika sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jina la Sheria limerekebishwa na badala yake litakuwa *PPF Pensions Fund 2012,* kwani kuendelea kutumia neno *Parastatal* kunakinzana na dhana ya kuruhusu Mfuko huu kufungua wigo kwa wanachama wa sekta rasmi na isiyo rasmi. Vilevile inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria hii ili kutambua wanachama ambao ni waajiriwa walioko katika majaribio na pia kutambua uanachama wa mwajiriwa ambaye amebadili ajira au amejiuzulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii pia inaweka majukumu ya mwajiri, ikiwa ni pamoja na kusajili wafanyakazi wapya kwenye Mfuko huu wa *PPF* kwa wale ambao si wanachama wa Mfuko wowote na kuwasilisha michango

kamili ya wafanyakazi, pale ambapo wafanyakazi hao wamesimamishwa kazi kwa nusu mshahara. Aidha, marekebisho hayo yameweka wazi umri wa kustaafu kwa hiari kwa mwanachama kuwa ni kuanzia miaka 55, isipokuwa uanachama wake utakoma pale ambapo mwanachama huyo atatimiza umri wa miaka 60. Inapendekezwa pia kwamba, mwanachama ambaye hajatimiza muda wa kuchangia, yaani *qualified period*, anapostaafu apewe michango yake na ya mwajiri pamoja na riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma, Sura ya 371, yaani *The Public Service Retirement Benefit Act, Cap. 371,* kwa kufanya marekebisho katika kifungu cha tatu kwa kupanua wigo wa Sheria ili waajiriwa wa sekta rasmi na isiyo rasmi waweze kuwa wanachama. Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho kwa kufuta baadhi ya tafsiri za maneno na kuyatafsiri upya ili kwenda sambamba na vifungu vya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135.

Sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 33 ili kuweka masharti ambayo yataitaka Bodi kusimamia na kuongoza Mfuko kwa kufuata masharti ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, miongozo na maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na mamlaka hiyo. Aidha, yapo mapendekezo ya kurekebisho kifungu cha 52 kuruhusu kuwa na Bodi inayozingatia uwakilishi wa utatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba inahusu marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135, yaani *The Social Security Regulatory Authority Act, Cap. 135.* Marekebisho haya yanapendekeza kurekebisha kifungu cha sita ili kuipa mamlaka uwezo kutoa maelekezo mbalimbali ya usimamizi kwa ajili ya Sekta nzima ya Hifadhi ya Jamii. Sehemu hii pia inapendekeza

kumtoa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka kwenye Bodi na kumfanya awe Katibu wa Bodi hiyo. Sehemu hii vilevile inapendekeza kuipa uwezo mamlaka kusimamia mambo ya kitaalam kwenye maeneo ya huduma za afya kwa kushauriana na Waziri anayehusika na masuala ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane inahusu marekebisho katika Sheria ya Bima, Sura ya 394. Marekebisho katika Sheria hiyo yanapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 13 cha Sheria kwa lengo la kuweka bayana idadi ya Wajumbe wa Bodi ambayo haitazidi saba na kwamba idadi ya Wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar haitapungua wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho hayo pia yanabainisha sifa za mtu anayefaa kuwa Mjumbe wa Bodi kuwa ni mtu mwenye elimu na uzoefu katika masuala ya Bima, Uchumi, Sheria, Fedha, Utawala na Uhasibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho haya ya Sheria za Hifadhi ya Jamii, wadau walileta maoni mbalimbali yaliyopelekea Jedwali la Marekebisho ya Muswada, yaani Schedule of Amendments ambayo yatasomwa pamoja Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kupanua wigo wa Hifadhi ya Jamii kwa waajiriwa katika sekta binafsi na wanaojiajiri katika sekta rasmi na isiyo rasmi kwa Mfuko wa *LAPF.*

Pili, kumtaka mwajiri kuwasilisha michango ya waajiriwa wake ambao ni raia wa kigeni kwenye Mfuko husika.

Tatu, kuongeza uwakilishi wa Wajumbe wa Bodi kati ya saba na tisa ili kuweka uwiano kati sawa wa vyama vya waajiri na vyama vya waajiriwa.

Nne, kuwianisha tafsiri ya neno mwajiriwa katika Mifuko yote ili iwe na tafsiri moja ambayo ipo katika Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Namba Sita ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi, Namba Saba ya Mwaka 2004.

Tano, kuruhusu mwajiriwa aliyeacha kazi na kutokuwa mwanachama kwa kipindi fulani kurudia uanachama wake baada ya kuajiriwa tena kwa Mfuko wa *PPF.*

Sita, kutoa adhabu kwa mwajiri anapochelewa kulipa mafao ya mwanachama.

Saba, kuhamasisha baadhi ya majukumu ya Mamlaka, kuhamisha baadhi ya majukumu ambayo ni ya kisera kwenda kwenye Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kuwashukuru wadau wote ikiwa ni pamoja na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Chama cha Waajiri na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa maoni na ushauri wao uliochangia katika kuboresha Muswada huu. Aidha, napenda kuwashukuru wataalam wetu wa Sheria na Watendaji wa Wizara na Taasisi nyingine zilizohusika katika hatua mbalimbali za maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kukushuru tena wewe binafsi na Kamati yako, kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa mliotupatia sisi Wizara katika kukamilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nakushukuru. Baada ya kuwasilisha hoja yako, nimeona imeungwa mkono kwa mujibu wa kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Muswada na kwa taarifa tu ya Bunge hili; Mwenyekiti aliyechambua Muswada huo ni mimi niko hapa mbele leo, lakini sasa nitampa mamlaka hayo Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, atasoma taarifa ya Kamati yetu kwa niaba yangu.

Mheshimiwa Saidi Mtanda.

**MHE. SAIDI M. MTANDA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge hili ili kuweza kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii. Pia nitumie fursa hii kutoa salamu za rambirambi kwa Wananchi wa Kata ya Nangaru katika Jimbo la Mchinga, kufuatia mvua kubwa zilizonyesha na kuathiri na hatimaye kuchukua maisha ya kijana Abdallah Mtambule katika eneo hilo.

Nitumie fursa hii pia kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Katibu Mkuu wa CCM, kufuatia kifo cha msaidizi wake wa karibu na familia hiyo.

Baada ya maelezo yangu hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa 2012 *(The Social Security Laws (Amendments) Act of 2011).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 86(5), naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, 2012 (*The Social Security Laws (Amendments) Act, 2012.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata nafasi ya kujadili Muswada huu katika vikao vilivyofanyika katika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam. Katika kikao cha kwanza kilichofanyika tarehe 27 Machi 2012, Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Dkt. Milton M. Mahanga, Mb, alitoa maelezo ya jumla yanayohusu madhumuni ya Muswada. Kikao hiki pia kiliwashirikisha wadau mbalimbali miongoni mwao wakiwemo Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi *(TUCTA),* Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE),* Chuo Kikuu Mzumbe, *Tanzania Higher Learning Institution Trade Union (THTU),* Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa *(LAPF),* Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF),* Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma *(PPF),* Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa Serikali *(GEPF),* Mfuko wa Hifadhi za Jamii *(NSSF)* na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, Kamati inawashukuru wadau wote walioshiriki na kutoa maoni ambayo yamezingatiwa na Kamati katika kuishauri Serikali ili iyazingatie katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikao vingine vilifanyika terehe 3 Aprili 2012, tarehe 4 Aprili 2012, tarehe 11 Aprili 2012 na tarehe 12 Aprili 2012 ambapo Waziri wa Kazi na Ajira na Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, walifafanua na kutoa majibu ya baadhi ya hoja zilizokuwa zimejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria za Hifadhi za Jamii kwa

madhumuni ya kuiwezesha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi za Jamii kufanya kazi yake ya kusimamia na kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu nane ambazo Kamati imezifanyia kazi na kutoa mapendekezo ya kuziboresha na hatimaye kuwa na Sheria inayofaa kwa mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sememu ya kwanza inaelezea Jina la Muswada na maudhui yanayofanya kupendekeza kutungwa kwa Sheria hii. Kamati haikuwa na tatizo lolote katika sehemu hii na imekubali mapendekezo ya Sheria hii kuanza kutumika tarehe 1 Juni 2012, kama yalivyoletwa mbele ya Kamati katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, Sura ya 407 *(The Local Authorities Pensions Fund, Act, Cap.407).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia sehemu hii kwa makini, Kamati inashauri marekebisho yafuatayo yafanyike ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii:-

(i) Kifungu cha 2 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ambacho hakikuletwa kwenye marekebisho haya, kirekebishwe ili kuruhusu Mfuko kusajili wanachama kutoka katika sekta rasmi na isiyo rasmi kama ilivyofanyika katika Muswada huu, kifungu cha 79 cha Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma na kifungu cha 120 cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma.

(ii) Kifungu cha nne cha Muswada kinachofanya marekebisho kwenye kifungu cha 3 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, tafsiri ya neno *"employee"* haijitoshelezi; hivyo, iongezwe tafsiri iliyopo katika kifungu cha

61 cha Sheria ya Taasisi za Kazi *(Labour Institutions Act, 2004)* ili kupanua tafsiri ya nani ni mfanyakazi na hivyo kupanua wigo wa wafanyakazi wengi zaidi kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, marekebisho haya yafanyike sehemu zote ambapo neno *"employee"* limetafsiriwa katika Muswada huu. Aidha, Kamati inashauri tafsiri ya neno *actuarial valuation* iwe moja katika Mifuko yote kuliko ilivyo sasa ambapo kila Mfuko una tafsiri yake.

(iii) Kifungu cha saba cha Muswada kinakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha nane cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa kuongeza kifungu kipya cha tatu ambacho kinaelezea muda wa Mkurugenzi Mtendaji kushika ofisi kwamba ni kipindi cha miaka mitano na anaweza kuongezewa miaka mingine mitano kama itaonekana inafaa. Kamati inashauri neno *"shall"* lililopo kwenye mstari wa pili lifutwe na badala yake liandikwe neno *"may"* ili uteuzi wake kwa mara ya pili utegemee utendaji wake wa kazi kwa kuzingatia Sheria zilizopo sasa na mkataba wa ajira. Marekebisho haya yafanyike pia kwenye vifungu vya Muswada vya 32, 42, 85, 129 na 144 ambavyo vinahusu uteuzi wa Wakurugenzi wa Mifuko yote ya Hifadhi za Jamii.

(iv) Kifungu cha 13 cha Muswada kinachofanya marekebisho katika kifungu cha 27 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa kuongeza kifungu kipya cha 27A kinachoongelea kuhusu kutoa *bonus* kwa mtumishi ambaye amefikisha umri wa miaka sitini na anaendelea kuchangia kwenye Mfuko. Kamati imeona kifungu hiki ni kizuri na ni vyema ikaangaliwa namna ya kuingizwa katika Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, kifungu cha 28 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ambacho katika Muswada huu hakijafanyiwa marekebisho kifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno *"commuted pension"* yaliyopo kwenye kifungu cha kwanza na kuongeza maneno *"subject to subsection (1)"* mwanzoni mwa kifungu cha pili na kuacha neno *"gratuity"* ambayo ndiyo anayotakiwa kupewa

mwanachama anayekufa akiwa kazini lakini amechangia kwa kipindi cha chini ya miezi 180.

(v) Kifungu cha 18 cha Muswada ambacho kinafanya marekebisho katika kifungu cha 38 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, kuwezesha Mfuko kurudisha fedha ambazo mwanachama atakuwa amezidishiwa *(overpaid)*. Kamati inashauri kifungu hiki pia kizungumzie suala la mwanachama kupunjwa *(underpaid)* iwapo litajitokeza. Aidha, kutokana na mwanachama kupunjwa, Kamati inapendekeza Mfuko kulipa mafao yote ya mwanachama pamoja na *penult* ya asilimia mbili ya mafao yote ya mwanachama.

(vi) Kifungu cha 19 cha Muswada kimefanya marekebisho machache ya kifungu cha 39 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, Kamati inakubaliana na Kifungu hiki kwa kuwa kinamruhusu mwanachama aliyeacha kuchangia kwa kipindi fulani kurejea. Vilevile, kitamsaidia mwanachama kupata mafao yake kana kwamba hakuwa ameacha kuchangia.

(vii) Kifungu cha 21 cha Muswada kinachofanya marekebisho kwenye kifungu cha 49 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, ambacho kinaongelea kuhusu Mfuko kuwekeza fedha za wanachama, Kamati inashauri kwamba ni vyema sasa Mfuko kuanza kuwafaidisha wanachama kutokana na uwekezaji huo kuliko hivi sasa Mfuko kuwekeza katika biashara mbalimbali hasa za ujenzi lakini faida kwa mwanachama haionekani.

(viii) Kifungu cha 28 cha Muswada kinachofanya marekebisho kwenye Jedwali la Kwanza, ambacho kinaongelea kuhusu muundo wa Bodi, Kamati hairidhishwi na Bodi kuwa na uwakilishi wa Wajumbe saba tu. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali kuwa idadi hiyo imetokana na suala zima la kutaka kupunguza gharama za uendeshaji; Kamati inashauri

badala ya kupunguza idadi ni vyema suala la malipo ya Wajumbe liangaliwe upya. Aidha, Kamati inashauri idadi ya Wajumbe iwe ni kuanzia Wajumbe saba hadi tisa kulingana na ukubwa wa Mifuko ili kuwa na uwakilishi mzuri wa waajiri, wafanyakazi na wataalam. Aidha, marekebisho haya yafanyike kwenye Muundo wa Bodi zote za Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

Vilevile katika kifungu kidogo cha (e), yaongezwe maneno *"members representing the most representative employers association"* ili uwakilishi utoke kwa chama chenye wanachama wengi kwa mujibu wa Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Marekebisho haya pia yafanyike katika Kifungu cha 76(1)(b), Kifungu cha 118(1)(c) na 136(1)(f).

(ix) Kifungu cha 31 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, kinachozungumzia kuhusu maslahi ya mwanachama kujitoa kwenye Mfuko kwa sababu ya ndoa au uzazi, hakijafanyiwa marekebisho. Kamati inapendekeza kifanyiwe marekebisho ili kutoruhusu wanachama wanawake kujitoa kwenye uanachama kwa sababu ya ndoa au uzazi ili kwenda sambamba na dhana nzima ya hifadhi ya jamii.

(x) Kifungu cha 37 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa hakijafanyiwa marekebisho. Kamati inapendekeza kufanya marekebisho ili kuwezesha wastaafu kuwa na uhuru wa kuchagua kulipwa kwa mkupuo *(lump sum)* iwapo haitazidi asilimia 50 ya akiba na riba yake na asilimia 50 inayosalia alipwe kwenye malipo ya kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395 *(The National Health Insurance Fund, Cap. 395).* Katika kuchambua na kupitia sehemu hii, Kamati inashauri Kifungu cha 38 cha Muswada kinachokusudia kufanya marekebisho ya kifungu cha 43 cha Sheria ya Mfuko wa Taifa Bima ya Afya kwa kuongeza kifungu kipya cha (3), maneno

yafuatayo yana makosa ya kiuchapaji; neno "*instate*" lifutwe badala yake liandikwe "*instituted*" na neno "*concert*" lifutwe badala yake liandikwe "*consent*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mabadiliko ya Sheria hii, Kamati haikuona kama kunahitajika marekebisho makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50 *(The National Security Fund, Cap. 50*). Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Kifungu cha 48 cha Muswada kinaandika upya kifungu cha 18 cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii. Kwanza, Kamati inapendekeza kifungu cha 18(1) kisitaje *(Order Number XXXV),* kwa vile *(Order Number XXXV)* inaweza kubadilika wakati wowote na hivyo kulazimu kurudi tena Bungeni kufanya marekebisho. Aidha, marekebisho haya yafanyike popote ilipotajwa *(Order Number XXXV).*

Pili, kifungu cha 18(2) ambacho kinalazimisha Mfuko kupata idhini ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (*DPP*) kabla ya kufungua mashtaka ya jinai, Kamati inashauri ili kuharakisha usikilizaji wa kesi za aina hii. *DPP* apewe mamlaka ya kuteua mtu atakayesimamia mashtaka haya kwa niaba yake.

(iii) Kifungu cha 68 cha Muswada kinachoandika upya kifungu cha 74 cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Kamati inapendekeza kifungu kidogo cha (1) na (2) neno "*may*" lisomeke "*shall*" ili kuweka uzito katika jambo hili.

(iv) Kifungu cha 72 cha Muswada kinachorekebisha kifungu cha 82(3) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, kinapendekeza maneno "*a*" au "*any*" yaongezwe baada ya neno "*where*" ili kuondoa utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma, Sura ya 372 (*The Parastatal Organisations Pensions Scheme, Cap. 372).* Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Kifungu cha 80 cha Muswada ambacho kinatoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Sheria hii, Kamati inashauri maneno **"***actuarial valuation"* na *"actuary"* yaliyopo mwishoni mwa ukurasa wa 44 wa Muswada yafutwe kwa kuwa yameshatolewa tafsriri katika kifungu cha 80(a). Vilevile neno *"member"* lililopo katika ukurasa wa 45 lifutwe kwa kuwa limetolewa tafsiri katika ukurasa wa 46.

(ii) Kifungu cha 86 cha Muswada ambacho kinakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 8 cha Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma, pamoja na marekebisho yaliyopendekezwa katika Muswada, Kamati inapendekeza kuongezwe marekebisho mengine ya kumlazimisha mwajiri yeyote atakayekuwa amemwajiri raia wa kigeni kupeleka michango yake kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Marekebisho haya yafanyike pia kwenye Mifuko yote ya Hifadhi Jamii.

(iii) Kifungu cha 5 cha Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma ambacho kwenye Muswada huu hakijafanyiwa marekebisho, Kamati inashauri kifungu hiki pia kifanyiwe marekebisho ili kuruhusu wanachama ambao watakoma kuwa wanachama kwa sababu yoyote ile wakiwa hawajatimiza umri wa kustaafu, endapo wataajiriwa tena waruhusiwe kuwa wanachama.

(iv) Kifungu cha 21(4) cha Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma ambacho kwenye Muswada huu hakijafanyiwa marekebisho, Kamati inapendekeza kifanyiwe marekebisho kwa kukifuta kwa kuwa marekebisho yaliyofanyika mwaka 2001 kwa Sheria Na. 25, yaliondoa neno *"National Insurance Corporation"* na kuweka neno *"Fund"* kwa kuwa kwa sasa

hakutaweza kuwa na mgogoro kwani Bodi na Mfuko ni kitu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma, Sura ya 317 *(The Public Service Retirement Benefit Act, Cap. 371).* Kamati inashauri, Kifungu cha 123 cha Muswada kinachofanya marekebisho kwenye kifungu cha 6 cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma kwa kukiandika upya kuwa kifungu hiki kirekebishwe kwa kuwa kimekwenda kinyume na kifungu cha 25 cha Sheria Na. 8 ya Mwaka 2008, ambacho kimeipa Mamlaka jukumu la kuweka viwango vya kuchangia na siyo Bodi kama ilivyoandikwa kwenye Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135 *(The Social Security (Regulatory Authority) Cap. 135).* Kamati inashauri yafuatayo yafanyiwe marekebisho:-

(i) Kifungu cha 142(b) cha Muswasda kinachokusudia kufanya marekebisho katika kifungu 7 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kufuta kifungu kidogo cha (f) ambacho kinamwondoa Mtaalamu wa Masuala ya Hifadhi ya Jamii kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Kamati inashauri kifungu hiki kisiondolewe kwani Mjumbe huyu ni Mwakilishi muhimu sana katika Bodi hii ili kusaidia masuala ya kitaalam yatakayokuwa yanaamuliwa na Bodi.

Vilevile, kifungu cha 142(c) cha Muswada kinachokusudia kuongeza kifungu kipya cha 3 kwa kumfanya Mkurugenzi Mkuu kuwa Katibu wa Bodi. Kamati imekubaliana na maelezo ya Wizara kwamba, huo ndiyo utaratibu kwa mashirika yote lakini ili kutenganisha jukumu la usimamizi na utendaji, Kamati inashauri kifungu hiki kitamke wazi kabisa kuwa Mkurugenzi

huyu hatakuwa na haki ya kupiga kura kama ilivyowekwa kwenye kifungu cha 118(b) cha Muswada huu ambacho kinafanya marekebisho katika kifungu cha 6 cha Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma.

(ii) Kifungu cha 147 cha Muswada kinachofanya marekebisho katika kifungu cha 38 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa kuongeza Kifungu cha 38A. (2) (a). Kamati inashauri Mwenyekiti wa Kamati hii awe ni Afisa wa Serikali aliyestaafu au mtu yeyote ambaye hafungamani na upande wowote.

Vilevile katika Kifungu cha 38A (2) (d), neno *"Commissioner for Labour"* lifutwe kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria za Kazi hakuna cheo hicho badala yake liandikwe *"Labour Commissioner."* Aidha, Kifungu cha 38A. (2) (e), Kamati inashauri kuwa idadi ya Wawakilishi kutoka Uwakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi iongezwe kutoka mtu mmoja na kuwa watu wawili.

Vilevile Kamati inashauri kiongezwe kifungu (f) ili kuweka uwakilishi wa waajiri kwani dhana ya msingi ya utekelezaji wa Sheria hii inazingatia zaidi masuala ya utatu.

(iii) Kifungu cha 148 cha Muswada kinachokusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 47(2) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kukifuta na kukiandika upya. Kamati inashauri ni vyema kifungu cha zamani kikabaki kama kilivyo kwa vile kinaendana na kifungu cha 48 ambacho kinaipa Benki mamlaka ya udhibiti na siyo ushauri kama inavyofanywa na mabadiliko haya.

(iv) Kifungu cha 150 ambacho kinafanya marekebisho katika kifungu cha 49 cha Sheria Na. 8 ya Mwaka 2008 kwa kuongeza kifungu kipya cha 49A. ili mamlaka iweze kutoza tozo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na pia kuwekeza kwenye hisa *(share)* na dhamana *(securities).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 49A.(1)na (2), kwanza, Muswada haukueleza tozo kusudiwa litatoka wapi. Baada ya maelezo ya Serikali kuwa tozo inayopendekezwa litatokana na punguzo la fungu la fedha za matumizi ya kiutawala *(administrative costs)* kwenye Mifuko husika na bila kuathiri michango ya wananchama. Kamati inakubaliana na marekebisho haya ya Serikali kuhusiana na dhana nzima ya tozo ili kuiwezesha mamlaka kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Pili, Muswada unapendekeza Waziri akishirikiana na Waziri wa Fedha na Benki ya Tanzania kuamua kiwango cha tozo kwa kutangaza kwenye Gazeti la Serikali bila kuwashirikisha wadau. Kamati inashauri kifungu hiki kifanyiwe marekebisho ili kumlazimisha Waziri kisheria kushirikisha wadau katika jambo hili.

Tatu, kifungu cha 49A.(5) kinachohusiana na suala la Mamlaka kupewa uwezo wa kuwekeza kwenye hisa na dhamana. Kamati inapendekeza kuwa kifungu hiki kifutwe kwa vile kinakwenda kinyume na lengo kuu la kuanzishwa kwa mamlaka na majukumu yake kama yalivyoorodheshwa kwenye kifungu cha 5 cha Sheria Na. 8 ya Mwaka 2008 ambapo jukumu hili halipo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Pia kuiruhusu Mamlaka kuingia kwenye uwekezaji, itakuwa inaingilia shughuli zinazofanywa na Mifuko ambayo Mamlaka ndiye mdhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Bima, Sura ya 394 *(The Insurance Act, Cap. 394).* Kamati imepitia sehemu hii na haikuwa na tatizo; hivyo, inakubaliana na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla; pamoja na kutoa mapendekezo ya jumla ya Muswada, Kamati ina maoni mengine ya ziada kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria za

Hifadhi ya Jamii kwa manufaa ya wanachama wake kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa mchakato wa kuiweka Mifuko ya Hifadhi za Jamii chini ya Wizara moja ni wa muda mrefu na inasisitizwa pia na Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii, Kamati haikuona sababu kwa nini marekebisho ya Muswada huu hayakuja na pendekezo la kisheria la kuiwajibisha Mifuko kuwa chini ya Wizara moja. Kamati inashauri ili kuwa na uendeshaji bora wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii ni wakati mwafaka sasa Mifuko hii ikawajibika chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, tofauti na sasa ambapo Mifuko ipo katika Wizara mbalimbali. Aidha, kwa kuwa Kamati inapendekeza Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kuwajibika chini ya Wizara yenye dhamana ya Hifadhi ya Jamii ambayo kwa sasa ni Wizara ya Kazi na Ajira; ni vyema ikaanzishwa Idara Maalum ndani ya Wizara itakayoshughulika na Hifadhi ya Jamii ili kuweza kusimamia utekelezaji wa shughuli hizi katika ngazi ya Wizara kwa vile kwa sasa Idara hiyo haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile inapendekezwa kifungu cha 5(1)(e), (f) na (i) cha Sheria Na. 8 ya Mwaka 2008 kinachoelezea majukumu ya Mamlaka kifanyiwe marekebisho ili majukumu haya yafanywe na Wizara ya Kazi na Ajira chini ya Idara inayopendekezwa ya Hifadhi ya Jamii kwa sababu ni ya kisera zaidi na siyo ya kiutendaji. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, jukumu kuu la mamlaka ni kudhibiti Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, masuala ya Kisera ya jinsi ya kuiboresha Sekta hii ni ya Wizara.

(ii) Kwa kuwa *formula* ya ukokotoaji wa mafao ya mwezi ni tatizo kwani kila Mfuko una utaratibu wake hivyo kusababisha viwango vya pensheni kutofautiana kwa kiwango kikubwa. Kamati inashauri Mamlaka *(SSRA),* iliangalie suala la *formula* kwa kina na kwa kuzingatia yafuatayo: Kiasi cha juu cha miaka ambayo mtumishi ametumikia; muda wa kuishi baada ya kustaafu *(commuting factor);* mshahara wa mwisho aliostaafu nao; pensheni irekebishwe kutokana na mporomoko

wa thamani ya fedha na mfumuko wa bei; uzingatie kipindi mtumishi alichokuwa kazini katika sehemu mbalimbali; na kiwango cha pensheni kisipungue asilimia 70 ya pato la mtu kutokana na ngazi yake.

(iii) Kwa kuwa Kifungu cha 30 cha Sheria Na. 8 ya Mwaka 2008 kinatoa uhuru wa watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza au ambao hawajaandikishwa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kujiunga na Mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii. Kamati inashauri waajiri wote nchini kuwapa nafasi watumishi wao kuchagua Mifuko wanayotaka kujiunga nayo kuliko ilivyo sasa ambapo mbali na kuwepo kwa kifungu hiki bado watumishi wengi hawana uelewa na hawaeleweshwi kama kuna uhuru huo. Aidha, kwa vile sasa Mifuko imeruhusiwa kupata wanachama kutoka sekta isiyo rasmi, basi ni vyema Mifuko ikajiandaa vyema kwa kuwawekea mazingira mazuri ambayo yatawanufaisha.

(iv) Vilevile, suala la mwanachama kuruhusiwa kuhamia Mfuko mwingine liruhusiwe na lisiathiri mafao yake, jumla ya vipindi alivyochangia ndiyo vitumike.

(v) Pamoja na kwamba Mifuko imeruhusiwa kuwekeza lakini mpaka sasa Kamati haijaona faida inayokwenda kwa wanachama kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Mifuko hii. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa ni wakati mwafaka sasa Mifuko kujielekeza zaidi katika kuboresha maslahi ya wanachama wake kutokana na uwekezaji huo.

(vi) Iwapo Muswada huu utapita na kuwa Sheria, Kamati inapendekeza kuwa ni vyema marekebisho yote haya yakachapishwa na kuingizwa kwenye Sheria husika na kutolewa upya ili kuondoa usumbufu wa kusoma sheria mama na mabadiliko haya. Hii itasaidia uelewa wa wanachama na wadau mbalimbali wa mambo haya.

(vii) Kwa vile ripoti za tathmini ya afya ya kifedha ya Mifuko *(actuarial reports),* hupelekwa kwenye Bodi za Mifuko husika, Kamati inashauri Wajumbe wa Bodi waone wajibu wa kuwajulisha wanachama wao juu ya ripoti hizo ili wajue hali halisi ya Mifuko yao.

(viii) Mafao ya kifo yanayotolewa kwa sasa kwa wategemezi, Kamati inashauri yaendelee mpaka mjane afariki na mpaka wategemezi watakapofikisha umri wa kujitegemea.

(ix) Kwa kuwa Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* Na.102, umeorodhesha mafao tisa ambayo mwanachama anapaswa kupewa, Kamati inashauri kuwa ni vyema Mifuko kujielekeza kwenye kutekeleza Mkataba huo na vigezo vya ushindani viwe ni mafao ya ziada. Aidha, fao la tiba ambalo lipo kwenye Mkataba huo wa kazi, inashauriwa litolewe kwa wastaafu wote ambao walikuwa Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

(x) Utaratibu wa sasa ambapo watumishi waliopo kwenye Mkataba mara wamalizapo muda wao kulipwa pensheni na wakati huo huo kuongezewa Mkataba mwingine. Kamati inaona utaratibu huu unaliingizia Taifa hasara na inapendekeza mtumishi akiongezewa Mkataba asilipwe kiinua mgongo mpaka pale atakapomaliza muda wa Mkataba alioongezewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishukuru Serikali kwani mapendekezo mengi ya Kamati yamezingatiwa katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati inaamini kuwa, Muswada huu umebeba maoni mengi ya wadau na bila shaka utakapokuwa Sheria kamili, Kamati inaishauri Serikali, Kanuni zitakazotungwa zizingatie maoni ya Wadau na endapo kuna maeneo yanayohitaji marekebisho, Serikali isisite kuleta mabadiliko mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Pia namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge. Aidha, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga na Wataalam wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Eric Francis Shitindi, kwa ushirikiano walioipatia Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa michango na mapendekezo yaliyoboresha Muswada huu. Ninapenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kwa majina:-

Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa John Damian Komba, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi na Mheshimiwa Hamad Ali Hamadi, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Ramadhani Haji Salehe, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Abdallah Haji Ally, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Katibu wa Bunge - Daktari Thomas Kashililah na Ofisi yake, kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Vilevile Makatibu wa Kamati; Ndugu Hosiana John na Ndugu Asia Minja, kwa kuratibu kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada na naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mtanda, kwa kuwasilisha Taarifa hiyo ya Kamati vizuri kabisa kwa niaba ya Mwenyekiti wako, Mheshimiwa Jenista Mhagama; hongera sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa David Ernest Silinde, kuja kutoa Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu, naomba niombe Meza ya Makatibu na wale wanaotusaidia kutuhudumia humu ndani, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri haijasambazwa kwa Wabunge. Wamekuwa wakiniuliza, kwa hiyo, wanahitaji kuipata, naomba mnisaidie waipate. Jedwali la Marekebisho la Wizara kama bado halijasambazwa katika Ukumbi huu naomba sasa ifanyike hivyo. Ile *schedule of ammendment* ya Wizara kwa sababu ni wakati mwafaka sasa Wabunge kuanza kuoanisha yale yanayosemwa na Kamati na Wizara na upande wa Kambi ya Upinzani na marekebisho ambayo yamefanyika ili wajiweke sawa katika kuchangia na hatimaye kuupitisha huu Muswada.

Kwa hiyo, ningeomba hayo mambo niliyoyasema yafanyiwe kazi wakati tukiendelea na hizi taarifa. Baada ya tangazo hilo, sasa naomba kwa heshima zote nimwite Mheshimiwa David Ernest Silinde, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ili aweze kutoa maoni.  Mheshimiwa Silinde tafadhali karibu.

**MHE. DAVID E. SILINDE – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni ya Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 kwa niaba ya

Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii adhimu kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, aliyeshinda katika Uchaguzi Mdogo wa Arumeru Mashariki na Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge Viti Maalumu, anayeziba pengo lililoachwa na Marehemu Mheshimiwa Regia Mtema. Pamoja na kuwapongeza wananchi wote katika maeneo husika kwa kusimama kidete kuhakikisha kuwa wale wagombea waliowahitaji ndiyo waliotangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika pongezi napenda kuwapongeza watani wetu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), kwa kukubali matokeo; hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamepata majeraha mbalimbali kwenye miili yao na wengine wamepewa kesi katika mchakato mzima wa Chaguzi Ndogo za Ubunge na Udiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi huo, kabla ya kupitia baadhi ya vifungu ambavyo tunaona vinatakiwa kufanyiwa marejeo, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kama Muswada huu pamoja na kanuni zake za utekelezaji zitatumika ni dhahiri kuwa wanachama katika Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii watapata kile walichokuwa wanastahili, sambamba na mamlaka kudhibiti Mifuko inayofanya uwekezaji usiokuwa na tija kwa wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni utaratibu uliobuniwa na kuwekwa ili kuhakikisha kuwa wanajamii wanakuwa na uwezo wa kumudu gharama

za maisha kwa kuwawezesha kupata mahitaji yao ya msingi na hivyo kuishi katika kiwango cha maisha kinachokubalika kwa vigezo vya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la kuwepo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kumlinda mwananchi na tishio la kupungua kwa uwezo wake kiuchumi, kumhakikishia mwanachama kiasi fulani cha kipato baada ya kupoteza uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wanaishi vijijini na wengi wao wanapata riziki zao kutegemea kilimo na ni ukweli uliowazi kuwa Watanzania hao waishio vijijini na kujihusisha na kilimo ndiyo wanaolisha Watanzania wote kwa ujumla wetu. Madhumuni ya Sera ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii yameweka wazi kwamba malengo ya 2025 ni kuhakikisha huduma za hifadhi za jamii zinawafikia Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 15 cha Muswada kinachoongeza kifungu cha 29A kwenye sheria mama kinachohusu mgawanyo wa *pension* ya mwanachama aliyefariki kwa watoto na mke au mume. Kambi ya Upinzani inasema kuwa Tanzania ina Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352.

Lengo kuu la Sheria hii ni kutoa utaratibu wa kusimamia mali za marehemu baada ya kifo chake ikiwemo kuhamisha umiliki wa mali hizo kutoka kwa marehemu kwenda kwa watu wenye haki ya kuzipata mali hizo. Nia hasa ni kwamba mali alizoacha marehemu zisibaki zikiharibika na kupotea bure au warithi halali au watu wenye maslahi na mali za marehemu; kwa mfano, wale wanaomdai hawapotezi haki hiyo, bali awepo mtu ambaye atazisimamia na kuzigawa kwa wahusika wakiwemo wadai na kuepusha mgongano katika jamii husika. Hivyo, sheria inamuweka msimamizi wa kugawa mirathi husika na mamlaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka mgawanyo wa asilimia kwa fedha za *pension* za marehemu ni kutokuzingatia matakwa ya Sheria ya Mirathi, Sura ya 352. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kukifuta kifungu hiki kwani kinaweza kupelekea kuvunjwa kwa maelewano miongoni mwa jamii zetu ambazo zinafuata na kuzingatia Sheria ya Mirathi, Sura ya 352.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wazee takriban 2.1 milioni katika nchi yetu. Asilimia 82 ya wazee wote nchini wanaishi vijijini. Mpaka sasa ni asilimia nne ya wazee wote nchini wanaopata pensheni. Wazee hawa ni wale ambao walikuwa wameajiriwa katika ajira rasmi. Mbili ya tatu ya wapatao pensheni kwa sasa ni wanaume. Asilimia 96 ya wazee wote kwa sasa, wengi wao wakiwa ni wakulima na wafugaji, hawana pensheni ingawa nao wamechangia kwa kiasi kukubwa kulijenga Taifa letu. Takriban asilimia 30 ya walemavu wote ni wazee. Takwimu zinaonesha kuwa kaya zilizo na wazee, ambazo ni karibia robo ya kaya zote nchini ni maskini sana. Kiwango chao cha umaskini katika kaya hizi kipo juu kwa asilimia 22.4, ukilinganisha na wastani wa umaskini wa Taifa (asilimia 40.9%) ukilinganishwa na asilimia 33.4 ambayo ni wastani wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dhana ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni pana sana, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kuzingatia pendekezo letu la kuweka mfumo utakaowafanya wazee wote kupata pesheni (*universal pension*) kila mwezi kwa kiasi cha shilingi ishirini elfu kwa kuanzia ili kuwapunguzia wazee wetu ambao wengi wao wanaishi vijijini gharama kubwa za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba, japokuwa kwenye Muswada umeanza kuonesha nia kwanza kwa kuweza kuwalipa kiinua mgongo kwa watumishi ambao walikuwa kwenye sekta iliyo rasmi na wale ambao hawakuwa kwenye sekta iliyo rasmi. Hii ni kwa

mujibu wa kifungu cha 120 cha Muswada huu kinachofuta kifungu cha 2 cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma, Sura ya 371 *(The Public Service Retirement Benefit Act, Cap. 371*). Huu ni mwanzo mzuri, lakini bado tunasisitiza pendekezo tulilotoa hapo juu na kwenye hotuba zetu za bajeti kuwa Serikali ilifanyie kazi, kwani huu ni muda mwafaka wa kuwasaidia wazee wetu waliojitolea kuhakikisha sisi tunafika hapa tulipo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia mamlaka kuanzisha mchakato utakaopelekea kutungwa kwa sheria ambayo itatambua haki ya wazee kulipwa pensheni bila ya kujalisha walikuwa watumishi au hawakuwa watumishi katika sekta za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vya 21 na 62 vya Muswada vinahusu uwekezaji wa fedha za mifuko ya hifadhi. Kifungu cha 21 kinakifanyia marekebisho kifungu cha 49 cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa *(Local Authorities Pension Fund Act- CAP. 407).*

Kifungu kipya cha 49(1) kinaipa bodi uwezo wa kuwekeza fedha za mfuko kwa kadri itakavyoona inafaa, wakati kifungu cha 49(3) kinasema kuwa pale uwekezaji uliofanyika kama utakuwa kinyume na kifungu cha 49(1), basi wahusika katika utoaji wa maamuzi hayo ya uwekezaji watawajibika binafsi kwa adhabu na faini kama zilivyoelezwa kwenye Sheria ya Mdhibiti wa Hifadhi za Jamii ya mwaka 2008 katika kifungu cha 49(3), kuhakikisha mfuko unafuata taratibu za uwekezaji kama zilivyowekwa na Benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kipya cha 49(4)(a),(b) na (c) kinachoipatia Benki mamlaka ya kurekebisha mifuko pale uwekezaji unaofanywa na mifuko unapokuwa sio mzuri. Kambi ya Upinzani inaona kuwa nguvu hizi inazopewa Benki maana yake ni kuinyang'anya mamlaka majukumu yake ya msingi

kwani kazi za Benki Kuu zimeelezwa wazi kwenye sheria ya mamlaka kwenye kifungu cha 48. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vyenye kuleta utata kama hiki hutoa mwanya kwa Bodi kwa kushirikiana na mfuko kufanya uwekezaji usiokuwa na tija, naomba kununukuu taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa hesabu za Serikali kuhusu uwekezaji kwa baadhi ya mifuko "… Mamlaka ya Mfuko wa Hifadhi ya Serikali za Mitaa *(LAPF)* ilikopesha *GK Hotels & Resorts* dola 535,000 katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, ambapo kufikia Juni 30, 2008 deni lilifikia kiasi cha dola 722, 000 wakati kampuni husika ilikuwa inadaiwa pia kodi ya kupanga katika jengo la *LAPF* dola milioni1.127."

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, taarifa hiyo imeonyesha matumizi ya fedha yasiyofaa kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ambayo imekuwa ikitumia fedha za wanachama wa mfuko huo kuwalipa wafanyakazi wake *bonus* eti kwa kazi nzuri wanayofanya wakati huo ni wajibu wao kwa mujibu wa ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* nayo imehusika katika kutoa mikopo na hata misaada ya fedha kwa watu na makampuni binafsi wakiwemo vigogo ndani ya Serikali bila utaratibu wowote kwa vile hakuna sheria iliyokuwa inazuia maamuzi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kutokea hapo baadae kama ambavyo Mifuko ya Hifadhi imekuwa ikifanya uwekezaji usiokuwa na tija kwa wanachama. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kifungu cha 91 cha Muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 13A.(1) kitumike kwenye kifungu cha 21 kinachorekebisha kifungu cha 49(1) pamoja na kifungu cha 62 kwani kifungu hicho kinatoa utaratibu na kanuni za kufuatwa pale uwekezaji utakapofanywa na mifuko, badala ya kusubiri makosa yamekwishatokea na hasara imekwishatokea ndipo Benki Kuu iwe na uwezo wa kuingilia kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dhana nzima ya uwepo wa Muswada huu ni kuhakikisha Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zinafanyiwa marekebisho ili kuipa Mamlaka ya Udhibiti nguvu zaidi za usimamizi ili kuhakikisha fedha za wanachama zinakuwa salama zaidi na wanachama wanapata mafao yaliyo bora zaidi. Kwa dhana hiyo ndiyo imeipelekea Kambi ya Upinzani kutoa pendekeza hilo hapo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 36 cha Muswada kinafanya marekebisho katika kifungu cha 39 cha Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya kwa kuongeza kifungu kipya cha 39A, kifungu hicho kinahusu taarifa ya uthamini wa mali na madeni ya mfuko. Kifungu kidogo cha 39A.(3) kinasema kuwa kwa kutumia taarifa hiyo mamlaka inaweza kutoa maelekezo kwa mfuko kuchukua hatua stahiki kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa na taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu yanayoonekana katika taarifa mara zote huwa yanatokana na utendaji usioridhisha na kama mapungufu hayo ni ya kibadhirifu yaliyofanywa na uendeshwaji wa kila siku wa mfuko, ni kwa vipi wasimamzi wakuu wataweza kurekebisha mapungufu hayo? Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sheria iweke wazi kuwa pindi mapungufu yanapojitokeza katika taarifa za mthamini ni adhabu za aina gani mamlaka inatakiwa izichukue dhidi ya watendaji wa mfuko, badala ya mfuko wenyewe kuambiwa urekebishe mapungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 66 cha Muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 71B, maelezo ya pembeni *(marginal notes)* yanasema kuwa taarifa ya mtathimini ipelekwe Benki Kuu, lakini maelezo kwenye kifungu hayaonyeshi kuwa taarifa ya mtathmini inapelekwa Benki Kuu badala yake inaonyesha kuwa taarifa inapelekwa kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na mamlaka. Hivyo

basi, Kambi ya Upinzani inaona *marginal notes* irekebishwe ili iendane na maelezo kwenye kifungu husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 150 cha Muswada kinachoongeza kifungu cha 49A.(2) kwenye Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma, Sura ya 371 kinataka kuwepo na tozo kwa mifuko yote kwa kiwango kitakachoamuliwa na Waziri mwenye dhamana kwa mashauriano na Waziri wa Fedha na Benki kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na dhana nzima ya mamlaka ya kuwa na chanzo cha uhakika cha fedha ili kuweza kufanya kazi zao vyema, tunashauri kuwa itakuwa ni vyema tozo hilo kutozwa kwa kuzingatia asilimia ya faida na uwekezaji *(total income of each scheme)* ili mradi isiguse fedha za wanachama na baadae Waziri mwenye dhamana airekebishe asilimia hiyo kwa kadri ya utendaji wa mifuko husika. Hii itaenda sawa na sheria zingine za udhibiti kama *TCRA, EWURA, REA* na kadhalika ambazo tozo zao zimewekwa kwa asilimia ya *total income.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maoni ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa David Silinde kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kama Waziri Kivuli wa Wizara ya Kazi na Ajira na sijui utaendelea kuwa kivuli sasa mpaka lini? Lakini hongera sana Mheshimiwa Silinde. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ndefu ya wachangiaji na naona Waheshimiwa Wabunge wengi wamehamasika kuchangia Muswada huu, nawashukuru, nawapongeza kwa maandalizi hayo mazuri. Kwa hiyo, nitaomba sasa nianze kutaja majina matatu ya wachangiaji wa mwanzo ili waanze kutoa michango yao na tutakuwa tunapeana taarifa kadri muda unavyozidi kwenda. *(Makofi)*

Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni Zanzibar na atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Mohamed Missanga naye ajiweke tayari. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kupata nafasi hii ya kwanza ya kuchangia hoja hii ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Jamii. Mifuko hii kama inavyotajwa kwamba ni ya jamii, lakini kwa utaratibu ilikuwa ipo chini ya Wizara mbalimbali na wafanyakazi pekee ambao ndio walikuwa wanapata fursa hizi za kuwa wanachama kwenye mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli dhana hiyo au utaratibu huo ulikuwa kwa muda wote ukiwanyima wengine ambao walikuwa si watumishi katika Wizara mbalimbali na walikuwa hawapati nafasi ya kujiwekea angalau hatma zao kwa maendeleo na maslahi ya baadaye wanapokuwa hawana nguvu tena za kujituma au kufanya shughuli mbalimbali. Lakini pia katika hali hiyo utaratibu huo pia ulionekana kwamba katika kila Wizara ilikuwa ni jukumu la Wizara na mfuko wao kujipangia wenyewe utaratibu wa kufanya shughuli zao, lakini jambo hili pia lilipelekea kwamba wanachama kwa mfuko ule walikuwa hawafaidiki vyema kwa sababu watendaji walikuwa wanaonekana kwamba wakiangalia zaidi maslahi inayotokana na mifuko hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa zisizo rasmi kwamba baadhi ya mifuko ilikuwa watendaji wanalipana mishahara zaidi ya shilingi milioni 10, lakini pia wakipeana posho kubwa kubwa kwenye vikao vyao vya zaidi ya shilingi 500,000/=. Jambo hili lilikuwa haliwatendei haki wanachama wa mifuko hiyo kwa sababu wao ndio wamiliki na ndio wenye mali ambayo wao walikuwa wakiitumia vile wanavyopenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya sasa imependekezwa nami naungana na mapendekezo kwamba

mifuko hii yote iwe chini ya mwamvuli mmoja wa Wizara ya Kazi jambo ambalo litapelekea mifuko hii kuwa chini ya usimamizi mzuri na Wizara inafaa kabisa na ni vyema ikaanzisha idara maalum kama ambavyo imependekezwa ili iweze kuwa na udhibiti mzuri wa mifuko hii kwa nia na dhamira ya kulinda maslahi ya wanachama wa mifuko hiyo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la mifuko hiyo mbalimbali kuna jambo lingine ambalo lilikuwa linaonekana halikuwa na udhibiti mzuri, aidha, lilikuwa halitendi haki kati ya mchangiaji wa mifuko na mdhibiti au mdhamini wa mifuko. Kulikuwa kunaonekana kwamba sheria ilikuwa inamtaka mchangiaji anapochelewesha kupeleka mchango wake basi kulikuwa kuna *penalty* ambayo ilikuwa inaonekana kwamba asilimia tano ilikuwa inaonekana ni adhabu kwa mchangiaji aliyechelewesha mchango wake. Katika sheria hiyo hili lilikuwa ni adhabu kubwa kwa mchangiaji kwa sababu kuchelewa ni ubinadamu na ni jambo la kawaida, linamkumba hata yoyote. Lakini pia kwa sababu ilikuwa inaeleweka kwamba hata mfuko wenyewe unaweza ukachelewesha mafao kwa mstaafu au mwanachama wa mfuko anapostaafu. Basi ilikuwa ni vyema kwa sheria hiyo hiyo basi na huu mfuko ukawa na wenyewe unakumbana na adhabu hiyo kwa kiwango hicho hicho ambayo alikuwa mwanachama anatozwa. Lakini kwa sheria ya sasa au aidha, mapendekezo ya sheria ya sasa ya kwamba adhabu ile ya asilimia tano ni kubwa sana nami naungana nayo lakini pia kama anatozwa mwanachama aliyechelewesha basi na mfuko wenyewe ungestahili kwamba ukakumbwa na adhabu hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sheria hizi zinarekebishwa sasa basi mimi nadhani ni wakati muafaka wa kuhamasisha wale wafanyakazi wasio rasmi ili na wenyewe wajiunge katika mifuko hii ili waweze kufaidika na kile ambacho wanakipata au waweze kujikusanyia mapato haya kwa maslahi ya baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mchango mrefu kwa sasa na naomba nisipoteze muda sana niwaachie wenzangu ili nao wachangie yale ambayo wanakusudia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi na mimi nichangie Muswada huu ambao kwangu mimi nauita ni ukombozi kwa wastaafu, wafanyakazi walio katika hifadhi ya jamii. Ni mkombozi kwa sababu marekebisho yake jinsi yalivyo kwa kweli yameletwa wakati muafaka. Niseme kwamba yamechelewa hapana, yamekuja wakati muafaka kwa sababu viongozi wetu wameweza kukaa na kuona kwamba wapi turekebishe ili kusudi Muswada huu uwe mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mapendekezo kadhaa, nianze na kule kwenye madhumuni. Mapendekezo hayo pia yatatoa fursa kwa watumishi wa umma upeleke maombi kwa Rais ili wapewe msamaha kwa baadhi ya masharti ambayo yanaweza kumzuia kupata pensheni. Tukiruhusu hiyo kwamba kila mlalamikaji apeleke malalamiko yake kwa Rais Ikulu patajaa na inawezekana hata Mheshimiwa Rais anaweza hata kushindwa kufanya kazi zake.

Mimi ningeshauri malalamiko haya kama kuna malalamiko basi yaanzie kwa Waziri ili kusudi ikishindikana kwa Waziri huyu mtu awe na uwezo wa kukata rufaa kwa Rais. Lakini akianzia kwa Rais akishindwa kwa Rais anakwenda wapi? Lakini Rais anao washauri wake ambao ni Mawaziri kwa hiyo ukianzia kwa Mheshimiwa Waziri hapa, Waziri mwenye dhamana ikienda Zanzibar Mheshimiwa Waziri atatoa mapendekezo yake kwa mujibu wa sheria. Mapendekezo hayo yangekwenda kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nashauri kwamba malalamiko yasiende moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais yaanzie kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kuangalia kwenye ile *Part Five A(2). Director General* ataripoti kwenye *authority,* huyu wa kwa *NSSF.* Lakini wengine ma-*DG* hawakutajwa waripoti wapi. Ningeshauri kama ni utaratibu huo basi na ma-*DG* wengine nao waripoti kwenye *authority* kuliko kumuachia huyu wa *NSSF* ndio aripoti kwenye *authority.* Lakini nimejaribu kuulizia *authority* kama ya *EWURA, Director General* wa *TANESCO* anaripoti moja kwa moja Waziri. Kwa nini hao ma-*Director General* hawa wasiripoti moja kwa moja kwa Waziri wanaripoti kwa *authority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine aya ya 147 ambayo nafikiri nimeisemea kwamba ni vizuri kwa sababu Mheshimiwa Rais amewaamini watu wake kuna Waziri ni vizuri hizi kazi zingine ambazo za kiutendaji zingeanzia kwa Mawaziri na baadae ziende kwa Mheshimiwa Rais tusimpe kazi ngumu sana Mheshimiwa Rais ya kufuata mambo ambayo mengine yangeweza kumalizwa huku na kwa Wizara. Lakini kwa upande wa Wajumbe wa Bodi mfano halisi *NSSF* na Bodi zingine kwa sababu mfuko huu ni mkubwa sasa ningeshauri wale wanaochagua kwa mfano nikianza na Bodi ya *NSSF* mapendekezo yaliyokuja tuliyoambiwa ilikuwa ni kwamba wanatakiwa watano sasa *quorum* isipotimia tutafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni la kwanza, lakini la pili, tunatakiwa tuingize *board member* mle ndani wanaowawakilisha wafanyakazi, lakini itasaidia kupunguza malalamiko ya wafanyakazi kwa sababu Wajumbe hawa wa Bodi watasaidia kwenda kusema kwenye hizo bodi zao. Kwa hiyo, ombi langu hapa ni kwamba Wajumbe wa Bodi wa Mifuko yote hii wachaguliwe kufuatana na sifa zao. Tusichague tu ili mradi yaani huyu mtoto wa shangazi, huyu ni fulani, hapana. Tuchague kufuatana na sifa zao. Ukifanya hivyo utauona ni ushauri mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuhusu mafao, *NSSF* wana mafao ya matibabu, Bima ya Afya ina mafao ya

matibabu. Mwajiri kama amejiunga sehemu zote mbili hizi kuna ulazima wa kujiunga. Kwa hiyo, Mwajiri huyu atapeleka mafao ya matibabu kwa mwajiriwa *NSSF* na atapeleka Bima ya Afya. Makato yote ni ya matibabu kwa hiyo mnamkata mara mbili. Nafikiri nimeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mafao ya *NSSF* ni matibabu. Kwa hiyo, mwajiri anapeleka hela ya matibabu *NSSF.* Lakini Bima ya Afya wao wanashughulika na matibabu. Kwa hiyo, mwajiri anapeleka hela za matibabu kwa mtu mmoja.

Kwa hiyo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri baadaye mlitazame vizuri. Lakini kuhusu ukokotoaji wa mafao, endapo mifuko hii haitakuwa na *uniform* mfanyakazi huyu kwa sababu kapewa uhuru wa kuamua kwenda sehemu ambako kuna mafao mengi ipo hatari baadhi ya mifuko itakufa. Mimi nitapenda kwenda sehemu ambako ina mafao mazuri zaidi. Kama kima cha chini cha mshahara ni 135,000/= lakini pensheni ni 50,000/= lakini inawezekana sehemu nyingine kima cha chini ni 135,000/= pensheni ni 60,000/= au 70,000/=. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aiangalie sana mifuko hii, vinginevyo baadhi za mifuko inaweza ikafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni ushauri, kama nilivyosema kwamba ni vizuri zaidi tunapoteua Ujumbe wa Bodi, sisemi mimi niteuliwe hapana, msije mkaninukuu vibaya. Nazungumzia mifuko, ili mifuko hii iwe endelevu lazima Wajumbe wa Bodi wateuliwe kufuatana na ujuzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo niseme nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na *staff* wake wote lakini pia niwapongeze sana Wakurugenzi kwa maana ya ma-*CEO* pamoja na Wajumbe wa Bodi wa Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niseme machache tu kama mchango wangu katika Muswada huu muhimu. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, tena nafasi ya mapema ili niwahi sala ya Ijumaa, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukushukuru naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada mzuri ambao kwa kiasi kikubwa umejieleza vizuri na nia ya Serikali hapa kwa kweli inaonekana wazi, nia ya kuboresha mifuko hii ya jamii ili kutoa ukombozi kwa wanachama na hususan wafanyakazi wale walio rasmi na hata wale wa *informal sector* kama ilivyoelezwa humu ndani.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na wote katika Wizara ile kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Lakini nikushukuru wewe kwa upande mmoja kama Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati yako yote. Pamoja na mwakilishi aliyesoma kwa niaba yako, kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana hongereni sana. Yale ambayo nilikuwa nafikiria fikiria mengi naona yamo kwenye kile kitabu chako. Hongera sana Mheshimiwa Nkamia kwa kufanya kazi kubwa ambayo mmeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sitaki kuyarudia lakini nitoe mifano miwili ambayo mmenifilisi kwa mfano. Suala la *composition* ya Bodi ya Wakurugenzi, naona mapendekezo yalikuwa ni ya kuwapunguza kuwa watano, sijui wengine wakasema saba lakini mimi nadhani nikubaliane na ninyi kwamba tisa ni vizuri kidogo. Kwa sababu *experience* yangu mimi nimeshawahi kufanya kazi hizo za Bodi ya Wakurugenzi ingawa Mama Kabaka hajaniona, *Inshallah* ataniona siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *experience* yangu inaniambia kumbe kuna Kamati mle kwenye Bodi. Sasa unapokuwa na Wakurugenzi watano. Shirika kubwa kama *NSSF,* hata *PPF*

unatakiwa uwe na Kamati kama tatu za kuangalia maeneo mbalimbali kurahisisha kazi za Bodi, hivi wale watu watano unawagawaje? Kwa hiyo, ukipata watu tisa unawagawa vizuri, watatu, watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niunge mkono wazo la Kamati kwa kweli watu tisa na mfano mzuri ni huo kwamba angalau utakuwa na Kamati tatu za watu watatu, watatu kwa kusaidia kufanikisha kazi za Bodi. Huo ni upande mmoja mliosema lakini upande wa pili ni ile habari ya kuangalia uwezekano wa mifuko hii kuwa chini ya Wizara moja na hili halikuanza leo, tumelizungumza siku nyingi toka kwenye ukumbi wa Msekwa mpaka sasa tutaenda nalo. Sasa Serikali yetu ni Serikali sikivu nadhani wataendelea kusikia hili nalo waliangalie. Nasema hii ni mifano miwili ambayo mmeisema na mimi nilikuwa nayo pamoja na mengine mengine, sitaki nirudie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni au mafao yoyote yanayotolewa kwa kustaafu mfanyakazi baada ya kutumikia utumishi wake yanakusudia kumsaidia mstaafu yule katika maisha yale asiharibikiwe afanane fanane kidogo na maisha yale ambayo alikuwa nayo wakati akiwa mtumishi, ndiyo makusudio. Asiwe *destitute* eti kwa sababu amestaafu, hapana sio hivyo. Pensheni nia yake ni kumsaidia huyu walau afanane fanane, hawezi kuwa sawasawa kama alivyokuwa wakati yupo kazini lakini walau akurubiane na wakati ule alipokuwa na utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama mtu alikuwa anapata shilingi milioni tatu, ukaja ukampa pensheni ya shilingi 20,000/=, 30,000/= au 40,000/= kwa kweli kuja kuja kujiweka sawa inamchakua taabu sana ndiyo maana watu wengine wanasema ukistaafu *hardly two or three years you go.* Sasa tusifike huko, tusiwauwe watu kabla ya siku zao ingawa viongozi wa dini hawawezi kuruhusu hilo lakini nasema ni vizuri kuliangalia hili na mantiki wewe unafahamu tulipokuwa

tunafanya marekebisho ya viongozi wetu wakuu tulisema kiongozi wetu mkuu kafanya kazi nzuri, tusimharibie angalau asilimia 80 ya *incumbent* huyu mstaafu apate. Ndiyo viongozi wetu wakuu wanavyopata *80 percent* wastaafu hawa, mimi sitaki kuwataja wenyewe wanajijua maana wengine wapo humu ndani na wengine wapo nje wananisikia.

Sasa hiyo iporomoke mpaka chini tusiiache kule kwa wakubwa tu ije mpaka chini angalau hawa wakistaafu wapate angalau *80 percent* ya kile ambacho walikuwa wanapata, ndiyo nia yenyewe hiyo. Tusiwapendelee wale walichonacho hawa ambao hawana ndiyo wa kuwaporomosha zaidi. Kwa hiyo, nasema hilo ndilo liwe lengo na hapa nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza *NSSF* kwa sababu naambiwa wewe ni mtaalam zaidi kuliko mimi, naambiwa katika *NSSF* kima cha chini ni *80 percent* ya kima cha chini cha mshahara cha kiwango cha Serikali ndivyo ninaambiwa sina hakika. Lakini kama hivyo ndivyo kwa mfano sasa hivi kima cha chini shilingi 100,000, kwa hiyo, pensheni ya chini ya *NSSF* itakuwa ni shilingi 80,000/=, haijambo kwa lugha ya kule visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria niseme na mifuko mingine nayo iwe hivyo. Kwa hiyo, naiomba hii *Social Security Regulatory Authority* iangaliwe isiwe *NSSF* peke yake bali iangalie *across the board* ili kusudi wakistaafu angalau wapate *80 percent.* Ninyi hapa mmesema *70 percent* mimi pia sioni tatizo, tunakushukuru kwa hilo, kama sio *80 percent* tukafanana na wakubwa, viongozi wetu wa juu kule wakiwa asilimia 70 mimi nadhani hiyo naweza nikaikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 17 kifungu cha 21, imezungumziwa pale habari za...

**MWENYEKITI:** Kifungu 21 cha Muswada au cha ripoti?

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muswada.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama niko sawasawa Kifungu cha 21 pale, mnapozungumzia habari ya *investment.* Mimi naliunga mkono hili kwa sababu ni ukweli kabisa kwamba *investment* ambazo zimefanyika katika mifuko yetu hii zimesaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa wanavutana wengine hivi wengine hivi, lakini imesaidia. Nichukue mfano wa *NSSF,* wote tunajua uwekezaji walioufanya katika *Kagera Sugar,* wote tunajua kwamba ujenzi wa *UDOM, NSSF* wameshiriki vizuri tu na mpaka tumepata chuo kile pale, wote tunajua jengo hili hapa la Bunge pana mchango mkubwa sana wa *NSSF* humu ndani wote sisi tunajua, wote tunajua daraja la Kigamboni linajengwa kwa msaada wa *NSSF* na mkandarasi yupo kwenye *site* tangu mwenzi Februari mwaka huu. Nafikiri yale malumbano yalishaisha sasa hivi mkandarasi yupo kwenye *site,* yote yanafahamika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nakubaliana na hilo ingawa nakubali na tahadhari nao hawa *Regulatory Authority* lazima wawe makini kuona kwamba pamoja na *investment* inayofanywa lakini vilevile na wanachama lazima waangaliwe ili kusudi na wao wanufaike na *investment* ile na wanufaike na michango yao ambayo wanatoa. *Investment* ifanywe ili nchi inufaike lakini na wanachama nao lazima wakumbukwe waweze kunufaika.

Sasa kwa *NSSF* upande wa wanachama naambiwa kuna mafao saba. Sasa haya saba si kidogo. Wakati *ILO* nilikuwa nasikiliza hapa ile *convention* inataka mafao tisa. Sasa hawa wenzetu wameshafika mafao saba, haijambo. Kwa hiyo,

ninaomba kama na wengine nao wajitahidi kuona kwamba wanafikia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi mlizungumzia *actural valuation.* Mimi ningependa niambiwe hapa kuna Mtanzania ambaye ni *actural?* Maana mimi kwa *experience* yangu toka niko kwenye mambo ya *Trade Unions* mpaka sasa hatuna sisi Mtanzania na ni *very vital* kazi ya kufanywa. Sasa tutakuwa tunanawakodisha watu kutoka Kenya na Ulaya kila siku itakuwa *very expensive*. Ningependa kujua yupo, kama hayupo kwa kweli *is high time* kama nchi tufanye jitihada za makusudi katika vyuo vyetu tupate wataalam hawa ili watufanyie hizi *actural valuation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna kitu kinaitwa *indexation* katika masuala haya ya hifadhi ya jamii, mimi sina hakika kama linafanyika maana kuna mifuko hapa, kuna watu wamepata pensheni ya shilingi 20,000/=; 30,000/= miaka zaidi ya kumi, ishirini anapata hizo hizo 20,000/= toka amestaafu mpaka leo 20,000/= kwa sababu haijafanyika hii *indexation*. Lazima lifanyike hili na hii ndiyo kazi ya hii *regulatory authority* kuona kwamba *indexation* inafanyika. Baada ya *actural valuation* na kuona kwamba hali ni nzuri wanaruhusu kuwekeza lazima *indexation* ifanyike ili kumwondoa huyu mtu aliyekuwa anapata 20,000/= aendane na hali ya maisha. Nimesema pale pensheni maana yake ni kumsaidia mtu huyu apate kama kile ambacho alikuwa anapata. Sasa *inflation* imepanda, gharama za maisha imepanda, wewe pensheni uliyompa toka mwaka 1970 unaendelea kumpa mpaka leo, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili nipate maelezo ya bayana je, *indexation* inafanyika katika mifuko yetu ya hifadhi ya jamii au ni maneno tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Ndassa sikubaliani kumwongezea Rais. *Already* siku zote wanalalamikia na hasa Wapinzani wanasema Rais

tumemwekea majukumu makubwa mnakwenda kumwongezea tena hili lingine kwamba eti kwa sababu watu hawafanyi vizuri na nini tupeleke taarifa kwa Mheshimiwa Rais. Jamani hata hili, hivi Waziri hawezi, Bodi haiwezi nani hawezi? Tumpelekee Mheshimiwa Rais akaangalie na hili tena? Hapana sikubaliani na hilo.

Halafu lingine ambalo sikubaliani nalo ni lile la miaka kumi kwa Mkurugenzi Mkuu. Kwa nini iwe ni mifuko ya hifadhi peke yake miaka kumi. Mashirika yote, iwe ni Bandari, iwe ni *TANESCO,* iwe *TCRA* kama ni miaka kumi iwe wote.

Lakini yule wa *TANESCO* akae miaka 30, wa *NSSF* akae miaka 10, wa *PPF* akae miaka 10, wa shirika gani miaka 45, aha! Jamani haiwezekani. Kama kuna haja ya kupunguza kuweka miaka kumi basi iwepo chini ya Sheria ile ya *Public Cooperation Act* iwekwe mle ndani kwamba viongozi wa taasisi basi muda wao ni miaka mitano akimaliza anaweza akaongezewa miaka mitano mingine au zaidi ya hapo. Lakini nasema kama ni lazima iwepo iwe *across the board* sio kwenye mifuko ya hifadhi peke yake, mashirika yote ya umma iwekwe hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwaonee hawa tu kwa kuwaonea kijicho *unless* itafsiriwe hapa kwamba kuna mtu tunamlenga hapa. Tuseme ukweli, lakini kama nia ni nzuri twende kwa mlango wa mbele kwamba mashirika yote ya umma iwe ni miaka kumi basi na haitakuwa kwenye mifuko hii itakuwa kwenye *Public Cooperation Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 47 nafikiri nimekizungumzia kinachosema kama mwajiri hapeleki michango kwa nini taarifa ipelekwe kwenye *authority.* Sheria si ipo? Hapeleki michango, sheria ipo apelekwe mahakamani ashughulikiwe. Sasa tujaze mabarua sijui na nini nadhani tutakuwa tunawalimbikizia kazi ambazo hazina sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nadhani muda umekwisha nashukuru kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku hii ya leo lakini pia nakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kazi pamoja na wewe mwenywe, pamoja na Wakurugenzi wote wanaoshughulikia mifuko hii bila kusahau Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko kwa kazi nzuri ambayo wameifanya mpaka sasa lakini pia kwa kuleta Muswada huu kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa na wenzangu lakini kuna masuala ambayo kwa kweli inabidi tusisitize. Jambo la kwanza ni juu ya Bodi itakayohusika katika kushughulikia mifuko hii. Naomba sana tumeshakuwa na misingi ya kusema kwamba uwakilishi uangalie pia masuala ya kijinsia na wakati mwingine unakuta tunahama kidogo kidogo, tunasema uwezo. Lakini kwa hali ya Tanzania sasa hivi jinsi ambavyo Serikali imejitahidi chini ya chama chake tawala kusomesha watu, unakuta kwamba sasa hivi kwa upande wa wanaume na wanawake watu wanayo elimu ya kutosha katika maeneo hayo. Ni vema basi tuone kwamba kuna ulazima wa kuzingatia pia suala la jinsia ikiwemo wanawake, lakini pia hata yale makundi maalum ambayo yanatakiwa kuangaliwa na mifuko hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hilo nasisitiza kwamba hata idadi ya Wajumbe kutoka kwa wafanyakazi au kutoka kwa wale ambao wanachangia mfuko ni muhimu iongezeke, isiwe tu mjumbe mmoja ili kuona kwamba wao wana *share* kubwa katika huo mfuko, basi idadi yao iwe angalau ni wawili ili kuweza kupata taarifa mbalimbali zile za kwenye maeneo halisi, isiwe tu katika utekelezaji wa mfuko katika misingi ya

michango, lakini hata katika uhalisia wa ustawi wa watu kutoka katika maeneo hayo yanayochangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu ambacho kimekuwa-*repelled* cha 47 kutoka kwenye *principal act* kwa Muswada huu ambao ninao, sasa sielewi kama kuna marekebisho yamesogea zaidi. Pale inazungumziwa kwamba kusiwe na *double payments*. Sasa isitoshe tu kusema mtegemezi kwamba yeye hastahili kulipwa mara mbili na kwamba wataangalia kutokana na mafao mazuri zaidi ambayo yanastahili kulipwa. Tatizo kubwa linalojitokeza ni kwamba huyu mtegemezi wakati mwingine hafahamu haki halisi za huyo ambaye ametangulia mbele za haki kiasi kwamba inamchukua muda, anahangaika, anazubaa huku na huku, hajui kinachoendelea na kinachomhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo basi, iwe ni wajibu kiongezwe kifungu kitakachosema wajibu wa mwajiri au mwenye mfuko kumfahamisha yule *dependant* kwamba ni kiasi gani anastahili kutokana na huo ulinganisho wa mafao yanayostahili kulipwa ili basi na yeye aweze kujua anafuatilia vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisisitiza katika hilo, leo tunachangia tukiwa katika hali nzuri, tuna uwezo na ukiacha sisi Wabunge, hata wale wenzetu wanaoshughulikia hii mifuko. Lakini kuna usumbufu mkubwa katika maeneo hayo na ninaongea nikiwa naongea kwa uhalisia, mara nyingi napenda kutoa mifano ambayo ni halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaye ndugu wa kuzaliwa naye tumbo moja, toka mwaka 2009 mpaka leo hii hajaweza kulipwa. Ukifuatilia pale *PSPF* unaambiwa kwamba faili halionekani, Mkurugenzi wa Idara fulani hajaleta, Mkurugenzi huyu sijui hakufanya hiki yaani ni usumbufu mkubwa mno. Familia zinapata shida. Kwa sisi ambao tunatoka huko mikoani

tunafahamu ni jinsi gani watu wanahangaika kufuatilia mafao yao na hawayapati kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina faida gani basi kama mtu atakuwa anakatwa mafao yake akitegemea yatamsaidia na familia yake, lakini baadaye anapata usumbufu wa kiasi hicho, sababu zipo nyingi nyingi, nyingi, nyingi ambazo pengine siyo za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kwa dhati kabisa, katika kuhakikisha kwamba mifuko pia inawajibika katika kulipa mafao ya hao watumishi kwa wakati, lazima tuongeze kifungu cha kuwataka ndani ya muda fulani wawe wameshalipa. Mimi napendekeza ndani ya miezi sita wawe wameshalipa. Kwa sababu haina maana kumfanya mtu anateseka kwa kitu ambacho kipo, faili halionekani, yaani huyu mtu ina maana mpaka anakufa, wanasema faili halionekani, siku zote kazini alikuwa anaishi vipi kiasi kwamba faili lake lisionekane? Hatutendi vizuri hata kidogo na hilo ni jukumu letu sote, siyo chama kimoja, siyo Serikali peke yake, bali mihimili yote inayohusika kuhakikisha kwamba ustawi wa wananchi unalindwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango pia limezungumzwa kwa upande wa Upinzani, wenzetu wamechangia hoja ya wazee kulipwa 20,000/= kwa mwezi. Mimi naungana nao kwa upande mmoja, lakini ningependa tuliboreshe sana. Uboreshaji wangu ninaozungumzia ni nini, wamependekeza 20,000/=, lakini ni kigezo gani tumefikia kusema iwe ni 20,000/=? Huko kwenye maeneo tayari Serikali ilishaweka mpango wa wazee kupata huduma ya afya bure na kwa bahati nzuri hospitali karibu nyingi zimetenga madirisha maalum kwa ajili ya wazee. Lakini unakuta pengine dawa hazipatikani kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiria pengine mifuko ione sasa namna ya kurudisha sehemu ya faida kwenye

maeneo hayo ya wazee. Ninapozungumzia wazee, simaanishi tu wale waliokuwa katika ajira rasmi. Kwa sababu Tanzania tumeelezwa kwamba ajira ni yoyote ile inayompa mtu kipato kilicho halali. Akifanya shughuli zake, akipata kilicho halali ni ajira. Huko tuna wafugaji, huko tuna wakulima ambao kwa kweli nchi inalishwa na watu hao. Hawaonekani kwenye *payroll*, lakini bila hao sisi hatuwezi kuishi. Ni jinsi gani tunaangalia mifuko hii ya jamii kurudi kurudisha heshima kwa hao watu wanaolisha nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sheria ya wazee inazungumzwa lakini haijafika hapa. Niiombe sana Wizara ichukulie kwamba ajira sasa itoke kwenye ajira rasmi peke yake, iangalie ajira hizi ambazo siyo rasmi ili sheria ya wazee iweze kuangaliwa. Watoto ambao wapo vijijini ambao wangestahili kuhudumiwa kutokana na hizi ajira ambazo siyo rasmi, basi mifuko hii pia iweze kuona namna ya kuendeleza maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko tunaipongeza sana, imetusaidia sana, mfano ni Chuo Kikuu cha Dodoma na maeneo mengine mengi. Lakini niwaombe sana kwenye maeneo ya mikoa huko mingine ya pembezoni bado kuna tatizo la huduma. Watoto inafikia mahali wako wengi, *actually* idadi ya watoto ni kubwa, idadi ya vijana ni kubwa kuliko hata hao watu wazima. Sasa watu hao ambao wengi wako vijijini, hawawezi wote kuja kukaa mjini, wengine itabidi waendeleze shughuli zao kule. Kuna maeneo wanayofanyia shughuli za minada, kuna maeneo wanayofanyia shughuli zao mbalimbali, zinakosa uboreshaji. Lakini hao ni soko, ni soko kubwa sana kama litawezeshwa kuifanya mifuko hii iweze kuzidi kutuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana, tuangalie sasa namna ya kutafuta soko kubwa zaidi kwa kuwezesha maeneo hayo, itasaidia sana wao kufaidika, lakini pia jamii yetu kuweza kuboreka vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu waliosema kwamba ni vema kama ambavyo imeangaliwa, mifuko hii kuwa chini ya mwamvuli mmoja, hiyo itasaidia sana kuliko kila mfuko unajitegemea na Wizara yake, mambo mengine hayaendi inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika suala hili la uwekezaji unaoendelea, naomba sana tuangalie namna ya kuwafanya hawa watumishi wanaochangia waweze hata kukopa kwa wakati kwa ajili ya uwekezaji wao ili waweze kufaidi matunda kabla hata ya kusubiri mpaka anapokuwa mzee. Kweli uzee unatisha, uzee una taabu, lakini pengine ungepewa huo mkopo mapema zaidi ili rehani yako iwe ni hayo mafano yako, ingekusaidia kujipanga vizuri zaidi na ikaongeza siku za uhai. Lakini sasa unakuta unapata mafao, tayari na muda wako umeshakuwa mkubwa, kuwaza hata hiyo miradi yenyewe ni ngumu, watoto umeshindwa kusomesha kwa sababu hukuwa na uwezo wakati huo unafanya kazi, matokeo yake hali inazidi kuwa ni mbaya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi katika hili ninaomba sana mifuko iweze kurudisha sehemu kwa wale wenyewe wanaochangia kwa kuwawezesha kupata mikopo ambayo itakuwa ina riba nafuu. Kwa mfano, kama walimu wanaingia kwenye mikopo mingine mpaka unaona huzuni, wanakuja wanakwambia sisi tulikopeshwa na kampuni fulani (siitaji kwa heshima), lakini unakuta sasa katika hiyo kampuni tunadaiwa, deni ulishamaliza, bado unadaiwa tena. Kwa hiyo, vitu vinakuwa havieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ombi langu, nafahamu mifuko imejitahidi sana, imefanya kazi zake vizuri, lakini tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza tukasaidia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza maneno haya, nirudi kwetu sisi wenyewe Wabunge. Ipo haja pia na

Wabunge kuweza kuwa katika hii mifuko. Si tu ilivyo sasa hivi kwamba ni *option* ya Mbunge kuamua aingie, kwa sababu inavyokuwa *option*, naamini anakosa sehemu ya mwajiri. Sidhani kama mwajiri anachangia kwa sababu inakuwa hakuna *compulsory* ya yeye kuchangia. Lakini kama itakuwa imewekwa vizuri zaidi itasaidia, hata kampeni hazitakuwa chungu kama zilivyo. Sasa hivi mtu anachukua nafasi ya kufa na kupona kwa sababu anajua nikimaliza hapa, mimi ni mwisho wangu na bahati mbaya sana kazi hii ya Ubunge ni tofauti na kazi nyingine, *style* yake ya kuingia ni tofauti na kazi nyingine. Mnapigana huko mpaka mtu amechoka, ndiyo anayefanikiwa anaingia hapa. Na ukimaliza, ukiacha Wabunge wa Viti Maluum, sharti ni kwamba kama ulikuwa kwenye ajira, uache ajira yako. Sasa unakuta mtu mwingine bado ana nguvu, lakini sababu tu alikuwa ameingia kwenye Ubunge, kurudi kwenye ajira haiwezekani, matokeo yake anachanganyikiwa, yaani anaona kama hakuna maisha mengine mbele. Kumbe tungefungua milango kwamba mtu afike kwenye kazi hii kama ni sehemu ya kazi, lakini wakati huo achangie. Na mambo hapa yakiwa ameshindwa kupata, ili demokrasia ifanye kazi yake vizuri, aendelee na kazi yake kama bado ujuzi wake upo. Hili eneo lina utata.

Mimi nawaombeni sana Wabunge tulione hili kwa nguvu zote. Tukifanya jambo lolote la kurekebisha mazingira haya, naamini hata demokrasia ya nchi itakuwa nzuri zaidi kuliko hii hali iliyopo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimjiwa Mwenyekiti, baada ya maeneo hayo, nichukue nafasi hii kuwakaribisha wenzetu wenye mifuko watembelee pia mikoa yangu miwili; mkoa wa Ruvuma nilikozaliwa na mkoa wa Rukwa ambako nafanyia kazi, wataona namna ya kutusaidia, namna ya kuona kwamba wananchi pia wanaboreshewa maisha yao katika kuwekeza hali ambayo inastahili. Lakini pia na mikoa mingine ambayo hata wenzangu wakuu wa mikoa wangekuwepo labda wangeisemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa. Hatujakusikia siku nyingi, leo tumepata nafasi ya kukusikia.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani naweza kuwa na nafasi za Waheshimiwa Wabunge wawili. Kama nilivyosema, nilimwomba Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo na nafasi itakayobaki nadhani inaweza kumtosha Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kutoa mawazo yangu juu ya Muswada ulioletwa mbele yetu unaohusiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili ningependa niipongeze Serikali kwamba mifuko hii zamani ilikuwa ikiitwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini ilizingatia zaidi wafanyakazi wa Serikali. Leo mifuko hii kuingizwa katika sekta binafsi, niseme kwamba ni ukombozi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba kujiunga na mifuko hii kutaongeza idadi kubwa ya wanachama ambao kujiunga kwao pamoja na kutoa michango yao ni kulipatia Pato Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niseme kwamba mifuko hii, nipendekeze sawa na wale wenzangu ambao walisema kwamba mifuko hii basi ni lazima iwekwe kwenye Wizara moja nayo ni Wizara ya Kazi. Kwa sababu kila Wizara kama itakuwa inabeba jukumu la mifuko hii, basi ni kuvunja nguvu kazi ya Wizara ya Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi kwamba makampuni yasiwe na mifuko yao, wanaweza wakawa na Mifuko yao ya Hifadhi ya Jamii, lakini kwa upande wa Serikali, basi Wizara ya Kazi iwe ni dhamana juu ya mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna kitu cha adhabu ambacho kimetamkwa kwenye kifungu cha 29(a), kinatoa adhabu kwa mwanachama wa mfuko anayechelewa kutoa mchango wake. Sasa hebu niulize, kama ikiwa mwanachama wa mfuko aliyechelewa kutoa michango yake, anapewa adhabu, je, kuna adhabu gani imewekwa kwa huyu mwenye dhamana ya mfuko huu ambaye atakosa kumpa mafao yake mwanachama wake ambaye amekwishastaafu, yaani kachelewa kumpa mafao yake? Kwa hiyo, ni lazima kuwekwe kitu ambacho au kifungu ambacho kitakuwa kwamba atafidiwa yule mwanachama ambaye ameshastaafu na yeye kacheleweshewa kupewa mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine niseme kwamba nilitaka nieleweshwe hapa palipotajwa neno sekta binafsi. Hawa ni watu wa mashirika ya umma au ni pamoja na wajasiriamali? Sasa kama wajasiriamali wapo, mimi naunga mkono moja kwa moja. Lakini ningependekeza, ikiwa hawamo, basi kuna wajasiriamali ambao wana kipato kikubwa kuliko wafanyakazi na wao waingizwe katika sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependekeza lingine ambalo linahusu wafanyakazi kwa upande wa Zanzibar. Kipato cha wafanyakazi kwa upande wa Zanzibar ni kidogo. Sasa sheria hii izingatie na kipato cha wafanyakazi wa chini kwa upande wa Zanzibar. Tukisema kwamba ni shilingi 80,000/=, basi kwa mfanyakazi wa Zanzibar, baadhi yao unawaambia wasijiunge na mfuko huu. Kwa idadi kubwa, kwa asilimia 70 ya wafanyakazi wa Zanzibar unawaambia wasijiunge na mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuwapa fursa na wao ya kujiunga na mfuko huu, nadhani wangepunguziwa makali kidogo, wakawekewa kiwango cha chini ili mwanachama aweze kujiunga angalau kwa shilingi 50,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni suala la uwakilishi katika mifuko hii. Kutaundwa chombo na katika chombo hiki katika sheria imesemwa kwamba Zanzibar angalau itapata nafasi mbili. Ningeomba kwanza zizingatie jinsia, vilevile kama alivyosema Mheshimiwa Stella Manyanya. Lakini vilevile ni kwa mgawo gani uliotolewa mpaka Zanzibar ikapewa nafasi mbili? Nilitaka nijue ni idadi gani ya hao wajumbe ambao watateuliwa ili Zanzibar iweze kupata nafasi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu lingine ni suala la malipo ya uzeeni. Nadhani ilipotajwa 20,000/=, bado tutakuwa hatujazingatia gharama za ukali wa maisha na kama tungezingatia gharama za ukali wa maisha, basi nadhani tungefanya fungu la huruma ili kuongeza chochote ambacho kitaweza kuwasaidia hawa wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nashukuru sana. naomba sasa nimwite Mheshimiwa Subira Mgalu, nadhani ndiye atakuwa msemaji wetu wa mwisho leo.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa na mimi leo niweze kuchangia Muswada huu muhimu unaohusu masuala ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama ambavyo walitangulia kusema wenzangu, mifuko hii ina umuhimu mkubwa hasa kwa ustawi wa jamii ambayo inachangia mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niipongeze kazi nzuri inayofanywa na mifuko hii ya jamii, niwapongeze

Wakurugenzi Wakuu wa Mifuko hii, bodi zao na niipongeze Serikali kwa kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa mifuko hii. Nimpongeze pia Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo mama Irene kwa uteuzi wake na ninaamini kupitia Mamlaka hiyo ya Usimamizi wa Mifuko hii ni wazi kabisa wanachama wa mifuko hii watafaidika kwa huduma ambazo zinatolewa na mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza kwa dhati kabisa Kamati yako kwa kupitia Muswada huu na kwa kweli niungane na wenzangu waliosema kwamba mmefanya kazi nzuri na maeneo mengi ambayo mmeshauri kwa namna moja au nyingine ni wazi kabisa itasaidia sana kuona kwamba mifuko hii inawajibika kwa wachangiaji wa mifuko hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza sana katika kfungu cha 18 ambacho kinafanya marekebisho ya kuwezesha kwamba wanachama wa mifuko hiyo wanaochangia kwamba mifuko hiyo iweze ku-*refund* wanachama ambao wamelipa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na maoni ya Kamati yako kwamba isiangalie upande mmoja tu kwamba mifuko imelipa zaidi kwa wanachama ambao wamestaafu iangalie pale ambapo pia wanachama hao wanalipwa pungufu. Kwa sababu imekuwa ikijitokeza mara kwa mara hata kwenye hoja za ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba kuna watu wanaolipwa zaidi lakini kuna watu wanaolipwa pungufu.

Kwa hiyo, niombe kwamba kifungu hiki kiangalie pia endapo mwanachama analipwa pungufu na yeye apate haki ya kurudishiwa na pia apate haki ya kulipwa na *interest. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika Muswada huu kifungu Kifungu cha 21 ambavyo vimeongelea namna gani

mifuko hii iweze kuwekeza katika miradi mbalimbali ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kuleta faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili na mimi niungane na Wabunge wenzangu kuipongeza mifuko hii katika uwekezaji wa maeneo mbalimbali ambayo yameweza si kusaidia tu katika kuleta huduma lakini pia imesaidia kuona kwamba mifuko hii inaweza ikiwezeshwa. Kuna uwekezaji uliofanywa *UDOM* kama wenzangu walivyosema, kwenye jengo hili ambalo tupo na maeneo mengine ambayo yanachangia kwenye huduma za jamii tumeona maeneo ya shule mifuko hii inachangia, lakini tumeona mifuko hii inajenga majengo ya kitega uchumi, kwa mfano *LAPF* imejenga *Millenium Tower. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kushauri kwamba ifike wakati sasa zitolewe taarifa ni namna gani mifuko hii inasaidia wanachama katika michango yao na siku ya mwisho katika mafao yao wanayopata na ninaamini mamlaka hii ambayo imeundwa kudhibiti hii mifuko itakuwa inatoa taarifa kila mwaka kuona maeneo ambayo mifuko hii imewekeza imechangia kiasi gani kupanua wigo wa huduma zinazotolewa na mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe pamoja na kuipongeza mifuko ya *NSSF, LAPF, PSPF* na mifuko mingine lakini ufike wakati sasa mwanachama wa kawaida anapoyaona yale majengo anapoona ule uwekezaji unaofanyika pia na yeye ajivunie kwamba uwekezaji huu umefanyika kutokana na pesa ambayo nimechangia na mimi kama mwanachama wa kawaida nitafaidika vipi na uwekezaji huu. Lakini hali ikiendelea kwamba majengo ni mengi, kweli uwekezaji unatusaidia kwa namna moja au nyingine lakini kama mwanachama wa kawaida ambaye ndiyo anatoa mchango wake hajui ni namna gani atafaidika na uwekezaji huo inaweza ikavunja moyo wachangiaji wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kifungu hicho cha 21 na 62 katika hii Sheria kumeweka pia kifungu ambacho kitatoa adhabu endapo bodi au mtu yeyote atawekeza kwenye maeneo ambayo yanaweza yasiisaidie shirika hilo au isisaidie kwa ujumla wake faida ambayo itapatikana katika uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapendekeza kwamba inaonekana kama kile kifungu ile adhabu labda mtu atapewa penati naona kama ni ndogo kwa sababu tumeshuhudia uwekezaji wa mabilioni, tunazungumzia uwekezaji wa mabilioni kuanzia bilioni 100, bilioni 50, kwa hiyo, nilidhani mtoa hoja akija pengine katika labda marekebisho ambayo ameleta kwamba kiwepo kifungu ambacho kwa kweli itaonekana kama ni adhabu stahili inayoendana na uwekezaji uliofanyika. Lakini tukiacha kwamba atapewa labda adhabu au atawajibika nadhani itakuwa hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na maoni ya Kamati yako na Wabunge ni namna gani kwamba ifike wakati Serikali yetu sasa itathmini maoni haya ya Wabunge ya kwamba hii mifuko ni lazima iwajibike kwenye Wizara moja kuliko ilivyo sasa *NSSF* ipo Wizara ya Kazi na Ajira, *PSPF* ipo Wizara ya Fedha, *LAPF* ipo TAMISEMI, kwa kweli kama tumeunda Mamlaka ya Udhibiti ambayo itadhibiti hiyo mifuko yote na mamlaka ipo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira basi hiyo mifuko iwe chini ya Wizara ya Kazi na Ajira lakini siyo ilivyo hivi sasa kwamba *DG* mwingine atawajibika kwa Waziri wa Fedha, mwingine atawajibika kwa Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilikuwa naona katika mapendekezo ya *schedule of amendment* ya mtoa hoja ni kwamba katika kifungu cha 81(a) kwamba kuna *obligation* ya *employer* ndani ya miezi sita ahakikishe huyu mstaafu analipwa mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Stella Manyanya kwamba ni ukweli ulio wazi kwamba tatizo la kulipa mafao kwa wazee wetu wanaostaafu wanapata shida sana. Mtu anastaafu, taarifa zake zipo wakati wa kupeleka michango hakuna tatizo, lakini pale anapostaafu sasa na *notice* imeshatolewa na mwajiri ameshapeleka kwa mfuko husika kwamba ndani ya miezi sita mtumishi wangu fulani atastaafu, tatizo linakuja akishastaafu kufuatilia malipo yake, kwa kweli wengi wanakufa wanaacha mafao hayajalipwa na inachukua muda mrefu wanafuatilia, gharama zinakuwa kubwa ambazo hazijumuishwi kwenye malipo yake, kwa hiyo, niombe kwa kuwa kifungu hiki kimewekwa na adhabu imewekwa pengine ya kulipa *interest* lakini Serikali ifuatilie kwa makini Wizara kwamba mamlaka hiyo ya usimamizi wa haya Mashirika ya Hifadhi ya Jamii ni namna gani tutawawezesha wastaafu wetu, hiki kifungu kifuatiliwe kwa makini. Ndani ya miezi sita walipwe pesa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni kama vile mtu ambavyo unawekeza pesa zako benki unategemea kwamba zile ni za kwako umekatwa kwenye mshahara wako, kwa nini ichukue muda zaidi ya mwaka mmoja, miaka miwili mpaka watu wanapoteza maisha hawajalipwa fedha zao na wale warithi wanachukua muda mrefu sana, kwamba mara barua ya ajira haionekani, kwa hiyo, tuone ni nani anastahili kuadhibiwa katika wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nipongeze tu kwa Muswada huu na niamini kwamba wastaafu wetu kwa namna moja au nyingine au hata sisi wachangiaji wa mifuko hii kwa namna moja au nyingine tutafaidika. Nashukuru kwa fursa hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola dakika zilizobaki 10 zinakutosha?

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikaenda haraka haraka.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hii mifuko ni mifuko inayolenga wanachama ambao wamejiunga na mifuko hii. Mimi nina maombi machache au ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameshaongea kwamba kuna urasimu mkubwa sana katika uchukuaji wa fedha kwa wadau wanachama, unaweza ukaona mtu anafuatilia michango kama Wajumbe walivyosema kwamba inaweza ikazidi hata miaka miwili, sasa baada ya kugeuka kwamba anapata faida sasa anapata adhabu.

Sasa naomba wale ambao wanasimamia mifuko hii lazima wafuate sheria ambayo imewekwa na mwanachama akibainika kwamba anachukua muda mrefu akiwa anafuatilia haki yake basi sheria ichukue mkondo wake kwa yule mtu anayehusika kumcheleweshea mtu mchango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nilikuwa naomba kwamba hii mifuko inaonesha kwamba ni faida kwa wanachama, kwa nini wasianzishe *system* ya *ATM* kwa mfano mtu amechangia miaka mitano na fedha yake ile kabla hajafa anapenda aweze kupata faida mapema, awe ana-*access* kwenye *ATM* anaweza akawa ana kadi akaenda hata benki akachukua pesa yake ile, badala ya kwenda kufuatilia miaka mingapi, anapoteza muda mrefu mtu anaumwa au ana mgonjwa hospitali mpaka afuate zile *procudures* za kujaza fomu matokeo yake inakuwa ni usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba kwa sababu ni fedha ya wanachama mtu amejiwekea fedha yake pale, basi aruhusiwe kuchukua kwenye *ATM* na atumie *ATM card* kama tunavyochukua fedha benki, hii itasaidia sana kwa wananchi ambao ni wanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeongelewa hapa ni suala zuri sana. Kwa mfano, mifuko hii kama itatumika kuwalipa wazee wale ambao wamestaafu na wazee wengine ambao wapo vijijini wanakuwa na maisha magumu sana, itakuwa ni kitu cha maana sana kwa Watanzania wetu kuwasaidia, kwa sababu kwenye vijiji vyetu kuna wazee wengi sana wanashindwa hata kujenga nyumba, hata maisha ya kawaida tu wanashindwa. Kwa hiyo, hii mifuko kama itatumika italiona hilo itawalipa wale wazee tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia wenzetu nchi zilizoendelea ukizingatia kwamba kuna watu wengine hata vijana wanaotembea mitaani hawana kazi wanalipwa pesa, sasa sisi kwa nini tushindwe kuwalipa pesa wazee waliostaafu wapo majumbani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo naliomba kwa wale ambao wanasimamia mifuko waweze kuliangalia hilo kwa undani na waangalie sheria kama wataweka kwenye sheria ya kuwalipa wazee watakuwa wamesaidia sehemu kubwa sana ya wazee wetu ambao wapo hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hii mifuko kama itasaidia pia kutoa mikopo kwa mfano wale wanachama, mtu anashindwa kwenda kukopa pesa benki basi anaweza kukopa katika mifuko hii, mifuko hii huwa inatoa mikopo lakini inatoa mikopo kwa watu kadhaa, kwa wale watu ambao wanafanya biashara kubwa, mifuko itoe mikopo kwa mwanachama yeyote ili mradi anataka kuchukua mkopo, kusiwe na ubaguzi, isiwe inaangalia mtu fulani kwa sababu yeye ni tajiri ndiyo

anapewa mkopo, mwanachama yeyote aruhusiwe kupewa mkopo katika mifuko hii, hii itasaidia sana. Sasa ikitokea kwamba mwanachama anaenda kuomba mkopo na sheria inasema mwanachama yeyote anaruhusiwa kupewa mkopo halafu asipewe mkopo basi sheria imlinde huyu ambaye hapewi mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba hili nalo liangaliwe katika sheria kwamba kwenye mifuko yoyote ile, basi mwanachama kama ameomba kuomba kupewa mkopo apewe mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nimeona kwamba kuna wanachama wengi wamejiunga kwenye mifuko mbalimbali, kwa mfano mtu anakuwa kwenye mfuko wa *LAPF* anakuwa kwenye mfuko wa *PPF, NSSF* sasa kufuatana na mishahara yetu hii midogo unaweza ukaona mwisho wa mwezi anakatwa anabakia labda na kitu kidogo sana anashindwa kuishi, mifuko iwe na sheria. Kwa mfano, mtu amejiunga *NSSF* au amejiunga *LAPF* basi asiruhusiwe kujiunga na mfuko mwingine, kwa sababu *at the end of the day* anakuja kupokea mshahara ambao hawezi kuishi kwa muda wa mwezi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nimeiona kwa mfano kwenye makato sasa hivi *payee* yetu makato yaani kodi ni kubwa, sasa akikatwa kodi, akatwe kwenye mfuko wa kawaida na akiwa na makato zaidi ya matatu unaweza ukaona yule mwanachama anapotoka pale mwisho wa mwezi hana fedha ambayo inaweza ikamsaidia kwa mwezi mzima. Matokeo yake ndiyo wanaanza tena kwenda kukopa kwenye mabenki anaingia kwenye mikopo ya vikundi, anaingia kwenye mikopo ya ajabu, ajabu na baadaye anakuja kuuziwa nyumba yake, hii tumeiona vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba mifuko iwe na masharti inayosema kwamba kama mtu amejiunga kwenye

mfuko mmoja asiruhusiwe kujiunga kwenye mfuko mwingine, hii itasaidia katika maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu niishie hapo, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kutumia muda vizuri na kutusaidia kuongeza idadi ya wachangiaji wa leo jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, labda nimtangaze mchangiaji wa kwanza tutakaporudi saa kumi na moja jioni ili kusudi aweze kujiandaa, tutampa nafasi Mheshimiwa Halima Mdee, halafu tutaendelea na Mheshimiwa Kibona na wengine watafuatia, kwa hiyo, naomba Makatibu muiweke hiyo orodha yangu vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wapo wengi lakini nadhani tutapata nafasi sana sana labda watano ama sita kadri ya atakayekaa kwenye meza atakavyoona, anaweza kutayarisha muda wa kutosha wa kupitia kwenye vifungu kwa sababu Muswada wenyewe kwa kweli ni mkubwa na jedwali la marekebisho pia nalo ni kubwa, tunaishukuru Serikali baada ya kufanya *consultation* ya muda wa kutosha na Kamati wamekuja na jedwali kubwa sana ambalo limeboresha sana Muswada. Kwa hiyo, nadhani tutahitaji kuwa na muda wa kutosha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo *Presiding Officer* atakayekaa hapa mezani anaweza akaangalia aongeze wachangiaji wangapi na tupate muda wa kutosha wa kutupitisha kwenye vifungu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana kwa *session* hii ya asubuhi, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuweza kupata nafasi ya kuchangia. Lakini awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza Wabunge wawili wa Chama cha CHADEMA walioapishwa jana. Pongezi zaidi ziende kwa wananchi Arumeru ambao waliona kwamba inawezekana kabisa katika uchaguzi mdogo kuchagua Chama cha Upinzani na kuweka historia katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwanza kwa kupongeza kwa kiasi fulani marekebisho ambayo yameletwa na Serikali asubuhi, marekebisho ambayo yamefanya *schedule of amendment* za kwangu nizitoe kwa sababu kimsingi yalikuwa yanalenga katika maeneo hayo hususan suala la utatu, lakini kubwa zaidi kuweza kuingiza tafsiri ama kuweka tafsiri pana ya mfanyakazi kwa kuchukua tafsiri ya *presumption to who is an employee* kama ambavyo imeelezwa kwenye *Labour Institution Act 2004*.

Kwa hiyo, hili suala ni jema sana kwa sababu hii sheria imeelezea kwa mapana mfanyakazi ama mtu anaanguka katika kundi la wafanyakazi kama mazingira kadha wa kadha ambayo yameainishwa kwenye sheria husika yatafutwa na Vyama vyetu vya Wafanyakazi kama vikitekelezwa wajibu wao ipasavyo kwa kuweza kuangalia tafsiri ya Sheria hii ya mwaka 2004. Tafsiri hii inaweza ikasaidia kwa kiasi kikubwa sana kuwawezesha watu mbalimbali ambao wanatumikishwa Tanzania, lakini kwa kuwa hawajui Sheria wanakuwa hawapewi au michango yao haiwasilishwi na waajiri katika hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwa hiyo, ni badiliko pana na ambalo nadhani litaangalia maslahi mapana ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa badiliko ambalo lilikuwa haliko kabisa mwanzo la kipengele cha tano (5) cha Sheria ya *PPF,* 372 ambacho kilipanua wigo vile vile kuweza kuruhusu mtu ambaye labda alifukuzwa kazi, kakosa ajira kwa kipindi cha muda fulani lakini akipata ajira nyingine kumwezesha sasa yeye kuendelea na michango kama kawaida, kitu ambacho kilikuwa hakijawa *aware addressed* kwenye hii sheria na vile vile kilikuwa hakijazungumzwa kabisa kwenye sheria iliyopita. Kwa hiyo, kwa ufupi Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni; kwa hivi vitatu mmewatendea haki kidogo wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye mchango wangu. Kwanza ni hiki kipengele cha 29A, kipengele ambacho kimezungumzwa kwa kina sana na maelezo ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni na ni kipengele cha 29A kipengele kipya ambacho kinaongezewa kwenye kile kipengele cha mwanzo cha 29 katika Sheria ya msingi. Kipengele hiki pamoja na mambo mengine kinahusu mgawanyo wa pensheni wa mwanachama aliyefariki kwa watoto wake, mke, mume ama warithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikisoma huu Muswada naona kwamba, tunataka ama kujikanganya na sheria nyingine ama kuingilia mamlaka nyingine ambazo zimepewa jukumu la kusimamia suala la mirathi. Kwa sababu nikisoma hii 29A inasema naomba kunukuu *the survivors pension payable to a dependant shall be made on the base of percentage prescribed here in namely (a) in the case of a widow/widower 40% of the pension and where there are more than one widow the amount shall be divided equally amongst the widows.* Hii inaendelea kipengele (a), (b), mpaka (e) kutegemeana na mazingira mbalimbali ya watu ambao wanaainisha.

Sasa sote tunajua kwamba Sheria ya Mirathi ama masuala ya urithi yamekuwa *governed* na Sheria ya Mirathi ambayo ni Sura namba 352 na sheria husika inaeleza bayana

kabisa ni taratibu gani ambazo zinatakiwa kuchukuliwa pale ambapo mtu amefariki. Naamini kabisa, michango yote pasipo kujali yako katika mfumo gani wa mafao ni mali ya mchangaji na siyo mali ya shirika kwa mantiki ya kwamba mchangaji anatoa *percentage* yake, mwajiri naye anatoa *percentage* yake. Sasa sheria kuweka moja kwa moja kwa namna gani michango ya hawa watu inatakiwa igawanywe inakiuka Sheria ya Mirathi kwa sababu imetamka bayana:-

Kwanza, imetamka mamlaka ambazo zina jukumu la kushughulikia masuala ya mirathi, mamlaka ambayo ni Mahakama ya Hakimu Mkazi na vile vile ni Mahakama ya Wilaya kutegemeana na kama mtu aliyekufa, alikufa ndani ya *jurisdiction* ya Wilaya husika lakini vile vile mali zikiwa hazina thamani kubwa sana. Lakini vile vile tunajua Sheria yetu ya Mirathi kwa kufahamu kwamba Watanzania wana imani mbalimbali wengine wanaamini kimila, wengine wanaamini katika dini ya Kikristo, wengine wanaamini katika dini ya Kiislam, imeweka mazingira gani yatumike ili mali za marehemu zilizobaki *whether* ni majengo ama ziko kwenye mifuko ya pensheni ama ziko kwenye mabenki zinagawanywa kwa utaratibu gani. Sasa nadhani tukiruhusu hiki kifungu cha 29A kiwepo, tafsiri yake ni kwamba, tutajikuta tunaingilia utawala binafsi wa watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kifungu chote cha 29A *unless* kama Waziri, Mwanasheria Mkuu na Naibu Waziri watakuja na maelezo ya kuweza kuweka hiki kifungu vizuri ili kieleweke, sidhani kama kina manufaa. Kitu pekee kinachoangaliwa na Mahakama ni *will* mwenye mali amependekeza nani arithi mali zake, ndio kitu cha msingi kinachoangaliwa na wakati ikiwa katika utaratibu wa kugawa mali za marehemu. Sasa kama mahakama ndio imepewa na katika ile Sheria ya Mirathi *will* ndio kitu cha kwanza kinachoangaliwa tena maandishi, kama haipo ya maandishi *original, photocopy,* kama haipo *photocopy* basi ya maneno, lakini inayoendana na ushahidi wa ziada. Sasa tukiingiza

vipengele kama hivi tunaweza tukajikuta vinaleta utata wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba pamoja na busara iliyotumika nilikuwa nashauri kifungu cha 29A cha *Local Authorities Pensions Fund* kiweze kuondolewa ili tusiingie kwenye vita ambavyo havituhusu, vita vya kugawa mali za marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine nipongeze kwa mantiki ya huu Muswada ambao naamini kabisa utakuja kuwa sheria, madhumuni yake ni kudhibiti Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ni kitu chema kwa sababu tunajua Mifuko yetu inatengeneza fedha nyingi sana, fedha ambazo ni makusanyo ya wafanyakazi katika mazingira mbalimbali. Lakini kwa kuwa wenzetu wana fedha ambazo zinakusanywa kwao wanaweza wakajikuta wanasahau na kuzitumia fedha kinyume na utaratibu. Ushahidi upo tumekuwa tukiona. Nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ya Mashirika ya Umma, Serikali ilichukua zaidi ya bilioni 800 kutoka kwenye haya mashirika mbalimbali kwa madhumuni ya kujenga *UDOM* lakini ilikuwa ni vita baina ya Kamati na Serikali za muda mrefu ili waweze kukubali kwamba hizo fedha zilitolewa na zilipokelewa na hivyo kuanza kulipa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali anazungumzia bilioni 58, hiyo ni hoja yake ya miaka minne iliyopita, ambazo zilichukuliwa na Serikali kutoka *PSPF* kwa ajili ya kupeleka kwenye Bodi ya Mikopo Tanzania kuweza kuwalipa wanafunzi, hadi leo mwaka sijui wa tano zimelipwa sijui bilioni saba, zimebaki bilioni 51. Kwa hiyo hii Mifuko inakuwa *abused*. Tumesikia *NSSF* wanataka kufanya *project* ya umeme, hatukatai; tumesikia *NSSF* inataka kujenga majumba, hatukatai; tumesikia *PSPF* wanataka kujenga majumba hatukatai, lakini la msingi ni kujiuliza haya majumba yanayojengwa, hizi *project* zinazotengenezwa kila mwaka kwa sababu ukisikia kitu hiki NSSF, je, zinalipwa kwa wakati, zina

faida ya haraka? kwa sababu tumeshindwa ku-*generate funds* kwa kukusanya mapato tunageuza hii Mifuko ambayo ni ya akiba ya wafanyakazi maskini kuwa sehemu ya kutatua matatizo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Kigamboni ni busara, lakini kweli *project* ya dola milioni 130 *NSSF* inashirikiana na Serikali tena *NSSF* inatoa fedha nyingi zaidi, hili daraja litakuja kulipa lini shirika lipate faida ili wafanyakazi ambao wamedunduliza waweze kuja kupata faida? Kwa hiyo, nadhani kuletwa kwa huu Muswada itakuwa ni njia madhubuti ya kudhibiti watu ambao wanaona wana hela nyingi zimewazunguka lakini wana *abuse*. Inawezekana kabisa *in the long run project* ambazo wameingia kwa sababu walikuwa hawana watu wa kuwadhibiti, zikafa na wafanyakazi wakashindwa kupata faida iliyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisema kuna watu walifanya *actual evaluation* ya haya mashirika, kuna shirika moja la Serikali liliambiwa uhai wake *(life span)* yake ni 2018, Shirika la Serikali. Mashirika mengine makubwa tu *life span* zao zilikuwa ni ndogo, kwa nini, kwa sababu wanawekeza katika miradi ambayo tija yake haionekani moja kwa moja. Kwa hiyo, nadhani ni busara, tunaambiwa wenzetu tena wanataka kujenga majumba huko Ubalozi wa Kenya, sijui Rwanda, sijui Sudan, jamani tusipoangalia hii Mifuko yetu inaweza ikaathiri wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba watu ambao wamepewa dhamana licha ya hii sheria kuwepo, tuhakikishe kwamba sheria inatekelezwa ipasavyo ili tuweze kulinda maslahi ya wafanyakazi. Naomba nipatiwe ufafanuzi wa kutosha kuhusu kifungu cha 29A ili isije ikawa inaingilia sheria nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Lakini naomba vile vile nipate maelezo ya kina sana kutoka kwa Serikali. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kidogo katika Muswada ulioko mbele yetu. Nianze tu kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. Naunga mkono hoja kwa sababu mapendekezo mengi yaliyoko katika mabadiliko yaliyoko mbele yetu ni mazuri hasa hasa la udhibiti wa Mifuko hii unaopendekezwa kufanywa na hii *SSRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho mazuri yaliyowasilishwa asubuhi na Waziri, yako maeneo bado ambayo nadhani yanapaswa yaangaliwe kwa makini zaidi ili kweli nia ya Mifuko hii kutoa mafao bora kwa wachangiaji wake iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya Mifuko hii huko nyuma inasikitisha kwa sababu wachangiaji wengi mara wanapostaafu mafao yao yamekuwa yale yale hayabadiliki kwa maisha yao yote mpaka wanafariki. Hili ni tatizo ambalo lazima hapa niweze ku-*declare interest* kwamba lilimkumba marehemu baba yangu nikiona waziwazi namna hii. Amechangia vema tu kama mtumishi lakini uchumi ulipoanguka na shilingi yetu kupoteza thamani kiasi alichokuwa anapata hakikubadilika, akaendelea kiasi hicho hicho na sisi tukawa maskini wa kutupwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili naomba katika mabadiliko haya liwekewe kabisa utaratibu kwamba, ni lazima uwepo utaratibu wa ku-*index* hiyo *pension* kutokana na *devaluation* inayotokea kwenye sarafu yetu. Mungu akitujalia na sisi fedha ikaanza ku-*gain* sheria iliangalie hivyo pia kwamba fedha iki-*stabilize inflation* ikawa ndogo basi na mafao kwa wastaafu yawe yanakwenda sambamba. Natoa mfano tu mtu aliyekuwa analipwa pensheni ya shilingi 15,000

mwaka 2000 kwa sheria ya sasa anaendelea kulipwa hiyo hiyo 15,000 mwaka 2012, hiyo shilingi 15,000 ukilinganisha na 15,000 mwaka 2012 ni kichekesho kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba la kwanza, Sheria hii Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha labda aone ni utaratibu gani unaweza kuwekwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, fedha watakayokuwa wanalipwa wastaafu iwe inayowawezesha kukidhi maisha yao. Napendekeza kama itaonekana inafaa basi iwe asilimia 40 ya mtumishi mwenye ngazi ile ile ya mshahara aliyoko kazini wakati huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia muda unaopendekezwa wa uhai wa mstaafu unaotarajiwa kitu kinaitwa *commuting factor* kwa sasa ni mdogo sana ukiangalia pamoja na kwamba *life expectants* ya Mtanzania imeshuka kwa sababu ya matatizo haya ambayo wote tunayafahamu. Lakini hatuwezi tukaishi kwa mashaka tu namna ile, lazima tuwe na utashi wa kuamini kwamba maisha yetu yataboreka, haya matatizo yaliyopo yanayosababisha ile *life expectants* kushuka yataongezeka na kwa uchache basi *commutting factor* iwe angalau miaka 15, kwamba *at* 60 mtu akistaafu tutegemee tu kwamba *minimum* ataishi miaka 15 au 16 zaidi. Kwa sasa ni miaka minane sijui, ambayo ni kidogo sana. Watu wengi kwa kweli baada ya hapo hesabu ile inapunguza fao lao kwa sababu *commutting factor* inayotumika ni ndogo katika ukokotoaji wa pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linasikitisha pia katika sheria hii na halijafanyiwa kazi vizuri pamoja na mabadiliko yanayopendekezwa, ni muda wa jumla wa mtumishi aliyefanya kazi. Nimemsikia dada yangu Halima analisema lakini kwa maneno mengine, wako watumishi wanaohama ajira kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Sheria haizungumzii kutambua utumishi wao katika nafasi mbalimbali walizotumikia alipokuwa labda Mwalimu

baadaye akabadilisha akaja kuwa Mbunge, akatoka Ubunge akaenda kuwa mtumishi sehemu nyingine, lakini huu wote ni utumishi kwa wananchi ambao unapaswa uzingatiwe mwishoni katika Mfuko atakaokuwa anachangia huyu wakati wa kukokotoa mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa, mtu akiwa mtumishi Serikalini, kwa mfano, bahati nzuri akateuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa, kama alikuwa anachangia Mfuko mmoja, hapo basi uchangiaji utasitishwa na kwa hiyo ataingia kwenye *scheme* ya mafao ya viongozi wa kisiasa. Kwa hivyo, kule anasimama, atakuja kulipwa kutoka Hazina atakapoondolewa au atakapostaafu katika utumishi huo wa kuteuliwa. Sasa huku alikokuwa anachangia anasimama, ile mita haiendelei tena kusoma, anasimamishwa pale huku akitumika miaka 20 au 30, atakuwa analipwa ile pensheni yake kutoka kwenye *scheme* hii, lakini mwishoni sasa akitimiza miaka 60 akarudi kwenye Mfuko aliokuwa akichangia, muda huo ambao amekuwa akitumika kwenye nafasi hizi za uteuzi na kwa maana hiyo kuhamishiwa katika Mfuko wa Mafao ya Viongozi wa Kisiasa, haujumuishwi katika kukokotoa mafao yake. Nadhani hii ni *anomaly* kubwa. Mtu huyu amepata heshima ya kuchaguliwa na wananchi au kuteuliwa na Rais, lakini mwishoni anapokuja sasa kustaafu sasa kwamba alipwe pensheni yake, hayo yote yanasahaulika, muda huo wote unasahaulika na kwa hiyo hauingizwi katika kukokotoa mafao yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo waathirika wa hili, japo sipendi kusema kwamba, mimi ni mmoja wapo, lakini wako watu wengi ambao hili jambo limewagusa na kwa kweli pensheni sasa watakayokuwa wanapata ni ndogo mno kulinganisha tu hata na mishahara ile waliyokuwa wanapata wakati wakiutumikia umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo yaliyopo mezani mojawapo ni namna ya uendeshaji wa Mamlaka ya

Udhibiti. Inapendekezwa kwamba, Mamlaka iwe inapata asilimia kadhaa kutoka kwenye Mifuko hii ili iweze kujiendesha. Nashauri kwamba mifuko inazidi kupanuka, kwa maana wanachama wanakuwa wengi zaidi kwa sababu uhamasishaji wa kuingiza *the private people* na nini ni mkubwa sana. Sasa kwa asilimia iliyotajwa, ile mamlaka ukiiangalia ilivyo ndogo kwa muundo, asilimia iliyotajwa ya tozo kwa Mifuko yote hii ni *billions of money* na hawa watu sio wengi wa ku-*warrant* matumizi yote makubwa ya pesa namna hii. Hii pesa ndugu zangu kama wachangiaji wengine walivyosema ni fedha ya wanachama waliochangia, sasa isije ikawa tumetafuta tu tena nafasi ya kumfanya mtu mmoja au watano, thelathini, hamsini waogelee katika fedha *on the expense of the members* wa hii Mifuko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kuna woga gani kwamba Mamlaka hii isiendeshwe tu kwa bajeti ya Serikali ya kawaida. *Yes* kuna wanaodhani kwamba kupitia bajeti huenda isiwe na fedha ya kutosha, lakini watumishi wengine wa Serikali wanaishi kwa bajeti hii hii tunayo-*approve* hapa Bungeni. Hii ni Mamlaka tu ya udhibiti na bahati mbaya sana hii Mifuko lengo lake ni kuboresha mafao, sisi tungependa kuona wanafika mahali siku moja wanasema mstaafu atapata asilimia 80 ya mshahara aliokuwa anapata wakati anastaafu, badala ya kuelekeza pesa kwenye mishahara na mambo mengine kwa mamlaka ya udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu wasinielewe vibaya, lakini nadhani kama ni *percentage* basi ishuke au vinginevyo tuwapeleke tu kwenye kuhudumiwa na Wizara moja kwa moja. Walipwe tu kama mamlaka zingine zinazoendeshwa kwa usimamizi wa Wizara moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezekano wa hii mamlaka kudhibiti Mifuko ni mkubwa sana. Iko *debate,* najua watu wanazungumzia kwamba labda tuwe na aina tu mbili za Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kwamba Mfuko wa watumishi wa

Serikali na Mfuko wa watumishi wasiokuwa wa Serikali. Lakini nadhani huko sio pazuri sana, tuiache tu mifuko i-*operate* kama ilivyo, washindane na kwa sababu naamini katika ushindani ndiyo watumiaji wananufaika zaidi, lakini mamlaka kama inavyopendekezwa kwamba na yenyewe sasa iweze kufanyafanya aina fulani za biashara, sioni kama hili ni jambo la busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wabakie na kazi yao ya udhibiti, wasitumbukie kwenye shughuli ambazo zinaweza kuwaweka kwenye ushindani na watu wanaowadhibiti. Habari ya kusema watajihusisha na wao kununua *Treasury Bills* sijui nini huko, *shares* kwenye *market* na nini? Hapana, hiyo iachwe iwe kazi ya Mifuko ile kuboresha mafao, kupanua Mifuko yenyewe na wao wabaki kuangalia kama hizo *activities* zinazofanywa na Mifuko ni sahihi na zinalenga kweli kuiboresha kwa manufaa ya wachangiaji katika mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kengele ya pili inikute. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada huu ulioko mbele yetu. Kwa mujibu wa kanuni ingawa si kwamba nina maslahi binafsi ya Muswada huu, lakini naomba tu niseme mengine nitakayoyasema yanaweza kugusana moja kwa moja na yale ambayo tumekuwa tukiyajadili kwenye Kamati. Kwa hiyo, napenda tu kwa mujibu wa kikanuni, ili nijiweke vizuri ni kwamba, Muswada huu umejadiliwa sana katika Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni tabu na sidhani kama nakatazwa kwanza kabisa kwa kweli kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati tulioshirikana katika kufanya kazi hii ya kuchambua huu Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge kwa kweli niwashukuru wale walioliona hili na kweli Kamati imefanya kazi kubwa sana na ndiyo maana hata unaona ile *schedule* ya *amendments* lile jedwali la mabadiliko limekuwa kubwa na hii imetokana na kazi nzuri iliyofanywa na Kamati kwa kushirikiana na wadau kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, pia nawashukuru sana wadau wote kwa kazi kubwa waliyoifanya ndani ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa asilimia kubwa unaona Serikali imesikiliza kwa kina yale ambayo tulidhani yakiletwa katika sheria hii, yatasaidia sana kuboresha sekta hii ya hifadhi ya jamii. Mwaka 2008 Bunge hili Tukufu lilitunga hiyo Sheria Na. 8 ya mwaka 2008 ambayo iliunda mamlaka ya udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii. *The Social Security Regulatory Authority.* Baada ya mamlaka ile kuundwa, ni takriban sasa miaka kama miwili, mitatu imepita, tumeona kabisa kwamba mamlaka hii kwa Sheria ile Na. 8 ilikuwa imepewa kazi muhimu sana kwa Taifa letu la Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hifadhi ya jamii, katika nchi yetu ya Tanzania, ni suala ambalo kwa mtazamo wa ulimwengu wa sasa ni lazima lipewe kipaumbele. Kwa hiyo, kuwepo kwa hii mamlaka, kunasaidia sasa Mifuko hii itekeleze wajibu wake kwa kuona umuhimu wa yale ambayo wadau kwa maana ya wachangiaji wa Mifuko wanayategemea kutoka kwenye Mifuko yenyewe. Sasa ukiacha tu hii Mifuko inajiendesha yenyewe bila kuwa na kiranja wa kuwasimamia, unagundua kabisa kwamba wakati mwingine ndiyo hakuna ile *fair play*. Wakati mwingine hata ndani ya Mifuko hakuna haki kwa wale wachangiaji wa Mifuko wenyewe na umeona wafanyakazi wamekuwa na malalamiko ya hapa na pale, wengine wakiona wanapunjwa mafao yao hayaendi kadiri inavyotakiwa na wakati mwingine ile mikataba ya Kimataifa ambayo inatakiwa ifuatwe na Mifuko inashindwa kufuata kwa sababu hatukuwa na hicho chombo cha usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria hii leo inakwenda kusaidia kubadilisha zile Sheria zilizounda Mifuko ile yote na kuifanya sasa mamlaka ipate meno ya kuingia kwenye ile Mifuko, ili kwenda sasa kufanya kazi yake halisi ya kudhibiti Mifuko ile kwa manufaa ya wanachama wa Mifuko ambao ndiyo Watanzania wafanyakazi na sasa tunasema sekta isiyo rasmi na wenyewe watapata nafasi ya kuingia kwenye Mifuko hii. Kwa hiyo, kwa kweli naipongeza sana Serikali na naishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamezungumzwa na Kamati yangu na tumejadili kwa kina na kuomba marekebisho mbalimbali yaweze kufanyika katika Muswada halisi ulioletwa na kama nilivyosema kwamba mengi yamezingatiwa kwenye lile jedwali la marekebisho. Sasa nitajikita katika mambo yafuatayo na wakati mwingine naweza kusema kwamba ni mambo ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini naomba pia nikumbushe kwamba hoja hii ya pensheni kwa wazee si tu kama ni hoja ya Kambi ya Upinzani bali ni hoja ya Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii. (*Makofi*)

Kamati ya Maendeleo ya Jamii ukiangalia kwa takriban sasa miaka kama sita na ukifuatilia na mimi nashukuru nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Maendeleo ya Jamii huu ni mwaka wa saba. Kwa hiyo, naelewa Kamati hii imeshafanya kazi kwa kiasi gani kuhusiana na hoja ya pensheni kwa wazee. Sasa tulipokuwa tunaunda hii mamlaka, lengo letu lingine lilikuwa mamlaka hii itufikishe kule ambako tutaweza kuongeza uwanda au mawanda ya pensheni ili iweze kufikia kada za watu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nilipe taarifa Bunge lako hili, tulipoanza kufanya kazi ya ndani kuhusu pensheni kwa wazee, mamlaka ya udhibiti ikaanza kufanya kazi vizuri sana na

imeanza kufanya *study* vizuri sana. Lakini baadaye tulipomuita Mkuu wa mamlaka hii na Mwenyekiti wa Bodi, tuligundua mamlaka hii haina fedha za kutosha za kuweza kutekeleza majukumu yake, ikiwemo kumaliza kufanya *study* ya kuona ni namna gani wazee wataingizwa kwenye pensheni na kutekeleza majukumu mengine muhimu sana ya hifadhi ya jamii. Ndiyo maana leo naishukuru Serikali ilipotuletea kwenye Muswada kifungu ambacho kinataka ile Mifuko ichangie sasa *levy* kwa ajili ya kuimarisha mamlaka hii iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata sisi tuliona, hivi ni namna gani *levy* ile inaweza ikakusanywa kwenye Mifuko? Hofu yetu ilikuwa kumpa nguvu huyu mamlaka kwenda kuchukua fedha za wanachama kwenye Mifuko kwa ajili ya kujiimarisha, lakini baadaye tulikuja kukubaliana na tukaishauri Serikali. *Levy* hii ni muhimu, itamsaidia huyu mdhibiti kufanya kazi, lakini *levy* hii itokane na fedha zile za uendeshaji, *administrative cost* za kila Mfuko. Pia unapokwenda kuchukua fedha kwenye zile *administrative cost*, hu-*affect* kitu chochote katika mafao ya wanachama kwa sababu pesa ile uichukue, usiichukue tayari imeshakuwa *budgeted* kwa ajili ya masuala yake ya kiuendeshaji. Kwa hiyo, hata ukiichukua au usipoichukua ile itaendelea kutumika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona pale ukienda kuichukua ile ukampa nguvu huyu mdhibiti, akafanya hii kazi tunayoitaka, ikiwemo kazi ya kuhakikisha sasa tunaanzisha pensheni pia kwa wazee, unaona kabisa kwamba tutakuwa tumefanya jambo jema sana. Kwa hiyo, naomba niishukuru Serikali na nawashawishi Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli mamlaka hii ipatiwe fedha ili meno yake yaweze kufanya kazi ya kuweza kudhibiti Mifuko na kuhakikisha suala zima la hifadhi ya jamii katika nchi yetu linafanyiwa kazi ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia suala hilo la kuipa mdhibiti fedha, mdhibiti alikuja kweli na ile hoja kwamba

na yeye aanze kuwekeza. Ukiangalia katika suala zima la uwekezaji, kile kifungu cha 150(49) (a) (5), kifungu kile kwa kweli tulikubaliana kiondoke. Kwa sababu katika Sheria ile Na. 8 ya mwaka 2008, kifungu kidogo cha tano (5) kinatamka waziwazi kazi za mdhibiti, kazi za *SSRA*. Sasa ukienda kwenye kazi zile za *SSRA* hukuti kama ana kazi pia ya kujenga mapato ama kujenga uchumi zaidi ndani ya himaya yake kama mdhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuligundua kwamba, huyu mdhibiti akianza sasa kushughulika na uwekezaji, ile kazi yake ya udhibiti ataisahau, kazi ya kusimamia uwekezaji ni nzito kuliko hata hii ya udhibiti. Kwa hiyo, tukakubaliana na lazima mdhibiti abaki kudhibiti, masuala ya uwekezaji awaachie mifuko na yeye aende akaisimamie hiyo Mifuko ili uwekezaji ule uwe kwa manufaa ya wanachama na tumesema, tunamwomba Waziri aiangalie sasa *SSRA*, faida zinazopatikana kwenye uwekezaji ziwafikie wanachama na ziweze kuboresha pensheni zao mpaka angalau kwa asilimia 70. Kwa hiyo, hiyo ndiyo ilikuwa ni lengo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumegundua, wakati Mheshimiwa Rais anaanzisha Wizara ya Kazi na Ajira, aliondoa Idara ya Maendeleo ya Vijana akaipeleka kwenye Wizara nyingine. Sasa alipoanzisha Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Rais wakati anakabidhi kazi kwa Waziri mwenye dhamana, alimkabidhi jukumu pia la ulinzi na kuhakikisha kwamba suala zima la hifadhi ya jamii linawekewa mkazo. Lakini tunasikitika mpaka sasa hivi, Wizara haijaanzisha *directorate* katika Wizara yake inayohusiana na masuala ya hifadhi za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunaiomba Serikali, kama tunataka kwenda mbele kuboresha hifadhi ya jamii, *directorate* ya *social security* chini ya Wizara ni kitu cha msingi sana na nafikiri kabla mwaka huu haujaanza, tutataka kusikia Waziri ameshaanzisha Idara hiyo na inaanza kusimamia masuala haya ya social security ndani ya Wizara yake

vinginevyo, hata hii hoja ya kuirudisha Mifuko yote iwe chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, haitakuwa na msingi kama katika Wizara, hakuna kitengo kinachosimamia masuala haya ya hifadhi za jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba sana iletwe haraka hapa Bungeni sheria, ifanyiwe mabadiliko ya haraka kwa sababu Sera zote za Hifadhi za Jamii zinasimamiwa sasa hivi na Wizara ya Kazi na Ajira na ndiye huyu mwenye sera ambazo zinaweza kutafsiriwa na Mifuko. Sasa leo tunapoona Mifuko hii imetawanyika katika Wizara mbalimbali na anayesimamia Sera ya Hifadhi ya Jamii ni Waziri ambaye mwenye dhamana ya kazi na ajira na anaanzisha hiyo *directorate* ya *social security*. Nafikiri kwamba kuna umuhimu sasa kufanya mabadiliko na lazima Mifuko hii iwajibike sasa chini ya Wizara moja. suala hili sio la mchezo na naiomba sana Serikali na Kamati yangu sisi tumekubaliana huko mbele kwa kweli kama hili halitatekelezwa tutakuwa na ugomvi mkubwa sana. Kwa sababu ni suala la kimsingi, linalopelekea nia njema ya kuifanya Serikali isimamie ipasavyo sekta hii ya hifadhi ya jamii kwa manufaa ya wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri pia kuna umuhimu, wakati tukijadili kwenye Kamati tuliona pia kile kifungu cha 8(5) cha uanzishwaji wa mamlaka zile, kazi zilizotafsiriwa kwenye kifungu hicho kidogo cha namba 5, zinaifanya mamlaka ya udhibiti, itekeleze majukumu mengine ya kisera ambayo yanatakiwa kutekelezwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali, viko vifungu vidogo vitatu pale, kwenye jedwali la marekebisho vimeletwa, tutaviondoa vile vifungu na kuvirudisha Wizarani ili sasa mamlaka ibaki na kazi yake ya udhibiti na ile kazi ya kisera ya kuhakikisha sekta ya hifadhi ya jamii inakuwa nchini ibakie kuwa ni kazi ya Mheshimiwa Waziri na Wizara yake. Kwa hiyo, nadhani hilo pia ni badiliko lingine jipya ambalo ni badiliko la

kuwekewa nguvu. Tunashukuru sana Serikali imekubali na tunaamini kwamba badiliko hilo litasaidia sana sana kugawa haya majukumu kati ya Mamlaka ya Udhibiti na Wizara kwa maana ya kwamba ndiyo mwenye jukumu kubwa la kuhakikisha hayo yote yanakwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali kuhakikisha dhana ya utatu katika uwakilishi wa Bodi za Mifuko imezingatiwa na nashukuru sana Serikali kwa kukubali wenye Mifuko kwa maana ya dhana ile ya utatu, wafanyakazi, waajiri, lakini pia na Serikali yenyewe kuwa na uwakilishi wa Wajumbe wawili wawili katika kila Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tunalishukuru sana kwa sababu huwezi ukawa na nyumba yako halafu ukamwacha mtu mwingine akulindie hiyo nyumba. Fedha hizi ni za wanachama. Serikali ilipokuja na mapendekezo ya Wajumbe watano kwa maana ya wenye Mifuko kuwa mjumbe mmoja katika Bodi ilikuwa haitendi haki. Lakini tunashukuru sana tumeelewana na sasa wale wawakilishi wa waajiri lakini wawakilishi wa wafanyakazi watakuwa na uwakilishi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja itakwenda kuleta maendeleo makubwa sana kwenye Sekta hii ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. Sasa nitamwita Mheshimiwa Aliko Kibona na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Eugen Mwaiposa.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa ajili ya nafasi hii adimu. Kabla ya kuanza kuchangia Muswada uliopo mbele yetu napenda mapema kabisa niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia ku-*declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Kwenye mchango huu mashirika haya kwa sehemu yamefanya kazi nzuri na kwa hiyo nitahitaji kutoa pongezi. Natoa pongezi kwa Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka. Natoa pongezi kwa Kamati iliyoshughulikia na kuleta *amendment* mbalimbali ambazo nilipozipitia kwa kweli zimefanya Muswada uwe mzuri kuliko kawaida. Napenda nichukue nafasi hii kupongeza Menejimenti, Bodi za Mashirika mbalimbali za Hifadhi za Jamii, Wakurugenzi, watumishi na wafanyakazi wote katika Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii. Sote tumeshuhudia jinsi gani Mifuko hii imeweza kusaidia katika miradi mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nizungumze machache juu ya *Social Security Schemes.* Mtaalam mmoja alisema *a social security scheme is a job where you can work and an income when you can't work.* Sisi sote tulio watumishi baada ya muda tutakoma kufanya kazi. Tutahitaji kupata kipato cha kuishi. Hiyo ni kazi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa Tanzania iko mingi. Bahati mbaya sana haiwagusi wafanyakazi au watu ambao siyo waajiriwa. Haiwagusi kwa lazima wale ambao wamejiajiri wale ambao hawako katika utumishi wa Serikali. Nitoe mapendezo sasa kwa sababu Sheria hii nimeiangalia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye ushauri na mapendekezo mbalimbali kwenye sehemu ambazo nimedhani kwamba ni budi nichangie. Naomba Mifuko hii huyu R*egulatory* chombo hiki sasa kianze kujikita kushauri mifuko hii kushauri Serikali ione ni namna gani tunaweza

kuwashirikisha wafanyakazi kwenye sekta binafsi waliojiajiri. Mtu yeyote mwenye kipato sasa umefika wakati awe mwanachama wa Mifuko hii sio tena kwa hiari bali kwa lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja na mapendekezo kwenye idadi ya Mifuko. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ulimwenguni pote sana sana unakuwa Mfuko mmoja au miwili. Nilkuwa napendekeza Tanzania tuna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mingi mno. Wanasema ukitaka watu wawe wanyonge wagawanye kila mmoja awe kivyake. Mifuko hii tukishafanya ikawa mingi kiasi hicho haiwezi kufanya kazi sawasawa. Nashauri, Mifuko iwe miwili na huu ndiyo ukweli unaweza leo tukauacha lakini baada ya miaka kadhaa ijayo ukweli huo utaibuka, tutakapokuwa hatupo hapa watakaotubadili ni lazima watakuja kurejea kutaka au kuona haja ya mifuko hii kuwa miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Mfuko mmoja, *scheme* moja iwe ni kwa ajili ya *public sector, Government, Local Authorities* na mashirika ya umma. Nashauri Mfuko mwingine ushughulikie sekta binafsi, *NGOs, International Organization, Religions Organizations* na kadhalika hata watu binafsi mmoja mmoja mradi ana *income* aweze kuchangia kwenye Mfuko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ikishindikana kupunguza idadi ya Mifuko hii basi *Regulatory* wa Mifuko hii ahakikishe kwamba Mifuko hii inashindana kwa huduma na siyo kwa *pension.* Nashauri kwamba *pension* katika Mifuko yote *formula* iwe moja, *pension* zifanane isipokuwa zile huduma zingine zingine ziweze kutofautiana kadri Mfuko utakavyokuwa una-*perform.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze juu ya matibabu kwenye Mifuko hii kwa mfano, napendekeza, Mfuko wa *public sectors* ndiyo wanachama wake wachangie

*National Health Insurance Fund.* Huu Mfuko mwingine utakaoshughukia Sekta Binafsi ujikite uende mpaka vijijini kwa wakulima na uweze kusaidia matibabu na zile tulizoahidi hospitali au *dispensary* au zahanati kujenga kwenye vijiji zote zishughulikiwe na Mfuko huu kwenye sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena *Regulatory,* msimamizi huyu aangalie aweze ku-*harmonize pension* za *scheme* zote tulizonazo hapa nchini. Hatari yake ni nini, baadhi ya *scheme* hapa nchini mtumishi wake anapostaafu ile *package* ya kwanza anayoondoka nayo inaweza kufika hata milioni 50 hata milioni 40. Lakini kuna Mifuko mingine hapa hapa nchini mishahara ilikuwa ile ile lakini anapoondoka, kabla ya *pension,* anaondoka na milioni tano, milioni nne na kadhalika. Hii inaleta ugomvi kwa wafanyakazi kati ya Idara na Idara. Naomba tafadhali *Regulatory* ahakikishe kwamba ana-*harmonize pension* zake zilingane kwa Mifuko yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wengi Waheshimiwa wamechangia maeneo kadhaa, lakini nami nichangie pengine itakuwa sehemu ya usahihishaji au kuwekana sawa. Nimpongeze mchangiaji wa Kambi ya Upinzani, amependekeza *pension* angalau kima cha chini kiwe asilimia 70 ya mshahara wa mwisho wa mfanyakazi. Nakubaliana naye lakini nilifikiri kwamba isiwe hapo alipopendekeza, labda pia tuhame tuende kwenye asilimia 80 maana tayari tuna mashirika au tuna *scheme* ambazo *minimum pension* yake ni asilimia 80 ya kima cha chini cha Serikali. Kwa hiyo, ni vizuri tukaanzia hapo kwenda juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia pia mmoja wa wachangiaji pengine nilidhani niweke sawa hili. Alizungumza kwamba, ili upate matibabu kwa Shirika la *NSSF* kwa mfano, unapaswa kuchangia mchango kwa ajili ya matibabu. Ukweli, labda pengine niweke sawa. Ukweli ni kwamba ukiwa mwanachama wa *NSSF* ni sifa ya kupata mafao ya matibabu

katika *NSSF*. Kwa hiyo, hakuna michango kwa ajili ya matibabu ya *NSSF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Regulatory* atakapoanza kazi kwa Sheria hii atusaidie kwa wafanyakazi walioko Serikalini ambao kwa bahati kama ni wale walio *Member* wa *NSSF* wanakatwa asilimia tatu ya mshahara wao kwa ajili ya *NHIF,* Mfuko wa Bima ya Taifa. Nadhani kwamba umefika wakati kwa sababu wao ni *member* wa *NSSF* haina sababu tena kuumia kuchangia *National Health Insurance Fund* wakati tayari wana sifa ya kupata mafao ya *NSSF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia pia malalamiko kidogo juu ya gharama, watu kujilipa kwenye Mifuko hii *pension, no, no,* kujilipa bonasi na mafao na mishahara mizuri. Ukweli ni kwamba Sheria kwa mfano ya *NSSF* iko dhahiri kile kinacholipwa ni kutoka kwenye kiwango au asilimia iliyokubalika kisheria kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Mfuko. Moja ya jambo kabla sijamaliza ambalo nataka Waziri aelewe ambalo sijakubaliana nalo, ni ukomo au uteuzi wa Wakurugenzi wa Mifuko hii. Nimeambiwa pale ukifanya kazi miaka mitano Mkurugenzi, baada ya miaka hiyo mteuzi au mamlaka inayomteua ikiridhika kwamba anaweza kuendelea kuwa *CEO* wa Shirika, mwisho wa ukomo ni miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa, kama *CEO* wa Mfuko ana utalaam, ana juhudi, ni mahiri katika kuendesha Mfuko, kwa nini tumwekee *limitation* ya muda? Sasa tunataka kugeuza Mifuko nayo iwe kama ni siasa. Nadhani tuseme kwamba,mtu ambaye anaweza kuendesha Mfuko kwa mahiri na ukafanya vizuri aendelee mpaka pale ambapo yule mwenye mamlaka ya kumteua atakapoona inafaa vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishaanza kusema miaka kumi mwisho, nikiwa mahiri katika kuendesha Mfuko wa Bima ya

Afya eti niondoke kwa sababu nimefika miaka kumi, nadhani kwamba hapo tunahitaji maelezo na pengine marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani nichangie hayo machache, niweze kuruhusu wenzangu nao waweze kuendelea na hatua nyingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aliko Kibona. Sasa nitamwita mchangiaji wetu wa mwisho, naye ni Mheshimiwa Eugen Mwaiposa.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nishukuru kupata nafasi. Lakini pia niungane na wenzangu katika kuwapongeza sana Mawaziri pamoja na Watendaji na Serikali kwa ujumla. Pia nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati husika kwa jinsi ambavyo imeshughulika na mabadiliko ya Muswada ulioko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba sasa nichangie kile kifungu cha 13 cha Muswada. Lakini katika Sheria ya Mfuko ambayo imeongeza kile kifungu cha 27(A), kifungu ambacho kinasema kwamb, mtu anapokuwa amechangia kwa miaka 60 na akaendelea kuchangia baada ya kupumzika kufanya kazi, basi apewe bonasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki nimekipenda, lakini nilikuwa nategemea kwamba kije na ni kiasi gani sasa cha bonasi mtu huyu atategemea kutoka katika Mfuko. Lakini hata kama hakikuwa kwenye kiasi wangeweza wakatuletea hata kwa asilimia tu kwamba atapata asilimia ngapi ya kitu gani. Hiyo ingeweza sana ikawapa watu moyo, lakini kila mtu akawa anajua uwazi wa jambo lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kwamba mtu anachangia kwa miaka labda 30, nilitegemea kwamba, kifungu hiki kije na bonasi hata kwa wale ambao

wamechangia tu kwa umri huo wa miaka 60 bila kuangalia kwamba je, baada ya miaka 60 anaendelea au haendelei. Kwa sababu ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo wanachama wanachangia kwa kipindi kirefu hicho ni kwamba, fedha hizo zinawekezwa kwenye miradi mikubwa na ni miradi ambayo inaleta faida. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea kabisa kwamba, hata kama amechangia kipindi hicho kirefu bila kuendelea basi na yeye apewe bonasi. Lakini pamoja na bonasi hiyo nilikuwa nategemea tu kwamba, kuwepo na marekebisho ya kuwalipa wanachama *pension* yenye thamani ya hali halisi ya maisha ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumlipa mtu *pension* ya shilingi 50,000 ni hela kidogo ambayo haiendani kabisa na hali halisi. Lakini wakati alipokuwa anachangia wakati huo fedha hiyo ilikuwa na thamani. Sasa kwa sababu thamani ya fedha ya shilingi imeshuka tukiendelea kumlipa kwa kiasi hicho basi tutakuwa tunamfanya ashindwe kuishi kwa hicho ambacho anapewa. Lakini pamoja na hilo nilitegemea pia kuwa kipengele hiki kingekuja na malipo ya kuwalipa wazee ambao hawakupata fursa ya kuajiriwa, lakini walipata fursa ya kufanya kazi nyingine ambazo zilileta ufanisi mkubwa katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu haikuja, niombe sana Serikali na Waziri mhusika alichukulie jambo hili kwa umuhimu mzito ili wazee wote waweze kupata *pension.* Nafikiri jambo hili nililizungumza kwa kirefu sana mwaka jana wakati nachangia Bajeti ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie tena kifungu cha 49(A) ile sehemu ya (v) ambayo inazungumzia Mamlaka kupewa mamlaka au uwezo wa kuwekeza katika hisa au amana. Jambo hili limeongelewa na wazungumzaji wengi na napenda kuunga mkono kwamba mamlaka iendelee kudhibiti

na suala la kuwekeza liachiwe Mifuko ndiyo waendelee kuwekeza kwa sababu inakuwa ni vigumu sana mtu kuwa mdhibiti na hapo hapo kuwa mwekezaji au uwe unaweza kuwekeza zile fedha. Kwa sababu ikitokea wewe ukafanya kosa hakuna ambaye anaweza akakudhibiti. Kwa hiyo, huwezi ukawa unafanya shughuli wewe mwenyewe na kujidhibiti wewe mwenyewe. Lazima hapa kutakuwepo na *conflict of interest.* Kwa hiyo, naungana na wenzangu na kushauri Serikali kwamba wao wabaki kama wadhibiti na kazi ya kuwekeza basi iachiwe Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende tena kwenye kipengele kingine cha uwajibikaji wa Mifuko katika Wizara Tofauti. Jambo hili nalo limezungumziwa, naomba sana Wizara pamoja na Serikali iliangalie kwa umakini na ikiwezekana kabisa kwa kipindi kifupi liweze kupata ufumbuzi ili Mifuko hii yote iweze kuwa chini ya Wizara moja ili, hata huyu Mdhibiti ambaye tunamzungumzia iweze kuwa rahisi sana kwake kufanya kazi yake kwa sababu vyombo hivi vyote vitakuwa chini ya Wizara moja. Pia hata vyombo vyenyewe vitakuwa vinafanya kazi vizuri kwa sababu, vitakuwa vinawajibika katika Wizara moja na chini ya Katibu mmoja na wafanyakazi wote watakuwa wanawajibika kwa mwajiri mmoja. Kwa hiyo, naomba pia hili lipewe umuhimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia fursa ambayo Mifuko imepata ya kupata wanachama au kuchukua wanachama kutoka katika sekta zote. Hili ni jambo zuri na limezungumzwa, lakini naomba sana kwa sababu, litaamuliwa hapa, basi Mifuko hiyo sasa ianze kuandaa utaratibu wa kuwaelimisha wananchi wote wenye vipato vya chini, vipato vya kati, ili wote waweze kujua na waweze kukimbilia sasa hii fursa ya kuwekeza katika Mifuko hii. Pamoja na elimu hiyo basi, niombe sana kwamba kuwepo na utaratibu au *modality* nyingine ambayo itawafanya watu hawa waweze kupeleka fedha zao katika Mifuko hiyo, bila kulazimika kwenda Benki, kupanga foleni kwa ajili ya kuweka fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba, wangeweza wakatumia simu kwa kupeleka kwa *message* au wakatumia vyombo vingine kama *SACCOS* ambazo ziko vijijini ambazo ziko karibu zaidi na wananchi. Lakini pia, hilo naliacha kwa Mifuko hii, ili waweze kuandaa utaratibu mzuri wa wananchi wote kuweza kulipa fedha au kuchangia Mifuko hii bila usumbufu au gharama nyingine kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la taarifa kwa wadau; wadau wakubwa na wenye Mifuko ni wananchi, ni wajiriwa na sasa wanakuja wananchi wengine ambao hawajaajiriwa. Pamoja na utaratibu mzuri ambao Serikali inao wa kutoa taarifa kutoka kwenye Mifuko hii kupeleka katika ngazi mbalimbali za juu, naona kwamba, kuna umuhimu wa kuandaa tena mfumo mzuri wa kutoa taarifa kwa wadau ambao ni wachangiaji katika Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa si utawala bora, wananchi wanachangia kwenye Mifuko hii, lakini hawapati taarifa ya kwamba ni kitu gani kinafanyika ni kitu gani kimefanyika, hali ya Mifuko iko namna gani? Naomba, hata kwa mwaka mara moja, kuwepo utaratibu ili wachangiaji katika Mifuko hii waweze kujua kabisa kwamba, hali ya Mifuko iko namna gani? Mifuko imefanya nini na inafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, nilikuwa ni mtu wa mwisho, naona tu kwamba, haya niliyochangia yanatosha. Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi, lakini nashukuru pia kwa kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwaiposa. Sasa kwa wachangiaji basi ndio tunaishia hapo, wale ambao wamekosa, basi tusameheane maana muda wetu hauwezi

kutosha, Muswada huu una vifungu vingi sana. Kwa hiyo, sasa nitawaita upande wa Serikali, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kadiri mlivyojipanga kwa muda wa saa moja, ili kuweza kujibu baadhi ya hoja, lakini pia kufafanua.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Dokta Makongoro Mahanga.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 *(The Social Security Laws (Amendments) Act. 2012).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba, Mifuko ya Jamii ambayo kwa muda mrefu imejichukulia mamlaka ya kufanya biashara kwa kutumia fedha/michango ya wachangiaji wa Mifuko hiyo bila ridhaa yao, kuwepo na kipengele cha Sheria kinachozuia kufanya hivyo. Kwa mfano, *NSSF* imetumia fedha nyingi ambazo ni michango ya wafanyakazi, kujenga majumba ya kupangisha na faida inayopatikana haifahamiki kama wanachama wa mifuko hiyo wanafaidikaje. Endapo wataendelea kufanya biashara na fedha za wachangiaji, basi wanachama wanufaike na biashara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* imewatangazia wanachama wake *benefits* zilizopo, ambapo ni pamoja na kupata msaada wakati wa mazishi kwa wanachama wake. Ukiritimba uliopo unakatisha tamaa. Ili kupata fedha hizo kwa ajili ya maziko, inaweza ikapita hata wiki mbili baada ya maziko, ndipo fedha ikapatikana. Hii inadhihirisha kwamba, Mfuko huu wa *NSSF* hauko makini sana katika kutekeleza yale wanayosema kwa wachangiaji wa mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema wanachama wakafaidika na Mifuko hii bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mifuko ya Jamii kuwa chini ya Wizara moja, yaani Wizara ya Kazi na Ajira, itasaidia sana katika uwajibikaji wa ufuatiliaji kwa utekelezaji wa shughuli za siku hadi siku ya Mifuko hii ya Jamii. Ni vyema suala hili likachukuliwa kwa uzito mkubwa ili kuondoa kero na usumbufu wowote unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pensheni kwa wazee vijijini ni la umuhimu mkubwa. Lichukuliwe kwa uzito mkubwa, kwani wazee wengi na hasa wanawake wazee vijijini wanasumbuka na kuteseka kwa kukosa msaada wa kifedha ili kumudu maisha yao na familia zao kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao marekebisho mengi ni ya msingi sana kwa maslahi ya wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mamlaka ya Usimamizi ikisimamia vizuri itaboresha utendaji kazi wa Mifuko na kuhakikisha inafanya kazi kwa madhumuni yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza marekebisho yanayolenga kuiingiza sekta isiyo rasmi katika Hifadhi za Jamii kwa sababu, wananchi katika sekta hii hawana jinsi ya kujiwekea mafao ya uzeeni na hivyo kupata taabu sana wanapofika umri mkubwa. Lakini sasa hivi mifuko ina bidhaa mbalimbali kama za uzazi, mazishi, na kadhalika, ambazo mtu ambaye hayupo katika moja ya wanaohudumiwa na hifadhi hawezi kuzipata. Mifuko ya Hifadhi ulimwengu mzima, ndiyo inatoa mikopo ya muda mrefu kwa Serikali na Makampuni kwa ajili ya maendeleo. Ninapongeza mifuko yetu kwamba pia inatoa mikopo hiyo, lakini ni kwa nini basi kusiwe na Kitengo

ambacho kinaweza kutoa mikopo midogo kwa riba nafuu ya muda mrefu? Sasa hivi, wananchi wameelewa na wengi wapo na wameanzisha vikundi vya *VIKOBA* na *SACCOS.* Kwa nini basi Mifuko isiweze kukopesha na wanachama wa mifuko wakakopa kupitia vikundi hivyo? Hii ingesaidia wanachama kupata mitaji kwa gharama nafuu kuliko ilivyo sasa ambapo riba inafikia mpaka zaidi ya 48% kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachama wa mifuko wanapofika umri wa kustaafu bado wana nguvu ya kufanya kazi wao wenyewe, ikiwa ni pamoja na biashara. Kwa nini, Mfuko usiwalipe kwa mkupuo angalau 75% ili mtu aweze kuzitumia kuliko hata utaratibu huu unaopendekezwa wa 50%. Mwanachama kwa kutopata fedha za mkupuo anahangaika na kulazimika kwenda kutafuta mkopo ambao una gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la Bodi ya watu watano, ni hatari sana na halieleweki. Hivi ina maana gharama ya mkutano ni watu watatu? Mifuko hii ina maslahi ya mamilioni ya watu, ni vipi watu watatu waamue masuala ya mamilioni kama siyo mabilioni? Hii italeta mtafaruku usio na sababu. Namba ya watu 11 ni muafaka ili basi akidi iwe watu wasiopungua sita. Hapa tutapata angalau uwakilishi utakaowachanganya angalau fani zote. Bodi pamoja na kuwa na watu wenye uelewa wa Mifuko, ni lazima uwe na Wajumbe muhimu kama Wanasheria, Wahasibu, Wachumi, watumiaji wa Mifuko japo kutoka vyama vitatu ili kulinda maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napendekeza kuwa, kwa sababu Mifuko inakopesha na kufanya biashara, ni kwa nini faida Mfuko inayopata isitoe gawiwo kwa wanachama husika, kuliko ilivyo sasa ambapo mwanachama hana faida yoyote na biashara inayofanywa na Mifuko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda tena kuipongeza Serikali. Naomba izingatie mawazo muhimu na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa Watanzania wengi waishio vijijini kufikiriwa katika kuingia katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii ifikapo mwaka 2025. Nashauri kuwa lengo hilo ni zuri sana, lakini muda wake wa utekelezaji usingoje mpaka miaka hiyo ya 2025 badala yake Serikali ingeanza sasa na ifikapo mwaka 2025 Watanzania wengi wawe wamepata elimu ya kutosha na kutambua umuhimu wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii ili waweze kujiunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema mifuko ikajielekeza pia katika kuboresha maslahi ya wanachama wake kuliko kuendelea kuwekeza zaidi katika maeneo ambayo hayawagusi moja kwa moja wanachama kwa vile hali za wananchi zinaendelea kuwa mbaya na kipindi apatapo mafao yake siku zake za kuishi zinahesabika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Mifuko ya Hifadhi za Jamii ikawawezesha kwenye maeneo ya misitu kama ilivyo mifuko ya hifadhi katika nchi nyingi za Ulaya na hasa nchi za *Scandinavia* na eneo hili linatoa ajira kwa watu wengi na Mifuko ya Hifadhi inaweza hasa kuongeza wigo wa wanachama katika maeneo ya vijijini ambako zoezi zima la upandaji wa misitu ndipo lilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema mafao ya kifo yaendelee kutolewa kwa wategemezi, lakini ni vyema pia kuangalia madeni kama yapo. Ni vyema Serikali ikaangalia upya watu ambao sio watumishi hasa wazee, hili linajenga matabaka katika jamii. Serikali iweke utaratibu mpya na wa haraka zaidi kwa Watanzania ambao sio watumishi ili waweze

kujiunga na kupata nafasi ya kuja kufaidi matunda ya mfuko siku za baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni vyenzo muhimu za kutekeleza Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ili kuongeza ustawi wa wananchi na nchi kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, marekebisho yaliyowasilishwa ni machache ambayo hayashughulikiwi kikamilifu, malengo ya sera husika na mapendekezo mbalimbali ambayo Wabunge tuliyatoa katika Mkutano wa Nne wa Bunge mwaka 2011 kuhusu masuala ya kuzingatia katika marekebisho. Hivyo, katika majumuisho, Serikali ielekeze ni nini hatma ya mapendekezo mengine ambayo Wabunge tuliyatoa ambayo hayajaingizwa katika Muswada tunaoujadili katika Mkutano huu wa Bunge.

Aidha, wigo wa mjadala wa hifadhi ya jamii unapaswa kupanuliwa hususan wakati wa mchakato wa Katiba mpya ili kuhakikisha hifadhi ya jamii inakuwa ni haki ya lazima ya wananchi wote. Uamuzi huu uende sambamba na kuweka mfumo wa kikatiba, kisera na kisheria ambapo kila mwananchi kupitia mfumo wa hifadhi ya jamii kwa wote *(Universal Social Security)* atapata gawio kutoka katika mapato ya rasilimali na maliasili za nchi ikiwemo madini, mafuta, gesi asili na kadhalika. Mfumo wa hifadhi ya jamii unapaswa kuhusisha pia wananchi walio kwenye sekta isiyo rasmi, wazee wote ikiwemo waliokuwa wakulima na wafanyabiashara ndogo ndogo na vijana wasiokuwa na ajira kwa marekebisho ambayo yamewasilishwa sasa; yaongezewe nguvu zaidi katika masuala muhimu mawili ambayo yanagusa kwa kiwango kikubwa wananchi ikiwemo wa Jimbo la Ubungo:-

Mosi, kudhibiti Mifuko ya Hifadhi ya Jamii dhidi ya uwekezaji usiokuwa na tija kwa wanachama na usiolinda kikamilifu fedha za wachangiaji wa mifuko husika.

Pili, kuhakikisha wigo wa mafao unapanuliwa na kuwezesha wanachama kupata stahili zote na kwa wakati. Nguvu hizo zinapaswa kuongezwa kwa Serikali kuwasilisha jedwali la marekebisho juu ya vifungu vifuatavyo:-

(i) Kifungu cha 15 kinachoongeza kifungu cha 29A – kuviainisha na taratibu na tamaduni muafaka za mirathi.

(ii) Kifungu cha 21 kinachofanyiwa marekebisho kifungu cha 49 – kuwianisha mamlaka ya Benki Kuu na yale ya mamlaka ya udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhusu uwekezaji.

(iii) Kifungu cha 66 kinachoongeza kifungu cha 71B – kuondoa mkanganyiko uliopo kati ya kifungu na maelezo ya pembeni kuhusu mamlaka yenye dhamana ya kupokea taarifa.

(iv) Kifungu cha 150 kinachoongeza kifungu cha 49 A(2) – kiwango cha tozo kizingatie faida za uwekezaji ili wanachama wasibebeshwe mzigo wa gharama.

Katika majumuisho, Serikali ieleze pia hatua ilizochukua kutokana na tuhuma mbalimbali za ufisadi katika matumizi na uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kati ya mwaka 2005 mpaka 2010, ili kufungua ukurasa mpya wenye kuzingatia uwajibikaji.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kusema naunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SSRA* itakuwa na jukumu la kutunga *investment guidelines* zitakazoelekeza Mifuko ya Jamii

kuhusu masuala ya uwekezaji. Ombi langu kwa *SSRA* iweke *investment* katika masuala ya kijamii *Social related investments* wenye manufaa ya moja kwa moja kwa wanachama yaani wafanyakazi mfano, wafanyakazi wakopeshwe fedha na Mfuko kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kabla ya kustaafu na dhamana ya mkopo huu iwe ni mafao yao ya kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ni Mifuko kukopesha wanachama ambao labda wamechangia zaidi ya miaka mitano au kumi kwa ajili ya kujiendeleza kielimu, mwanachama huyu anaweza kuchukua masomo ya digrii ya kwanza au digriii ya uzamili na kadhalika. Mafao yake ya uzeeni yawe dhamana na pia Mfuko unaweza kutoza riba ndogo ili Mfuko nao ufaidike na mwanachama afaidike pia. Naunga mkono kuwekeza katika miradi mbalimbali mfano, Chuo Kikuu cha Dodoma, Daraja la Kigamboni na kadhalika, lakini pia Mifuko iache kuwasahau wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi, mafao anayolipwa mwanachama baada ya kustaafu kukatwa kodi siyo sahihi kwani mafao haya yanatokana na makato ya mshahara wake ambao unakuwa umeshakatwa kodi tayari ya *PAYE*. Hivyo, kukata kodi kwenye mafao ya mwanachama aliyestaafu ni kumtoza kodi mara mbili (*double taxation)*, kodi hii iondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei, ni tatizo linalotakiwa kuangaliwa kwa umakini kwani mwanachama mstaafu kiwango anacholipwa mstaafu kila mwezi huwa hakiongezeki kulingana na mfumko wa bei kwa wakati huo. *SSRA* isimamie suala hili la malipo ya pensheni yasiyozingatia mfumuko wa bei. Pendekezo langu lingine ni kwamba, *SSRA* itumie *indexation* yaani mafao ya kila mwezi yabadilike kutokana na mfumuko wa bei kadri unavyokuwa ili uwezo wa kununua vitu kwenye soko ubaki ule ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti ya mafao kati ya Mfuko na Mfuko wa jamii, sasa hivi Mifuko ya Jamii inatoa mafao

yanayotofautiana mfano, *NSSF* 2% na *LAPF* 5%, *PSPF* mafao mazuri zaidi pengine kuliko mifuko mingine. Nashauri *SSRA* iharakishe zoezi zima la *harmonization* ya mafao kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuondoa tofauti iliyopo. Pia tabia ya kutoa faida kwa mwanachama kutegemea kukamilika kwa mwaka wa fedha ifutwe, badala yake faida itolewe kwa kila mwezi kadri mwanachama alivyochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SSRA* iharakishe zoezi la kuhakikisha Mifuko ya Jamii yote iwe chini ya Wizara ya Kazi tofauti na ilivyo sasa hivi kwani utakuta *PPF* iko chini ya Wizara ya Fedha, *LAPF* iko chini ya Wizara ya TAMISEMI, *NSSF* iko chini ya Wizara ya Kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mifuko yote iweze kuruhusu watu wote hata wasio wafanyakazi kujiunga na Mifuko hii mfano, wafugaji, Wamachinga, mama ntilie, walina asali na kadhalika. Riba itakayotolewa iwe ni ya kuridhisha kwani fedha inachakaa, riba inayotolewa ni ndogo sana ni ya kinyonyaji, iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kugharimia miradi ya kilimo, mazoea yaliyopo ni kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kugharimia miradi mikubwa katika sekta nyingine kama afya na miundombinu, lakini Mifuko hiyo haijahamasika kugharimia kilimo. Iko miradi ya kilimo ikiwemo miradi ya umwagiliaji ambayo inahitaji fedha nyingi. Kwa mfano, ujenzi wa bwawa kubwa unaweza kutoa huduma nyingine ya maji ya kunywa, maji ya kilimo, maji ya kutoa umeme na kadhalika, huduma ambazo baadaye zinaweza kutoa huduma kwa jamii. Napendekeza utafutwe utaratibu unaowezesha wadau wa

kilimo ikiwemo Serikali kukopa fedha kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kugharimia kilimo.

Aidha, wastaafu ambao wanalipwa mafao waruhusiwe kutumia mafao yao kupata mikopo kwa ajili ya kugharamia shughuli au miradi midogo ya maendeleo ikiwemo miradi ya kilimo. Utaratibu huu utawezesha wastaafu wakiwa nje ya sekta rasmi kupata msaada kutoka katika fedha za umma kupitia katika Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na pendekezo la Mifuko yote ya Hifadhi kuwa chini ya Wizara ya Kazi na kupitia Sheria itasaidia kubana Mifuko inayokiuka taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Mifuko kukiuka taratibu na kujilipa fedha nyingi na mingine kukiuka taratibu za ajira kwa kujilipa mara mbili. Pia sheria hii itasaidia kubana baadhi ya mifuko inayotumia fedha za umma vibaya. Mfano, Mifuko wa hifadhi wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* wamekuwa na matumizi mabaya ya fedha. Pia kuingia mkataba mbovu wa ukodishaji wa *GK* Hoteli kwa makusudi kwa ajili ya maslahi machache ya viongozi wa Mfuko huo na kuisababishia hasara Taifa ya mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna taarifa kwamba si mara ya kwanza kuingia mkataba mbovu na walikuwa wakipeana kwa zama viongozi wa Mfuko huko kukodisha Hoteli ya *Pickcok Hotel Millennium Tower* kwa lengo la kufanya biashara na kuacha watu wenye sifa. *Please,* Mheshimiwa Waziri afuatilie sana Mfuko huu.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nipongeze Wizara na watendaji wake wote

kwa uamuzi wa busara walioufanya wa kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Mifuko ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri ya kutoa ushauri mzuri kwa Wizara ambazo wametusaidia katika kurahisisha kazi kubwa ya kupitia Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa mamlaka maalum ambayo itasimamia Mifuko ya Jamii ni jambo zuri katika ku-*monitor* haki za wananchi na kuona kama mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mifuko hii kuamua sasa kuchangiwa na wafanyabiashara na wajasiliamali ni jambo jema kwa sababu nchi yetu ina upungufu mkubwa wa ajira kwa vijana. Vijana walio wengi wanajiajiri wenyewe kwa mitaji yao midogo. Lakini kama watapewa elimu ya kujiwekea akiba katika Mifuko ambayo itawasaidia katika kipindi kitakachoendelea hata kama si uzeeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kipya cha 49(4)(a), (b) na (c) kinachoipatia Benki mamlaka ya kurekebisha Mifuko pale uwekezaji unaofanywa na Mifuko unapokuwa siyo mzuri. Nakubaliana na kifungu hiki kwa maslahi ya Watanzania. Kwa kuwa Mifuko yetu inafanya uwekezaji mkubwa kama *NSSF* hali hii inaweza kusababisha mafao ya wananchi yakakosekana au kuyumba. Kwa hiyo, benki itarekebisha hali hiyo na kuweka mambo sawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mchango wangu katika sheria hii ikihusu marekebisho. Nashauri Mifuko hii inapokusanya fedha za wanachama isitumie fedha hizo bila ridhaa za wanachama, hivyo uko

umuhimu wa kupata ridhaa toka kwa wanachama. Hivi sasa Mifuko hii inaamuliwa na watumishi wa Mifuko hii. Mfano, wanachama hawafaidiki na fedha au michango yao moja kwa moja katika kipindi chote cha michango ingawa fedha zao wanazochangia zinafanya uwekezaji kwa kuwapa mikopo wafanyabiashara wakubwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa kwa mifugo hiyo kuwekewa sheria ya kuruhusu Mifuko hiyo kutoa mikopo kwa wanachama ambao kulipa kwao mikopo hiyo kutakuwa na uhakika. Mikopo hiyo itaboresha Mifuko kwa riba itakayotokana na mikopo hiyo ambapo naamini itakuwa na riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Mifuko itaweka utaratibu wa kukopesha wanachama kwa riba nafuu itavutia wanachama ambapo kwa sasa wananchi wengi wanahangaika kukopa kwenye vyombo vinavyokopesha na vyombo hivyo kujipatia faida kubwa.Mfano, wapo Wabunge wengi wamejiunga na Mifuko hiyo, lakini mikopo wanakopa Benki kwa riba kubwa.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuhakikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweka mikakati ya kuhakikisha huduma wanazotoa kwa jamii zinaboresha maslahi ya Shirika na wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wazo la Kamati kwamba Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii iwe chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, hii itasaidia katika usimamizi wa uendeshaji wa Mifuko hiyo na pia itapelekea uanzishwaji wa Idara ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika naungana na maoni ya Kamati kwamba Muundo wa Bodi uwe na watu zaidi ya tisa (9) ili kupanua wigo wa Wajumbe wa Bodi, kwani

Wajumbe wa Bodi wanaingia kwa taaluma zao. Hivyo, wingi wao utaingiza watu hao wenye taaluma (kama vile Wanasheria, Wahasibu na wengineo) ambao watatumia taaluma zao na kuongeza chachu ya maendeleo ya Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za uendeshaji wa Bodi za Mifuko hiyo yaachiwe Mashirika husika. Hivyo basi, nashauri Bodi iwe na Wajumbe zaidi ya tisa (9) kwani kazi yao ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko iwe na wanachama wa sekta zote rasmi na zisizo rasmi ili wananchi wapate fursa hiyo. Nawasilisha.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa wazo juu ya uendeshaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwamba marekebisho ya Mifuko ya Jamii yameondoa ubaguzi uliokuwepo baina ya wafanyakazi wa Serikali na wale wa sekta binafsi na pia umeondoa dhana ya kuitwa Mifuko ya Jamii wakati ilikuwa ni Mifuko ya Wafanyakazi wa Serikali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutolewa fursa hii kwa sekta binafsi kujiunga na Mifuko ya Jamii kutatoa fursa kwa wajasiriamali wengi kuongeza idadi ya wanachama wa Mifuko ya Jamii na hivyo kuongeza uzalishaji na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika marekebisho ambayo yanataka kufanywa kwa maslahi ya Taifa basi mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii iwekwe katika Wizara moja tu nayo ni Wizara ya Kazi na Ajira, kwani kila Wizara ikiwa itabeba idadi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Wizara ya Kazi itakuwa imevamiwa na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni vibaya hata kidogo kuona kuwa makampuni yanakuwa na mifuko yao ya Hifadhi ya Jamii lakini kwa upande wa Serikali Wizara ya Kazi iwe *responsible.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 29A kinatoa adhabu kwa mwanachama wa mfuko anayechelewa kutoa mchango wake. Sasa kwa nini sheria hii haijaeleza mwanachama ambaye amecheleweshewa kupewa mafao yake baada ya kustaafu nini kitafanyika ili kufidiwa muda ambao amecheleweshewa mafao yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa asilimia wa fedha za pensheni zinazohusu marehemu, naomba kwa heshima zote kwamba ni lazima wakati huo sheria ya dini inayotuongoza kwenye mirathi, Sura namba 352 izingatiwe katika mgawanyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya Muswada Zanzibar imetajwa kwamba haitapungua Wajumbe wawili. Wajumbe wote wa Bodi ni wangapi? Kumetumika kigezo kipi mpaka Zanzibar ikapewa nafasi mbili na je, utoaji wa nafasi umezingatia vipi masuala ya jinsia?

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia vifungu vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 129 kinachoeleza muda wa Mkurugenzi Mtendaji uwe ni miaka mitano. Muda huu hautoshi kwa Mtendaji Mkuu wa Taasisi kuweza kutekeleza majukumu yake hasa kuhakikisha huduma zinawafikia Watanzania wengi japo kufungua ofisi zao katika Wilaya zote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipangp mingi ya kitaasisi utekelezaji wake unalenga siyo chini ya muda wa miaka mitano hadi kumi. Hivyo nashauri muda wa Mtendaji Mkuu uwe miaka kumi ili kumpa fursa kutekeleza majukumu yake vizuri.

Kwa kuzingatia kwamba Mkurugenzi Mtendaji anateuliwa na Rais, pia anawajibika kwenye Bodi, endapo itaonekana ameshindwa kutekeleza majukumu yake basi mamlaka zilizo juu zitamwajibisha ikiwemo kusitisha au kumuondoa kwenye nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifungu cha 43, wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi waruhusiwe kujiunga na mifuko ya *PSPF* na *LAPF.* Naunga mkono kifungu hiki kwa sababu kitasaidia vijana ambao ni wengi na wamejiajiri kwenye sekta isiyo rasmi mfano; kwenye uchimbaji mdogo wa madini, uvuvi, saluni na kadhalika kufaidika na huduma zinazopatikana ikiwemo kujiwekea akiba kwa ajili ya uzeeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi wamehamasishwa kupitia Serikali na wameweza kujiunga na vyama vya kuweka na kukopa ikiwemo *SACCOS,* wanafanya biashara hata wengine kufikia uwezo wa ku-*import goods and services*. Aidha, wanawake wamekuwa wahanga wakubwa wa kupoteza fedha na mali zao kupitia upatu, *DECI* na kadhalika. Hii yote ni katika kujaribu kutafuta fursa ya kuweza kujiwekea akiba. Hivyo kuruhusu sekta isiyo rasmi kujiunga na mifuko hii kutasaidia wanawake kujiwekea akiba na kuweza kupata huduma bora zikiwemo huduma ya uzazi, matibabu, mazishi na kadhalika ambazo hutolewa na mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nashauri mifuko yote ya jamii iwajibike na kusimamiwa na Wizara ya Kazi na Ajira. Hii itasaidia ku-*regulate/control* hii mifuko katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naonga mkono hoja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mola na pia nikiipongeza Wizara na Kamati kwa kazi nzuri ifanyikayo ikiwa ni moja ya huduma muhimu kwa jamii. Pamoja na kuipongeza

napenda nitoe yangu machache kuiomba Wizara iangalie kwa makini mifuko yake maana baadhi ya mifuko mingine ina mapungufu ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumzie juu ya Mfuko wa Pensheni. Kiukweli lengo la mfuko ni zuri na utekelezaji wake mwanzoni ulikwenda vizuri ila sasa unawachanganya wanachama wake kutokana na kile kitendo cha kuwalipa wahusika nusu ya miezi sita yaani Januari – Juni badala yake ikidaiwa kwamba hiyo mingine ilishalipwa toka nyuma mwanzoni mwa mfuko. Hata hivyo, kumekuwa na usiri wa kutoa nyongeza ambayo imekuwa ikitazamiwa toka siku nyingi ya shilingi 20,000/= kwa mwezi. Kulingana na kupanda kwa gharama za vitu huwa hazitoshi, hivyo ni vyema hilo liangaliwe. Vilevile utata wa miezi mitatu kwa baadhi ya wanachama na miezi sita kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mfuko wa Bima ya Afya nao huleta mkanganyiko kwa vile utendaji wake hutoa huduma kwa wanachama. Wanachama walishawishika sana wakati wa awali kulingana na maelezo ya ushawishi. Walitegemea kunufaika sana na mfuko huu waendapo kutibiwa, lakini mambo yanakuwa kinyume na matarajio hayo. Hivyo, Wizara iangalie vema na upya utoaji wa huduma ili kuwapa imani wanachama.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuanzisha mamlaka mbalimbali kwa lengo zuri, lakini haki zitendeke na usawa wa usimamizi wa mifuko yote kwa ujumla. Mifuko isimamiwe katika kuhakikisha fedha za Watanzania zinatumika vizuri si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya wafanyakazi inayofanya vizuri kama *NSSF* katika uwekezaji Serikali nayo isaidie kufanya mrejesho wa uwekezaji badala ya kuonekana mfuko fulani haufai wakati sisi wenyewe ndio tunaiangusha.

Matumaini yangu mamlaka hii itaisaidia *NSSF* na mifuko mingine kufanya vizuri na kurudishiwa fedha za walizowekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni mkombozi kwa wastaafu, wafanyakazi na kadhalika katika maisha. Lakini matumaini ya mifuko hii imetoweka kutokana hasa na wastaafu kupoteza matumaini ya maisha yao kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kucheleweshewa mafao yao kwa wakati au kutopata kabisa mafao yao na malimbikizo ya mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kwenda mbali ningeishauri Serikali kwa nia njema kufanya marekebisho haya, Serikali itatue kero hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wastaafu ambao wamestaafu tangu miaka ya 2004 lakini mpaka hivi leo hawajui hatma yao. Wengine wamefariki dunia na kuacha mafao yao na familia zao hawajui watazipata vipi au watalipwa na Serikali ya awamu ya ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo familia ambazo zinadai mirathi kiasi cha watoto kushindwa hata kuendelea na masomo, lakini wamekuwa wakizungushwa hasa pale mwanamke anaedai hana elimu ya kutosha na kuwa na ujasiri wa kudai haki yake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isimamie sana suala la jinsia na jinsi gani hasa wananchi kutoka vijijini ambao hawafikiwi na elimu ya kutosha ya mafao haya.

Je, kwa wazee wa vijijini na wa mama wasiofikiwa na elimu hii ya mafao haya Serikali imejipanga vipi ili huduma hii wanufaike nayo? Naomba jibu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuleta marekebisho ya mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa napongeza sana suala la kuingiza wanachama kutoka sekta rasmi na isiyo rasmi katika Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma na kifungu cha 120 cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho ya Utumishi wa Umma kwa vile wananchi wataweza kuwa na wigo mpana wa kuchagua mifuko wanayopenda kujiunga nayo.

Hata hivyo, bado kuna malalamiko toka kwa baadhi ya wanachama kwamba katika Sheria ya Mfuko wa Mashirika ya Umma kuna kanuni za ukokotoaji mafao *(factor)* ya mwanachama za aina mbili ingawa kanuni iliyokuwa inatumika tangu mwaka 1978 - Juni, 1988 kukokotoa mafao ya 1/960 ilikiwisharekebishwa tangu Julai, 1988 na kuanza kutumika kwa *formula* ya 1/600 ambayo ni bora kwa wananchi husika.

Hata hivyo, pamoja na uboreshaji huo wa 1988, kuna utata bado unaendelea na wanachama hao kuendelea kupunjwa mafao yao ya utumishi wa umma. Kwa msingi huo naomba sana Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi sahihi wakati atakapokuwa anamalizia uwasilishaji wa hoja hii ili kuwaelimisha wanachama wanaoendelea kupunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua fursa hii kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Muswada una marekebisho mengi lakini yote ni muhimu sana kwa Wanachama na uhai wa Mifuko hii kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Kamati kwenye kifungu cha 21 cha Muswada kinachofanya marekebisho kwenye kifungu cha 49 cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, ambacho kinaongelea kuhusu Mfuko kuwekeza fedha za Wanachama. Katika hili, nakubaliana na Kamati mia kwa mia kuwa Mifuko sasa kuanza kuwanufaisha Wanachama kutokana na uwekezaji huo kuliko hali iliyopo sasa ya Mifuko kuwekeza katika biashara mbalimbali hasa za ujenzi. Ukiangalia hali halisi kwa sasa kuna majengo mengi ya Mifuko; ni vizuri kwa upande mmoja kwani inaonesha wazi uhai wa Mifuko hiyo, lakini vile vile Wanachama ambao ndiyo wenye Mifuko hiyo ni lazima wafaidike nao. Nina mategemeo makubwa Muswada huu ukipita utasaidia kwa kiasi kikubwa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mifuko kuwa chini ya Wizara moja ni muhimu sana, pia itarahisisha sana kazi ya *SSRA;* ijapokwa Muswada huu haukuja na pendekezo hilo, lakini naungana na Kamati kuiomba Serikali kuliangalia suala hili kwa umuhimu wake na kulipa kipaumbele cha hali ya juu. Ni kweli kabisa ili Mifuko hii iweze kwenda vizuri na kwa uhai wa Mifuko hii, lazima tukubali kuwa huu ni wakati mwafaka sasa Mifuko ya Hifadhi za Jamii ikawajibika chini ya Wizara ya Kazi na Ajira badala ya hali iliyoko sasa ambapo Mifuko ipo katika Wizara ya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mifuko hii ni muhimu sana kwa jamii na kwa hali ya sasa ambapo tuna mamlaka inayo-*regulate* Mifuko hiyo, ninakubaliana na Kamati kuwa ni vizuri ikaanzishwa Idara Maalum ndani ya Wizara itakayoshughulika na Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na suala la Wanachama au Waajiriwa kujiunga na Mfuko kuachiwa wenyewe kuchagua Mfuko wanaoutaka, ni suala zuri sana nami naliunga mkono kwani Wanachama wengi walikuwa wakilalamika kwa sababu ya kulazimishwa na Waajiri wao kujiunga na Mifuko wasiyoitaka. Hivyo, Muswada huu ukipita na kuwa sheria, utawasaidia sana Waajiriwa wote kuwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuliona hili la sekta isiyokuwa rasmi kujiunga katika Mifuko hii ya Hifadhi. Kiuhalisia, asilimia 80 ya nguvukazi ya Tanzania inajishughulisha katika sekta isiyo rasmi; na endapo kundi hili litaachwa, itakuwa hatujawatendea haki. Ninadhani kuna baadhi ya Mifuko wameshaanza kulifanyia kazi kama *NSSF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na mapendekezo yote yaliyotolewa; ni mazuri na yameangalia pia mtu wa chini isipokuwa la kumwongezea kazi Rais sikubaliani nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea kuchangia tena na hasa kupongeza tena kwa kuona haja ya Mifuko hii kwenda mikononi mwa jamii. Bado naendelea kushauri utaratibu wa Mifuko ushuke katika vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Dar es salaam kuna vyuo vingi vinavyotoa taaluma mbalimbali. Wanafunzi hawa iwapo watapewa elimu ya kufahamu umuhimu wa maslahi ya Mifuko hii, itawajengea vijana utaratibu mzuri wa kujiwekea akiba mapema kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Serikali iwasimamie wafanyabiashara wa kati, wadogo na wale wakubwa, kwa maslahi yao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, familia za wafanyabiashara wanapokufa au mitaji yao inapoanguka, wanakuwa hawana hata pa kupata msaada zaidi ya kukabiliwa na madeni mengi pasipo faraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wimbi la watoto wa wafanyabiashara walioanguka au kufa, kukosa ada za shule linazidi siku hadi siku Mkoani Dar es Salaam. Ni vyema mamlaka hii itakapoanzishwa basi iangalie changamoto mbalimbali na itoe ushauri kwa Mifuko kupanua wigo wake katika kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mmoja, napenda kuchangia hoja hii na kupongeza kuwa imekuja wakati mwafaka.

Nakubaliana na marekebisho yote yaliyofanywa na hasa yale yanayoangalia manufaa zaidi kwa wenye Mfuko, yaani wachangiaji wa Mfuko. Ni kweli Mifuko hii imekuwa ya manufaa kwa wachangiaji lakini mimi naona ni bora zaidi kuona wachangiaji wa Mifuko wanaanza kunufaika na Mifuko wakati mrefu zaidi, yaani wakiwa katika umri wa kutafuta riziki kwa familia yao. Hivyo, nashauri kuwa suala la kutoa mikopo kwa wachangiaji ili waweze kutimiza mambo mengine liwe la msingi sana. Siku za nyuma mashirika mengine kama Bima ya Maisha yalikuwa yakitoa mikopo kwa ajili ya vifaa muhimu vya nyumbani hata ujenzi, lakini siku hizi yameacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza kuwa Mifuko hii iwanufaishe zaidi wachangiaji badala ya kuwaendeleza tu waajiriwa na Mifuko badala ya wenye Mifuko. Mishahara yao

hasa ngazi za juu ni kufuru na posho ndiyo usiseme. Wanatumia magari bei mbaya huku wenye Mifuko wanaishi katika lindi la umaskini na wengi kufa hata kabla ya kufaidi hata kiduchu cha jasho lao. Mwisho, muda wa mtu kupata mafao yake bila kuchangishwa uwe wazi. Pia elimu itolewe kwenye vyombo vya habari na mafunzo ya makusudi kwa wanajamii. Tutengeneze motisha za makusudi ili watu wachangie wenyewe bila kulazimishwa kwa vile wanayaona manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nguvu zote ninaunga mkono wazo la kuwapa kiinua mgongo wazee wote *(senior citizens)* angalau shilingi 100,000 kwa kila mwezi wala isibague, hii ina maana kuwa Serikali nayo kwa makusudi ichangie kiasi fulani cha fedha yake toka kwenye mapato ya madini, gesi, misitu na kadhalika, iweke fedha ya kuwatunza wazee wake walioitumikia nchi hii kwa uaminifu kabisa kuliko hata Viongozi wa Kitaifa ambao wengine wamelifisadi sana Taifa letu.

Kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yetu. Marekebisho haya yataboresha sana ukusanyaji na hivyo kuleta tija kwa wanachama. Sheria hizi zitasaidia pia kuweka wazi matumizi ya fedha, kwani hali ilikuwa mbaya au kutokuwa na mpangilio mzuri hadi kuleta mvutano mkubwa hasa ilipobainika kuna vigogo waliokopeshwa fedha. Vilevile Sheria hii italinda maslahi ya Wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi ya wastaafu kutokulipwa pensheni zao kwa wakati na wanakuwa wanafuatila kwa muda mrefu bila mafanikio. Nilitegemea Muswada huu ungekuwa na kipengele cha jinsi gani Mifuko hii itakuwa na muda maalum wa kulipa mafao hayo na wakishindwa basi *pensioner* huyo alipwe *interest rate.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Bodi wachaguliwe kutokana na sifa zao kwani watasaidia sana kuboresha Mifuko hii ambayo ni tegemeo kubwa kwa wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoona, Mifuko ni mingi lakini ipo katika Wizara mbalimbali. Kutokana na hali hii imefanya usimamizi uwe mbovu na kutokuwa na *uniformity*; ipo hatari baadhi ya Mifuko kufa. Ni muhimu Mifuko hii iwe chini ya Wizara moja na iundiwe Kitengo Maalum.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Wataalam wake na Viongozi wa Mifuko hiyo, kwa kufanya kazi nzuri ya kuiongoza Mifuko hiyo kwa manufaa ya umma. Hivyo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba Mifuko hiyo pia ifanye kazi na Zanzibar na pia iwe na Ofisi Zanzibar na kuja kutoa elimu kwa Wazanzibari ili nao waweze kujiunga kwa wingi.

Je, Mfanyakazi wa SMZ huko Zanzibar anaruhusiwa kujiunga na Mifuko hiyo; na je, atakuwa akikatwa kwa kupitia njia gani au awe analeta fedha mwenyenyewe? Naomba kueleweshwa.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana juu ya mipango ya maisha na maendeleo kwa ujumla. Kwa hivyo, ni lazima marekebisho yote yazingatie haki na usawa wa hifadhi na kulinda Mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wafanyakazi uwe katika Wizara moja tu na sio kila Wizara. Hii italeta ufanisi wa usimamizi wa Mfuko huu, na itarahisisha uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mfuko huu, ni vema kuwe na mkataba maalum kwa kuzingatia matumizi ya biashara za Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho, kifungu cha 5(i)(e), (f) na (i) cha Sheria Na. 8 ya mwaka 2008, kinachoelezea majukumu ya mamlaka kifanyiwe marekebisho ili majukumu haya yafanywe na Wizara ya kazi na ajira chini ya Idara inayopendekezwa ya hifadhi ya jamii kwa sababu ni ya kisera zaidi na sio ya kiutendaji.

Mheshimiwa Waziri, kifungu 49A(1)(2), Muswada haukueleza tozo lililokusudiwa litatoka wapi, tozo hizi ni lazima kuelezwa kwa kuzingatia athari ya michango ya wanachama.

Zingatio:- Fedha za Mfuko ambazo ziko katika Mfuko wa Hifadhi zisikopeshwe Serikali kwani ni kuufanya Mfuko huo ushindwe kufanya malipo ya wanachama kwa wakati.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeza Serikali kwa kufanya jambo zuri ambalo litawasaidia wananchi kwa ajili ya kupata maisha mazuri, wao na familia zao na hasa ukiangalia wadau wote wameshashughulikiwa, wafanyakazi, waajiri na hata wale wasio na sekta rasmi, ili waweze kujiunga na Mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kuongelea juu ya kufanyika kwa tathmini ya mali na madeni ya Mifuko. Hili ni jambo zuri ambalo mamlaka itajijua kiwango chake na udhaifu wake ili waweze kujirekebisha na kuwa na maendeleo mazuri, lakini tathmini hii ataifanya nani? Kutaajiriwa watu kutoka nje au hapa hapa petu? Je, ikiwa watu kutoka Tanzania, uwezo wanao kwa mambo haya? Kama kutoka nje malipo yatakuwaje?. Ushauri wangu ni kwamba, ni vema kuwa na *competition* ili kujua uwezo wa hawa watakaofanya tathmini hiyo pamoja na malipo yao ili kazi iwe na ufanisi mzuri.

Kifungu cha saba cha Muswada kinafanya marekebisho juu ya muda wa Mkurugenzi Mtendaji kushika ofisi kuwa ni muda wa miaka mitano na baadae kufikiriwa kwa miaka mingine mitano. Kwa nini iwe kwa Mfuko wa Pensheni? Ni sababu zipi zilizopelekea hivyo kwamba kuwe na muda maalum, wakati kuna Wizara nyingine za Serikali watendaji wake wakuu wanafika hata miaka 20 mpaka 30 wanashikilia nafasi hiyo? Hivyo, ni vema kukawa na mfumo maalum kwa watendaji wote wa Serikali, mashirika *unless otherwise* wawe wameiba au wamekwenda kinyume na nidhamu au maadili yaliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21 cha Muswada kinazungumzia Mfuko kuwekeza fedha za wanachama. Si vibaya Mfuko kutafuta njia nyingine ya kuongeza mapato ili usije ukasambaratika, lakini pia ni vizuri kuwakumbuka wale waanzilishi ambao ni wanachama kwa kupata mafao mazuri na kwa wakati. Pia kupewa nafasi ya kukopeshwa kupata mikopo kulingana na makato yao na *interest* ndogo ili waweze kutoa badala ya kuwapa wafanyabiashara wakubwa matunda ambayo wanaweza kuyahimili kwa wepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 22 kinachozungumzia haki kwa mfanyakazi ambaye anaachishwa kazi aweze kulipwa mafao ya pensheni au mafao ya mkupuo *(gratuity)*. Ni vizuri lakini mafao ya mkupuo wake usichukue muda kulipwa kwani kuna tabia ya Mifuko hii kutowalipa watu kwa haraka na wengine hukaribia kufa huku fedha yao hawajaipata. Hapa huwa ni tatizo kwa upande mwingine kwani familia mnaitia kwenye matatizo hasa wakati wa kurithi na wanaopata shida ni watoto na mama yao kutokana na mila na desturi za Tanzania Bara, lakini kwa upande wa Zanzibar, Sheria ya Kiislam hutumika kwa Waislam na kwa Wakristo huwa ni mtihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 30 kinatoa uhuru wa watumishi kujiunga na Mfuko wowote wautakao, ni vema hapa pakatolewa elimu itakayohusu kujiunga na Mifuko hii ya jamii. Pia waweze kujua hasara zake pale utakapojiunga mifuko yote. Wizara pia itoe toleo au *circular* itakayowafahamisha kujua asilimia ya makato yake, faida au hasara itakayompata ikiwa atajiunga zaidi ya Mifuko miwili na kuendelea. Kuhusu Bodi ambayo haitazidi Wajumbe saba na haitakuwa ndogo? Hasa ukiangalia *quorum* wakati wa kufanya mikutano, ni vema idadi ikaongezeka kwani wajumbe hawa wanaweza wengine wakawa nje ya nchi au mkoa ikawawia tabu kupata *quorum* ni vema wajumbe hawa wakawa 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kujua *ratio* iliyochukuliwa, hata Zanzibar watoe wajumbe wawili.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumpongeza Waziri wa Kazi na Ajira kwa kuwasilisha Muswada huu. Aidha, nawapongeza wadau wote waliohusika kuchambua Muswada. Naomba kuelekeza mchango wa hoja hii katika kutoa ushauri. Itolewe elimu ya kutosha kwa wanachama kuhusu haki zao baada ya kustaafu. Zitolewe njia mbalimbali za kuwafanya na kuwanufaisha pia wananchi walio wengi hasa wakulima. Kilimo kimeajiri zaidi ya asilimia 70 ya ajira zote nchini. Tuangalie wenzetu nchi zilizoendelea wanafanyaje kuhusu hifadhi kwa wakulima wao.

Kuna baadhi ya waajiri wengine ambao hawako tayari kuwaelimisha watumishi wao kuhusu Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni Mifuko muhimu sana kwa Mtanzania yeyote, hivyo basi, elimu kwa njia mbalimbali itolewe sio tu kwa wanachama lakini kwa watu wote wafanyabiashara, wakulima na kadhalika. Hata hivyo, naipongeza Wizara kwa hatua hii. Miaka michache iliyofanya suala la Mifuko hii ya Hfadhi ya Jamii lilihusu watumishi wachache tu, lilikuwa la kiofisi tu lakini kwa sasa liko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja hii napenda kusema yafuatayo:-

Kwanza, uwekezaji wa fedha za Mifuko. Hii inafanyika bila ridhaa ya wanachama wa Mifuko na hawapati manufaa (riba) yoyote, ni kinyume cha haki za binadamu.

Pili, wanachama wengi wanacheleweshewa kulipwa mafao yao mara kwa mara, inawalazimu kufungua madai Mahakamani. Nashauri kuwe na Baraza Maalum (*Tribunal*) ya kuamua mashauri hayo.

Tatu, Pensheni maana yake ni kumwezesha mstaafu kuweza kupata mapato kila mwezi. Wastaafu hasa wale wa Serikali walipwe kila mwezi badala ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Wizara maalum itakayohusika na Mifuko ya Jamii. Mifuko yote iwe chini ya Wizara ya Fedha.

Mwisho, nashauri wazee na watu wote waliokosa ajira wapewe *weekely living allowance* kama shilingi 20,000 au mahitaji maalum; unga, mchele, maharage, mafuta au kodi ya nyumba kwa mwezi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu kwa mustakabali wa wafanyakazi wa nchi hii. Nina ushauri ufuatao:-

Mifuko hii iwahusishe watu wote hususan wakulima katika nchi ili waweze kujikimu kimaisha.

Kwa kuwa wadau wa Mifuko hii sasa wanaruhusiwa kujiunga katika Mfuko wowote Waziri aangalie kiwango ambacho Mifuko hii inalipa ikibidi sasa waangalie kwa pamoja kima cha chini na hata kiasi cha pensheni kwani vinginevyo mifuko mingine itakosa wateja.

Muda wa malipo ya pensheni uainishwe na au kwa Mifuko yote, isitokee kwa Mifuko fulani inalipa kila baada ya miezi mitatu na mingine kila baada ya mwezi.

Faida ya uwekezaji igawiwe kwa wanachama sio kwa wafanyakazi.

Mafunzo yatolewe kwa wanachama mara kwa mara ili wajue stahili zao badala ya kubaki kutabiri pensheni zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri, Muswada huu ni muhimu sana kwa Wizara yake.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kuleta Muswada wa kufanya marekebisho katika Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Baada ya uuzaji wa Mashirika ya Umma na ubinafsishaji wa mashirika hayo, kuna haja Mifuko ya Jamii *PPF, NSSF, LAPF, PSPF* na kadhalika kushindanishwa ili itoe tija na pensheni nzuri kwa wateja wake.

Hatua hii ni nzuri kwa sababu kila Mtanzania anayependa kujiwekea akiba ya uzeeni anaweza kuchagua Mfuko anaoupenda na ana haki ya kupata mafao ya uzeeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 85(7)A, 42(3) na kadhalika vinataja kipindi cha miaka mitano cha Mkurugenzi Mkuu kuongoza Mfuko na miaka mingine mitano atakayoongezewa. Je, Serikali haioni kwamba itakuwa haitendi haki kwa Mkurugenzi Mkuu ambaye kwa muda wote wa uongozi amekuwa anafanya vizuri kiasi cha kuzidi malengo? Kuna haja gani kumwondoa Mkurugenzi kama huyu baada ya miaka kumi na kumwajiri mwingine wa majaribio. Kipindi hicho kiongezwe kisomeke: "*For a term of five years (renewable) or 15 years but subject to his/her performance".* Kipindi cha miaka kumi ni kifupi kwa Mkurugenzi anayefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 135(24)A(3) ni hatua gani zitachukuliwa endapo ripoti ya *evaluation* imegundua tatizo (*anomaly*) inaandikwa *measure to rectify an anomaly discovered in the report*". Kama Mfuko umefanya vibaya na ikagundulika kuna tatizo kubwa mfano wa mauzo ya *assets* bila taarifa, *mishandling, misappropriation* kutatakiwa hatua au sheria izingatiwe kutoa adhabu zaidi na sio maelekezo tu kama ilivyotajwa katika kifungu kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifafanue hili. Kifungu 149 na 150(49A) kinasomeka kwamba kutakuwa na tozo (*levy*) kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo italipwa kila mwaka kwa wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tozo (*annual social security levy*) ni kiasi gani asilimia ngapi ya mapato ya mfuko? Hofu ni tozo isiwe kubwa kiasi cha kufanya Mfuko ushindwe kufanya vizuri na mwisho wa siku Mfuko ukifilisika itakuwa kero kubwa kwa wananchi waliochangia.

Mfuko kama *NSSF,* Muswada unasema Bodi itaamua kiwango kutegemea na tathmini ya mali na madeni ya Mfuko. Je, ikitokea Mfuko umeshindwa kukusanya madeni, mwananchi aliyechangia Mfuko kushindwa kumlipa mafao kiwango cha kutosha kwa sababu ya uzembe wa Mfuko kutokukusanya madeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Mfuko umefilisika, mwananchi aliyechangia atalipwa na nani michango yake ya pensheni? Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni mingi (6) na yote ni mikubwa kifedha na *assets*. *Regulator* atakuwa na uwezo wa kui-*regulate* yote *efficiently*? Nashauri apewe *enough staff* na *very competent staff.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi wa niliyoandika hapo juu, nitaunga mkono hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupe shukrani kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu wa Waziri wa Kazi na Ajira, Muswada wa Sheria ya *Social Security Laws.* Lakini kabla ya hapo nichukue nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa misiba mikubwa iliyotupata kama nchi, lakini vile vile nitoe rambirambi kwa msiba uliotupata katika Jimbo la Segerea na Kata ya Segerea kwa kufiwa na Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mzee wetu Abdul Malifedha; Mwenyezi Mungu alaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwapongeze Wabunge wapya walioapishwa jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichangie kidogo hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kujaribu kujibu baadhi ya maoni, mapendekezo pamoja na hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa muda niliopewa, nitajibu baadhi tu ya hoja na Mheshimiwa Waziri, atakuja kuhitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na Mheshimiwa Christopher Chiza, *Engineer;* alizungumzia masuala ya Wastaafu wanaolipwa mafao kwamba, waruhusiwe kutumia mafao kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kwenye Kifungu cha 38 cha Sheria ya Mamlaka, suala hili limewekwa bayana na tumeanza na suala la mikopo ya nyumba kwa ajili ya makazi ya wanachama. Lakini kwa mikopo mingine midogo midogo, hili inabidi tuliangalie zaidi, lifanyiwe tathmini na kuangalia uwezo wa mifuko, baadaye Mamlaka itatoa maelekezo. Kwa sababu, tunahitaji kuwa makini ili tusije tukaumiza Mifuko hii. Lakini tayari tumeanza na mikopo ya nyumba na hiyo imo kwenye Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Mnyika, alizungumzia masuala kadhaa. Moja, alizungumzia kwamba, hapo nyuma Wabunge walishatoa mapendekezo mengi sana, lakini marekebisho yaliyoletwa ni machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tumwambie tu kwamba, kwa kweli hii ni awamu ya kwanza ya marekebisho yenye lengo la kuainisha Sheria za Mifuko ili iendane na Mamlaka hii ambayo tumeianzisha. Lakini tutakuja tena na awamu ya pili ya *reforms* ambayo, vile vile itahitaji kuletwa Bungeni kwa ajili ya kurekebisha Sheria au kuongeza baadhi ya Vifungu. Kwa hiyo, mambo mengine kama atakavyosema Waziri, yanaweza kuja kwenye awamu ya pili likiwemo hilo suala ambalo limezungumzwa sana la Mifuko hii kuripoti kwenye Wizara ya Kazi, lakini vile vile kuwa na Mifuko labda michache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hayo tutayaangalia wakati huo, lakini kwa sasa tukubali awamu hii ya kwanza ya marekebisho haya tuliyoyapitisha, basi yapite ili yawezeshe Mamlaka na Mifuko sasa, kuendelea kufanya kazi vizuri. Alizungumzia vilevile masuala ya Katiba ya Jamhuri inayokuja na sisi tunasema vema; baadhi ya mambo kama yatakuwa

yameingia kwenye Katiba Mpya basi marekebisho, sio Sheria hii tu ila Sheria nyingine bila ya shaka zitaendelea kurekebishwa kulingana na hayo yatakayokuwa yamekuja kwenye Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, amezungumzia suala zima la ukokotoaji wa Mfuko wa *PPF,* ile *factor* ya 1 chini ya 960 na kwenda 1 chini ya 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii ilikuwepo na haya marekebisho yalifanywa na *PPF* mwaka 1984, sio 1988. Wakati huo, kama tunakumbuka, ni kwamba *PPF* bado ilikuwa na ule utaratibu ambapo wengine walikuwa wanachangia 12.5% kwa maana kwamba mwajiriwa 5% na mwajiri anatoa 7.5% na baadaye wengine wakawa na 20% kwa maana ya wengine 5% wengine 15%. Lakini baada ya mabadiliko Mfuko uliendelea kulipa mafao kwa kutumia Kanuni zote mbili, lakini tueleze tu kwa sasa *factor* inayotumika kuanzia tarehe 1 Machi, 2001 imeanza kutumia *factor* moja tu ya 1 chini ya 600 kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge, amependekeza. Hii inatumika hata kwa wale ambao bado wameendelea kuchanga 12.5% kwa ujumla wao, mwajiri na mwajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mahmud pamoja na Mheshimiwa Sara Msafiri, walizungumzia masuala mazima ya kwamba, Serikali iweke utaratibu wa Watanzania ambao sio watumishi, ili wajiunge na Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema haya ndio hasa malengo ya Muswada ambayo ni pamoja na kupanua wigo. Kwa maana hiyo sio tu watumishi wa Serikali, lakini hata wale wanaotoka kwenye sekta isiyo rasmi, sio tu wale wa sekta rasmi, lakini vile vile hata wale wanaotoka kwenye sekta isiyo rasmi, nao kwa mujibu wa Sheria hii sasa watakuwa wanaruhusiwa kuwa wanachama. Kwa hiyo, tunaomba tupitishe Muswada, ili kutoa fursa sasa kwa wananchi wengi ambao sio watumishi kuweza kujiunga na Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Silinde, alizungumzia masuala mengi. Kwanza, alizungumzia masuala ya pensheni kwa wazee kwamba, iwe 20,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limeelezwa sana kwamba, linaendelea kufanyiwa kazi, ni suala zito ambalo lisingeweza kuletwa kwenye Muswada huu. Kama alivyosema hata Mwenyekiti wetu wa Kamati, tafiti bado zinaendelea na *SSRA*,. Nadhani katika bajeti ijayo wakipata fedha za kutosha watakamilisha utafiti huu ili kuona na tutajua kwamba, sasa pensheni hii ya wazee kwanza iwe ngapi na ilipwe kwa mfumo gani na Mfuko gani kati ya hii au Mfuko mwingine utakaokuwa umeamuliwa na Serikali, ndio utumike kulipa hawa wazee. Lakini kwa sasa Mifuko hii inashughulikia wale wanachama ambao wanachangia tu kwenye Mifuko husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Silinde vile vile alizungumzia uwekezaji usiokuwa na tija, akatoa mfano wa *LAPF* kukopesha, ambao *CAG* ameuzungumzia na *NSSF* kutoa mikopo bila kufuata ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba, kwa sasa *SSRA* na *BOT* wanaweka *regulations* kwanza za huo uwekezaji, lakini vile vile kutakuwa na Miongozo itakayokuwa inaongoza vizuri masuala ya mikopo pamoja na hiyo ya uwekezaji. Kwa hiyo, nadhani Sheria hii mpya sasa au marekebisho haya yatawezesha usimamizi mzuri zaidi kwenye suala zima la uwekezaji na kutoa mikopo kwenye Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndassa, amezungumzia masuala kadhaa. Kwanza amezungumzia Bodi zizingatie utatu na tunasema unazingatiwa sana katika uwakilishi na tusiteuwe tu mtoto wa shangazi kwenye Bodi hizi; hilo litazingatiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini amezungumzia vile vile suala zima la matibabu ambayo *NSSF* pamoja na *NHIF* kuna *dublication* au *double contribution;* niseme tu kwamba, hili linafanyiwa kazi. Ni kweli kwamba, wafanyakazi hasa wa ngazi ya chini Serikalini, wanatoa michango mara mbili; kuna wale wanaochangia kwenye *NHIF* na *NSSF.* Kwa hiyo, hili litaangaliwa ili marekebisho yafanyike kwenye Kanuni ambazo zitakuwa zinatolewa, hili litaendelea kuangaliwa. Lakini amezungumzia vilevile tathmini ya kuona kwamba, Mifuko hii inaangaliwa isije ikafa. Nasema kwamba, hilo linafanyiwa kazi na nadhani baada ya kuipa nguvu sasa *SSRA* hili litazingatiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Blandes na yeye amezungumzia masuala kadhaa pamoja na suala la uwekezaji vilevile ambalo nimeshalisemea. *Regulations* ambazo zitatolewa na Benki Kuu ikishirikiana na *SSRA* zitazingatia hizo *Social Related Investiments* kama kwenye kilimo na kadhalika. Vile vile suala la kuingiza Kifungu ambacho kinazungumzia masuala ya mikopo kuweza kutolewa kwa wanachama, nimelizungumzia hilo. Mafao yasikatwe kodi, ni kwamba hayakatwi. Mafao yaendane na mfumuko wa bei, hilo kwa kweli ni jambo la msingi ambalo litakuwa linaangaliwa kila wakati na Mamlaka. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo kweli limekuwa likiumiza sana wanachama na hiyo tofauti kati ya Mifuko ni suala ambalo linaendelea kufanyiwa kazi na Mamlaka na hii ndio hatua mojawapo tukirekebisha Muswada wa Sheria hizi za Mifuko, sasa Mamlaka itapata uwezo wa kulisimamia suala hilo vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine aliyechangia ni Mheshimiwa Subira Mgaya, ambaye alizungumzia Kifungu Namba 18 kwamba, mwanachama vipi na yeye alipwe *interest* kama akilipwa pungufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kifungu hiki kwa kweli kinazungumzia tu Mifuko kurudisha fedha ambazo zimelipwa

zaidi ya kiwango ambacho kilistahili au kabla ya muda wa malipo, ziweze kurudishwa. Lakini hilo la kuchelewesha malipo ya mwanachama, nadhani tumelizungumzia kwenye eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Diana Chilolo, tunakuahidi kwamba hili ulilolipendekeza la kusimamia kuondoa mapungufu, tutaendelea kulishughulikia. Hili la kulipa wanachama kwa miezi sita, *PSPF* kwa kweli wanalipa kila baada ya miezi mitatu tena mwanzo wa mwezi wa tatu. Kwa hiyo, nadhani hilo halina matatizo. Pia kuongeza pensheni nadhani tumelizungumzia; kwa *PSPF* tunalipa pensheni kwa mwanachama aliyestaafu kulingana na Kanuni iliyotumika kukokotoa mafao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na yeye amezungumzia suala zima la Mifuko kukiuka taratibu za ajira na matumizi ya fedha. Kwa kweli hili labda wawe wana mtu anayevunja Sheria, Kanuni na Taratibu. Lakini Kanuni zipo na kama kuna lolote ambalo linaonekana, basi *CAG* ataliona au taarifa zitapatikana, lakini kwa kufuata Kanuni na sasa Mamlaka ipo nadhani hili halitatokea. Hili la Waziri, afute Mikataba mibovu, hilo limeshakuwa *handled* na *POAC* na hata liko kwenye Kamati ya *CAG.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa David Silinde vile vile na Mheshimiwa Mdee, wamezungumzia sana suala zima la kwamba, Kifungu Namba 29 cha Sheria Mama, tunafuta ile Mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba labda Waziri, atakuja kuelezea vizuri zaidi. Ni kwamba, Sheria ya Mirathi inabaki vilevile, hapa tunachofanya kwa kweli ni kuhakikisha kwamba, hizi *contributions* ambazo ni za wanachama zinagawiwa kama ilivyotegemewa. Kwa sababu, nia hasa ya michango hii ni kumwezesha mwanachama na wale warithi wake wa karibu waweze kufaidika. Sasa unapopeleka tu

Mahakamani aliyesimamia mirathi akaamua kupeleka maeneo mengine, inakuwa sio lengo la *contributions* hizi au michango hii. Kwa hiyo, ile itaendelea, lakini sisi tumeamua kuweka hii ili wale wanaosimamia mirathi wasije wakapeleka kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni Mheshimiwa Susan Kiwanga, aliyezungumzia suala zima kwamba, Mfuko unapokusanya fedha za wanachama, usitumie fedha hizo bila ridhaa ya wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kwa sababu kuna Bodi za utatu ambazo zinasimamia masuala yote ya fedha za wanachama na kuna wawakilishi kutoka kwa wafanyakazi, waajiri na Serikali, sioni namna gani Mifuko hiyo inaweza ikatumia fedha vibaya. Wapo watu wanaowawakilisha wanachama kwa hiyo, nadhani hili halitakuwa na tatizo mradi usimamizi uwe mzuri. Kwa sababu, kila baada ya muda kutakuwa na uangalizi kutoka kwenye Mamlaka ambayo sasa ipo, nadhani sasa hilo halitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kusimama na kutoa majibu ya Waheshimiwa Wabunge kama walivyochangia na maelezo mengine. Nakushukuru pia kwa jinsi unavyoendesha vikao vyetu vya Bunge hili Tukufu.

Pili, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mjadala huu wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Sikujua kama mngekuwa wengi namna hii kwa maandishi na kwa kuongea, lakini hii inaonyesha jinsi mlivyovutwa na marekebisho ya sheria hii ya Muswada huu. Kwa hiyo, nawashukuru sana, na

michango yenu yote kwa kweli tumeitambua, ni michango mikubwa, tukianza na Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii, wameuboresha sana Muswada huu na kufanikisha marekebisho yake.

Aidha, natambua mchango wa Kambi ya Upinzani, wametupa mawazo mazuri na nitajitahidi kutoa maelezo kama nitakavyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia nikianza na waliochangia kwa kuandika, ambao ni Waheshimiwa 16 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Anjellah Jasmine Kairuki, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Mahamoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Mch. Luckson L. Mwanjale, Mheshimiwa Zaynabu M. Vullu, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa William A. Mgimwa, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza na Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kuzungumza ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa David E. Silinde - Msemaji Kambi ya Upinzani, na Wajumbe ni Mheshimiwa Hamad Ali

Hamad, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Aliko N. Kibona, Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Dkt. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Sara M. Ally, Mheshimiwa Mustafa B. Akunaay, Mheshimiwa Naomi A. M. Kaihula, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Suzan L. A. Kiwanga, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo na Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutegemea mambo yangekuwa mengi hivi, lakini naomba niseme kwamba, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu sehemu kubwa ya wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa maelezo kwamba, mifuko hii ilipoundwa kama tunavyofahamu na kama nilivyoeleza katika maelezo yangu asubuhi, kwa kweli ilikuwa na madhumuni mbalimbali ambayo yalilenga wafanyakazi wa aina fulani. Majina yake kama yanavyojieleza, yanaonyesha madhumuni ya kuundwa kwa mifuko hii. Kwa wakati huo kama tunavyofahamu, hapakuwa na mdhibiti, wala msimamizi wa masuala ya hifadhi ya jamii ambaye angeweza kuitambua na mifuko kumtambua. Kwa hiyo, madhumuni ya marekebisho ya sheria hii ya leo ni hilo la kutambuana, mifuko kutambua mdhibiti na mdhibiti kuitambua mifuko ili mdhibiti huyu sasa aweze kufanya kazi, ambayo ndiyo hiyo maana ya kuundwa sheria hiyo ya mdhibiti ya mwaka 2008.

Katika kuchangia kwenu Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli wamezungumzia masuala mengi ambayo yamejitokeza katika Muswada wenyewe na haya ni marekebisho ndani ya Muswada huu, yamegusa vifungu vingi vya Sheria ya Mifuko

mbalimbali, lakini pia na sheria ambayo ni ya mdhibiti. Mambo mengi yalikuwa mapya na ndiyo hayo mengi mmeyazungumzia nami nitajaribu kueleza hasa yale mapya ambayo yalileta utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ambacho wachangia wengi wamekizungumzia ni suala la ukomo. Mimi siliiti la ukomo, lakini tunazungumzia vipindi viwili vya miaka mitano, mitano vya Watendaji Wakuu wa Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tufahamu kwamba sasa hivi Serikali kote tuna-*reform* kwa ajili ya Watendaji hawa na wengine wameendelea kwa kushauri kwamba, kama mifuko, Watendaji Wakuu wa mifuko wanawekewa vipindi vya miaka mitano, basi hii iende katika mashirika yote ya umma, na nafikiri huko ndiko tunakoelekea. Maana hata jana katika Sheria ya Taasisi ile ya *research* ya mifugo nafikiri na wenyewe wameweka vipindi vya miaka mitano na hii ni sababu kubwa ni kuboresha utendaji na kutoa nafasi kwa watendaji wengine kujitokeza.

Juzi kuliulizwa swali kwamba kwanini tunaachia watu wanastaafu halafu wanaendelea na mikataba? Maana yake ni hiyo kwamba tuache wigo watu wafanye kazi waonyeshe utendaji, na tunasema baada ya miaka mitano akiendelea tena mitano, akaendelea huyu Mtendaji Mkuu anaweza akatuma maombi kwenye mfuko mwingine na bado akachukuliwa na akaendelea. Wengi wamesema waendelee, lakini wengine wamesema wasiendelee. Lakini tunasema, hii ndiyo taratibu na itaendelea katika maeneo mengine. Hili halilengi mtu yeyote; asubuhi kuna mchangiaji alisema au tunamlenga mtu? Watendaji wetu wote waliopo tunawapenda na wanachapa kazi, ni taratibu, kwa hiyo, sheria hii haimlengi mtu na hii itaanza baada ya hii sheria kupitisha, leo mkishaupitisha huu Muswada, na baadaye Mheshimiwa Rais akasaini akaupitisha, basi ndiyo hapo tutakapoanzia,

haturudi nyuma. Kwa hiyo, tunaomba mtusaidie, Muswada upite ili shughuli hii ianze.

La pili lililozungumziwa na wengi ni suala la Bodi za Mifuko, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza, mimi labda nielezee kipengele cha utatu katika mifuko hii. Sisi ni wanachama wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO).* Shirika la Kazi Duniani linaendeshwa kwa utatu, iwe katika Bodi, iwe katika Mikutano yake. Utatu maana yake, kunakuwa na wawakilishi wa wafanyakazi, kunakuwa na wawakilishi wa waajiri na Serikali. Huo ndiyo utatu. Kwa hiyo, haina maana kuwa Bodi itakuwa na watu watatu, hapana!

Bodi hii mwanzo tulifikiri ingekuwa na watu kati ya watano na saba, lakini baada ya Kamati kutoa maoni, basi tukaona ni vyema tukubaliane nao tuongeze iwe na watu kati ya saba hadi tisa. Tukamwongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye mwakilishi atakuwa katika kila mfuko pamoja na mtaalamu. Kwa hiyo, kila mifuko itakuwa na watu wanane na mingine itakuwa na watu tisa na hii ndiyo maana ya utatu niliouzungumza.

Mheshimiwa Mweyekiti, suala lingine lililojitokeza ni suala la *levy* au tozo la *SSRA*. Kama mlivyoona, sasa hivi itakuwa ndiyo *moderator* wa mifuko yote. Mifuko sita katika ku-*moderate* kuna mambo kadhaa ambayo itabidi ifanye, ikiwemo kufanya hata *study* ili kuweza kujua wenzetu katika nchi nyingine wanafanya nini kuhusiana na masuala ya Hifadhi ya Jamii ili uweze kuchukua yale mazuri na kuyaleta. Stadi hizi zinahitaji pesa, lakini pia *NSSRA* itakayokuwa ina-*initiate actuarial valuation* inaweza kuwa yenyewe inatafuta *valuer actual hour*. Kama tulivyosikia asubuhi, ukweli ni kwamba hatuna ma-*actuarial* Tanzania. Hawa wataalam wakufanya *actuarial valuation* hatunao wote, ni wa nchi za nje. Kwa hiyo, kuna wale ambao *SSRA* itaona kwamba kuna haja ya kupitia mifuko yote ikiacha ile *normal routine* ya mfuko wenyewe kufanya *actuarial valuation.* Hii itamhitaji awe na pesa na

mambo mengine mengi ambayo yanagusa majukumu ya *SSRA*.

Mwenyekiti wa Kamati amelielezea vizuri sana, lakini nachotaka kuongezea ni kwamba pesa yetu ya *OS* siyo *reliable* kiasi kwamba kila wakati *SSRA* anapotaka kufanya kazi hizi ambazo kwa kweli ni kazi ambazo ndiyo kwanza anazianza, na ni kazi ambazo asipozifanya mashirika haya kama tunavyorekebisha sheria hayataweza kutimiza wajibu wake kama tunavyotarajia, kwa hiyo, kwa kutumia pesa ya *OS* ambayo wakati mwingine siyo *reliable* kwa wakati wake, haiji, siyo rahisi *SSRA* kuweza kufanya kazi zake.

Hii pesa itatokana na wanachama kwa maana kwamba itatoka katika kile kifungu tu ambacho ni cha *administration* ambacho kwa vyovyote kingetumika tu. Kwa hiyo, anachukua *percent* na hii *percent* itakuwa inakuwa *determined* na Waziri mhusika na masuala haya mara kwa mara kulingana na mahitaji. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwamba hii tozo ni muhimu na mashirika mengi yanafanya tozo, *TCRA* wanafanya, *EWURA, TIRA* wanafanya, na ni kwa nia njema.

Tulichosema ni kwamba, basi kutokana na hilo, wasiwe wawekezaji wasiwekeze kwenye dhamana, kwenye labda vitega uchumi. lakini hizi pesa wazitumie tu kwa ajili ya *administrative costs* zao na kufanya kazi ambazo zitawezesha kufanya kazi zao na kudhibiti na kusimamia mifuko hii ya Hifadhi za Jamii. Tukumbuke katika mifuko yote, jumla ya wanachama hawazidi milioni moja. Sasa ukisema utumie *OS*, ambayo ni ya walipa kodi bilioni 40, mimi nafikiri itakuwa *unfair*. Itakuwa *fair* zaidi kama kutumia fedha ya wanachama wenyewe kufanya kazi ya uanachama.

Lingine liliongelewa katika Muswada huu ni Kamati ile ya kumshauri Rais ambayo inaitwa *retirement benefit committee* ambayo Kamati hii ilikuwepo. Kama mmesoma ile Sheria ya

*PSPF* hii Kamati ilikuwepo na ilikuwa kwenye mfuko huu kwa sababu ilikuwa inashughulika na wafanyakazi hawa wa umma. Lakini tunasema mifuko hii sasa wafanyakazi hawa wa humu wanaweza wakajiunga na mfuko wowote wakitaka na wakatoka huko wakajiunga na mfuko mwingine. Katika hizi *transfer* zao au katika tatizo lingine lilojitokeza wakajikuta hawawezi ku-*qualify* kupata pensheni yao ya mwisho.

Sasa hii Kamati siyo kwamba huyu mwanachama kama ilivyoonekana asubuhi katika wachangiaji, huyu mwanachama ana-*apply* kwa Rais hapa. Huyu mwanachama au mfanyakazi ambaye katika sababu moja au nyingine anaonekana hawezi ku-*qualify* au ameshindwa ku-*qualify* kupata pensheni kutokana na tatizo lolote, anapeleka maombi kwenye hii Kamati kwa *authority* yake, kwanza kwa yule mtu aliyemwajiri kwamba mimi kutokana na hili, mimi na-*qualify* kupata mafao. Sasa *authority* itapeleka maombi haya kwenye Kamati. Katika kuitazama hii Kamati itamshauri Rais kwamba huyu tum-*exempt* kutoka kwenye hili tatizo alilokuwa nalo na a-*qualify* kupata pensheni. Kwa hiyo, haina maana kwamba mwanachama atakuwa anachukua kalamu anamwandakia Mheshimiwa Rais ili aweze kuondokana na ile *exemption* ambayo inamzuia kupata *exemption.* Nafikiri itakuwa imeeleweka.

Kamati hii tumesema sasa haitakuwa chini ya Mfuko wa *PSPF*, bali itakuwa chini ya *SSRA*, ni tofauti na ile *tribunal* ambayo iko *SSRA,* kazi zake ni tofauti. Hii ni Kamati ya kumshauri Rais kuhusu *retirement* ya watumishi wa umma ambayo kwa namna moja au nyingine walikuwa wasipate pensheni.

Suala lingine lililoongelewa ni pensheni ya wazee. Limezungumziwa na watu wengi na Mwenyekiti wangu amelielezea vizuri. Kwa kweli ni suala ambalo Kamati ilishatuleta na tuko katika hatua nzuri tu na maelezo ambayo tutatoa baadaye wakati muafaka ukifika kuhusiana na suala

hili la kuwapa wazee pensheni, na kama mlivyoshauri, tungependa iwe *universal* pensheni kiwango bado hatujajua kwa sababu kwa kweli inabidi tufanye *study* kwenye nchi mbalimbali kujua wenzetu wanalipaje, na changamoto zilizopo katika kulipa hii pensheni. Lakini ni nia ya Serikali na utashi wa kisiasa kwamba, lazima pensheni ya wazee ilipwe. Niliwahi kusema kwamba kama ni *legacy* katika Wizara hii, basi ningependa moja ya *legacy* yangu ziwe ni kukamilisha kulipa pensheni za wazee katika nchi hii. *(Makofi)*

Lingine ambalo limeongelewa ni uwekezaji wa mifuko. Mheshimiwa Naibu Waziri amelielezea vizuri, wote tunafahamu kwamba mafao ya wafanyakazi ya wanachama yaboreshwe. Ili mafao haya yaboreshwe, kitu cha kwanza lazima mifuko hii iweze kukusanya pesa kutoka kwa wanachama. Lakini pesa ile ukiikusanya, ukaja kuiweka benki, ikakaa tu inasubiri kulipa. Sidhani kama akili ya kawaida inakuonyesha kwamba ile pesa itakuwa na faida kubwa kama vile ambavyo sasa hivi wanafanya kwa kuiwekeza. Niseme wazi kwamba, mpaka sasa hamna Shirika la hifadhi ya jamii au Mfuko ambao umeshapata hasara kwa kuwekeza. Inawezakana pesa inakaa sana, lakini hakuna hasara, kwa sababu kungekuwa na hasara maana yake wanachama wale wangekuwa hawalipwi, na mafao yale yangekuwa hayaongezeki. Kwa sababu mfuko kama *NSSF*, unafanya hicho kitu kinaitwa *indexation* kila wakati kulingana na *inflation* kulingana na mfumuko wa bei.

Kwa hiyo, mwanachama anaongezewa mafao kila mara na baada ya Muswada huu kupita na kuwa sheria na kumruhusu Mdhibiti na Msimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii, sasa atapitia mifuko yote kuangalia kwamba inafanya *indexation* kuhakikisha kwamba mafao ya wanachama yanaongezeka mara kwa mara hasa wale wanachama wa kipato cha chini. Hii itawezekana tu kama mifuko hii itawekeza, lakini iwekeze mahali salama na hii ndiyo tunasema *SSRA.* Kazi moja ni kuhakikisha kwamba inaangalia uwekezaji wa mifuko ili kulinda pesa za wanachama zisipotee. Kwa hiyo, hii *vicious*

*circle* inajua kwamba ukifanya hiki inaongezea hii. Kwa hiyo, ukiwekeza vizuri, unaongezea pesa, unalipa mafao mazuri ya wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona haya niyaelezee zaidi. Nisisahau hili suala la wategemezi, lakini nafikiri na lenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri amelielezea vizuri. Limeongelewa na wengi kwamba tunapingana na Sheria ya mirathi iliyopo. Hili suala limejitokeza kwenye Mfuko wa *LAPF* lakini kila mfuko una namna yake ya kulipa mafao na una *formula* yake ya kulipa mafao.

Jambo kubwa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kuhakikisha kwamba hii pesa inakwenda kwa walengwa na kwa wakati. Mahali ambapo kunatokea ugomvi, basi *formula* hii inarekebisha ugomvi huo kwa sababu ukisema kwamba kwa mwanafunzi ambaye anasoma shule apewe 60% au mahali ambapo kuna wajane wawili wagawane mafao 60% sawa kwa sawa, nafikiri inaleta hali nzuri ya maelewano katika mgawanyo wa mafao. Vile vile tukumbuke kuwa hii siyo mirathi, bali ni michango ya wanachama ambayo baadaye ndiyo wanapewa gawio na kama anastaafu anapewa gawio lakini kama amekufa wanapewa wategemezi. Pia tumejaribu kuiweka vizuri hasa katika Mfuko wa *PSPF* ambapo mtegemezi alikuwa tena na mtegemezi mwingine, kwa hiyo, hii inaweka *a clear part line* jinsi ya kupeana mafao. Lakini Sheria ya Mirathi iko palepale, kwa sababu mirathi anaitoa mwajiri wa mfanyakazi na siyo shirika ambalo umelipa kutokana na michango yako. Ndiyo wanaokupa mirathi. Kwa hiyo, tutenganishe hivi vitu viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka katika masuala mengine ambayo yamechangiwa. Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar amesema kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ifanye kazi Zanzibar. Tunasema masuala ya hifadhi ya jamii hayapo katika orodha ya mambo ya Muungano. Kwa misingi hiyo, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliyopo Tanzania Bara

kisheria hairuhusiwi kufanya kazi Zanzibar. Hata hivyo, upo mfuko maalum unaotoa huduma hizi kwa wananchi wa Zanzibar, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuhamasisha wananchi wa Zanzibar kujiunga kwa wingi katika mfuko huo.

Lingine ambalo ameuliza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba je, mfanyakazi wa Zanzibar atatumia utaratibu gani kuwasilisha michango yake? Mfanyakazi wa Zanzibar anaruhusiwa kujiunga na mifuko hii endapo atakuwa anafanya kazi Tanzania Bara na endapo anafanya kazi Zanzibar atatakiwa kujiunga na Mfuko wa Hifadhi wa Jamii wa Zanzibar, yaani *ZSSF*. Mfanyakazi atawasilisha michango yake katika mfuko kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, ameuliza kwamba matumaini ya wastaafu yametoweka kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kucheleweshewa mafao yao au kutopata kabisa mafao yao, Serikali itatue kero hizi.

Tunajibu kwamba, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni mkombozi wa wastaafu na wafanyakazi kwa ujumla. Ukweli huu umethibitishwa na manufaa makubwa wanayopata wastaafu na wafanyakazi kupitia mafao mbalimbali yanayotolewa na mifuko. Hata hivyo, Serikali inakiri kuwepo na upungufu katika mifuko hii na upungufu huo ndiyo msingi wa kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii na pia marekebisho yanayowasilishwa. Ni maratajio ya Serikali kuwa upungufu mwingi katika mifuko hii utapungua kama siyo kutoweka kabisa, mara baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa programu ya maboresho ya Sekta ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa sababu sheria hii ikishapita, ndiyo itampa uwezo mdhibiti kuweza kuingilia mifuko na kuwaambia sasa boresheni mafao yenu au zingatieni uwekezaji na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mbunge pia alisema, wapo wastaafu ambao mpaka hivi leo hawajui hatma yao. Nafikiri ni

mwendelezo wa kuonyesha jinsi wastaafu wanavyoteseka. Mheshimiwa Mbunge anaombwa kuwasiliana na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti ili kuweza kuona namna ya kushughulikia matatizo ya wastaafu aliowataja, labda hii *specifically* waone Mamlaka ambao wapo hapa uweze kuwasiliana nao moja kwa moja ili upate ufafanuzi.

Jambo lingine ni kwamba, Serikali isimamie sana suala la jinsia na jinsi gani wananchi kutoka vijijini ambao hawafikiwi na elimu ya kutosha ya mafao. Ushauri wako umepokelewa na utazingatiwa.

Je, wazee wa vijijini na wamama wasiofikiwa na elimu hii ya mafao wafanyaje? Serikali inachukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa wigo wa huduma za Hifadhi ya Jamii unapanuliwa ili kuwafikia wananchi walio wengi ikiwa ni pamoja na wazee na akina mama wa vijijini. Hatua hizo ni pamoja na kuruhusu wananchi katika sekta rasmi na isiyo rasmi kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay anasema: "katika kuchangia hoja hii napenda kusema yafuatayo: Uwekezaji wa fedha za mifuko hii inafanyika bila ridhaa ya wanachama wa mifuko na hawapati manufaa." Anasema pia kwamba uwekezaji wa fedha hii unafanywa bila ridhaa ya wanachama wa mifuko hiyo na pia hawapati manufaa. Kwa mfano, hawapati riba yoyote, na hivyo ni kinyume cha haki za binadamu.

Tunasema kwamba wanachama wa mifuko wanashirikishwa katika maamuzi ya uwekezaji kupitia uwakilishi wao katika Bodi na pia kupitia mikutano ya wadau ya kila mwaka. Kama tulivyosema, Bodi zetu ni za utatu, kwa hiyo, wawakilishi wa wafanyakazi wapo ambao ndio wanachama. Kwa hiyo, wanawakilishwa katika maamuzi hayo ya uwekezaji. Hakuna Shirika la Hifadhi ya Jamii linalowekeza bila kupitisha mawazo na maombi hayo katika Bodi zao.

Pili, anasema kwamba wanachama wanacheleweshewa kulipwa mafao mara kwa mara, inalazimu kufungua madai Mahakamani. Nashauri kuwe na Baraza maalum, yaani *tribunal* ya kuamua mashauri hayo. Sisi tunasema kwamba Baraza linalopendekezwa lipo na limeundwa chini ya sheria ya *SSRA*, ndiyo hiyo nilikuwa nasema, Baraza hili au *tribunal* msilichanganye na Kamati hii ya kumshauri Mheshimiwa Rais kuhusu mafao ya wazee.

Tatu, anasema *pension* maana yake ni kumwezesha mstaafu kupata mapato kila mwezi. Wastaafu hasa wale wa Serikali walipwe kila mwezi badala ya miezi ya mitatu. Ushauri umepokelewa.

Suala lingine anasema Wizara maalum itakayohusika na mifuko ya jamii, mifuko yote iwe chini ya Wizara ya Fedha. Mwisho, anashauri wazee na watu wote waliokosa ajira wapewe *weakly leaving allowance* kama shilingi 20,000/= au mahitaji maalum na ameyataja kama vile unga mchele, maharage, mafuta au kodi ya nyumba kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi utakapokuwa umeboreka nafikiri ushauri huu unaweza ukafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, anasema: "Muswada huu ni muhimu kwa mustakabali wa wafanyakazi wa nchi hii. Nina ushauri ufuatao: Mifuko hii iwahusishe watu wote hususan wakulima katika nchi hii ili waweze kujikimu kimaisha. Kwa kuwa wadau wa mifuko hii sasa wanaruhusiwa kujiunga na mfuko wowote, Waziri aangalie kiwango ambacho mifuko hii inalipa, ikibidi sasa waangalie kwa pamoja kima cha chini na hata kiasi cha *pension* kwa vinginevyo mifuko mingine itakosa wateja.

Mheshimiwa Pauline Gekul, hii ndiyo maana ya kuleta marekebisho haya ili muipe meno sasa *SSRA* iingie kwenye mifuko, irekebishe, ishauri na pale ambapo kuna tatizo iweze

kutoa maamuzi na ku-*direct*. Baada ya hapa, kama tunasema hii ni awamu ya kwanza ya marekebisho, awamu ya pili sasa itaingia kwenye mafao, uchangiaji na hata katika mafao yale itaweza kuhitaji mifuko iweke *segmentation* kama ni fao la matibabu ni asilimia ngapi, kama ni fao la mazishi ni asilimia ngapi. Kwa hiyo, yote hayo yatawezekana baada ya sheria hii kupita.

Muda wa malipo ya *pension* uoanishwe na mifuko yote ili isitokee kuwa mifuko fulani inalipa kila baada ya miezi mitatu na mingine kila baada ya mwezi. Mimi nafikiri hapa anazungumzia *pension* ya watumishi wa umma. Ushauri umepokelewa.

Faida ya uwekezaji igawiwe kwa wanachama na siyo kwa wafanyakazi na pia mafunzo yatolewe mara kwa mara ili wajue stahili zao badala ya kubaki kutabiri *pension* zao. Tunasema kwamba faida ya uwekezaji hutumika kulipa mafao ya wanachama wa mfuko husika na faida hii haiendi kwa mfanyakazi wa mfuko, labda kama na yeye ni mwanachama wa mfuko huo.

Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah anasema kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana juu ya mipango ya maisha na maendeleo kwa ujumla, kwa hiyo, ni lazima marekebisho yote yazingatie haki na usawa wa hifadhi na kulinda mifuko hiyo. Ushauri umezingatiwa.

Mheshimiwa Waziri, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wafanyakazi uwe katika Wizara moja tu na siyo kila Wizara. Hii italeta ufanisi wa usimamizi wa mfuko huu na itarahisisha uendeshaji. Ushauri huu umetolewa mara nyingi na unaendelea kutolewa na hata Kamati imeshauri sana. Suala hili litakwenda kwa mchakato kwa sababu siyo jambo dogo, lakini tunatambua umuhimu wa kuwa na hilo na tutaendelea kulifanyia kazi haraka na mapema kadri tutakavyoweza.

Kuhusu marekebisho, kifungu cha 5(e), (f) na (i) cha Sheria namba 8 ya *SSRA* kinachoelezea majukumu ya mamlaka kifanyiwe marekebisho ili majukumu haya yafanywe na Wizara ya Kazi na Ajira chini ya Idara. *In fact,* tumeshafanya marekebisho hayo katika *amendments*.

Mheshimiwa John J. Nyika, Mbunge wa Ubungo, anasema Muswada wa Sheria ya Marekebisho, Sheria za Mifuko ya Jamii ni nyenzo muhimu za kutekeleza Sera ya Hifadhi ya Taifa ya Jamii, ili kuongeza ustawi wa wananchi na nchi kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, marekebisho yaliyowasilishwa ni machache ambayo hayashughulikiwi kikamilifu. Malengo ya sera husika na mapendekezo mbalimbali ambayo Wabunge tuliyatoa katika Mkutano wa Nne wa Bunge mwaka 2011 kuhusu masuala ya kuzingatiwa katika marekebisho, hivyo katika majumuisho Serikali ieleze nini hatma ya mapendekezo mengine ambayo Wabunge tuliyatoa ambayo hayajaingizwa katika Muswada tunaoujadili katika mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mnyika sasa kwa kuwa hujayataja, lakini niseme tu kwamba marekebisho hayo kama nilivyosema awali, ni awamu ya kwanza, yaani kwanza kutambuana mifuko hii na *SSRA*. *SSRA* ikishapata utambuzi ikapewa meno na nyenzo, sasa itaingia kufanya marekebisho katika mifuko na ita-*coordinate* mifuko. Kwanza nikwambie kwamba imeshaisajili yote, imeshaitembelea, na imeshajua matatizo na *actuarial valuation* zote wanazo na wanajua hata *assets* za mifuko zimekaaje. Kwa hiyo, afya za mifuko tayari *SSRA* anazo, tatizo hajakuwa na uwezo bado na hajatambulika kisheria kuingia na kuwashauri kwamba *formula* hii iwe hivi na mambo mengine kadhaa. Kwa hiyo, sina hakika hayo uliyoshauri yanahusu haya ambayo bado tunayafanya awamu ya pili au vipi. Kama ndiyo hivyo, nashauri kwamba maboresho ya Sekta ya Hifadhi za Jamii, yanayohusisha hatua ya pili, tusubiri tutayaleta hapa kwenu na yataboreshwa na yatashughulikiwa.

Aidha, wigo wa mjadala wa hifadhi ya jamii unapaswa kupanuliwa hususan wakati wa mchakato wa Katiba mpya ili kuhakikisha hifadhi ya jamii inakuwa na haki ya lazima ya wananchi wote. Uamuzi huu uende sambamba na kuweka mfumo wa kikatiba, kisera na kisheria ambapo kila mwananchi kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wote, yaani *Universal Social Security* atapata gawio kutoka katika mapato ya raslimali na maliasili ya nchi ikiwemo madini, mafuta, gesi asilia na kadhalika. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii unapaswa kuhusisha pia wananchi walio kwenye sekta isiyo rasmi ambayo tumefanya, wazee wote, wakiwemo waliokuwa wakulima na wafanyabiashara ndogondogo na vijana wasiokuwa na ajira kwa marekebisho ambayo yanawasilishwa sasa. Hatuwezi kwenda kwa haraka kiasi hicho. Nguvu zaidi iongezwe katika masuala muhimu ambayo yanagusa kwa kiwango kikubwa wananchi ikiwemo Jimbo la Ubungo. Tunakubaliana na wewe, tupe muda, tutafanya hivyo hatua kwa hatua, lakini kwa hatua za haraka.

Mosi, kudhibiti Mifuko ya Hifadhi ya Jamii dhidi ya uwekezaji usiokuwa na tija. Nafikiri tumejaribu kueleza kwamba uwekezaji wowote mtu hawezi kuendelea kuwekeza kama hakuna tija. Kwa hiyo, kuna tija na ndiyo hiyo inayoleta faida kwa wanachama.

Pili, kuhakikisha wigo wa mafao unapanuliwa na kuwezesha wanachana kupata stahili zote na kwa wakati. Nguvu hizo zinapaswa kuongezwa kwa Serikali kuwasilisha jedwali la marekebisho juu ya vifuatavyo:-

Kifungu cha 15 kinachoongeza kifungu cha 29, kimeainisha na taratibu na utamaduni muafaka za mirathi. Hili nimelieleza.

Kifungu cha 21 kinachofanyia marekebisho kifungu cha 49 kuwianisha Mamlaka ya Benki Kuu na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhusu uwekezaji, tumesema

katika uwekezaji wote lazima wafuate miongozo na *guidelines* na taratibu zinazotolewa na Benki Kuu pamoja na Mamlaka kama mtaalamu katika suala hilo la uwekezaji. Kwa hiyo, hili tumelizungumza na katika kila mfuko, mahali ambapo walikuwa wanawekeza kiholela na tumesema atakayewekeza mahali ambapo ni hatarishi wa fedha za wanachama, kuna hatua na adhabu ya kuchukua. Pia tumesema kwamba katika masuala yote ya kupata hata hiyo thamani ya uwekezaji, thamani ya pesa yao ya *actuarial valuation,* lazima sasa Mamlaka ihusike lakini masuala yote ya uwekezaji, lazima yafuate *guidelines* za Benki Kuu pamoja na Mamlaka yenyewe. Iko katika jedwali la marekebisho.

Kifungu cha 66 kinachoongeza kifungu cha 71(b) kuondoa mkanganyiko uliopo kati ya kifungu cha maelezo ya pembeni kuhusu Mamlaka yenye dhamana ya kupokea taarifa, hapo sijaelewa kidogo, lakini tutakapokuwa tunaendelea na vifungu, nafikiri tutaelezana vizuri zaidi.

Kifungu cha 150 kinachoongeza kifungu cha 49(a)(2), kiwango cha tozo kizingatie faida na uwekezaji ili wanachama wasibebeshwe mzigo wa gharama. Nimesema katika hii tozo mwanachama wala hata-*feel* kwa sababu ni ile ile pesa ambayo imekuwa ikitumika katika masuala ya *administration*. Kwa hiyo, mwanachama hataguswa kwani mafao yao yako pale pale, kama wataongeza mafao yeye ataendelea kuongezwa na huku tozo litafanyika kwa kupitia mfuko wenyewe.

Katika majumuisho, nilitaka nieleze pia hatua zilizochukuliwa kutokana na tuhuma mbalimbali katika matumizi ya uwekezaji wa Mfuko wa Jamii. Upi sasa? Kati ya mwaka 2005 – 2010 ili kufungua ukurasa mpya wenye kuzingatia uwajibikaji, kama unazungumzia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *LAPF* kuhusiana na hoteli ya *Millennium Tower,* suala hilo lipo sasa hivi kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ambaye ameambiwa aingie afanye *audit* ili kusudi

aweze kugundua, ingawa hili lilishafanyiwa kazi na Kamati iliyopita ya Hesabu za Serikali, lakini wakaambiwa wafute ile kwa sababu kwa kweli lile jengo lilirekebishwa na ni la kwao, ingawa walimkopesha yule jamaa wa *South Afrika.* Lakini lilirekebishwa, kwa hiyo, wakaambiwa mnaweza mkafuta haya madai. Lakini bado wana madai mengine, sasa *CAG* atakagua, ataangalia hali halisi na taarifa itatolewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la Rebecca Michael Mngodo kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya msaada wa mazishi hasa kwenye Mfuko wa *NSSF*. Sheria iliyounda Mfuko wa *NSSF* ambayo ni *Cap. 50* inaruhusu uwekezaji kupitia Bodi ya Wadhamini, haya ni masuala ya uwekezaji.

La pili, linasema malipo hayo ya msaada mazishi ambayo wanasema yanacheleweshwa, lakini tukumbuke kwamba unapokuwa umefiwa ni *member* wa *NSSF* unachotakiwa kufanya ni kugharamia mazishi. Baada ya kugharamia mazishi, sasa ndiyo unakwenda *for embezzlement* ya hiyo fedha uliyotumia. Sasa hapo inavyoonekana ni kwamba malipo hayo yanayolipwa kwa ndugu, mara nyingine hawaleti maombi mapema kwa sababu ni lazima vielelezo au *receipt* ili kuonyesha gharama walizotumia mara wanapoleta vielelezo, malipo hufanywa, na *NSSF* wakati wowote iko tayari kuonana na Mbunge ambaye ameleta suala hili ambaye ni Mheshimiwa Rebecca kama kuna mwanachama aliyeathirika na suala hili, basi alilete ili liweze kufanyiwa kazi kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengi yanajirudia, lakini niseme, sikujibu masuala ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii kwa sababu kama alivyo-*note* Mwenyekiti, mengi tumeyaweka kwenye jedwali la marekebisho. Kwa hiyo, nikaona hapa kuyasoma ni kama *repetition*. Ni mengi, lakini yote tumeyazingatia.

Suala ambalo ningependa niwahahakishie Mwenyekiti na Kamati yake, waliloshauri kuhusu kuanzisha Idara ya Hifadhi ya Jamii, tumeizingatia kwa umuhimu wake kwa sababu tukiwa na Idara ndiyo sasa itakuwa inamshauri Waziri kwa umuhimu wake. Kwa sababu tukiwa na Idara ndiyo sasa itakuwa inamshauri Waziri kuhusiana na masuala yote ya kisera yanayohusu hifadhi ya jamii. Kwa hiyo, hili naahidi tutalifanyia kazi na Idara itaanzishwa. Naomba nisiahidi kwamba ni kuanzia lini, kwa sababu ni mchakato ambao unahusisha pia Idara Kuu ya Utumishi, lakini sisi kwa upande wetu tunasema tutalifanyia kazi. Ningependa kuona kwa kweli Idara hii inaanzishwa kwa sababu sasa suala la *SSRA* ili liweze kufanya kazi vizuri, ushauri uweze ku-*flow* kutoka *SSRA* kuja kwenye Wizara, lazima tuwe na Idara kamili ya *social security* chini ya Wizara hiyo ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimeacha mengine siyo kwa makusudi, lakini jambo kubwa hapa hasa linalohusu marekebisho ya hii sheria, nimeona *amendments* zimekuja nyingi. Sasa nikishaona *amendments* nyingi hivyo, naogopa, kwa sababu masuala ya kisheria haya ni magumu. Lakini mngekuwa radhi kutuletea masuala haya tukayajibu hapa, ingekuwa rahisi zaidi na tusingepoteza muda. Sina hakika hizi *amendments* nyingi tutazi-*accommodate* namna gani, lakini kwa ujumla, tukumbuke kwamba lengo la hii ni kupanua wigo wa hifadhi ya jamii na ndiyo maana tumeona mifuko yote sasa itoke katika ile *traditional way* ya kuchukua wanachama kutoka *only specific areas,* yaani *Parastatal Organisations, Local Governments, Public Servants,* lakini sasa ipanue wigo kwa kuchukua *private* rasmi, *private* wasio rasmi, lakini pamoja na sekta binafsi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Tanzania bado tunahitaji kupanua wigo. Ukisikia ni kwamba katika watu milioni 40, ni milioni moja ambao wako *covered* na hifadhi ya jamii. Kwa hiyo, naomba tushirikiane na hii inaweza kufanyika vizuri kama mamlaka hii itakuwa imeanza kazi vizuri na imeingia sasa

kwenye mifuko kuwahimiza na pia kufanya ushindani. Kuna mchangiaji mmoja amesema ushindani uwe wa mafao na usiwe wa wanachama. Ushindani utakuwa kwa sehemu zote mbili; utakuwa wa kuongeza wanachama, lakini pia wa kuboresha mafao.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba pamoja na *amendments* nilizoziona, tujitahidi kupitisha Muswada huu kwa haraka kwa sababu tumechelewa. *SSRA* imeanza mwaka 2008 kwa sheria ile, mpaka sasa hivi bado hatujaweza ku-*coordinate* hii mifuko kwa kutumia sheria hii. Kwa hiyo, ni wakati muafaka kwa kweli leo tupitishe Muswada huu ili tuweze kuanza hii kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 *(The Social Security Laws (Amendments) Act, 2012)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Marekebisho ambayo yamefanyika na Serikali, nakubaliana nayo pamoja na hoja ambazo Mheshimiwa Waziri amekuwa akizijibu. Lakini tunapofanya marekebisho haya katika sheria hizi ni lazima tuangalie faida na hasara ambazo tunaweza tukazipata. Kwa kufanya ambayo yameandikwa katika kipengele hiki kwamba, kuwe kuna ukomo wa Mkurugenzi au Mkuu wa Taasisi ambayo anaiongoza, kwanza kabisa itapingana na *Public Corporations Act* na *Public Service Act.* Kwa maana kwamba, sheria hizi zinampa mamlaka Rais kuteua mtu ambaye anaona anafaa. Tunapoweka *limitation* ina maana tayari kabisa tunambana Rais kutokuwa na mamlaka ambayo tumempa kikatiba.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuliangalie hili jambo katika upana unaoonekana kwa maana kwamba, pia ikiwa mtu ana umri wa miaka 35 leo amefanya kazi kwa kipindi cha miaka 10 na hawezi kuendelea, tayari huyo ni *retired officer* kwa miaka 45. Tunaipeleka wapi hii nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, unapomwekea mtu ukomo kwamba asiendelee tena katika kipindi ambacho atamaliza, itafika wakati watu watakuwa

wanajilimbikizia mali kwa kuamini kwamba hataendelea. Hii ni sawasawa na Mungu alipotunyima kujua siku zetu za kifo. Ingekuwa kila mtu hapa anajua siku yake ya kifo kwa kweli hii dunia isingekalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ikubaliane na hoja ambayo nimeileta kwamba tuondoe hicho kifungu mpaka pale ambapo tutafanya marekebisho kwenye mashirika mengine yote, lakini kwa kutoa uhuru ambao tumeutamka wenyewe kikatiba na katika sheria ambazo tumezitunga. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AJIRA NA KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mangungu ametoa hoja nzito. Sasa labda tungemwacha labda *AG* atusaidie kwa sababu amezungumzia mamlaka ya Rais na masuala mengine. Sisi tulidhani kwamba kwa kweli hii ndiyo njia nzuri ambayo Serikali imeshaamua kwenda nayo, lakini kwa mujibu wa hali ya mifuko hii, kwa sababu ni mifuko ambayo inasimamia fedha na tofauti na taasisi nyingine, hii hoja tunaweza tukaiangalia. Labda tupate ushauri wa *AG*.

**MWENYEKITI:** Kaa tu Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa nadhani, kwa namna nzuri, kwa sababu tuko kwenye Kamati na pengine watu wanasimama, nadhani mwenye hoja kasema, tuangalie kama ana wengine wanaomuunga mkono, halafu Serikali ikisimama ina-*consider* kwa upana wake kilichosemwa. Sasa nimruhusu Mheshimiwa Chenge halafu baadaye Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Mimi nimemwelewa sana Mheshimiwa Murtaza Mangungu kwa mapendekezo yake. Lakini tatizo ambalo ninaliona katika pendekezo lake ni kwamba, ukishafuta kile kifungu cha (7) ukakiondoa kabisa, utakuwa hujafanya kile ambacho amekielezea kwa ufasaha sana. Mimi naelewa tatizo hilo alilolisemea, na jana nilipata

matatizo kidogo kwenye ule Muswada tulioupitisha kuhusiana na Mkurugenzi Mkuu ambaye tumemfunga kwa sura hii, maana kwenye vyombo kama vya utafiti, kadri mtu anavyofanya kazi hizo ndiyo anapata ule uelewa mpana sana, na kwa mifuko hii ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuisaidia Kamati yako, badala ya kukifuta kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mangungu, tufikirie sasa kupata hoja anayoitaka yeye. Ukikisoma kifungu cha 7(3) tunaweza tukasema: "*The Director General shall hold office for a term of five years and may be eligible for re-appointment."* Sasa hiyo utakuwa umepata dhana nzima ambayo inamsumbua Mheshimiwa Mangungu na naamini na Waheshimiwa Wabunge wengi tu humu. Tukienda namna hiyo tutakuwa tumefanya kazi nzuri sana ya kutunga sheria hii kwa mifuko yote, maana tutalikuta mbele kwenye kifungu cha 32(5), 42(3), 83(3), 129(4) na 144(3). Yote haya yana sura hiyo hiyo, lakini napendekeza tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasimama kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mangungu, lakini naona Mheshimiwa Chenge amekwenda na wazo nililokuwa nataka kulisema la kwamba, ili kukiboresha badala ya kukifuta, tufute yale maneno tu yanayoishia pale mwisho kama alivyosema Mheshimiwa Chenge, "*the Director General."* Lakini sasa kwenye *shall* ile ya kwanza kwenye *amendment* ya Waziri ilishawekwa *"may"*. *May hold office for a term of five years and shall subjected to the satisfactory performance be eligible for re-appointment."*

Sasa tukiishia pale kwenye *"re-appointment for another term only"* ile tukiondoa sasa nadhani tutakuwa tumetekeleza ile azma nzuri aliyoisema Mheshimiwa Mangungu, lakini tutakuwa tumekwenda na *idea* hii aliyoisema Mheshimiwa Chenge na nafikiri tutakuwa tumetoa uwanda mzuri wa

kuwafanya hawa *directors* wetu wafanye kazi zao kwa uhuru, lakini kwa kujiamini, na pia kwa utekelezaji wa majukumu ambayo wamekabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja yangu nyingine ya msingi ni kwamba iko sheria ambayo inamlinda mteuzi wa hawa ma-*CEOs*. Sheria ile ya uteuzi wa hawa ma-*CEOs* inaonyesha namna gani mkataba wao wa kazi unaendana na kazi waliyokabidhiwa na mwenye mamlaka ya uteuzi. Kwenye sheria ile mwenye mamlaka ya uteuzi pia anayo mamlaka ya kumwachisha kazi *CEO* yeyote yule ambaye ataonekana kwamba ha-*perform* vizuri katika madaraka yale ambayo amekwisha kukabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaona kabisa kwamba yeyote atakayeteuliwa kama ataonekana sio mtu wa kutekeleza majukumu yake vizuri, bado mkataba wake na zile sheria na kanuni za uteuzi zitamfanya yule mwenye mamlaka ya uteuzi kumwondoa. Kwa hiyo, nadhani ushauri wa Mheshimiwa Mangungu ni mzuri, lakini tusikifute kifungu chote, nikubaliane na mawazo ya Mheshimiwa Chenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mimi mwenyewe sio Serikali, lakini kwa kweli ukiangalia unaposema, maana hata Ubunge, ukiambiwa Ubunge mwisho kipindi hiki, sijui kama hata huko Kimboni utakwenda kwenda. Sasa hebu mlione hili.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa wakati tunapitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kwamba, utungaji wa Sheria katika mfumo wa Vyama vingi ni mashauriano na wakati mtu anaposema *point* unaiona inakidhi nafikiri ni vizuri pia ku-*concede*. Sasa pendekezo la Mheshimiwa Mangungu nafikiri limefanyiwa marekebisho. Nia yetu ya mwanzo nafikiri tulikuja na nia kwamba, tuweke muda bila kufikiria kwamba haya

kweli ni mashirika ya fedha na mashirika haya ya fedha yanahitaji namna ya pekee ya kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge waliosema kwamba marekebisho haya tunaweza kuishia tu kwenye (naomba nisome): "*The Principal Act is amended in section (*8)." Halafu unasema: "*adding immediately after sub section (2) the following new sub section*." Sasa ukiangalia maneno hayo na sheria nzima, kile kifungu chote cha (8) utaona kwamba, mteuzi wa *Director General* pale ni Mheshimiwa Rais, na anakuwa *appointed on such terms and conditions as shall be determined by the President in the letter of appointment,* kama alivyosema Mheshimiwa Mhagama kwa sauti nzuri ya kupendekeza. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba kwenye yale maneno: `*the Director General shall hold office for a term of five years and may subject to satisfactory performance be eligible for reappointment."* tuishie pale tu na tufanye hivyo kwa vifungu vyote vinavyohusika na suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Lakini niseme tu kwamba, niliomba hoja ambayo imejengwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa *AG* ina mashiko na nashukuru kwamba na wao wameona *concept* ambayo nilikuwa nayo. Lakini ningependa tu kama tutakuwa tumeafikiana hivyo, tuishie pale ambapo inasema *for re-appointment* kwa maana kwamba, inasema *subject to satisfactory performance be eligible for re-appointment*. Kwenye vipengele vyote, nakubaliana na hivyo na sitakuwa na haja tena kusimama kwenye vifungu vingine vyote kwa sababu kwenye hii *schedule* ambayo nimei-*move* vipengele hivi vyote vinawiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 8

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, sentensi hizo zinawiana. Kwa hiyo, nilisema tu katika vipengele vyote ambavyo nimeviainisha humo, basi tukubaliane iishie pale kwamba, mtu atakuwa *re-apointed for other terms.* Kama utaisoma vizuri, iishie hapo hapo *for re-apointment* isiweke *limitation*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawasawa lakini isipokuwa kwamba sasa hakutakuwa na *re-numbering*.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, tunaweza tuka-*proceed, no re-numbering.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta *schedule* ya *amendment* kuhusiana na kifungu cha 12 cha Muswada unaoletwa hapa. Kifungu hiki kinazungumzia

kuongeza kifungu kingine kipya kwa maana ya kifungu cha 24A lakini baada ya kifungu cha 24A inapendekezwa ku-*retain* kifungu cha 24 cha Sheria ambayo tunaifanyia mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu hivi viwili kimsingi kimaudhui vinafanana wala havina tofauti kwa sababu kwenye kifungu hiki ambacho tunapendekeza kuweka sasa hivi ambacho mimi sina shida nacho, kinazungumzia kwamba Bodi kila baada ya miaka mitatu itakuwa inafanya tathmini ya mali au madeni ya mifuko na pia baada ya tathmini hiyo taarifa hiyo itakuwa inapekekwa kwa mamlaka husika pamoja na kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika. Baada ya hapo, mamlaka itatoa maelekezo namna ya kuondoa matatizo ambayo yatakuwa yamejitokeza.

Sasa hiki ndio kifungu ambacho tunapendekeza kiwepo kwenye sheria hii. Lakini hapo hapo wanasema baada ya kifungu hiki na kile ambacho kilikuwepo ambacho kinafanana na hiki *exactly* kwamba na chenyewe sasa kiendelee kuwemo na hicho kifungu kiwe kinapendekeza miaka mitano ifanyike tathmini ya madeni pamoja na mali, taarifa iende kwa Waziri na Waziri pia aelekeze namna ya kurekebisha hayo matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nasema kwamba hii ni kujirudia na ningemwomba Mheshimiwa Waziri alione hili kwamba tunapotunga sheria tunataka tutunge sheria ambayo imenyooka haina utata. Sasa vifungu hivi viwili vinafanana, hakuna sababu ya kuvirudia. Kwa hiyo, ningependekeza kifungu hiki kimoja ambacho ni 24A kibaki hapa, kile kingine kisiingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Blandes kwa umakini wake. Ni kweli kifungu hiki kinajirudia, kwa hiyo, kibaki kama kilivyo katika *amendment.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Katika kifungu cha 15(29) nilikuwa napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri kwamba ameyachukulia maoni ya wachangiaji wa Bunge kwa kiasi gani? Kwa sababu hiki kifungu kikienda kupitishwa kwa jinsi kilivyo, kitakuja kuleta hatari ya mchanganyiko kwa wale wanachama ambao wataingia katika mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu gani? Kwa sababu hiki kifungu tayari kimeshaweka asilimia kwamba ikitokea umefariki, mafao yako yagawanywe kwa jinsi gani. Nilikuwa nashauri kwamba hili liachiwe kwa wanachama kwa sababu hili siyo geni. Mashirika mbalimbali wameshawahi kufanya hivyo, inapotokea umefariki, basi kuhusu nani arithi, nani achukue hayo mafao yako, ikitokea huna *dependants* wanaokutegemea, mafao yako apewe mzazi wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inapofikia hatua kwamba na wazazi nao wamefariki, Kwa hiyo, tukipitisha hiki kifungu kama kilivyo, mimi nafikiri baadaye itatulazimu tena kufanya marekebisho katika kifungu hiki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akiangalie hiki kifungu tusikipitishe kama kilivyo, bali tuwaachie hao wanachama watakaojiunga katika hiyo mifuko waweze kuamua taratibu kwamba nani anachukua mafao yao badala ya sisi kuwapangia kwamba asilimia 40 apewe labda yule

mjane, asilimia 60 wapewe wanafunzi au wale watoto ambao wanasoma. Hapa kwenye hiki kifungu inaonyesha kwamba ni mtoto mmoja na hatujataja `*children'*, kinasema `*child'*. Kwa hiyo, hiki kifungu tusikipitishe kama kilivyo, bali tuzingatie yale maoni ambayo yametolewa. Ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza majibu ya Waziri nilijua angenieleza kwa kina, lakini hajaeleza kwa kina. Ameeleza kwamba Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi siyo mirathi ila ni michango. Sasa sisi tunajua kwamba mtu anapochanga ile ni mali yake kwa ajili ama ya akiba yake akistaafu ama kwa familia yake, chochote kitakachotokea.

Sasa kwa majibu ya Waziri tafsiri yake ni kwamba, na narudi katika mchango wangu tuna Sheria ya Mirathi ambayo inaeleza mali ambazo zinaachwa na marehemu zinaratibiwa kwa utaratibu gani? Nikaenda kuangalia kifungu cha 27 cha sheria mama ambacho tumekipachika kifungu cha 29.A kifungu hiki kinaeleza wazi kabisa kwamba fedha ambayo itabaki niseme kwa tafsiri ya Kiingereza, *the total amount standing to the depositor to be paid to him or her."* Katika mazingira yafuatayo kama aki-*retire* au akifa ama akiwa *terminated* kwamba anaweza akalipwa yeye ama warithi wake, sasa inakuwaje tunapachika kifungu kingine cha 29.A ambacho hakina uhusiano wowote na vifungu vingine kwenye sheria? Halafu tunafanya mgawanyo kwa mali ya yule mtu ambaye ameweka akiba yake kwa matakwa ambayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inataka?

Kwa hiyo, mimi nadhani ni hatari. Mnaweza mkatoa tafsiri ambazo mnataka kuzitoa nyinyi, lakini hiki kifungu kimepachikwa kienyeji, hakuna sehemu yoyote inayohalalisha uwepo wake. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili suala kwa kina. Kuna utaratibu umewekwa, mali za aliyekufa zinagawanywa vipi, kutokana na mila na imani na vitu vinavyofanania na hivyo. Kwa hiyo,

nilitaka nipate tafsiri sahihi kwa sababu, sheria mama haizungumzii chochote, mmepachika pachika tu. Sasa sijui mna malengo gani! Watu wasije wakauana huko kwa sababu wanajua sheria tayari inawalinda, waanze kuua wazazi wakijua kila mmoja ana *portion* yake. Kwa hiyo, hiyo ndiyo ilikuwa *concern* yangu. Ahsante.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi siko mbali sana na wenzangu. Kwa sababu mtu anapokuwa amefariki mali yake yote tayari inakuwa ni mirathi, iwe wapi na wapi; tuko watu tofauti, tunatumia sheria tofauti hususan kama sisi Waislam, kuna sheria mahsusi kwa mgao wa mirathi. Sasa hiki kipengele kitaleta shida sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri akiangalie upya kisilete matatizo ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ruhusa yako nitoe elimu kwanza ili twende pamoja. Ni vizuri twende pamoja kwa sababu nadhani nilimsikia sana dada yangu Mheshimiwa Mdee, alisema anataka kuelimishwa tu, sidhani kama ana nia ya kukwamisha.

Tunachozungumzia hapa, sio mirathi. Tunachozungumzia hapa, ni *survivors pension* na kifungu cha 29 kinazungumzia hiyo. Pia Waheshimiwa Wabunge kuna ile Sheria ya *National Social Security Fund,* wale ambao wanayo sheria, kile kifungu cha 34 kinazungumzia *issue* za *survivors pension*, ambacho ameleta Mheshimiwa Waziri hapa. Nitakwenda taratibu kusudi tuelewane, kwani sidhani kama kuna ujanja na sidhani kama kuna mtu humu baina yetu ambaye angekuwa *careless* kwamba atakapokuwa ameondoka ile pensheni yake iende kwa watu ambao hakutaka watumie, na mimi sitakuwa mmojawapo wala wa mwisho wala wa kwanza.

Waziri anasema hivi, kwenye kile kifungu kinachokuja kipya anasema: *"The survivors pension payable to a dependant shall be made on the basis of the percentage described herein."* Hiyo siyo mirathi, ni *survivors pension*. Watu ambao wanakutegemea kwamba, kama haupo wapate asilimia gani, hiyo ni *issue* ya sheria ya ku-*regulate* haki zako, wala sio mirathi. Sasa nasema kama wewe ni mjane au ni mgane, (mgane ni wale wanaume waliofiwa na wake zao) utalipwa asilimia 40. Utauliza swali kila mwezi, utaulizwa swali linakuwaje, asilimia 60 inakwenda wapi? Sasa naomba Waheshimiwa Wabunge, twende taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniwie radhi. Kama wewe ni mgane, umefiwa na mkeo alikuwa anapata hii *survivors pension,* unaipata kwa sababu ya mke wako aliyefariki, Mungu amuweke mahali pema Peponi, utapata asilimia 40. Kama ni mjane, ni hivyo hivyo na kila mwezi. Nasema wako ambao wanaona hawawezi kukaa na mke mmoja, ana wake wengi, ile asilimia 40 utagawa *pro-rata* kwa wake wote. Sasa kwa sababu sheria hairuhusu wanawake kuwa na wanaume wengi hapa mume ni mmoja tu. Kwa hiyo, mume ndio atapata asilimia 40. Hatuwezi kusema kama mwanamke ana waume wengi bado atapata *pro- rata.*

Sasa kama bahati mbaya hakuna watu wanaokutegemea, hakuna watoto, mjane au mgane atalipwa asilimia 100 ya hizo fedha. Hii hapa hatufanyi mgawanyo, wala siyo mirathi, hayo ni mafao. Sasa kama kuna mtoto mdogo ambaye anasoma atapata asilimia 60. Kwa hiyo, kama kuna mjane au mgane atapata asilimia 40, kama kuna mtoto anayesoma atapata asilimia 60.D, kama hakuna mjane wala mgane, wale watoto watapata asilimia 100. Sasa ile ya mwisho, "*in the case where there are no dependant, children; or dependant spouse"* hakuna mgane hakuna mjane, wazazi wako watapata asilimia 100 ya *survivors pension*. Kama hawapo, ndiyo suala ambalo nilikuwa najiuliza hapa na ndugu zangu. Kwa sababu maswali yenu ni mazuri, kama hawapo

inakuwaje? *Definitely,* itabaki kwenye mfuko. Nisikilizeni, ndiyo maana mnatakiwa mwandike wosia. Tuzungumze kama watu wazima, tusiseme tu aah! Unatakiwa uandike wosia. Wengine mnaogopa kifo, utakufa tu! Andika wosia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri kwamba hii ni *survivors pension* na suala la dini halihusiki wala mila na desturi hazihusiki. Hii hapa ni kwamba mfuko utafanyaje mafao hayo? Mheshimiwa sio kwanza tunaanza, ndivyo ilivyokuwa kwenye sheria ya *National Social Security* kile kifungu cha 34 ambacho nasema, kwa sheria niliyonayo hapa, kinasema hivi:

Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri elimu inahitajika hapa. *"The survivors pension payable to a dependant shall without presidency to the relevant laws of inheritance. But subject to any will of the deceased be in the prescribed percentage."* Yaani *percentage* hii itakuwa hivi, *unless* kama wewe au mimi nimeandika wosia wangu.

Sasa inasemaje. *"(a) In the case of a widow or a widower, forty percent of the pension, and where there more than one widow, the amount shall be divided equally amongst the widows. In the case of a dependant, child under18 years of age or under 21 years receiving full time education or the case may be, shall be paid 60 percentage of the pension to be divided equally among the children".*

Kwa hiyo, hivyo ndiyo hali yenyewe, lakini pia niliomba kusoma kwenye Muswada ule 29(a) angalia (e) narudia kwenye Muswada wenyewe ukurasa wa 15. *"In the case where there no dependant, children or dependant spouse, parents of the deceased shall be paid one hundred percent of the pension for the remainder of their life,"* au tuseme kama hawapo: Je, zile zibaki kwenye mfuko.

Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna msimamizi wa mirathi ambaye ameteuliwa kisheria, hizi fedha zitakuwa

*administered* na hii siyo kitu kipya, kifungu cha 29 kilicho kwenye sheria hizi, sasa kinasema hivyo kwenye kifungu cha 29(1) (c) na (d) kwamba kinaweza kwenda kwa *executor* or *administrator* au kwa *administrator general.* Kwa hiyo, nadhani Waheshimiwa Wabunge tunachohitaji ni kusoma hii vizuri na kupata elimu ya kutosha kuelewa. Hili siyo suala la mirathi, hili ni suala la mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Jamani, kwa ufafanuzi huo kwamba ni *survivors pension,* hiki ni kitu ambacho kipo, watu wanagawana, kitaendelea kuwepo isipokuwa watu ndio wanaondoka. Kwa hiyo, ukituwekea *formula,* hata wakiwa hawapo, ndiyo hiyo itabakia.

Kwa hiyo, kwa ufafanuzi huo, Waheshimiwa Wabunge, kuna haja ya kuendelea na mjadala au niwahoji tu kifungu hiki kama kilivyo pamoja na ufafanuzi huu uliotolewa, maana alisema atafundisha na ndiyo kazi yake humu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni mshauri wetu sote.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

**MBUNGE FULANI:** Zihesabiwe kura.

**MWENYEKITI:** Mimi ndio niliyesikia.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa!!!!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, anayesimamia uamuzi ni Mwenyekiti. Sasa kama tunaamua wote, sijui Mkutano huu utakuwaje. Nadhani kwa hakika nataka niseme hata kama tutaamua kufanya vile tutakavyoamua hatusaidii chochote katika jambo hili. Mimi nasema, jamani sheria ikitungwa hapa siyo mwisho wa dunia, siyo mwisho wa kila kitu.

Hata kesho mnaweza mkaleta *amendment* na tukabadilisha. Kajaribuni kusoma vizuri, kwa hakika hili jambo liko *very clear,* mimi ninavyoona. Napenda niwashauri kwa sababu, msimamo wa nyuma ulikuwa unatazama kama siyo kama *survivors pension* kama fungu fulani tu la fedha kwa maana linagawiwa na ndiyo hapo linaingia kwenye sheria za kimila na mambo mengine kama mlivyokuwa mnasema. Hicho kinachokuwa kinadaiwa kwa maana ya msimamo wa uchangiaji ni tofauti kabisa na kilichopo hapa.

Naomba sana kutokuharibu muda wa Bunge, niwaombe tuendelee na mimi ndio niliyesikia na waliosema ndiyo, ndio walioshinda. Kwa hiyo naomba tuendelee. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu muda wetu kidogo unakaribia kwisha, kwa mujibu wa kanuni ya 28(5) nitaongeza dakika 30 na kama itakuwa hatujamaliza, tutaomba tena tuongeze kwa sababu ratiba yetu imebana sana, hatuna muda wa kufanya siku nyingine kazi hii, na kuna vifungu zaidi ya 150, naomba tujitahidi sana tuweze kumaliza.

Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa napendekeza kifungu cha 21(4), *notwithstanding the penalty imposed under subsection (3) the Bank shall have the power to-*

*(a) regulate the Fund to comply with the investment procedures.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwa sababu tuna hii mamlaka ambayo tumeianzisha, nashauri kwamba mamlaka hii ipewe majukumu haya badala ta Benki Kuu lakini kwa kuwa kuna kifungu cha Sheria katika Sheria Mama ya 2008, kifungu cha mahusiano kati ya benki na hii *authority* kwamba Benki Kuu iwe inatoa ushauri lakini mamlaka ya nidhamu iwe katika mamlaka hii ambayo tunaitungia Sheria leo. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. La kwangu ni dogo sana ni la ufundi tu. Kwenye kifungu kidogo cha (2) mstari wa tatu kutoka chini, neno lile *guideline,* mimi nadhani lazima liwe *plural* yaani *guidelines*.

Sasa hoja ya msingi ni kwenye (3) mstari wa tano kutoka chini maneno '…*of the Fund taking part of the decision...'.* Mimi nadhani hapa kuna tatizo la lugha tu, ningeshauri isomeke, *'…any officer of the Fund who took part in the decision to invest...*'. Tukiiacha hivi haieleweki tunataka kufanya nini. Nataka *AG* anisaidie hapo, mimi nadhani kuna tatizo la lugha, ni hiyo tu.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kinachozungumzwa ni kwamba msimamizi mkuu wa msuala ya fedha katika *investment* ni *BOT* lakini sasa kwa kuwa kuna *authority* ambayo pia ina *guidelines* za kitaalam kuhusiana na masuala ya *investment* ya *social security in corroboration* na *BOT* wa-*issue guidelines* kuhusu *investment* za hii mifuko, ndiyo maana ya kuweka *BOT* pale. *BOT* ita-*appear* katika kila mfuko inapokuja kwenye mambo ya *investment* ya hizi pesa na ndiye mdhamini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haya maneno, mimi nafikiri nakubaliana na Mheshimiwa Chenge.

**MWENYEKITI:** *AG* una neno kuhusiana na maelezo ya Mheshimiwa Chenge?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yapo. Kwanza naungana na Mheshimiwa Chenge lakini hili la Benki naomba nilisemee, kwamba suala la ku-*regulate investments* za mashirika ya fedha katika mfumo wa huu tulionao wa *social security* kwa kweli ni la Benki Kuu na Benki Kuu haiwezi kuwa na mwenza kwenye hili, nafikiri tuwe *very clear on that one*. Kwa hiyo, *reference* ya *item (4)* ni *Bank of Tanzania*. Nafikiri benki ndio iliyokusudiwa na sio *authority*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *item (3),* kwanza neno *guideline* kuwa *guidelines* nakubali kwa sababu ni *plural* sio singular. *Item* (3) nadhani isomeke, '*where an investment is made in breach of subsection (1), each member of the Board of Trustees, director, manager or any officer of the Fund taking part in that decision shall be personally liable to a penalty of fine as prescribed under the Social Security Regulatory Authority'*.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maelezo haya mimi kidogo yamenichanganya kwa sababu Mheshimiwa Waziri alikuwa anaongea kitu kingine na *AG* alikuwa anaongelea kitu kingine. Sasa labda nipate ufafanuzi kidogo maana ilikuwa inaonekana Mheshimiwa Waziri alikuwa anakubaliana na hoja yangu lakini *AG* amekwenda kinyume kidogo na hoja hiyo.

**MWENYEKITI:** Kama ulisikiliza kwa makini, ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri ndiyo ulikuwa wa msingi, wa *AG* ulikuwa unaongezea tu. Sasa tuchukue tu ule wa Mheshimiwa Waziri kwamba mtazamaji wa mifuko hii ni Benki Kuu. Sasa uwepo kwenye utaratibu wowote ule hapa wala si jambo baya, labda

useme tu kama ile *schedule* yako unaiona *still valid* au unakubaliana na msimamo wa Serikali katika hili?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Nakubaliana na msimamo wa Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo huu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 33

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinasema kwamba Bodi itakuwa inafanya mapitio ya zile *rates* za *contribution* pamoja na zile *regulations* na *directives* ambazo zitakuwa *issued* na *Authority*. Tatizo ambalo nilikuwa naliona hapa ni kwamba Mamlaka hii inawezekana isiwe na ile *technical capability* ya kukaa na kuangalia hususani hapa nilikuwa nalenga katika Bima ya Afya. Nilikuwa nasema kwamba kabla haijatoa hizi *guideline* ingekuwa ni vyema wakawa wanashirikisha Wizara husika na nikawa nimeshauri kwamba tuongeze maneno pale itakapokuwa inaishia iseme kwamba *`after consultation with the minister responsible for health'* badala ya Mamlaka yenyewe iwe inaweka viwango hivi.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo yanayohusu *rates of contribution* ambayo sasa ni kazi ya Mamlaka, si mambo ya kiafya. Ni *contribution* za wadau na wanachama wa mfuko huu, kwa mfano sasa hivi ni asilimia tatu. Sasa Mamlaka inaweza ikasema, hapana, labda *rate* ipungue iwe asilimia mbili au *two point something.* Kwa

hiyo*, it has nothing to do with* masuala ya kiafya ambayo ni ya ku-*consult* wataalam wa afya.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, havina uhusiano?

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA**: Havina uhusiano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunafanya *amendment* katika kifungu hiki kinachohusiana na *The National Insurance Fund* Act, Cap. 395. Sasa mambo haya kidogo ni ya kitaalam kwa sababu hapa tunaongelea masuala ya bima ya afya, kuna gharama za matibabu ambazo kwa jinsi nilivyokuwa naiangalia hii Mamlaka haina uwezo kipekee kukaa pasipo kushirikisha wadau kujua kwamba gharama fulani za mahitaji zinaweza zikawa kubwa au zikawa ndogo. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwa angalizo tu katika suala zima la utendaji hata kama wao watakuwa na mamlaka ya ku-*issue guidelines* lakini wafanye *consultation* na wahusika katika sekta husika.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo yatahusu afya kwa kweli *Authority* itapata *consultation* na Waziri anayeshughulika na masuala ya afya lakini kama ni masuala ya pesa, *Authority* ile ina wataalam wa kutosha kuhusu masuala ya pesa na *contribution* na hiyo ndiyo kazi yao ambayo tunataka wafanye. Kwa hiyo, masuala ya pesa kama *contribution rate* na *formula*, Mamlaka hii inaweza lakini mambo yanayohusu afya hayo tutayakuta kwenye kifungu fulani, hayo lazima tutawasiliana na Waziri wa Afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile bila shaka umeelewa?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika. Mimi sioni madhara ya kukiweka

kwenye *explicitly* katika hii Sheria, haitatupunguzia jambo lolote itakuwa wazi. Kwa hiyo, naomba sana tuongeze haya maneno ili kifungu hiki kikae vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Hayo maneno yapo hapa kweli? Mheshimiwa *AG!*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba Mheshimiwa Ndugulile ana hoja kwa msingi kwamba anaona kwamba hili ni jambo ambalo pia linaangukia Wizara ya Afya lakini hapa kinachoangaliwa ni mawanda *(scope)* tunayotaka hapa kama anavyosema Mheshimiwa Waziri ni ku-*regulate* na nafikiri hatuwezi kuwa na *double regulators* na ni vizuri kama ilivyo hii kazi iachiwe *Authority*. Ukisema kwamba uongeze, kuongeza tu haitaleta ufanisi mbele ya safari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile nafikiri tukubaliane na Mheshimiwa Waziri kama ilivyo na kwamba *regulator* huyu apewe haya mamlaka yeye mwenyewe.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, labda kabla hujazungumza, ukisema hiyo *consultation* hapa *with minister of health* maana yake ume-*generalize* sasa lakini hizi *rates* zanamaanisha *rates* mbalimbali sio hiyo peke yake. Sasa kama huko mbele kutakuwa na hiyo inayohusu bima ya afya itakuwa *dealt specific* lakini kwa hapa ukiweka hiyo ume-*generalize* kwamba *rate* zote ziwe *consulted* na Wizara ya Afya, sijui Mheshimiwa Ndugulile unaionaje?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado nadhani hoja yangu ina msingi kwa sababu kifungu hiki kinaangukia chini ya *Act* ya *National Health Insurance Fund*. Kwa hiyo, mimi bado naona kwamba *consultation* na wadau wa sekta ile husiKa bado ni jambo la

msingi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba maneno machache *after consultation* yaingie, mamlaka bado yataendelea kuwa chini ya Mamlaka hii lakini bado kupata ushauri kutoka kwa wadau nadhani ni jambo la msingi.

**MWENYEKITI**: Labda tufafanue. Mheshimiwa Ndugulile ni kwamba, maana tuko kwenye Kamati tunaweza tukaogelea, tukashauriana. Ukisema kwamba tuweke tu *after consultation with the minister of responsible with health* labda ungesema *in health matters*, sasa ukisema hiyo una-*generalize*. Sasa ukisema hayo marekebisho tuingize hapa tutatunga Sheria mbaya. Isipokuwa kwa mambo yale ya *health* sasa kama tukienda huko kama haipo ndivyo tungeweza kusema hivyo lakini tukii-*plug* kama ilivyo tutatengeneza Sheria mbaya kwa sababu hizi *rates* sio za bima ya afya tu. Sasa mimi nadhani tupige kura. Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema katika kupitia hizi *rates* sio kwa hii bima ya afya tu, watafanya vilevile kwa *PPF*, watafanya kwa *NSSF* na kadhalika. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba tukifika huko vilevile tuseme wata-*consult* na Wizara ya Fedha, wata-*consult* na *local authority* tukienda kwenye *LAPF*, kwa sababu wataifanya kwenye mifuko yote. Sasa *consultation* za kawaida za kitaalam hatuwezi kuziandika kwenye Sheria na hizi zinafanyika kama tunavyojua kwamba wataalam wote watafanya kazi kwa *consultation* kutafuta wataalam wako wapi. Sasa tukienda kufanya kila mfuko wa-*consult* Wizara husika tutakuwa hatuamini mamlaka hii ambayo tunaianzisha na tunajua watakuwa na uwezo mkubwa na pale ambapo hawana watafanya *consultation* kwa mujibu wa kazi zao za kawaida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hoja ni hivyo basi nakubaliana na tunaweza tukapitisha kifungu hiki.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu alishasema amemaliza. Sasa hapo ni ule uandishi wa awali na tulivyoichukua ni kwamba baada ya kubalisha ile inabadilisha vifungu vingi. Mheshimiwa Chenge alisema vizuri sana. Nadhani ile inaendelea vilevile, kwa hiyo, kwa Mheshimiwa Mangungu hakuna *schedule* maana kwa mujibu wa Kanuni ameiondoa mwenyewe. Kwa mujibu wa Kanuni anaiondoa kwa utaratibu huo, maana haturuhusiwi kuondoa *schedule*. Tuendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa sawasawa na *discussion* tuliyokwishakuifanya. Kwa hiyo, *schedule* hii naiondoa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa na neno dogo tu. Kuna mahali pengi pame-*appear* habari ya *actuary* na mimi nilikuwa nimeuliza katika mchango wangu kwamba je, Tanzania tunao hao watalaam wa *actuary* kwa sababu mimi ninachojua hatuna hata mmoja na nikasema kama hatuna basi nipate maelezo ya Serikali kujua inafanya nini ili kupata hao wataalam. Suala la kuendelea kuwatafuta wataalam hawa kutoka Ulaya, Kenya, *we are spending a lot of money* na gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa. Naomba kupata maelezo.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba wataalam hao hatunao na Mamlaka mara nyingi inatafuta wataalam kutoka nje wanakuja kufanya kazi, ni kama *Auditor General* anapochukua mashirika ya hapa ndani yanasaidia kufanya *audit* maeneo ya Serikali kutokana na ukweli kwamba hawezi kufanya kazi zote peke yake. Ukweli ni kwamba wataalam wa *actuary* hatuna, tunachukua kutoka nje, wanafanya kazi lakini Mamlaka na sehemu zingine zinapata taarifa.

**MWENYEKITI:** Ni suala la ufafanuzi tu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Kifungu kipi?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimesimama toka kifungu, samahani.

**MWENYEKITI**: Bila shaka tutakufikia.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50
Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 53

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninachosimamia hapa kuna vifungu ambavyo vinasomeka kama 57, 52 na 53B, *schedule* yangu ndivyo inavyoonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi suala ambalo nalizungumzia hapa ni kwamba; kwanza, nashukuru Serikali imeona umuhimu wa kuona kwamba wanaolipwa mafao yao wasicheleweshwe kiasi cha kuweka mipaka kwamba angalau ndani ya miezi miwili wawe wamelipwa lakini sijaridhika na kifungu hiki kwa sababu katika mwendelezo wake kinasema kwamba endapo mfuko utakuwa umeshindwa kulipa ndani ya miezi miwili, basi ni kiasi tu cha kutoa taarifa kwa Mamlaka na huyu mwenye mafao. Ikishatoa hiyo taarifa tayari inakuwa kwamba baadaye mwenye haki ya kusema kwamba hiki kilifanyika vizuri au siyo vizuri inabakia mikononi mwa Mamlaka. Kwa hali hiyo kwa jinsi ambavyo kifungu kimekaa, kinaondoa ile haki yote ambayo mwanzo ilionekana kupewa huyu mtu mwenye mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, mimi nadhani kwa sababu nia ya Serikali ni njema ya kuhakikisha kwamba mifuko

inafanya kazi kwa wajibu, lakini vilevile ni kuona kwamba badala tu ya kufikiria kuwekeza katika maeneo mengine, wawekeze pia katika kuhakikisha kwamba hawa wafanyakazi au wanaochangia mifuko wanalipwa kwa wakati, kwa hali hiyo, nimeleta haya mabadiliko kwa kuomba kwamba kusiwe na hali ya kuzungukazunguka kwamba mhitaji mafao yake mpaka amwone nani, aende wapi! Kimsingi kama itakuwa imeshindikana kumlipa ndani ya ile miezi miwili ambayo imewekwa na endapo huyu mwenye kudai mafao yake au mtegemezi hajahusika kwa namna yoyote ile yeye katika kusababisha huo ucheleweshaji, basi awe na haki ya kuanza ku-*charge interest* na kufikia asilimia 15 kama ilivyo ghamara za benki tunapokuwa tumekopa. Suala hilo tusilionee haya, tuliunge mkono ili kuhakikisha kwamba watu wanahudumiwa inavyostahili lakini kama kuna maboresho mazuri zaidi yanayolenga kujenga, basi nitawasikiliza Waheshimiwa Wabunge wengine. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sasa mnao-*chipin* ambao hamna *schedule*, ningeomba tutumie dakika chache kidogo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nitatumia dakika chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninapongeza sana hoja aliyoileta Mheshimiwa Manyanya lakini mimi nilikuwa niko katika kifungu hicho cha 3 kinachozungumzia: *"where the Fund fails to pay retirement benefit to the member within a period specific under subsection (1),* ambayo ni *two months, it shall be required to give reasons in writing to the member and the Authority".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sasa ielezwe wazi ni muda gani *specific* ambapo hii *Authority* itaandika barua kwa Bodi, yaani hii Mamlaka itaiandikia Bodi barua hiyo kwa muda gani na yule *pensioner* pia ataandikiwa kwa muda gani. Hii ni kwa sababu mimi naamini kabisa *right delayed is right denied*. Kwa, hiyo naomba ionyeshe wazi huyu mtu ataandikiwa barua *within what particular time*.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono mapendekezo ya marekebisho yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Manyanya, kwa sababu ukiangalia kwenye jedwali, marekebisho mapya ya upande wa Serikali, kifungu kile cha 53(B), 49(3),(4) inaeleza kwamba mamlaka ya kupewa taarifa yako kwa Mamlaka na Mamlaka ndiyo inayoamua yenyewe ifanyeje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pendekezo la Mheshimiwa Manyanya lina ubora wa mambo mawili, moja, linaongeza kiwango cha asilimia cha faini. Pendekezo la Serikali lilikuwa ni asilimia mbili peke yake, pendekezo la Mheshimiwa Manyanya ni asilimia 15 kwa mwaka, ambalo naliunga mkono. Pili, linaweka mipaka ya uwajibikaji. Kwa sababu kwa pendekezo la Serikali, mamlaka ambayo kimsingi ingepaswa kuwa chombo cha rufaa ndiyo ambayo yenyewe inayoamua kama mtu apewe faini au asipewe, yenyewe ndiyo inayoamua. Sasa kwa pendekezo la Mheshimiwa Manyanya, yule aliyechelewesha anawajibika kwa mujibu wa sheria kulipa faini na hii itatoa fursa masuala ya rufaa yahamishwe kwa Mamlaka kama mtu hatoridhika na kiwango cha rufaa ama namna ilivyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile upande wa Serikali utakapotoajibu, nitaomba utoe ufafanuzi kwa sababu kifungu hiki kinachohusika pamoja na marekebisho yaliyopendekezwa, hakielezi utaratibu wa uwasilishaji wa malalamiko na ushughulikiaji wa malalamiko. Sasa kama si lazima kuweka kwenye sheria, basi kuwe na kifungu kidogo fulani kinachotoa

mwanya wa kutengenezwa kwa kanuni namna gani mtu aliyeathirika anaweza kuwasilisha *complaints* ili kuwe na *channel* hiyo ya uwasilishaji wa *complaints*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama!

**MWENYEKITI:** Ulisimama Mheshimiwa?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo nilisimama.

**MWENYEKITI:** Sikuwa nimekuona kwa kweli. Niliwaona hao ambao wamesema, utapata fursa baadaye. Sasa kwa sababu muda wetu tuliouongeza unakaribiakuisha na kazi yetu bado mbichi kabisa hapa na hata vifungu tulivyovifika, hatujafika cha 50 na viko 150, kwa hiyo, Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge)!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 150, naomba Bunge lako Tukufu likubali kutengua kifungu cha 28(2)(5) ili muda uongezwe hadi tutakapomaliza kazi iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Kanuni ya 28(2)(5) ilitenguliwa kuruhusu Bunge kuendelea)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii wa Mwaka 2012 *(The Social Security Laws (Amendment) Act, 2012***

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani…

**MWENYEKITI:** Tupo kwenye yale marekebisho ya Mheshimiwa Manyanya.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** *Yah!*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kifungu cha 53B, nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Waziri kwa sababu nafahamu kwamba wakati fulani makosa haya hayatokani na mifuko bali waajiri. Nimemsikia Mheshimiwa Mnyika anasema kwamba mifuko hii inaweza kupeleka hizo *penalties* kwa waajiri wenyewe lakini kimsingi nakubaliana na marekebisho yaliyoletwa na Mheshimiwa Manyanya na naomba yaingizwe kwenye eneo hilo ambalo limesemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Manyanya anasema tufute kifungu cha 3 na tufute pia kifungu cha 4 na tuingize maneno yale ambayo ameweka kwenye marekebisho yake, mimi sina tatizo na hilo. *(Makofi)*

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, marekebisho yameingia na hivyo tunakuwa tumetengeneza kitu kizuri, kwa kweli na mimi niipongeze Serikali kwa kuwa *flexible*, hapa mmefanya kazi kubwa.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa *Eng*. Manyanya na uamuzi wa Kamati na Serikali kuyakubali hayo. Lakini kama nilivyomwelewa mtoa hoja hii, ni vizuri *record* ikakaa sawa, alisema iwapo Kamati yako itakubaliana na mapendekezo haya, basi katika kila eneo la Muswada huu ambapo kuna sura kama hii, lazima marekebisho husika yafanyike na mimi nataka niisaidie Kamati yako eneo la kwanza, ingawa yeye alianza mbele, lakini sura hii unaikuta ukurasa wa 4 wa marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukishakubali hiyo, lazima uanzie huko halafu ndiyo ufike kwenye ukurasa wa 6 wa marekebisho ya Serikali ambayo ndiyo tumeyachukulia uamuzi sasa lakini kwa kutoa tahadhari utayakuta tena ukurasa wa 7 kwenye marekebisho ya Serikali, halafu utayakuta tena ukurasa wa 9 wa orodha ya marekebisho ya Serikali, nadhani hilo ndilo eneo la mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nayasema haya ili kuisaidia Kamati yako kwamba uamuzi huo haulengi tu kwenye kifungu hicho ambacho uamuzi umechukuliwa na Kamati yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kama nimeeleweka.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Chenge kwa kuisaidia Kamati ili tuweze kutengeneza sheria kwa sababu

hapa tunapotengeneza itakwenda kurekebishwa. Sasa marekebisho haya yatapatikana wapi, ni kwenye *Hansard*. Kwa hiyo, kwa maana ya ufafanuzi wa Mheshimiwa Chenge na wenyewe uinge kama sehemu ya Mheshimiwa Manyanya katika kuweka sasa *record* sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tunakubaliana.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Tuendelee!

Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 68

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 76

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 83

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu! Aah, alishaondoa, alishaondoa!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuweke kwenye kumbukumbu sahihi kwamba sijaondoa, nimekubaliana na marekebisho tuliyoafikiana na Serikali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, sawa!

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 84
Ibara ya 85

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88
Ibara ya 89
Ibara ya 90

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 91

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94

Ibara ya 95
Ibara ya 96
Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99
Ibara ya 100
Ibara ya 101
Ibara ya 102
Ibara ya 103
Ibara ya 104

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 105

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108
Ibara ya 109
Ibara ya 110
Ibara ya 111
Ibara ya 112
Ibara ya 113
Ibara ya 114
Ibara ya 115
Ibara ya 116
Ibara ya 117

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 118

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 119
Ibara ya 120

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 121

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 122

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 123

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 124

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 125

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 126
Ibara ya 127

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 128

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 129

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 130
Ibara ya 131

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 132

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 133
Ibara ya 134
Ibara ya 135

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 136

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 137

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 138

*(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 139

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 140

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 141

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hicho kifungu nilikuwa naomba niongeze neno dogo ili lisomeke `*the Authority shall, in exercising its powers under this section, issue directions and guidance.* Nilikuwa naomba niongeze neno `*and guidance'* ili iipe *Authority* wajibu wa kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kwamba watapokea maelekezo *(directions)* lakini pia wawe na uwezo wa kutoa ushauri wa kitaalam ndiyo maana napendekeza tuongeze neno `*guidance',* nashukuru.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitakuwa na tatizo na hilo, isipokuwa mimi nilifikiri kwamba wazungumzaji wa Kiingereza wanaposikia neno *directions* inasema kwamba ni *how to do it,* itakuwa ni kazi ya huyu anayekuwa *directed* lakini ukiweka na *guidance*, sasa *supervision* ile itakuwaje. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba

ilivyokuwa kwenye sheria ni sahihi ingawa sina *objection* na hilo neno la ziada ambalo linaungana tu na hilo *directions*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo tunakubaliana nini, kwamba *directions* inameza hata lile neno *guidance* analolisema Mheshimiwa Mbunge?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye amesema *guidance*, anasema *give directions and guidance* kwa maana kwamba unawa-*direct* wafanye kitu fulani halafu unawaambia fanya namna hii A, B, C, D, nafikiri hii itakuwa ni kuingia jikoni. Kwa msingi wangu mimi nilikuwa nafikiri kwamba unapotoa *directions* usiende kusema sasa tekeleza namna hii, uwaachie hiyo nafasi wao wafanye kazi hiyo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kiingereza kuna tofauti kati ya neno *guidance* na *directions*, *direction is more over an order* kwamba unatoa maelekezo na unapotoa maelekezo ni kwamba unaambiwa hii ndiyo unatakiwa ufanye, sasa unapoleta neno *guidance*, *guidance* ni neno ambalo *is more friendly*, kwamba inatoa wajibu kwa mamlaka pia ku-*offer assistance*. Hiyo ndiyo *concept* ya *guidance* inavyokuja hapa, kwamba inatoa *assistance* ikiwemo na *technical assistance*, nashukuru.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama vile unaambiwa uende Dar es Salaam, *directions* nenda Dar es Salaam, sasa mwingine anaweza kwenda Dar es Salaam kupitia Arusha, mwingine akaenda Dar es Salaam kupitia Mtwara kutoka Dodoma, sasa tunachotaka kuipa Mamlaka ni kwamba inapowa-*direct* nenda Dar es Salaam kupitia barabara ya Morogoro *to* Dar es Salaam, ndiyo maana *Authority* ina wataalam ambao wanaweza kujua njia fupi ya kufika Dar es Salaam kutoka Dodoma. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba ni kweli kuna tofauti kati ya *guidance* na *directions* na *guidance* ni kwamba ni *polite*, unamwambia

mtu kama unatengeneza chakula, kama unapika ndizi, wale wapikaji wa ndizi watani zangu kuna wengine ambao ni wakwe zangu pengine ufanyeje, sasa hiyo unafika ni kuingia jikoni kwa sababu hiyo ni kazi ya mamlaka inayohusika yenyewe na siyo kazi ya *Authority*.

**MWENYEKITI:** Mimi ninadhani jambo hili halina tatizo kubwa pengine, mantiki ya Mheshimiwa Wenje ilikuwa ni kuboresha, lakini mwenye kazi ya kutafsiri humu ndani ya Bunge ni *AG*, kama ni kwa maana hiyo ambayo ina *accommodate* na lile wazo la Wenje mimi sidhani kama Wenje atakuwa na shida na hiyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 142

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilicho-*note* kwenye hicho kifungu cha 142 ni kwamba tutoe neno `moja' turudishe neno `mbili' ambayo ipo kwenye *Principal Act* ile kwa sababu ukiangalia hapa zile *Trade Unions* wenyewe wame-*maintain two*, lakini *Trade Unions* pamoja na *Employers Association* hawa ni *equal partners* kwenye *negotiations* kama hizi, hata kwenye miundo kama hii. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza wawakilishi wa *employers* na *Trade Unions* kama *Trade Union* wanabaki mbili hawa pia wabaki mbili. Kwa hiyo, tutoe neno `moja' ambalo limeletwa sasa turudishe neno mbili kama ilivyokuwepo kwenye *Principal Act*, nashukuru.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Wenje anafanya *reference* ya 142(1)(f) nadhani na sina tatizo na hayo kwa sababu ndiyo tumeshakubaliana kwamba kuna utatu katika mambo haya, kwa hiyo nakubaliana naye.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 143

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 144

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 145

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hicho kifungu cha 145 nilikuwa napendekeza tutoe neno *'six'* tuweke neno *`three'*, kwa maana kwamba Serikali wanapendekeza kwamba iwe ni *period of six month*, lakini mimi napendekeza iwe *period of three month* kwamba ukaguzi, hii Mamlaka, hizi ripoti kama ni *financial report* ziwe kwao *in every three month* kama ilivyokuwa kwenye *Principal Act* kwa sababu miezi sita ni *such a long time* kiasi kwamba kama kuna *mess* imeshatokea kuja kuirekebisha tayari *is too late* lakini kama kutakuwepo na ripoti zinaenda *after every three month* ni rahisi ku-*detect damage* na kurekebisha kabla haijawa *too big* au kabla haijachelewa. Ndiyo maana napendekeza *instead of every six month* turudishe *three month* kama ilivyokuwepo kwenye *Principal Act*, ni kwa nia njema tu ya kuhakikisha kwamba *followup* ya karibu inakuwepo mara kwa mara.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulibadilisha *from three to six month* ili kutoa muda kwa ajili zile *audited accounts* ambazo zinakuwa *Audit for every three month* wapate muda wa ku-*compile* na kupata ile taarifa kupeleka *every six month*, *auditing* ni *every three month*.

**MWENYEKITI:** Unawezekana ukapeleka in *every three month in time.*

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Kwa hiyo, wapeleke *every six month*, ili kupata muda wa kupeleka zile *audited accounts, three month is too short* kupeleka hizo *audited account.*

**MWENYEKITI:** Umeipata hiyo?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa Waziri, ila ninachosema ni kwamba *you don't need the century* ku-*compile a report, you can compile a report in one week*, na mkawasilisha. Ninachojaribu kusema ni kwamba ukimpa mtu muda mrefu sana kwa nia njema tu kwamba kama *damage* inatokea, *damage* itakuwa ni *too big* kwa sababu muda ni mpana, lakini kama kunakuwepo na *followup after every quarterly* kwa sababu miezi mitatu mitatu ina maana hii inaenda kuwa *quarterly followup*, ripoti inapatikana, inakaguliwa inaangaliwa, kama kuna *damage* ni rahisi kuzuia au kurekebisha kabla haijawa *too big* na Waziri kama kwenye *Principal Act* kule ilikuwepo kila baada ya miezi mitatu na kwa sababu hivi vitu watu siku hizi wanafanya kazi kwenye mitandao, *they have all the information and everything. Compiling a report* haihitaji *century,* ni kitu cha kufanya hata *one week*, nashukuru.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *actually* hii ni *standard* ya masuala ya *accounts*, kwamba ni lazima wapeleke *every six months* kwa sababu ni hesabu za kila mwaka, kwa hiyo huwezi kupeleka *every three months* na hizi ndiyo *standard*, imeshindikana, imeonekana haiwezekani.

**MWENYEKITI:** Unajua kuna utaalam mpya umeingia, kuna *IPSA*, sasa haya mambo pengine unaweza kukuta yamepelekea kumekuwa na ugumu kuyanya *within that range*

*of time*. Kwa hiyo, mimi nadhani *is a very technical thing,* hebu tusubiri tuone.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 146

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu cha 146 kinaipa *authority* lakini ina-*limit authority* ku-*consult* Waziri wa Afya kwa yale mambo ambayo yapo *healthy related*, lakini inaenda tu pale inatulia kwenye Waziri wa Afya. Mimi nimependekeza tuongeze neno pale mwisho `*or any other person or institution as deemed important by the authority'* kwa maana kwamba tusiwa-*limit* kum-*consult* Waziri tu peke yake, tuwape wigo mpana wa kuweza ku-*consult either* mtu au taasisi ambayo wao wanafikiri itawapa *knowledge* au maarifa itakayowasaidia kutekeleza majukumu yao kwamba tuwapanulie mlango ili waweze ku-*consult* zaidi ndiyo maana ya kuleta marekebisho haya.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo siyo baya kwa msingi lakini ukiangalia 146, *section* 36(3) tunachozungumzia hapa ni mamlaka, watu wengine hawazuiwi lakini ni mamlaka hasa ile ambayo inahusika na *healthy services* ambayo ni *Minister responsible for health*. Kwa hiyo, nafikiri kwamba hiyo ndiyo hasa inalengwa lakini hakuna kitu kinachomzuia kwa sheria au bila sheria, kwamba watu wengine wasiwe *consulted*. Kwa mfano Daktari Ndugulile kama mamlaka inaona kwamba huyu anajua hiki kitu inaweza wakazungumza naye wakapata maelezo yake, lakini kwa msingi ni kwamba wafanye *technical matters* na Waziri wa Afya. Kwa hiyo, nafikiri kwamba tungeiacha na Mheshimiwa Wenje angekubali tu tuiache hivi ilivyo na kwa sababu inahusu hiyo tu, mambo ya *health services*.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo kubwa ingawa *AG* ni Mwanasheria mimi siyo Mwanasheria, lakini nilikuwa naamini kwamba kwa sababu sheria ukienda hata kwenye Mahakama watakuhumu kwa vitu vilivyoandikwa. Sasa mimi nilikuwa nafikiria kwamba ikiachwa kama hivi *definitely* ina-*limit the scope of consultation* na ndiyo maana *I thought* ni muhimu sana kwamba tungei-*expand* lakini kama wanaotafsiri sheria wanaona kwamba haina tatizo na mimi sina tatizo.

**MWENYEKITI:** *Problem* ya hiki kifungu kinashughulika tu na suala la *health*, kwa hiyo kimetaka tu mamlaka ku-*consult* Waziri, kwa hiyo tukiweka kitu kingine chochote kinapanuka zaidi ya ile, sasa inakuwa *the other way around,* tunashukuru kwa kuwa umekubaliana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 147

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Kifungu cha pili kulikuwa na ile *composition* ya *Retirement Benefit Committee*, ukiangalia Wajumbe pale unakuta Katibu Mkuu Utumishi ni Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, Kamishana wa Kazi, wote hawa ni watu wa Serikali, katika masuala haya ya kuangalia utatu, mwakilishi wa wafanyakazi uko pale, lakini hapa nilikuwa na lengo kwamba tumwongeze na mwakalishi wa waajiri ili kuleta ule utatu katika suala hili.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mwajiri yupo ambaye ndiyo *Permanent Secretary,* Utumishi kwa sababu hawa ni watumishi wa umma, hii haihusu *private employees* wala *private sector*, kwa hiyo mwakilishi wa waajiri yupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile ipo *very clear* unasemaje juu ya hili.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Waziri.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwenye hicho kipengele inafanana na hoja ya Mheshimiwa Ndugulile.

*(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara mpya ya 148

*(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote*)

Ibara Mpya ya 149

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza niandike maana sitakumbuka. Kuna Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Wenje, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Mhagama, Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Daktari Mgimwa, Mheshimiwa Dokta Tizeba.

Waheshimiwa Wabunge kama jambo likishasemwa na mwingine kwa utaratibu wetu wa Kibunge haturudii, kwa hiyo tunaanza na Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi, katika hili tunaongelea suala la jinsi gani hii mamlaka ambayo kwa kweli

ni ya msingi itakavyoweza kufanya kazi. Ukiangalia uzoefu katika sehemu nyingi ili mamlaka hii iweze kujiendesha vizuri inatakiwa iwe *independent* hata *in terms of* jinsi gani inavyopata fedha. Hii inakuwa ni sawasawa na kama unapokuwa na timu zako za mpira kwamba timu zichangie gharama za *referee* wa ule mchezo lakini hilo tumeliona kwamba tuna vyombo vingi ambavyo vipo katika mifuko mingi ya hifadhi ya jamii ambao nao kwa kiasi fulani wanaweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu mimi lilikuwa kwamba katika maneno ambayo walikuwa wanasema kwamba wachangie sehemu ya jumla ya mapato yao kama gharama za uendeshaji, Mamlaka hii ni ndogo na haitakuwa na watu wengi. Sasa tutakapokuwa tunaita vyombo hivi vichangie sehemu kubwa ya mapato kwa sababu kiwajibu na kitaratibu na kisheria mamlaka zote hizi za hifadhi kuna asilimia ambayo wanaitoa kwa ajili ya uendeshaji ya ile mifuko, sasa tukiongeza na gharama uendeshaji wa hii mamlaka juu ya zile gharama za uendeshaji, tutakuwa tunamuongezea mzigo yule mchangiaji ambaye sisi wenyewe tunataka kuona kwamba mafao yake yanazidi kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba badala ya fedha za uendeshaji zitoke katika mapato ya hii mifuko, mimi nilikuwa nataka nitoe wazo kwamba tujaribu kuangalia kutoa fedha za uendeshaji katika gharama za uendeshaji wa mifuko badala ya kutoka mapato yote ya jumla ya mifuko, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, kwa utaratibu ni kwamba unapaswa kusema kile ulichokileta kwenye *schedule*. Sasa nikiangalia kwenye *schedule* naona kitu kingine na unachokisema hapa ni kitu kingine. Sasa tuchukue kipi, ulichokisema sasa au kilichoko kwenye *schedule of amendment?*

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nifute yale maneno ambayo yanasema kwamba `*based on the total income of each scheme at a rate´* yale yaondolewe, sasa utaratibu gani utakaotumika, watu wengine watachangia lakini yasiwe yale maneno, nilikuwa nataka yale maneno yaondolewa.

**MWENYEKITI:** Mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge, hebu twende *straight* kwenye jambo kwa sababu huu siyo wakati wa kuchangia ni wakati wa kurekebisha kilichopo kwenye sheria. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tutakwenda vizuri zaidi.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nikubaliana sana na hoja ya kimsingi aliyoisema Mheshimiwa Ndugulile ya kuona umuhimu wa ku-*consider* michango ya wanachama na siyo kuitumia tena kuipa hii Mamlaka ili kuweza kufanya kazi zake za udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubali kabisa hoja hiyo ni ya msingi lakini naomba nikubali hoja ya Serikali ya kuona kwamba Mamlaka hii pia inatakiwa ichangiwe ili iweze kufanya kazi zake za udhibiti.

Sasa pendekezo langu, hoja ya Mheshimiwa Ndugulile yeye anasema kwamba `*a levy imposed under this section shall be based on the,* ameamua kuondoa ile *on the total income of each scheme,* hilo ndilo pendekezo la Mheshimiwa Ndugulile kwamba tuiondoe. Sasa mimi katika kukubaliana naye nasema tungeibadilisha pale tukasema, *a levy imposed under this section shall be based on the reduction from administrative cost of each scheme at a rate to be determined by the Minister upon consultation with the Minister responsible for Finance and the Bank and shall be specified in order published in the Gazette by the Minister. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiondoa yale maneno ya Ndugulile, tukaongeza ile *reduction from Administrative cost of each scheme*, kwa hiyo, nadhani tutakuwa tumeweza kupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia na Kamati yangu inatoa maoni ilisema tutakapoingia kwenye zile *administrative cost* zile zipo kila siku, yaani iko sheria inayoiruhusu ile mifuko itumie kiasi fulani cha fedha. Kwa hiyo, ukienda kuchukua ile hata ukisema usipochukua ile inaendelea kubaki wala huingilii fedha za wananchi na wala hutavuruga utaratibu wowote. Kwa hiyo, naomba kuwashawishi Wabunge wenzangu tukubaliane na pendekezo la Ndugulile lakini tuongeze yale maneno pale kusudi tuwe kabisa tunajua tumemuagiza nini Waziri, fedha gani Waziri akaichukue na mahali pa kuichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kupendekeza hivyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Jamani kama haina tofauti kubwa na haya maana wasemaji hapa ni wengi. Hebu tumsikilize Mheshimiwa Mnyika, dakika moja na nusu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Dakika moja na nusu, Kambi ya Upinzani ilipendekeza kwa kuunga mkono mapendekezo haya ambayo yamewasilishwa kwamba *reduction* zitoke kwenye *profit and income from the investment* ili isimguse kabisa mwanachama kwa sababu *administration cost* na zenyewe zinatokana na mafao ya wanachama, matokeo ya kuingiza *regulator* kutegemea *administration cost* ni *scheme* hizi zitaongeza *administration cost* ili ku-*compensate* kiwango ambacho wanakwenda kulipa. Sasa *regulator* akipata mapato kutoka kwenye *profit* au mapato yanatokana na uwekezaji wa zile *scheme* atafanya kazi vizuri ya kusimamia zile *scheme* ili zizalishe mapato mengi zaidi akijua kwamba na yeye atapata kutokana na yale mapato kuliko gharama za

uendeshaji. Kwa hiyo, naunga mkono kuondolewa kwa haya maneno lakini maneno mbadala yawe yanayojikita kwenye kulinda maslahi ya wale wanachama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna haja ya kujali hoja ya Mheshimiwa Wenje baadaye na kuweka mipaka ya mamlaka ya Waziri katika kazi kwa kupitia kanuni badala ya kuwa na *Government Gazette* kwa maana ya *notice* ya viwango peke yake bila na kuwa na *regulation* za ukokotoaji na kadhalika. Kwa hiyo, bado hoja ya Mheshimiwa Wenje naamini itapata wasaa wa kuwasilishwa na yenyewe nitaomba niiunge mkono.

**MWENYEKITI:** Kwa namna yoyote kwa hoja hii tunakuwa na pande hizo mbili ambazo zinahitaji maamuzi na pengine utaratibu utafuatwa. Mimi sidhani kama wengine hapa kuna kitu kipya. Jamani kuna mwenye jambo jipya kwa sababu ya *time*?

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nisonge mbele kidogo kwamba waliozungumza wanazungumza kuondoa ile kwenye *total income of the schemes* lakini inamuachia bado Waziri *free hand* ku-*consult* tu na wengine kuweka *percentages* hizo. Sasa tusione tabu kuzitaja kabisa kwa sababu *I am sure* kwenye majadiliano kwenye Kamati *percentage* ilikuwa *proposed* na zikafanyiwa ukokotoaji zikaonekana zinafaa kuifanya *regulator* ajiendeshe. Sasa ni vema tukazitaja hapa ili tusitoe *loopholes* ambazo zinaweza baadaye kuja kuonekana tulifanya jambo bila kuwa na umakini wa kutosha, tuweke kama 0.04% iliyokuwa *proposed* au *whatever* lakini ijulikane kwamba *levy* ile itakuwa kwenye *administrative cost percent* fulani. Niombe tu kusema tukigusa kwenye *profits* za *investments* kule, *profits* hizi zinaweza kuwa kubwa zaidi sasa tukawa tumeingia tena kwenye kuvuruga hiyo mifuko na siyo kuwasaidia wachangiaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Jamani tatizo ni kwamba *schedule* ambayo mme-*chipin* ilikuwa na marekebisho yake. Sasa uki-*chip in* huanzishi jambo lako jipya ni ama unaunga mkono ama unasema haifai. Sasa hapa tunaanzisha vitu vingine, hapa hoja ni ya Ndugulile na wengine tulio-*chipin* tunajadili hiyo. Kwa hiyo, kilichoanzishwa hapa ni kitu kingine. Twende kwenye hoja ya Mheshimiwa Ndugulile ambaye anasema tubadilishe iwe *shall be based on the total income of each scheme at a rate,* maneno yale ndio anayosema yaingie pale. Sasa ukisimama unataka ku-*contribute* anasema yaondoke ama unaunga mkono ama huungi mkono. Sasa ukileta kitu kipya hapa hakuna cha kuamua, hatuna hiyo *schedule* sisi hapa. Serikali, karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukubaliane kwamba *SSRA* wanahitaji *levy* kutoka kwenye mifuko ili waweze kuwa na uhakika wa kufanya kazi zao kwamba fedha ipo ya kufanyia hizo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikiri tu kwamba hapa tulipaswa kubadilisha lakini hatukubalisha. Tulichokubaliana na Kamati na ambacho sasa hivi Mwenyekiti pia amekizungumzia, hii tozo itatoka kwenye fedha ile ya *administrative cost* ambayo lazima mifuko itaichukua tu kutoka kwenye fedha za wachangiaji, watake wasitake lazima wawe na *administrative costs.* Sasa inapobidi kwamba tupate tozo na Waziri ameridhika kwamba *SSRA* hawana fedha na wanahitaji tozo, tozo hii itoke kwenye *administrative cost at a rate* ambayo Waziri ataamua ndio maana hapa *rate* hatukuweka *from time to time* na *formula* ya kupata hizo fedha itakuwa *determined* na itakuwa *gazetted*. Kwa hiyo, suala la kusema *total cost,* hiyo ndio itawahusu wale wachangiaji, tutakuwa tunachukua fedha kutoka kwa wanachama ambavyo sisi hatutaki kuigusa, tunataka tu ile ambayo tayari mifuko imeshatenga kwa *administrative* zao ndio sasa na *SSRA* inachukua na yenyewe inafanyia *administrative cost*.

**MWENYEKITI:** Mimi kama naielewa vizuri kwa sababu *administrative cost* ni *fixed* yaani ipo, kwa hiyo, wanakuwa na uhakika zaidi ya kupata ile kuliko nyingine sijui ya wapi wakikuambia tuliko-*invest* tumepata hasara na wewe hupati. Kwa hiyo, inaleta shida, sijui Mwanasheria Mkuu wa Serikali unasemaje?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema kwamba katika *set up* yetu hii, huyu wakati wa ku-*negotiate* namna ya kutunga sheria, nafikiri kuna msingi wa hizi hofu, nafurahi kwamba Mheshimiwa Waziri ameiona, mimi nilikuwa nashauri kwamba tuweke kifungu kipya, tuache ile 49A.-(2) kama ilivyo, tuko *paragraph* ya zamani ya 150, tunashughulikia kifungu cha 49A, kwa hiyo nasema tuweke kifungu kinachosema, *there shall be levy payable to the Fund by the scheme, then (2), a levy imposed under this section shall be based on the total income of each scheme at a rate to be determined by the Minister upon consultation with the Minister responsible for Finance and the Bank and shall be specified in an order published in the gazette by Minister.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Bunge liweke *break* na hiki ninachosema sasa ndio naona ni *break* kama nimewasikiliza wote vizuri, kwamba kifungu kipya cha (3), kwamba *the total income prescribed under subsection* (2), hiyo niliyosoma, *shall be taken out of the administrative costs of the scheme.* Narudia tena kwamba *the total income prescribed under subsection (2), shall be taken out of the administrative costs of the scheme. And then,* Chenge anasema, unajua *he went to Harvard, I went to America,* kwa hiyo *language* nayo inatofautiana ni kama *Oxford* na... kwa hiyo, ni kwamba *shall be derived out of the administration costs of the scheme*. Ukishamaliza hivyo sasa kama Wabunge mtakubali hiyo ndio *break* kwa Waziri ili kwamba ifanyike hivyo. Sasa kama utakubaliana na mimi *then* tuna *renumber* vile vifungu vingine vinavyofuata kuwa vifungu vya 4, nafikiri vifungu vya 5, 6 na 7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila kuna kingine kile kifungu kidogo cha 5 ambacho kinasema *subject to approval by the Board, the Authority may invest any of its fund and securities or shares.* Nacho ni kitu ambacho mnatakiwa ninyi kama Bunge mkubali. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba kiondolewe kwamba hawa wasi-*invest* fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona Waheshimiwa Wabunge nyuso zao zinafurahisha. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Kwa hoja hiyo na makofi hayo Mheshimiwa Ndugulile unasemaje?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado siko *very comfortable* na kukiacha hicho kifungu kama kilivyo. Mapendekezo aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Jenista Mhagama na mimi naafikiana nayo, hayo maneno ya *total income* yaondolewe kabisa, tui-*paraphrase in the way* ambayo tulikuwa tunaitaka. Kwa hiyo, mapendekezo ya *AG* kwa kweli sikubaliani nayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sina hakika kama ulimpata maana alisema mengi.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia, nimemsikiliza vizuri sana lakini sikuona umuhimu wa kuongeza kile kifungu pale badala ya kuondoa tu yale maneno, *a total income* na ku-*replace* hayo maneno tunakuwa tunaongeza maneno mengi tu yasiyokuwa na msingi, ile *administrative costs* iwekwe pale na *total income* itolewe.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho watu wanaepuka ni kuweka Mwanasheria wako kwenye nafasi ya kushauri kundi

kubwa. Ninachosema ni kwamba kifungu kile cha (2) kilivyo ukishaondoa maneno haya ambayo Mheshimiwa Ndugulile anasema yaondoke, hakileti maana kabisa.

Mimi ninachosema ni kwamba haya *maneno, based on the total income of each scheme* maana yake ni nini, *at a rate to be determined by the Minister,* nafanya *interpretation* ya maneno hayo kwa kusema kwamba, *the total income prescribed under subsection (2) shall be derived from the administrative costs of the scheme.* Sasa nafikiri hata mimi nikianza kusema kwamba kwenye ugonjwa wangu huu *panaldo* itaniponyesha, Madaktari watanishangaa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa ni kwamba tunabishana humu ndani tunatafuta njia ambayo tutafikia *consensus,* tunayapa tafsiri maneno *based on the total income of each scheme at a rate to be determined by the Minister.* Kwa hiyo, inambana Waziri kwamba katika ku-*determine* hii *rate* ataegemea kwenye *administrative cost*. Sasa watu bora mseme *and I am saying very openly* bila ujanja na bila hiyana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ndugulile nilikuwa nakuomba ndugu yangu zamani tulikuwa tunaogelea wote kule Kigamboni tukubaliane tu halafu twende mbele ya safari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile nimekupa *benefit of doubt.*

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado nadhani turudi katika maneno, tuyaweke vizuri tu, bado hiyo kwa kweli hatujafikia muafaka vizuri. Tukate maneno yale, tuyaweke vizuri ili Wabunge na sisi tuweze kuridhika. *(Makofi)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na jitihada za Dkt. Ndugulile lakini kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuko kwenye Kamati na tunaangalia mapendekezo ambayo yameletwa mbele ya

Kamati. Sasa Mwanasheria Mkuu amesema sahihi kabisa kwamba ukichukua mapendekezo ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kama yalivyo, ukiyaondoa, kifungu kidogo cha (2) hakina maana kabisa. Ndio maana *AG* amejitahidi sana akasema *okay* tumsaidie msomaji wa Sheria hii kwamba tufafanue maana ya *total income* ya kila *scheme*. Kwa vile tunalenga sasa kujibu hoja ambayo imesemwa vizuri na Mheshimiwa Jenista Mhagama na yeye mwenyewe, mimi sidhani kwamba lipo tatizo baada ya kuyafafanua kama alivyofafanua kwamba *total income* ya *each scheme* itatokana na *administrative cost*. Kwa hiyo, mimi namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Ndugulile twende pamoja na tumefika mahali pazuri.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani *AG* hapa amesema vizuri kwamba mamlaka hii ni *Regulatory Authority,* wao kujiingiza sasa katika masuala ya *investment* haikuwa sahihi. Kama huo ndio msimamo wa Serikali mimi naafikiana nao.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninapendekezo kwenye kifungu cha 149.

**MWENYEKITI:** Tuwie radhi sana, kumbukumbu zetu hapa zilijichanganya kwa sababu marekebisho yalikuwa mengi, kwa hiyo, tuwie radhi sana na kwa sababu tulishakipitisha naomba utusamehe.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshawasamehe.

Ibara Mpya ya 150
Ibara Mpya ya 151
Ibara Mpya ya 152

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2012 *(The Social Security Laws (Amendments) Act, 2012***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2012 *(The Social Security Laws (Amendments) Act, 2012),* kifungu kwa kifungu na kuupitisha pamoja na marekebisho yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liukubali Muswada huu kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukishafikia hatua ya kusoma mara ya tatu maana yake tumekamilisha kutunga sheria. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, wataalam na Kamati kwa kazi kubwa ambayo mmefanya. Kipekee niwapongeze sana

Waheshimiwa Wabunge tuliokuwepo katika kazi hii toka asubuhi mpaka sasa hivi, ambapo ni saa tatu na zaidi. Kwa kweli tumefanya kazi kubwa, sheria ilikuwa ndefu lakini inachanganya mambo mengi sana, kwa kweli kipekee niwapongeze sana kwa kazi kubwa na nzuri tuliyoifanya kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Sasa nina matangazo, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ameomba niwakumbushe kwamba kesho kutakuwa na semina ya masuala ya anuani za makazi na kuhusu kuhama kutoka analojia kwenda dijitali na utekelezaji wa mawasiliano katika sehemu zisizovutia wawekezaji unaotekelezwa na *UCAF*. Semina hiyo itaanza saa 4.00 asubuhi, anaomba Waheshimiwa Wabunge kuwahi na kuhudhuria semina hiyo.

Mheshimiwa Daktari Mary Mwanjelwa, anaomba niwatangazie wanawake wote kwamba Chama cha Wabunge Wanawake Tanzania watakuwa na semina siku ya Jumapili kuanzia saa tano asubuhi.

Tangazo lingine limetoka kwa Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie kwamba kuna kikundi cha *Fast Trust* ambacho mlezi wake ni Mheshimiwa Celina Kombani, Mbunge na Waziri, watafanya maonyesho ya shughuli za kutunza mazingira kwa kufanya usafi katika eneo la Bunge kesho tarehe 14/4/2012 kuanzia saa tatu asubuhi. Zoezi hili lina lengo la kuhamasisha umma kutunza mazingira. Hivyo, wanawaalika Wabunge wote kushiriki kwenye zoezi hilo la kufanya usafi katika mazingira ya Bunge. Kwa hiyo, tukifanya usafi ndio tutaingia kwenye semina sasa.

Najua tumechoka, sina tangazo lingine hapa basi naahirisha Bunge hadi Jumatatu Saa Tatu asubuhi.

*(Saa 3.06 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 16 Aprili, 2012 saa tatu asubuhi)*

**KIAMBATISHO I**

**ISSN 0856 – 035X**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***BILL SUPPLEMENT***

***No. 1*** ***12th January, 2012***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 2 Vol. 93 dated 12th January, 2012*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

THE SOCIAL SECURITY LAWS (AMENDMENTS) ACT, 2012

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Sections* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title and commencement.
2. Amendment of social security laws.

PART II
AMENDMENT OF THE LOCAL AUTHORITIES
PENSIONS FUND ACT, CAP.407

3. Construction.
4. Amendment of section 3.
5. Amendment of section 4.
6. Amendment of section 7.
7. Amendment of section 8.
8. Amendment of section 11.
9. Repeal of section 15.
10. Addition of section 18A.
11. Amendment of section 22.
12. Addition of section 24A.
13. Addition on section 27A.
14. Amendment of section 29.
15. Addition to section 29A.
16. Amendment of section 30.

17. Amendment of section 35.
18. Amendment of section 38.
19. Amendment of section 39.
20. Addition of section 43A.
21. Amendment of section 49.
22. Amendment of section 50.
23. Amendment of section 59.
24. Amendment of section 60.
25. Repeal of section 65.
26. Amendment of section 78.
27. Amendment of section 81.
28. Amendment of the First schedule.

PART III
AMENDMENT OF THE NATIONAL HEALTH
INSURANCE FUND ACT, CAP.395

29. Construction.
30. Amendment of section 3.
31. Amendment of section 4.
32. Amendment of section 6.
33. Amendment of section 10.
34. Addition of section 12A.
35. Amendment of section 16.
36. Addition of section 39A.
37. Amendment of section 33
38. Amendment of section 43.
39. Amendment of the Schedule.

PART IV
AMENDMENT OF THE NATIONAL SOCIAL
SECURITY FUND ACT, CAP. 50

40. Construction.
41. Amendment of section 2.
42. Amendment of section 4.
43. Amendment of section 6.
44. Repeal of section 8.
45. Amendment of section 9.
46. Amendment of section 12.
47. Addition of section 15A.
48. Amendment of section 18.
49. Amendment of section 20.
50. Addition of section 20A.
51. Amendment of section 21.

52. Amendment of section 24.
53. Amendment of section 27.
54. Amendment of section 42.
55. Repeal of section 46.
56. Amendment of section 47.
57. Amendment of section 48.
58. Amendment of section 53.
59. Amendment of section 55.
60. Amendment of section 56.
61. Amendment of section 61.
62. Amendment of section 62.
63. Amendment of section 63.
64. Amendment of section 68.
65. Amendment of section 69.
66. Addition of sections 71A and 17B.
67. Amendment of section 72.
68. Amendment of section 74.
69. Amendment of section 76.
70. Amendment of section 77.
71. Amendment of section 81.
72. Amendment of section 82.
73. Repeal of sections 83, 84, and 85.
74. Amendment of section 89.
75. Amendment of section 91.
76. Amendment of the First Schedule.
77. Amendment of the Second Schedule.

PART V
AMENDMENT OF THE PARASTAL ORGANIZATIONS PENSIONS SCHEME ACT, (CAP. 372)

78. Construction.
79. Amendment of Section 1.
80. Amendment of section 2.
81. Amendment of Section 3.
82. Amendment of Section 4.
83. Amendment of Section 6.
84. Amendment of section 7.
85. Addition of section 7A.
86. Amendment of section 8.
87. Amendment of section 10.
88. Amendment of section 11.
89. Amendment of section 12.

90. Amendment of section 13.
91. Addition of section 13A.
92. Amendment of section 14.
93. Amendment of section 16.
94. Amendment of section 17.
95. Amendment of section 18.
96. Amendment of section 20.
97. Amendment of section 22.
98. Amendment of section 24.
